**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 6 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO:**

Taarifa ya Kwanza ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Ukaguzi wa Utendaji juu ya Menejimenti ya Kuzuia Mafuriko katika Bonde la Wilaya ya Babati *(A Report of Controller and Auditor General on the 1st Performance Audit Report of the Management of Prevention and Mitigation of Floods at Central Regional and Local Levels of the Government of Tanzania (A Case Study of Floods in Babati).*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Pamba Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Annual Report and Accounts of The Tanzania Cotton Board for the year ended 30 th June, 2006).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 158

**Upanuzi wa Barabara Jijini Dar es Salaam**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. ANIA S. CHAUREMBO)** aliuliza:-

Kwa kuwa upo mpango unaendelea wa upanuzi wa barabara kwenye maeneo yaliyojengwa bila mpango katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na Buguruni, Vingunguti na kwa Mganga Wilayani Ilala na Temeke na kwa kuwa, mpango huo una lengo la kuboresha huduma za jamii:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kwamba ni nani anayefadhili mpango huo na utagharimu kiasi gani cha fedha?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia ujenzi holela katika Jiji la Dar es Salaam ili kuwaondolea wananchi adha na kero hii wanayoipata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuboresha maeneo yaliyojengwa bila mpango maalum unatekelezwa na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kupitia mradi wa *Local Goverment Support Project* Unaoratibiwa na Ofisi yangu. Jiji linatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu kwa kushirikisha jamii na mradi wa kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato. Katika kuboresha miundombiunu mitaa 31 katika Kata 8 zenye watu 320, watanufaika. Huduma zitakazoboreshwa ni barabara za lami, changarawe, Njia za waenda kwa miguu, taa za barabarani, mifereji ya maji ya mvua, maji, vyoo vya uma na vifaa vya kuhifadhi taka. Kata zitakazaohusika ni Manzese, Kigogo, Mwananyamala katika Manispaa ya Kinondoni, Buguruni na Vingunguti katika Manispaa ya Ilala na Sandali, Chang'ombe na Azimio kwa Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza programu itagharimu dola za Kimarekani milioni 12.49 ambapo kati ya hizo, dola za Kimarekani milioni 9.69 ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Serikali Kuu inachangia dola milioni 2. Halmashauri na wananchi watachangia dola milioni. Awamu ya pili itaanza mwaka 2008 kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 15 ambapo asilimia 90 ni mkopo na asilimia 10 ni mchango wa Serikali, Halmashauri na wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linatekeleza mpango wa upanuzi wa barabara kwenye maeneo yaliyojengwa bila mpango maalum na miradi mbalimbali inayolenga kupunguza na kuondoa adha na kero kwa wananchi na Miradi na mipango hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa kuboresha miundombinu kwa kushirikisha wananchi *(CIUP) Community Infrastructure upgrading Program* ulioko chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

(ii) Mpango wa kuboresha makazi duni mijini *(Cities Alliance)* na unaofadhiliwa na *UN Habitat.*

(iii) Mradi wa kurasimisha rasilimali za wanyonge na utoaji leseni za nyumba zilizojengwa maeneo yasiyopimwa.

(iv) Mradi wa upimaji wa viwanja 20,000. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa kuzingatia juhudi hizi zinazofanywa na Serikali na kwa kuzingatia uelewa na ufuatiliaji, mkubwa alionao Mheshimiwa Mbunge, kuhusu mipango miji, ni mategemeo yangu kuwa atatoa ushirikiano katika utekelezaji wa mipango niliyoitaja hapo juu.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Msongamano ambao uko katika Mkoa wa Dar es Salaam, Serikali ina mpango gani sasa wa kuanzisha makazi mapya na Mji eneo la Kigamboni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama anavyosema mwenyewe Serikali inafahamu kabisa kwamba kuna msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, ni ukweli ambao haupingiki. Serikali kwa sasa ndiyo maana imeanza kupima hivyo viwanja na itatafuta sehemu nyingine ambazo zina nafasi ili kuendeleza makazi na kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na hiyo miradi mbalimbali yote inalenga katika kupunguza msongamano na ujenzi holela katika Jiji la Dar es Salaam.

Na. 159

**Mgogoro wa Ardhi Kijiji cha Mivumoni**

**MOHAMED RISHED ABDALLAH:** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Mivumoni Wilayani Pangani, kiliandikishwa tarehe 3/7/1999 chini ya kifungu Na. 22 cha Sheria Na. 7/1982 na kwa kuwa kijiji kimeandikiwa barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kuwa wananchi wasilime mazao ya kudumu baada ya kuzuka mgogoro usioeleweka:-

(a) Je, Ofisi ya wa Mkoa ina mamlaka gani ya kuwazuia wananchi kijijini humo wasilime?

(b) Je, ni nini uhalali wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kukiuka Katiba ya Nchi, tunaposema ardhi hii ni mali ya wananchi wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 shamba la Mivumoni lilipendekezwa kubinafsishwa toka Mamlaka ya Mkonge Tanzania na Mkataba wa kumwuzia mwekezaji *Larry Electric Works* wa Tanga ulitiwa saini tarehe 12/7/2006. Baadaye mwekezaji alibaini kuwa wapo watu wanaoendesha shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya shamba hilo. Taarifa ilipelekwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Tarehe 8/12/2006 Mkuu wa Mkoa wa Tanga alimwandikia barua Mwenyekiti wa *PSRC* ili atoe maelezo ya mauziano ya shamba hilo. *PSRC* walituma mwakilishi na kufanya kikao kati yake na uongozi wa Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya za Pangani na Muheza pamoja na Mfilisi. Tume iliundwa na kubaini mipaka ya shamba na uendelezaji uliofanyika. Tume imefanya kazi hiyo na kukabidhi taarifa *PSRC*. Mkuu wa Mkoa atapewa taarifa kabla ya *PSRC* kutekeleza uamuzi wowote utakaotolewa. Ofisi ya Mkoa wa Tanga, haikuwazuia wananchi wa kijiji cha Mivumoni kulima. Kikao cha tarehe 26/1/2007 kiliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri, kuwaagiza wananchi wote kusimamisha maendeleo ya kudumu katika shamba la Mivumoni ili kuepusha hasara kama suala la ulipaji fidia litajitokeza kwa mazao yaliyolimwa baada ya mgogoro huu na pia kuzuia uvunjaji wa amani baina ya mwekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria Na. 19 ya mwaka 1997 ya Tawala za Mikoa kifungu cha 4(1) na kifungu cha 5(1) hadi cha (3) na Kifungu cha 6(1) hadi cha (3), Mkuu wa Mkoa amepewa Mamlaka ya kusimamia shughuli zote za Serikali katika Mkoa ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama. Kwa hiyo, agizo la kusimamisha maendeleo ya kudumu kwa muda lilikuwa na nia nzuri tu ya kuzuia kutoweka amani baina ya mwekezaji na wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, haikukiuka Katiba kwa sababu Ofisi hiyo inao wajibu wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapewa fursa ya kumiliki ardhi bila kubaguliwa na wakati huo huo kulinda haki za wananchi wote pamoja na wawekezaji.

**MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali ni mazuri lakini yana utata bado kwa sababu eneo lile ni la Serikali ya Kijiji na kimepimwa na kina hati ya kwamba hii ni Serikali ya Kijiji na eneo lao limepimwa.

(a) Je, Serikali inaweza kututhibitishia kama *PSRC* wametoa kibali na kuwapa wawekezaji hao na kukiuka mipaka ya Kijiji kwa maana ya *overlapping*?

(b) Kwa kitendo hicho wananchi wa Mivumoni wameathirika kisaikolojia kwa maana wamekosa matumaini katika maisha yao kwa kukatazwa kuendeleza maendeleo yao katika kijiji. Je, hiyo si halali kwa wananchi hao, Serikali iko tayari wananchi hao waendelee na maendeleo yao kwa sababu kijiji chao ni halali na wao ndiyo wametangulia kupima? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kijiji

hiki kimepata usajili, Serikali inafahamu hilo na ni ukweli usiopingika kwamba huduma mbalimbali zipo katika kijiji hicho. Kinachofanyika sasa hivi ni kuangalia kwamba ni nani mwenye haki kati ya huyo mwekezaji au wanavijiji.

Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali imeingilia kati na Mkuu wa Mkoa, amefanya hivyo kwa nia nzuri tu kwamba kusiwe na vurugu katika eneo la kijiji hicho ndiyo maana ameingilia kati na amesema kwamba amesitisha kwa muda siyo kwa kudumu. Kwa hiyo, suala hili linaendelea kushughulikiwa na uongozi wa Mkoa pamoja na *PSRC*.

Kuhusu wananchi kuathirika kisaikolojia ni kweli inawezekana wananchi wameathirika kwa kiasi fulani. Lakini tunachotaka kusema ni kwamba tunawapa matumaini kwamba suala hili linashughulikiwa na Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, tukishapata taarifa kamili tutahakikisha kwamba ni (*solution*) ufumbuzi gani utafutwe ili kunusuru wananchi wapewe haki yao na mwekezaji pia apewe haki yake.

Na. 160

**Sekta ya Mifugo kuchangia pato la Taifa**

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefanya jambo zuri sana kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Mifugo hapa nchini kwa lengo la kuendeleza sekta ya mifugo ili iweze kuchangia pato la taifa kwa fedha za kigeni:-

Je, Serikali ina mpango gani unaotekelezeka na kupimika katika kufanikisha lengo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa iliyojiwekea mikakati ya kufikia malengo ya milenia *(Millennium Development Goals (MDGs)* ya mwaka 2015 ambayo pamoja na mambo mengine yanalenga kupunguza umaskini uliokithiri na njaa. Ili kutimiza malengo hayo, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini **(**MKUKUTA**)** uliandaliwa kwa kuzingatia dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka 2025. Sekta ya mifugo ni kati ya sekta zilizopewa umuhimu mkubwa katika MKUKUTA, ambapo sekta hii inatarajiwa kukua kwa asilimia 9 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010. Kukua huku kutaiwezesha Sekta ya Mifugo kuchangia kwa kiwango kikubwa katika pato la taifa, kuongeza kipato cha Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia MKUKUTA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sura ya 5 kifungu (32) Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2005, Mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo nchini wa mwaka 2001 na Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo nchini ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya MKUKUTA, Wizara yangu imeandaa mpango mkakati wa muda wa kati *(Medium Term Strategic Plan)* wa Wizara kwa kipindi cha mwaka 2007 – 2010. Mpango huo utaanza kutekelezwa kupitia Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Bajeti ya Serikali *(Medium Term Expendidture Framework (MTEF)* Kwa kipindi cha 2007/2008 – 2009/2010.

Katika mpango mkakati huo, dira ya Wizara yangu ni kuwepo sekta ya mifugo yenye hadhi ya kimataifa na ambayo ni endelevu kiuchumi, kijamii na inayozingatia hifadhi ya mazingira. Aidha, madhumuni ya mpango huo ni pamoja na Wizara kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2010:

(a) Pawepo na mifugo bora na mazao yake yanayokidhi mahitaji na viwango vya soko la ndani na nje?

(b) Uwekezaji katika sekta ya mifugo uwe umeongezeka kwa asilimia 15?

(c) Elimu kuhusu ufugaji wa kisasa iwe imetolewa kwa wafugaji na kuleta mabadiliko ya asilimia 50 kutoka hali halisi iliyopo sasa;

(d) Mifumo yote ya ufugaji iwe imeboreshwa na huduma za ugani ziwe zimeongezeka kwa asilimia 50 kutoka hali iliyopo sasa;

(e) Magonjwa yote ya mifugo yenye athari kubwa za kiuchumi yawe yamedhibitiwa au kutokemezwa nchini; na mwisho

(f) Kuwepo na ukusanyaji, utunzaji, usambazaji na matumizi ya takwimu sahihi za mifugo pamoja na matokeo ya tafiti mbalimbali kwa wadau wa sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yaliyotekelezwa katika mpango mkakati huo ni pamoja na:-

(a) Kutunga Sera ya Taifa ya Mifugo, ambayo imepitishwa na Serikali mwezi Desemba 2006 na sasa Wizara inaandaa mkakati wa kutekeleza sera hiyo;

(b) Kuanzisha mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji; na

(c) Kuongeza mauzo ya mifugo na mazao yake ambapo katika mwaka 2006/2007, jumla ya ng'ombe 2,542 na mbuzi 1,852 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.3 wameuzwa nchi za Comoro, Kuwait, Falme za Kiarabu, Oman na Burundi.

Pia, jumla ya tani 70 za nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe zenye thamani ya shilingi milioni 180 zimeuzwa nje.

Aidha, jumla ya vipande vya ngozi milioni 4.8 vilikusanywa ambapo kati yake vipande milioni 3.7 vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.2 viliuzwa nchi za nje. Mapato hayo ya mauzo ya mifugo na mazao yake yamechangia kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilio cha wafugaji wengi nchini kimekuwa katika suala la kujengewa majosho pamoja na kupata ruzuku katika madawa ya kuoshea mifugo.

Je, Serikali ina mkakati gani kwa kuanzia kwenye suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wafugaji wengi wana kilio cha kuwa na majosho ya kutosha na madawa yenye ruzuku.

Tumeeleza mara nyingi hapa kuwa suala la majosho linapaswa liibuliwe na wafugaji wenyewe huko waliko ili hatimaye Halmashauri husika ziweze kufikisha maombi yao kwenye mpango wa maendeleo ya sekta ya kilimo Wilayani *DADs* ili hatimaye fedha ziweze kupatikana na kuweza kujenga majosho.

Mheshimiwa Spika, namjulisha Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwa ujumla sisi tunao wajibu wa kuwahamasisha wananchi wetu wafugaji ili waweze kuibua miradi hiyo ili hatimaye tuweze kujitosheleza suala la kuwa na majosho.

Mheshimiwa Spika, suala la ruzuku kama tulivyowahi kusema hapa Bungeni ruzuku ya madawa ya kuogesha mifugo ilianza kutolewa kwenye mwaka wa fedha 2006/2007 ambapo Mikoa 18 ukiondoa Dar es Salaam, Ruvuma na Lindi ndiyo ambayo haikupata.

Lakini mingine yote imepata madawa ya ruzuku ya kuogesha mifugo. Kwa mwaka huu wa fedha mikoa yote 21 itapata madawa ya ruzuku ya mifugo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Lakini bado tupo kwenye masuala haya haya ya mifugo.

Na. 161

**Matatizo yanayosababisha wafugaji Kuhamahama**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa wafugaji wengi wamekuwa wakihamahama kwa sababu ya kufuata malisho, maji na huduma za dawa:-

(a) Je, ni malambo mangapi yamechimbwa hadi sasa katika Wilaya ya Misungwi?

(b) Je, Wilaya ya Misungwi ina majosho mangapi na kati ya hayo, ni mangapi yanafanya kazi?

(c) Je, ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo imetolewa na kwa sasa ni shilingi ngapi kwa lita na aina za dawa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba uhamaji wa wafugaji kwa kiasi kikubwa husababishwa na uhaba wa malisho, maji na kutafuta huduma ya madawa ya kuogesha mifugo yao.

Kwa kutambua hivyo, kati ya mwaka 2001 na 2007 Wizara yangu kupitia utaratibu wa kuchangia asilimia 50, Halmashauri za Wilaya asilimia 30 na vijiji asilimia 20, imejenga na kukarabati malambo saba (7) Wilayani Misungwi katika vijiji vya Mabuki, Misungwi, Nguge, Kanyelele, Ikungumkulu, Matale na Ngudama. Malambo hayo yamesaidia kuwapunguzia wafugaji tatizo la uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utekelezaji wa miradi sasa uko chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, natoa wito kwa Halmashauri hiyo kuibua miradi ya ujenzi wa malambo/mabwawa na miundombinu mingine ya mifugo kupitia miradi ya *DADPs* na *PADEP* ili kuboresha huduma muhimu kwa mifugo.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi, ina jumla ya majosho 39 yanayomilikiwa na wadau mbalimbali kama ifuatavyo:-

Halmashauri na Wilaya ya Misungwi majosho (31), shamba la kuzalisha mitamba Mabuki majosho (6), Taasisi ya utafiti na mafunzo ya kilimo Ukiriguru (1) na mtu binafsi josho (1). Kati ya majosho hayo 39, 14 yanafanya kazi ambayo yapo katika vijiji vya: Usagara, Kanyerere Koromije, Mwajombo, Matale, Kabale Mwagimagi, *LMU* Mabuki (6) na Ukiriguru.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali ilitoa fedha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo, ambapo wafugaji walitakiwa kununua dawa hizo kwa asilimia 60 ya bei ya soko na Serikali kulipia asilimia 40 kama ruzuku. Bei ya dawa kwa lita inatofautiana kulingana na aina ya dawa. Makampuni manane ya *Mukpar Tanzania Ltd. Tanzania Ltd, Bytrade Tanzania Ltd, Anicrop Services Ltd, Bajuta General Vet Agro, Ronheam International Company Ltd, Tan-Veterina Ltd.* na *Ultravetis Tanzania Ltd.* ambayo yaliingia mkataba na Wizara yalitakiwa kusambaza dawa za ruzuku katika mikoa yote nchini isipokuwa mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma na Mtwara ambayo itaingizwa kwenye awamu ijayo yaani 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kampuni za *Mukpar Tanzania* na *Tan-Veterina Ltd* zilitakiwa kusambaza dawa za mifugo Mkoani Mwanza ikiwemo Wilaya ya Misungwei.

Kampuni ya *Mukpar Tanzania Ltd.* ilitakiwa kuleta dawa aina ya *Paranex (Alphacypermethrin)* ambayo inauzwa shilingi 48,120 kwa lita na wafugaji kuinunua kwa takribani shilingi 29,000 tu na gharama iliyobaki kulipiwa na Serikali kama ruzuku. Aidha, Kampuni ya Tanzania *Ltd* nayo ilitakiwa kusambaza dawa aina ya *Norotraz (Amitraz)* ambayo inauzwa shilingi 14,000 kwa lita ambapo bei kwa wafugaji ni shilingi 8,400 tu. Tofauti ya bei ya dawa hizo kwa lita inatokana na ukali wa dawa na kiasi cha dawa kinachochanganywa kwenye maji.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonipa. Lakini pia nitoe pongezi kwa *WFP* ambao wameleta chakula cha kazi na kukarabati malambo ya Misasi, Fela, Kanyerere, Nguge na Gwanzamiso. Nawapongeza sana.
(a) Kwa kuwa Naibu Waziri alipotembelea Wilaya ya Misungwi akaenda Kijiji cha Kanyerere alikutana na wananchi wa Budutu. Yeye mwenyewe Naibu Waziri akiwa na watendaji wa Halmashauri ya Misungwi aliahidi wananchi wa Dudutu wangejengewa josho katika eneo lao la Budutu na Gambajiga.

Mheshimiwa Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hadi sasa hivi josho hilo halijajengwa, sasa sijui unawaahidi nini wananchi wa Budutu kutokana na ahadi yako hiyo? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa tatizo la madawa ya ruzuku bado ni kubwa zaidi hapa nchini na aidha, fedha inayotolewa ni kidogo mno, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuongeza fedha hizo ili angalau wananchi waweze kupata madawa hayo kwa bei ya nafuu zaidi na kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wananchi wa Kanyerere walinipa heshima kubwa sana nilipotembelea mwaka jana kwenye Jimbo la Misungwi na ni kweli niliahidi na bado nazidi kuahidi kuwa ahadi niliyoisema nitashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kuhakikisha kuwa josho katika Kijiji cha Kanyerere linajengwa.

Utaratibu nimeueleza hapa kuhusu ujenzi wa majosho na malambo kupitia *DADs*. Kwa hiyo, napenda kumwaahidi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Misungwi hususan Kijiji cha Kanyerere kuwa nitahakikisha josho hilo linajengwa na nitarudi Kijiji cha Kanyerere.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sasa Serikali inatoa asilimia 40 ya ruzuku kwenye dawa za kuogesha mifugo na itaendelea kufanya hivyo kwa sasa na kama nilivyosema kwenye suala la nyongeza la Mheshimiwa Zubeir, mwaka huu tunajumuisha Mikoa yote ya Tanzania Bara kuhakikisha kuwa inapata dawa za ruzuku kwa ajili ya kuboresha huduma ya mifugo kwa wafugaji wote nchini. *(Makofi*)

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Shinyanga ambazo zina mifugo wengi hususan ng'ombe; na kwa kuwa kufuatia ziara ya Naibu Waziri Wilayani humo mwaka jana aliwahamasisha wafugaji na wananchi wa Wilaya ya Kahama kuiunga mkono Serikali katika harakati zake za kuboresha huduma kwa mifugo hususan ujenzi wa mabwawa na majosho na ukarabati jambo ambalo wafugaji na wananchi wa Wilaya ya Kahama walilipokea kwa vitendo. Je Naibu Waziri anaweza kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba yuko tayari kuja Kahama mwezi huu kufungua moja ya majosho ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali mwaliko ambao tayari anao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Lembeli, kwa juhudi alizonazo za kushirikiana na wananchi wa Wilaya ya Kahama kuhakikisha kuwa mifugo inapata huduma zinazostahili za kuwa na majosho kwa ajili ya kuogesha na maji na hii ni kuzingatia kuwa si tu Kahama kama Wilaya lakini Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa wa kwanza kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo nchini na kwa hiyo napenda kuhakikishia, nafurahi kusema kuwa niko tayari, nimeupokea kwa mikono miwili mwaliko wa kwenda Kahama kwa ajili ya sherehe hiyo, isipokuwa tu ningependa kusema kuwa suala la tarehe naomba tujadiliane ili tuone tarehe muafaka kabisa ili kusudi sherehe yetu hiyo iweze kufana ili tusiwe na haraka tuweze kujimwaga vizuri kwamba sisi wa Shinyanga tunaongoza kwa mifugo kama tulivyo na nafasi. *(Makofi)*

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa katika Jimbo la Solwa kuna ng'ombe zaidi ya laki tatu mia tatu na arobaini na nne na kwa kuwa sasa hivi kati ya majosho 14 ni mawili tu yanayofanya kazi. Na kwa kuwa wananchi inavyoonekana hawana uelewa wa kuibua miradi ya majosho. Je, Serikali kwa nini isiwaelimishe wananchi hasa wa jimbo la Solwa

au kutoa mwongozo mzuri kwa wananchi ili kuongeza idadi ya majosho kukidhi ng'ombe au mifugo iliyoko katika jimbo la Solwa?

**SPIKA:** Unaruhusiwa moja tu kwa sababu siyo mwuliza swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli jimbo la Solwa lina majosho 14 lakini ni machache sana yanayofanya kazi. Kuhusu suala lake alilosema napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kama anavyofahamu Mkoa wa Shinyanga ulishatengeneza mpango kabambe wa maendeleo ya sekta ya mifugo ambao unajumuisha suala la ujenzi wa majosho na huduma zingine za mifugo. Mpango huu ulipitishwa mwaka jana na Kikao cha Mkoa cha mashauriano *RCC* ambapo sote tunawajibika pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi wetu wafugaji ili kuhakikisha kuwa wanaibua miradi ya ujenzi wa majosho.

Napenda basi kumwalika Mheshimiwa Ahmed ili tushirikiane sisi Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga ili kuhakikisha kuwa mpango huu unatekelezwa kikamilifu ili kusudi Mkoa wa Shinyanga kama ilivyo mikoa mingine ijitosheleze kwenye suala la majosho.

Na. 162

**Zao la Muhogo**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la muhogo ni muhimu kwa chakula hapa nchini hasa wakati wa njaa na kwa kuwa zao hilo linakosa virutubisho muhimu kwa afya ya binadamu:-

Je, Serikali haioni kuwa, kuna hoja ya kulifanyia utafiti wa *Biotechnology* zao hilo kama ule uliofanyika katika zao la mtama kwenye nchi za Ulaya kwa lengo la kulinda afya za wale Watanzania ambao chakula chao kikubwa ni muhogo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa zao la muhogo hauonekani wakati wa njaa tu. Muhogo unaliwa na watu zaidi ya milioni 250 katika nchi za Kiafrika na zaidi ya watu milioni 600 katika dunia nzima. Katika Tanzania Mikoa inayoongoza kwa kilimo cha muhogo ni pamoja na Kigoma, Tabora, Mtwara, Mara, Pwani, Morogoro na Tanga.

Aidha, zao la muhogo lina matumizi mengine mengi kama vile utengenezaji wa wanga kwa ajili ya viwanda vya nguo, utengenezaji wa vyakula vya mifugo na nishati

mbadala ya *bioethanol.* Muhogo unatumika pia katika viwanda vya kutengeneza biskuti na vifungashi *(packaging materials)* na hivi sasa unga wa muhogo unauzwa katika baadhi ya *super markets* katika miji mikubwa.

Kwa maelezo hayo, dhana ya zao la muhogo kuwa zao la njaa siyo sahihi inabidi ibadilike. Kinachotakiwa sasa ni kuongeza tija ya uzalishaji na kuwasaidia wakulima kupata soko la uhakika wa zao la muhogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kwa ufupi kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Salim Khamis kwamba iko haja ya kufanya utafiti wa bayoteknolojia kwa madhumuni ya kuongeza baadhi ya virutubisho katika zao la muhogo. Ziko tafiti zinazoendelea katika taasisi mbalimbali za kimataifa zinazojaribu kuongeza viwango vya protini, vitamini A na kupunguza kiasi cha kemikali aina ya *cyanogen* ambayo ni sumu inayopatikana kwenye majani na mizizi ya muhogo. Hata hivyo Wizara yangu haijaanza utafiti wa kuboresha virutubisho katika zao la muhogo kwa njia ya bayoteknolojia kwa sababu mbili zifuatazo:-

(i) Serikali bado inaifanyia kazi Sera ya Bioteknolojia ya Taifa ambayo itaainisha maeneo na utaratibu wa kutumia teknolojia hii mpya hapa nchini bila kuleta migongano ya sekta mbalimbali. Uandaaji wa sera hii unaratibiwa na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira inakamilisha mfumo wa udhibiti wa matokeo ya bioteknolojia *The National Biosafety Framework* pamoja na kanuni zake *Regulations* kabla ya kuruhusu utafiti na matumizi ya teknolojia hii mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la muhogo, hivi sasa Wizara yangu inatumia teknolojia ijulikanayo kama *molecular breeding* kutafuta aina ya mihogo yenye kutoa mavuno mengi na yenye ukinzani dhidi ya magonjwa ya bato-bato, bato-bakteria, michirizi ya kikahawia na wadudu wanaoitwa tanabui wa mihogo. Aidha Wizara yangu inatumia utaalamu wa *tissue culture* kuzalisha mbegu bora za mihogo isiyo na vimelea vya magonjwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zote za utafiti wa kitaalam wa kutumia bayoteknolojia unaoendelea duniani, siyo rahisi kupata aina moja ya muhogo au ya zao lolote lile ambalo litakuwa na virutubisho vyote vinavyotakiwa kwa afya ya binadamu. Hivyo napenda kuwashauri wananchi kubadili tabia ya ulaji wa vyakula na kuzoea kula aina mbalimbali za mikunde, nyanya chungu na soya ambazo zina virutubisho vingi ambavyo havipatikani katika muhogo na kisamvu tu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa matatizo makubwa ya nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanzania siyo tu upungufu wa chakula lakini ni chakula bora. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatumia watafiti wetu mbalimbali katika vituo tofauti vya

utafiti ili angalau kupunguza kama si kuondoa kabisa tatizo hili la upatikanaji wa chakula bora? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa maana ya Wizara inaendelea kufanya utafiti kwa kutumia vyuo vilivyopo na kushirikiana na vyuo vingine vilivyoko nje ya nchi. Nimesema katika jibu langu la msingi kwamba tafiti mbalimbali zinaendelea kufanywa na vituo mbalimbali vya kimataifa. Lakini pia hapa kwetu kituo chetu cha Ukiriguru kinaendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuboresha vyakula vyetu ambavyo tunavitumia. Pamoja na usindikaji wake.

Pia tunashirikiana na vyuo vingine, kwa mfano hapa tuna *International Institute for Tropical Agriculture Tanzania Office* ndiyo inashirikiana na vituo vyetu hapa pamoja na Wizara nzima na vyombo vingine na Wizara nyingine zinazohusika na suala hili la chakula bora. *(Makofi)*

Na. 163

**Matokeo ya Mitihani**

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY (K.n.y. MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS**) aliuliza:

Kwa kuwa, madhmuni makubwa ya kuwatahini wanafunzi ni kupima uwezo wao kielimu, na kwa kuwa, baadhi ya nyakati watahiniwa wa Kidato cha Nne na Sita baada ya kupata taarifa ya matokeo yao kuwa ni mabaya huamua kufuatilia matokeo yao Baraza la Mitihani na kukuta matokeo yao ni mazuri.

Je, ni sababu gani zinazosababisha utofauti wa matokeo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kumekuwepo na mabadiliko ya alama katika matokeo ya mitihani kwa baadhi yawatahiniwa wanaokata rufaa. Mabadiliko katika alama hutokana na makosa ya ujumlishaji na uhamishaji wa alama za watahiniwa. Hata hivyo, rufaa zinazobadilika ni ndogo sana kiasi cha asilimia 3 kwa kupanda asilimia 1 kwa kushuka na asilimia 96 ya alama hubaki bila mabadiliko.

Kwa taratibu za uendeshaji wa mitihani viwango hivyo vinaubalika kimataifa. Ili kupunguza uwezekano wa kujirudia kwa makosa ya aina hiyo, hatua mbalimbali zimechukuliwa za kuimarisha zoezi zima la usahihishaji wa mitihani. Hatua hizo ni pamoja jopo la watu wanaofanya kazi ya uhakiki wa usahihishaji na utumiaji wa kompyuta katika kujumlisha alama. Hatua za kuimarisha ukokotoaji na uhamishaji wa alama zitaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa kasoro zote zinaweza kusababisha utofauti wa matokeo zinarekebishika.

**MHE. KABUZI. F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja suala la rufaa. Matatizo yanayowapata wanafunzi katika kukata rufaa yanafanana na walimu wanapokuwa na matatizo katika kukata rufaa. Wanapata matatizo kutokana na kwamba mwajiri wao haeleweki wana waajiri wanne, wana Wizara ya Fedha, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Utumishi. Sasa hata kama umestaafu huwa ni shida sana kupata huduma. Wamekuwa wakiomba chombo kimoja cha kuajiri Walimu.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwamba sasa katika bajeti hii ameandaa nini kusudi waondokane na matatizo ya kuhangaika katika rufaa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ningependa Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba suala la kuwawezesha walimu kufanya vizuri kazini kwao ni la msingi sana ili kweli Sera ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi iweze kutekelezeka ipasavyo.

Kwa hiyo, namwunga mkono kabisa kwamba kuna umuhimu wa kuangalia ajira ya walimu ili kuharakisha huduma kwao ikiwa ni pamoja na kupanda madaraja na kupata haki zao kwa urahisi. Ningeomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa sababu kwa mwaka nzima wa 2006/2007 tumehangaikia sana suala la jinsi ya kuondoa urasimu katika ajira ya walimu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina, kusafiri nchi za nje, kuhusisha wadau wenyewe, pamoja na walimu wenyewe.

Namwomba avute subira ili suala hili lifuate mkondo hatimaye walimu waweze kupata huduma kwa urahisi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kama alivyosema Naibu Waziri kuwa matokeo yanaweza yakabadilika na yakamfikia mhusika vile yalivyokuwa hayakusudiwa. Je, mhusika anaombwa radhi na kama hakuombwa radhi na kama hakuombwa radhi anayo nafasi ya kujitetea kuishitaki Baraza?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba rufaa kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ni chache sana na wale wachache ambao ni asilimia 4 tu ya mabadiliko kimahusiano huombwa radhi. *(Makofi)*

Na. 164

**Mchango wa Kampuni za Uwindaji**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. DORA HERIEL MUSHI)** aliuliza:

Kwa kuwa, zipo Wilaya zenye maeneo makubwa ya uwindaji, kama ilivyo kwa Wilaya ya Simanjiro ambayo ina eneo lenye ukubwa wa takriban kilomita za mraba 20,000 (20,000$km^2$) ambazo zimezagaa wanyama kuanzia Kata ya Kitwai mpaka Emoret:-

Je, Kampuni za uwindaji zinachangia kiasi gani cha fedha katika Maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hizi *network* za Wabunge ni ngumu sana kwa Spika kuzielewa. Mtu usiyedhani anamwelewa mwenzie unakuta humu kumbe anamwelewa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Heriel Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 10(4)(b) ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2000 na marekebisho yake inazitaka kampuni za uwindaji wa kitalii kuchangia katika kusaidia miradi ya Maendeleo ya wananchi, uzuiaji ujangili na uendelezaji wa vitalu.

Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2002/2003 hadi mwaka 2006/2007, kampuni za uwindaji wa kitalii zilizopo katika Wilaya ya Simanjiro zimechangia jumla ya shilingi 135,832,365/= kwa Halmashauri ya Wilaya ambayo ni mgao wa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2002/2003 hadi 2006/2007, Kampuni hizo za uwindaji wa kitalii pia zimechangia jumla ya shilingi 208,683,155/= ili kusaidia miradi ya maendeleo katika vijiji vilivyo karibu na vitalu vya uwindaji wa kitalii katika Wilaya ya Simanjiro. Michango hiyo ilitolewa kama fedha taslimu, vifaa na huduma. Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa kutokana na michango hiyo ni pamoja na kusaidia ujenzi wa shule, majengo ya ofisi za vijiji, Zahanati, Uchimbaji wa Visima vya Maji, Ununuzi wa Madawati, Madawa ya Binadamu, Chakula wakati wa njaa na kadhalika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa hii asilimia 25 imekuwa ya muda mrefu

mpaka leo na kwa kuwa Serikali wakati inasoma Bajeti yake hapa ilisema wazi kwamba Idara ya Wanyamapori itaongeza mapato yake mpaka kufikia bilioni 34. Je, asilimia 25 nayo itafikiriwa kutokana na mapato hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Idara ya Wanyamapori inadhamiria na ina mikakati ya kuongeza mapato yake. Lakini mpaka sasa asilimia 25 ya mapato hayo inayokwenda kwa Wilaya ambazo ziko karibu na vitalu vya uwindaji wa kitalii itabaki kama ilivyo. Kwa sababu kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, si tu asilimia 25 ya mapato yanakwenda katika Wilaya husika. Vile vile kampuni za uwindaji wa kitalii huwa zinachangia miradi ya Maendeleo katika vijiji ambavyo viko karibu na vitalu vya kuwindia. Aidha, mfuko wa uhifadhi wa wanyamapori pia nao huwa unasaidia miradi ya Maendeleo katika vijiji mbalimbali.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri je, kwa vile biashara ya uwindaji inaonekana kupanuka mwaka hadi mwaka. Je, ni lini Serikali ilili-*revise* kwa mara ya mwisho *fees* za uwindaji ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata mapato yanayofaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii iliangalia upya hizi ada za uwindaji wa kitalii mwaka 2001.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Serikali iliyopitishwa ya Waziri wa Fedha, kuna ada mpya zitakazotozwa katika maeneo ya uwindaji. *(Makofi)*

Na. 165

**Ujenzi wa Laini ya Umeme ya Msongo wa 132 kv Makambako – Songea**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, tathimini ya kujenga laini ya umeme ya *132 kV* kutoka Makambako hadi Songea ilishakamilika:

Je, fedha za ujenzi wa laini hiyo zimeshapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli tathmini ya ujenzi wa laini ya Makambako – Songea ya Kilovoti 132 imekamilika na *project document* za upembuzi yakinifu zimeshapelekwa *SIDA*. Kwa

hivi sasa Serikali yetu ya Tanzania inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Sweden kufanikisha ufadhili wa mradi huu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwenye Bajeti inaonekana kwamba kuna pesa bilioni 9.5 zimetengwa na Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba mazungumzo yanaendelea. Je, ataweza kuwafahamisha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma juu ya hali halisi ilivyofikiwa?

Pili, kwa kuwa gridi ya taifa inategemea umeme kutoka vyanzo mbalimbali na kwa kuwa Bwana Andoya mzalishaji binafsi wa umeme wa maji anakerwa sana na Wizara ya Nishati na Madini kwa kutokushirikiana naye kama ambavyo anatoa ushirikiano kwenye taasisi nyingine kama *IPTL,* na wenzao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuongoza na mimi mpaka Mbinga ili aweze kusikiliza kilio cha Bwana Andoya? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu swali. Naanza kupata wasiwasi. Nashtuka na naanza kuona kwamba inapokuwa anayeuliza swali ni Mbunge mwanamke anamwomba Waziri mwanaume ndiyo afuatane naye. *(Kicheko/Makofi)*

Na inapokuwa kwamba anayeuliza swali ni mwanaume anamwomba Waziri au Naibu Waziri mwanamke ndiyo afuatane naye. Lakini hata hivyo Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kuhusu milioni 9.5. Naomba nifafanue kwamba Mkoa wa Ruvuma kwa bahati nzuri sana una miradi miwili. Nina hakika Mheshimiwa Mbunge kwa takwimu hizi na kwa kuzingatia kwamba Wizara yetu ya Nishati na Madini haijawasilisha Bajeti yake, inakuwa ngumu kidogo kuthibitisha anachokielezea Mheshimiwa Mbunge kuhusu milioni 9.5. Lakini kwa hakika ni kwamba mradi huu ufadhili wake utatoka Serikali ya Sweden.

Kuhusu suala la pili, Mheshimiwa Spika, kama ambavyo inatarajiwa nisingeweza kukataa mwaliko huu niko tayari kuandamana na Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Likokola na wewe unataka Naibu Waziri aje kwako? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali lingine la nyongeza. Je, Serikali inafahamu ya kwamba mji wa Songea una matatizo makubwa ya umeme na kama inafahamu Serikali inafanya nini kutatua kero hiyo kubwa ya umeme katika Manispaa ya Songea?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Tunafahamu kwamba mji wa Songea una matatizo ya umeme kutokana na uchakavu wa jenereta zao wanazozitumia sasa hivi. Sasa hivi jenereta zao mbili

zinafanyiwa ukarabati na vile vile tumekwishawasiliana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Songea kwamba *TANESCO* ilikuwa mbioni vile vile kutafuta utaratibu wa kupata jenereta mpya wakati tunangojea huu mradi mrefu ambao amekwisha uzungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri.

Na. 166

**Mchanga wa Madini Unaosafirishwa Nje ya Nchi**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia hamsini na tano (55%) ya mchanga wa madini unapelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kusafishwa:-

(a) Je, Serikali inajua kiwango halisi kilichopatikana kutokana na mchanga huo?

(b) Je, ni madini aina gani na yenye thamani gani yamepatikana kutokana na mchanga unaosafirishwa nje ya nchi kati ya mwaka 2002 – 2006?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, asilimia hamsini na tano (55%) ya dhahabu inayozalishwa na mgodi wa Bulyanhulu pekee ndiyo inayotokana na *gold-copper-silver concentrate* inayofahamika na watu wengi kama mchanga, unaosafirishwa nje ya nchi na sio asilimia hamsini na tano (55%) ya mchanga unapelekewa nje ya nchi kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, tofauti na migodi mingine, kwa sababu za kijiolojia mgodi wa Bulyanhulu unaomilikiwa na Kampuni ya Bulyanhulu *Gold Mine Limited* ambayo ni Kampuni tanzu ya *Barrick Gold Tanzania Limited* unazalisha aina mbili za mazao:-

(1) Vitofali vya dhahabu *(gold dores)* na

(2) Mchanga wa dhahabu na shaba (*gold-copper-silver concentrate*). Zao hili la pili ndilo linajulikana kama mchanga na husafirishwa kwenda nje nchini China au Japan kwa ajili ya kutenganisha dhahabu, shaba na fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kupata madini yaliyomo katika mchanga huo ni lazima yatenganishwe (kuchenjuliwa) kwa kutumia teknolojia ambayo haipatikani hapa nchini. Teknolojia hiyo ni ya gharama kubwa. Mtambo unaotumika kufanya kazi ya kutenganisha dhahabu, fedha na shaba (*gold-copper-silver refinery*) huhitaji mtaji wa kiasi cha kati ya Dola za Marekani milioni 400 hadi 600.

Mheshimiwa Spika, Mtambo huu unahitaji tani za mizani (*equivalent tones)* 150,000 za mchanga kwa mwaka ili kuuendesha, wakati mgodi wa Bulyanhulu huzalisha "mchanga" usiofikia tani za mizani 25,000 tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sababu hizi zimechangia kuchelewesha kupata wawekezaji wa kujenga mitambo ya kuchenjua dhahabu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kusafirisha mchanga kwenda Japan au China haufanyiwa na nchi ya Tanzania peke yake, bali pia hufanywa na nchi nyingine ambazo huzalisha mchanga wa namna hiyo kwa sababu kama hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya mchanga huo kusafirishwa kwenda nje ya nchi, kiwango cha madini yaliyomo na thamani yake hukadiriwa na malipo ya mrahaba hufanyika. Sampuli ya mchanga isiyozidi uzito wa kilo moja (1) huchukuliwa kutoka kwenye makontena yakiwa bado mgodini. Sampuli hizo hupelekwa kwenye maabara ya *Geological Survey of Tanzania* iliyoko Dodoma na maabara ya Kituo cha Madini cha Kusini na Mashariki mwa Afrika (*SEAMIC*) kilichopo Kunduchi Dar es Salaam kwa ajili ya kupimwa ili kujua wingi wa madini ya dhahabu, shaba na fedha yaliyomo kwenye sampuli hiyo.

Matokeo hayo hutumiwa katika kukokotoa na kukadiria wingi wa madini hayo kwenye mchanga uliomo kwenye makontena. Mrabaha hulipwa kwa kuzingatia kiasi cha madini yaliyokadiriwa kutokana na sampuli zilizochukuliwa (*provisional*). Baada ya hapo maafisa madini wakishirikiana na maafisa wa mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* huweka rakili. Kampuni nayo huweka rakili yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchanga kusafirishwa nje na utenganishaji wa dhahabu, fedha na shaba kufanyika, kampuni inayofanya kazi hiyo huleta taarifa Serikalini kuhusu kiwango halisi cha madini yaliyomo. Taarifa hiyo pia hupelekwa kwenye kampuni inayomiliki mgodi. Baada ya kupokea taarifa hiyo kampuni hulipa tofauti ya mrahaba.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu nilioueleza ni dhahiri kwamba Serikali inajua kiwango halisi kinachopatikana kutokana na mchanga huo.

(b) Mheshimiwa Spika, madini yanayopatikana kutoka kwenye *gold-copper-silver concentrate* ni dhahabu, fedha na shaba.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2002 na 2006 mgodi wa Bulyanhulu ulizalisha tani 139,890.84 za *gold-copper-silver concentrate* ambazo zilitoa wakia 940,668.15 za dhahabu yenye thamani ya Dola za Marekani 398,055,956.84 wakia 801,447.58 za fedha zenye thamani ya Dola za Marekani 6,279,090.37 na Paundi 42,162,784.83 za shaba yenye thamani ya Dola za marekani 62,982,574.92. Jumla ya Dola za Marekani 14,019,528.66 zilizopatikana kama mrabaha katika kipndi hicho.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna taarifa kwamba yupo mwekezaji kutoka Jamuhuri Cheke ambaye yuko tayari kuanzisha na kujenga kiwanda cha kusafishia madini pale Jijini Mwanza. Je, Serikali iko tayari kushirikiana na mwekezaji huyu katika kutaka kufanikisha ujenzi huu? Ili tuondokane na kupeleka mchanga huu nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa uelewa wake na maoni yake katika hili suala ni kweli iwapo wawekezaji kutoka Jamuhuri ya Cheke ambao kimsingi wamekubaliana kushirikiana na wawekezaji wa Kitanzania na wana mpango wa kujenga kiwanda cha kuchenjua ama kutenganisha dhahabu na mchanga hapa Tanzania na hasa mkoani Mwanza.

Tuna taarifa na hata leo asubuhi nimeongea naona baadhi ya viongozi wa mradi unaotarajiwa wameshapata tayari kiwanja pale Mwanza maeneo ya Nyamongolo, maeneo ya Igoma pale Mwanza na kuna mambo tu ya kawaida mbayo wanayakamilisha katika masuala ya kibiashara na wakishayakamilisha nadhani ujenzi utaanza hivi karibuni, tunaomba tuipokee kwa heri taarifa hii, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya habari hizo nzuri kwa taifa letu, tumefikia mwisho wa kipindi hiki cha maswali. Maswali yamekwisha na muda wa Mawali nao umepita. Sasa ni matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza wageni. Nafurahi kutangaza kuwepo kwa mgeni wetu mmoja ni Mheshimiwa Diwani Mstaafu wa Kata ya Buguruni na mchezaji wa zamani wa *Young Africans Sports Club* (Yanga) ya Dar es Salaam, Bwana Kitwana Manara. Lakini mgeni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Ndugu Kitwana Manara, katika historia ya michezo katika nchi yetu na hususan mchezo wa soka, jina lake nadhani kona zote za Tanzania tunmfahamu. Tunamshukuru sana kwa jinsi alivyolitumikia taifa na tunamshukuru na anaendelea kuwa mfano mzuri kwa vijana wanaochipua katika fani ya michezo na hasa soka hapa nchini Tanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 25 na walimu watano kutoka shule ya sekondari ya Kilakala Morogoro, tunaomba wasimame pale walipo. Karibuni sana Bungeni, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge shule ya Kilakala ni shule ya vipaji maalum. Kwa hiyo, mnaowaona hapo ndio ma-*scientist* wa baadaye, madaktari wa baadaye, wahandisi wa baadaye, Wabunge wa baadaye na si ajabu hata Spika

baadaye anaweza kutoka hapo hapo. Kwa sababu wakati huo viwango vitakuwa vimepanda, ahsante na karibu sana, mtusalimie Morogoro mtakaporejea huko.

Pia wapo wanafunzi wa Chuo cha Biblia *Assembly of God* Dodoma, naomba wasimame. Karibuni sana na tunawatakia mema katika kazi yenu ya kulinda maadili ndani ya nchi yetu ya Tanzania na kwingineko mtakapohudumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa George Lubeleje, mikutano sasa vikao, ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na mkutano leo hii saa 4:30 ukumbi Na. 231, huu ni mkutano muhimu sana ni kwenda kupitia Muswada wa kufanya mabadiliko katika vifungu mbalimbali vya sheria ya bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Kwa hiyo mnaombwa tafadhalini sana suala hili limo linazungumzwa sana katika jamii tunaomba Waheshimiwa Wabunge mkayazingatie ili muweze kutusaidia mabadiliko hayo ya Muswada, kwa hiyo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala saa 4:30 asubuhi hii ukumbi Na. 231 gorofa ya pili jengo la utawala.

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, ameniomba nitangaze kuwa Kamati yote inaalikwa na Balozi wa Uingereza nchini, kwenye chakula cha mchana saa saba mchana *Dodoma Hotel.*

Kutakuwa na usafiri wa *minbus* ya ofisi ya Bunge kutokea katika uwanja wetu pale jengo la zamani kuwapeleka na kuwarudisha Waheshimiwa wajumbe kwenda na kurudi kutoka *Dodoma Hotel.*

Kwa hiyo, saa saba mchana wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, wanaalikwa na Balozi wa Uingereza pale *Dodoma Hotel,* hayo ndiyo matangazo.

## HOJA YA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hii hotuba ya Waziri wa Kilimo na mimi nitangulize tu kwamba nimpongeze Waziri wa Kilimo kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa jana na Manaibu wake hotuba ambayo inatuelekeza tutafanya nini kwa kipindi kijacho, nawapongeza sana wataalam wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa hotuba yake nzuri.

Nitazungumza kwa uchache sana, nitachangia kama tunavyojua kabisa kwamba suala la kilimo katika nchi ndio uti wa mgongo, na nchi hii inategemea sana kilimo. Kwa hiyo, bila kilimo kwa kweli nchi hii haiendi na zungumza hasa katika wilaya ya Kiteto,

kama tunavyofahamu kabisa kwamba wilaya ya Kiteto hasa katika mazao ya chakula ndiyo inayolisha Jiji la Dar es Salaam, ukienda katika Soko la Tandale, bila kuzungumzia Kiteto hasa katika zao la mahindi. Jiji la Dar es Salaam halijapata chakula. Kwa hiyo, pale ndiyo unaweza kugusa Kiteto katika zao la mahindi, ndiyo utaelewa Matui iko wapi, Kibaigwa iko wapi, ndiyo utaelewa Kiteto. Kwa hiyo, kusimama kwangu mimi nasimama kwa niaba ya Kibaigwa, nasimama kwa ajili ya soko la Tandale. Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo inaweza kutambua kabisa kwamba nafasi ya Kiteto kwa chakula iko wapi?

Baada ya kutoka pale sasa hivi katika kilimo ya Kiteto tunakwenda katika zao la Alizeti, mafuta nazungumza hilo kwa sababu gani? Kuna mkakati mkubwa sasa hivi unaofanyika katika mkoa wa Singida, naanza katika Mkoa wa Singida, ambao wanalima zao la alizeti, na kuja katika Mkoa wa Dodoma ambao wamejikita sana sasa hivi katika zao la alizeti, mafuta ya karanga, ufuta na kadhalika na si pale Kiteto tumehama kwenda katika zao la alizeti, tunaomba Wizara ya Kilimo iangalie kwa makini sana zao la alizeti. Katika nchi hii bila sasa hivi kuhama na kuwekeza katika zao la mafuta ya alizeti hatutaweza kabisa kuwa wakulima wazuri, tuondokane kabisa, dunia nzima iko katika zao la alizeti, mafuta kwa hiyo tujiwekeze pale, hilo ndilo lililonifanya nisimame nichangie katika kilimo.

Kwa hiyo, naomba sana Kiteto, kila mwaka kuna trekta zinazoingia Kiteto karibu trekta 600-700 kwa mwaka kwa msimu, mwaka huu kilimo kinachokuja tutakuwa na shida kubwa kwa wakulima wetu. Kwa sababu bei ya mafuta imepanda, dieseli imepanda, lita moja sasa hivi ni shilingi 1,800 Serikali imesema kwamba ni 1300, tukizungumza sasa hivi lita moja ni 1700 mpaka 1800 fikiria mwakani, mkulima atalipa kiasi gani kwa eka, itakuwa ni vigumu sana kama Serikali haitaingilia kati itakuwa ni kazi kubwa kwa mkulima kulima mwakani, na atakopa wapi huyu mkulima maskini wa Kiteto, ili aweze kulima eka zake kumi itakuwa ni kazi kubwa sana.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijaribu kuingia kati ili huyu mkulima wa Kiteto aweze kupata mahala pa kukopa na kulima. Bila hivyo atashindwa, itakuwa ni gharama kubwa sana kuweza kuhudumia shamba lake. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuangalia suala hilo kwa makini sana ili mkulima aweze kupata mahali pa kukopa kwa ajili ya kilimo chake. Kwa hiyo, Serikali iweze kuliangalia suala hili. Vilevile ili Serikali iweze kujitegemea kwa chakula, suala kilimo cha umwagiliaji, lazima lizingatiwe sana katika nchi hii. Nia aibu kubwa sana nchi hii kuweza kuagiza chakula nje wakati kuna mabonde mazuri sana ya kuweza kilima, kuna mabonde mazuri sana ikizingatia sana kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Kwa hiyo tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji, ili chakula kiweze kupatikana vya kutosha katika nchi hii. Hiyo naomba nichangie sana.

Mwisho kabisa ambalo nauliza ni suala la ushirika. Kuna haya mazao mimi nashangaa sana kuna mazao ya biashara kama kahawa, pamba na kadhalika. Kuna mabonde, lakini haya mazao mchanganyiko nayo yatafutiwe namna ya kusaidiwa, kama hii alizeti, mahindi na kadhalika. Nayo yapate bodi za kusemea, nashukuru sana kule Singida wameshaanza Lakini tunaomba hayo tuweke nguvu haya mazao ili nao wapate wasemaji wake wakubwa katika sehemu na wapate mikopo na tunaomba Wizara ya Kilimo iunde bodi za mazao haya mchanganyiko. Pale Kiteto tulikuwa na chama cha

ushirika *AKU,* lakini pale Kiteto tunahitaji chama cha ushirika iondokana na unyanyasaji mkubwa ambao haya mazao ambayo yanatambulika ya kahawa ambaya yanagandamiza sehemu ambazo hazina mazao haya, ili nao waweze kujitegemea. Hiyo ndiyo suala langu kubwa kwamba waweze nao kujitegemea na ushirika tuanzishe vyombo vya ushirika ambayo kuna mazao mchanganyi. Vilevile naomba katika masoko, kuna masoko sisi pale Kiteto tuna soko pale Igusero, tunataka kulipanua tunaomba kabisa Wizara ya Kilimo iangalie tutaanzishaje soko pale Igusero, tumeshajenga, kuimarika kwa masoko yetu.Baada ya kusema haya yote nilitaka tu kuchangia kwamba Wizara ya Kilimo ituunge mkono tuinue soko la Igusero na Matui na pale Dogo. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. FELIX M. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kabla sijaendelea napenda niungane Wabunge wenzangu kwa kutoa pole nyingi sana kwa wafiwa ambayo inakwenda pamoja na Watanzania wote, ambao wamewapoteza ndugu zao kwa ajali za gari zilizoweza kutokea katika mikoa mbalimbali. Lakini pia nitoe pole kwa famili ya Marehemu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, ikiwa pamoja na mume wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Manaibu Mawaziri pamoja na wataalamu wa Wizara hiyo, ambayo kwa hakika hii hotuba ambayo wameiandaa wameiandaa kitaalamu wala haina kasoro hata kidogo. Kwa yale machache ambayo wameyasahau ndiyo haya sasa Waheshimiwa Wabunge tunasaidia kuwakumbusha ili safari ijayo wasiwasahau tena. Napenda niwapongeze wakulima ambao wanalima kilimo kigumu cha kutumia mikono na hasa mkoa wangu wa Kigoma ukiongoza katika hilo nawapa pole sana, lakini wako na Serikali. Serikali inawaona kwa jicho la huruma. Nina hakika baada ya muda mfupi basi watakuwa na kilimo bora kwa kutumia nyezo za kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kilimo tunazungumza kilimo cha mazao ya biashara na kilimo cha mazao ya chakula, na nadhani ndio wajibu wa Wizara hiyo inayohusika kwamba ni lazima isimamie kilimo cha namna hii ili wananchi waweze kufaidika na nini wanafanya. Nasema hivi kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kinaajiri watu wa kawaida karibuni asilimia 90 hasa kwa mkoa wangu ambao nina uhakika na takwimu hizi. Zaidi ya asilimia 90 wanaishi kwa kutegemea kilimo au wengine ndio hao wanafanya kazi Serikalini na nini kwa hiyo tukaona kwamba tunapoambiwa kwamba kilimo ni uti wa mgongo, ni kweli ni uti wa mgongo. Sasa ni kazi ya Wizara inayohusika kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa kinachosimamia na Wizara hiyo na Wizara iwatendee haki wananchi katika kuhakikisha kwamba kilimo kinaendelea kwa sababu wananchi wengi wanaishi kwa kutumia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nije kwenye madhara ambayo mimi nasema ndiyo yamesababisha kuwa duni, ama kukwamisha jitihada za kilimo, kitu kikubwa ambacho hapa nakiona na kila mtu anakiona ni kwamba ni zana zinazotumika ni duni. Sasa hapa mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye mkoa wangu wa Kigoma, kwamba mkoa wa Kigoma una neema, una neena kwa sababu kwa miaka na miaka umekuwa ni mkoa

ambao unalisha mikoa jirani, nchi jirani, kwa ajili ya kilimo ambacho wananchi wanalima kwa kutumia mikono. Lakini kwa kutumia ardhi ambayo kwa kweli ina rutuba kubwa, pamoja na kwamba suala la mbolea tunalitanguliza mbele lakini kwa mkoa wa Kigoma unaweza ukalima kitu bila mbolea na bado ukavuna mazao ya kutosha. Lakini hata hivyo sisemi kwamba Wizara imnyime mwana Kigoma mbolea, hapana ardhi yetu pia imeanza kuchoka. Kwa hiyo, mbolea ni kitu muhimu sana. Sasa jana tulikuwa na Mheshimiwa Mbunge Ligallama, ndugu yangu kule alizungumza kitu akasema hivi mwananchi unapomwambia unafanya upembuzi yakinifu *(visibility study)*, upembuzi wa kilimo mimi pia iliniingia na kwa uchungu ulionipa nikasema hili nitalizungumzia nikimwunga mkono Mheshimiwa Mbunge Ligallama. Nikija kwenye mkoa wa Kigoma wenye mabonde mengi yana mabonde mengi yana mabonde mengi sana nina bonde la Luiche Kigoma Mjini, Lugufu Kigoma Mjini nina mabonde zaidi ya matano, Kasulu lakini nina mabonde katika wilaya yangu ya Kibondo, haya ni mabonde kwa hakika kama yanaweza yakatumiwa vizuri kwa kusaidiwa na mkono wa Wizara hiyo basi ili neno la kusema kwamba tunatumia *visibility study,* kwa kweli halitakuwa sahihi kwa mabonde yale.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu haya ni mabonde ambayo tayari wananchi wanaishi kwa kilimo ambacho wanakijua kwa kupanda mazao ambayo wanayajua na hayo mazao yanastawi vizuri sana, leo nikisoma hotuba aliyoitoa Waziri nimeona kuna fedha kweli zimetengwa nashukuru sana fedha zimetengwa kwa ajili ya baadhi ya mabonde kuendeleza huu mradi wa kilimo cha umwagiliaji. Lakini nikiungana na Mbunge Ligallama, kule Mheshimiwa Mbunge mahali ambapo wananchi wanalima mpunga, wanalima kwa muda wa miaka mitano na kila anapolima anavuna magunia mengi sana hii *visibility study* ni ya nini si ya kumchelewesha mwananchi asilime, hizi fedha zinazotengwa kwenda kufanya upembuzi yakinifu mimi nilikuwa nashauri kwamba hizi fedha wapelekewe wananchi zisaidie hicho kilimo kiendelee sio upembuzi yakinifu tena Waziri Mkuu juzi alituambia kwamba sasa tunakwenda kwa mwendo wa ndege sasa tunapaa sasa tukianza kufanya hivyo hatutakwenda mwendo wa ndege tutakwenda mwendo wa kinyonga, hili napenda kulisema hivyo. Nilikuwa napenda kusema kweli Wizara ijipange vizuri itumie wataalamu ilionao waende yale mabonde ambayo hayahitaji utaalamu wa hali ya juu. Basi wananchi wapewe msaada wa nyezo za kutendea kazi, kazi ianze mara moja bila kutumia upembuzi yakinifu. Nakuja kwenye vyuo vya hawa *Extension Officer* hivi vyuo kusema kweli ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake, ameeleza kwamba kuna mpango wa kuajiri vijana waweze kwenda kufanya kazi ya ubwana shamba. Lakini mimi nilikuwa na oni lingine.

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wengi sana wana maliza darasa la 12 na wengine wanamaliza *form six,* hawa vijana hawana kazi wanazunguka wote wanakilimbilia kwenda kufanya kazi ya ualimu, lakini hawa vijana kama hili somo la kilimo lingeweza likapelekwa kwenye mashule na likafundishwa likaeleweka hawa vijana wangeweza kwenda kupelekwa kwenye hivyo vyuo na wakitoka hapo wakatoka na *certificate* na wengine *Diploma* wakaenda kufanya kazi huko vijijini na wananchi. Najua tatizo kubwa ni hao vijana au wahitimu kuogopa kwenda kufanya kazi vijijini, mimi nadhani suala sasa hilo liwe la msukumo, sawa na ambavyo Wizara ya elimu sasa itaanza kuwasukuma

wanaomaliza kozi ya ualimu kwenda kufundisha vijijini, kwa sababu kumekuwa na *trend* ya watu kuchagua waende mikoa ipi, lakini ukiangalia kwa kilimo ndio hivyo mabwana shamba hawapo, tangu zamani tumekuwa na mabwana shamba, mabwana shamba wanafanya kazi unakuta wanaishi sasa unamkuta mahali yuko Afisa Kilimo yuko makao Makuu ya Wilaya, ukimwuliza kitu kinacholimwa kijiji hajui kwa sababu yuko peke yake, kwa hiyo upungufu ni mkubwa sana, ninashukuru sana ninashukuru kwa sababu Wizara imeliona na kuhakikisha kwamba sasa itatoa ajira. Lakini inapotoa ajira isisahau sasa kwenda kusomesha watu wengine kwa ajili ya mpango wa mwaka mwingine wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tunacho kilimo ambacho pia kinaweza kikasaidia ama kinachangia kwa kiasi kikubwa kwa hawa wataalamu wetu wa kilimo kutofika na hii inaweza ikasababisha ama ikawa ndiyo chanzo cha kufanya hawa wataalamu wetu wakae maofisini tu washindwe kwenda. Ni hiki kilimo cha kuzagazaga, unakuta mtu ana kishamba cha nusu eka hapa nusu eka maili tano, hawezi akasaidiwa na wataalam hawa. Kwa hiyo, mimi nadhani huu mfumo wa kilimo cha viraka viraka, kama Wizara inaweza ikakisimamia na elimu ikatolewa kwa wananchi hawa wataalamu wetu ambao wataajiriwa na hawa tulionao nina hakika wateweza kusimamia suala la kilimo na wananchi wakaneemeka kutokana na kazi walizonazo.

Mheshimiwa Spika, lakini yote hayo yatafanikiwa endapo suala moja muhimu sana litatangulia. Mwaka jana tumepata matatizo ya njaa na ninajua kabisa Serikali imetumia pesa nyingi sana kutokana na kutafuta chakula cha kwenda kusaidia maeneo ambayo yalikumbwa na njaa. Yote hayo yalitokana na ukame na huu ukame umekuja baada ya kuchelewa kujua hali ya hewa ambayo ingeweza kusababisha wananchi waweze kulima mazao yanayoendana na kipindi ambacho hali ya hewa ingeweza kubashiri na kuona kwamba kwa kipindi labda cha miezi mitatu itakuwa kuna matatizo ya hali ya hewa kama hiyo. Wananchi wangeweza kujipanga wakalima yale mazao ambayo yanakwenda sambamba na hali ya hewa. Kwa hiyo, suala la kutabiri hali ya hewa kwa ajili ya kilimo, nadhani Wizara ingeweza kushirikiana na kitengo hicho ili kuweza kuelimisha wananchi na kuhamasisha ili waweze kulima mazao ambayo yanaendana na hali ya hewa ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na vituo vinaitwa *Research Centers.* Hivi vituo sasa hivi havipo na kama vipo haviwezeshwi. Nilikuwa najaribu kutafuta kwenye kitabu ambacho Mheshimiwa Waziri amesoma naona havipo na kama vipo mimi nadhani hizi *Centers* hazipewi pesa za kutosha na kama hazipewi pesa za kutosha zitafanya kazi namna gani? Naomba chonde chonde hizi *Centers* ziwe zinafanya kazi nzuri sana, zinatoa wataalam wazuri sana zipewe pesa za kuwawezesha kuendesha vyuo hivyo na kuweza kutoa utaalam unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu tunaita *chemicals* za asilia. Hizi *chemicals* za asilia hakuna elimu ambayo imetolewa kwa wananchi zikatumika. *Chemicals* za asilia kama vile majani ya mipapai, mwarubaini yakitengenezwa yakamwagiwa kwenye mimea yetu

wadudu wote wanakufa. Lakini naona havitajwa tunasahau tunakwenda kwenye madawa tu ya kigeni lakini hii miti tunayo sisi kwa nini tusishuhulikie kitu hiki na Wizara ikashughulikia mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo, tuna mbolea, kinyesi cha wanayama pamoja na mboji. Hivi ni vitu ambavyo kwa kweli ilitakiwa elimu itolewe kwa wananchi kuliko kungojea ruzuku ya mbolea anatayarisha shamba, analima, anapanda na wakati mwingine anavuna kabla mbolea haijafika. Kwa nini wananchi wasielimishwe wakatumia mbolea tulizonazo ambazo tunaweza kuzipata kwa wakati muafaka? Naomba kwa makusudi mazima elimu itolewe kwa wananchi ili tuweze kuanza kutumia mbolea hii kama nyongeza ya mbolea ambayo inatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipengele cha mbogamboga, matunda, maua kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi, hakijazungumziwa. Hiki ni kitu ambacho kinaingizia nchi fedha za nje na kuna Mikoa inalima sana vitu hivi. Kilimo hiki kisimamiwe ipasavyo ili Mikoa inayohusika kama vile Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Tanga, Iringa, Morogoro na Kigoma tunalima sana matunda tuweze kuhamasishwa na kulima kilimo cha namna hii ambacho kwa kweli wananchi wanakilima kutokana na jitihada zao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusema kweli wananchi wetu wanajitahidi kulima kwa mikono lakini kama wangekuwa wamepata msaada wa kukopeshwa matrekta wangeweza kulima sana. Kwa makusudi mazima nadhani Wizara hii inayohusika ingeweka mashindano kwa Mikoa inayofanya vizuri katika kuhamasisha ili Mkoa unaofanya vizuri basi Wizara inatoa zawadi.

Nadhani hii ni njia mojawapo ingeweza kuhamasisha kilimo kama tunavyofanya kwenye elimu. Hapa Bungeni tunawapokea wanafunzi wanaofanya vizuri nadhani hata kilimo nao wangestahili kuja hapa sio wanafunzi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la zana za kilimo kusema kweli ni kilio kikubwa sana kwa wananchi lakini mwananchi akishalima pia anategemea atoe mazao yake kule alikolima ayafikishe kwenye soko. Soko liko wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna wananchi wengi hasa kwa Mkoa wa Kigoma wenye neema....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita msemaji anayefuatia, napenda kuwafahamisha kwamba nimemtafutia kiti sehemu nyingine Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Alikuwa na sababu maalum na ningeomba asimame ili wajue sasa yuko wapi. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Alisimama)*

**SPIKA:** Basi wale wanaomtafuta pale ndipo atakapokuwa akikaa sasa. Tunaendelea.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN ATHUMANI NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa ambayo kwa kweli kama tutaitekeleza kama alivyoeleza hapa, naamini Taifa letu litaweza kujikwamua kwa kiasi kikubwa na kukifanya kilimo chetu kiwe ni cha tija.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na maeneo machache ambayo kwa ujumla nitayazungumzia kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini hasa lililonifanya nisimame ni kuhusiana na mambo ambayo sikuyaona kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilieleza kwamba kama Mheshimiwa Waziri angetembelea Jimbo la Mlalo, wananchi wa Mlalo wangemwambia kitu gani? Nikaeleza kulikuwa na masuala ya umwagiliaji na kadhalika na kadhalika. Kwa bahati mbaya hayo sikuyaona yanavyo-*apply* kwa Jimbo la Mlalo na Wilaya ya Lushoto kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwa ujumla katika hotuba yote hii kuna mambo mazuri tu jinsi gani ya kuboresha kilimo chetu lakini watu wa Wilaya ya Lushoto hasa tukizingatia mazingira yao ni tofauti kabisa na maeneo mengine ya Tanzania ukiacha sehemu ndogo tu ya Tarafa ya Umba wao wanatakiwa wafanye nini?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ni Wilaya ya zamani, mazingira yake ni ya milima, ina hali ya hewa nzuri sana naamini kila mtu anajua kwamba katika Tanzania na katika Afrika Mashariki ukitaka kupata matunda bora nenda Lushoto. Ukitaka kupata mboga nzuri nenda Lushoto. Sasa huo ndio utajiri wetu kule pamoja na kwamba tunalima chai na kahawa lakini tunalima mboga, matunda, huyu mwananchi anasaidiwa vipi, hilo sikuliona. Nimeona mipango inazungumzwa juu ya kusindika na kadhalika lakini sisi tayari tuna matunda kule. Kinachojitokeza hivi sasa ni kwamba uzalishaji wetu na ubora wa mazao yetu unazidi kushuka kwa sababu *inputs* za kitaalam hakuna. Mwananchi yule mkulima ameachwa kila mtu na lake. Nadhani ni vizuri Wizara ikaliangalia suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Lushoto ina jumla ya hekta zinazolimika 192,000 ukiondoa hekta 30 ambazo ziko kanda ya tambarare tunabaki na hekta 162,000 kule juu milimani. Humo ndio wananchi wale ambao ni zaidi ya nusu milioni wa Wilaya

ile wanamopatia maisha yao na maendeleo yao. Hawa nao wanahitaji kuangaliwa. Wanahitajika kuangaliwa vipi?

Mheshimiwa Spika, wakati natoa mchango wangu uliopita nilisema watu wa Lushoto ni wachapa kazi, wanachohitaji ni msaada wa kitalaam. Watu wa Lushoto wamekaa katika milima ile kwa miaka na miaka, ardhi ile imeanza kuchoka. Wenzetu katika maeneo mengine wanazungumzia matrekta, kule juu milimani huwezi kupeleka matrekta. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hatuhitaji matrekta labda tubadilishe mfumo wetu, tunaweza kuhitaji hizi trekta ndogo ndogo. Lakini hata hivyo itabidi tuchukue hatua za kutengeneza *terraces.* Naiomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ijielekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina maeneo ya kilimo, lazima twende sasa hatua moja mbele ya kuwasaidia wananchi wetu jinsi gani ya kutengeneza *terraces*. Wenzetu katika nchi za Asia, China, Japan, Vietnam wana milima kama sisi lakini ni watalaam wakuu wa kilimo cha milimani kwa sababu ya *terraces* na sisi tungependa utaalam huo uletwe huku kwetu ili wananchi wale waweze kujiletea maendeleo yao. *(Makofi)*

Naamini huo utaalam ukipatikana watu wa Lushoto na hasa Jimbo la Mlalo hawatataka mtu wa kuja kuwachimbia *terraces* hizo kwa sababu wao wenyewe wameanza pamoja na kwamba ni kwa kusuasua lakini wanahitaji msaada wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, niliutaja mradi wa umwagiliaji kule Kitivo. Mradi ule ulipobuniwa iliitwa *Kitivo Irrigation Project*. Ulikuwa ni mradi mkubwa tu nadhani ulianzishwa katika miaka ya 1980. Mradi ule nilikuwa naangalia katika *National Irrigation Master Plan* kitabu kilichotolewa na Wizara ya Kilimo, mwaka 2002, umerekodiwa hapa lakini *comment* yao ni nini katika kuutaja? Wanasema kwamba mradi huu uliharibiwa na mafuriko ya mwaka 1993 na yale ya 1996 halafu wakaweka kijisehemu unahitaji matengenezo. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba hakuna matengezo kutoka wakati huo. Mradi huo umeachwa kana kwamba hauna mwenyewe. Pamoja na kwamba *UNSDF* walipokuwa wameuanzisha na baadaye *World Bank* walitoa vifaa vingi sana lakini vifaa vile taratibu vimeondolewa pale. Wananchi wameachwa pale bila msaada wowote na uzalishaji pale umeshuka. Zipo hekta 600 nzuri tu na eneo lile ndio tegemeo la chakula cha watu wa Jimbo la Mlalo. Kule juu tunalima mboga, matunda na kadhalika. Lakini kwa upande wa mazao ya chakula tunategemea pale kwenye mradi. Mradi ule sikuuona unatajwa mahali popote. Nimeangalia majedwali yote katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kutoka 1-12 nasikia tu *scheme* hii, *scheme* lakini *Kitivo Irrigation Scheme* haipo, kulikoni? Ni nini hatma ya mradi huu? Kwa sababu na sisi ni sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nadhani mradi ule umekufa kutokana na utaratibu tuliokuwa tumejiwekea huu wa kanda ambao Waheshimiwa Wabunge wameuzungumzia juu ya Mikoa kuwekwa chini ya kanda nyingine. Ninazo taarifa kwamba vifaa vyote vile vlivyokuwepo pale taratibu vimeondolewa vikapelekwa makao makuu ya Kanda. Hivi sasa kumebakia vitrekta vinne ambavyo vyote ni vibovu. Miundombinu ya bwawa lile baada ya kubomoka Wilaya imeomba itengewe Sh.229mil ambazo hazikuonekana.

Nilijaribu ku-*check* nikaambiwa ati maombi yale yamepelekwa TAMISEMI. Ndio maana nasema huu utaratibu wa kanda hautufai kwa sababu kanda katika kusimamia unakuta wananufaisha upande mmoja, upande mwingine unaachwa. Afadhali kila Mkoa uwe na ofisi zake za umwagiliaji ili tuweze kukamatana vizuri.

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo la *Kitivo Irrigation Scheme* limeeleweka na nategemea Mheshimiwa Waziri atatupa maelezo ili watu wa Mlalo wajue mradi wao ule hatima yake ni nini. Mara nyingi kunatolewa *conflicting report*. Wataalam wamekaa mbali huko wanasema unajua wananchi wa pale hawashiriki. Sio kweli! Tuwaangalie wataalam hawa watatufikisha mahali pabaya. Kwa sababu taarifa wanazozitoa kwenye vitabu, wanatoa *reasons* na *excuses* nyingi kweli kweli lakini wanasahau kwamba sisi wanasiasa, wananchi ndio wanaotuuliza maswali. Nitaomba Wizara itueleze hatma ya mradi huu ni vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye lingine ambalo nataka kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nalo ni akiba ya Taifa ya chakula. Mwaka jana nilisema kwamba chakula ni sehemu ya usalama wa Taifa. Nchi haiwezi ikawa inaishi kwa kutegemea kwamba tukipata matatizo basi tutakwenda kutafuta chakula mahali pengine, tutakwenda kuhemea kama tulivyofanya. Leo hii tunaambiwa *SGR* ina akiba ya tani 128,000. Huu ni utani. Hitaji la nchi ni tani karibu 10mil kwa mwaka huu. Tani 100,000 zinatosha Watanzania kwa muda gani? Hivi hatutaki kujifunza kutoka kwa nchi nyingine?

Hao Mataifa mengine hawapati ukame? Inakuwaje Mataifa mengine ukiacha haya ya kwetu ya kinyongenyonge, ya Kiafrika yanapata ukame lakini hawapigi kelele ya chakula? Ni kwa sababu wana *strategic reserve* na wenzetu wanapozungumzia *strategic reserve* wanazungumzia miaka mitatu, minne na wengine mpaka miaka kumi. Hizi tani 100,000 zinatusaidia kwa kiwango gani? Ni lazima sasa tuangalie usalama wetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia hapa mwaka jana zilinunuliwa tani 92,000 za mahindi zenye thamani ya Sh.18bil hapo hapo tukaenda kununua tani 30,000 kwa sababu ya shida yetu tukatumia Sh.10bil. Hizi tulizonunua kutoka kwa wananchi tani 92,000 tulinunua kwa Sh.18bil tu hizi tulizokwenda kununua 30,000 tumetumia Sh.10bil maana yake ni nini? Si ingekuwa bora sisi tuwe tunanunua chakula hiki cha wananchi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vema sasa hivi wataalam na Wizara itujie na *project*. Ni kweli sasa hivi tunahimiza Watanzania kila kaya iwe na chakula cha akiba lakini kila Halmashauri iwe na chakula cha akiba kwa ajili ya watu wake halafu *SGR* ijikite huko kwenye Mkoa na Taifa. Nadhani kwa kuanzia hebu tujielekeze kuwa na tani 1,000,000 *as a starting point.* Haiwezekani kila dakika tukiwa na njaa tunakimbilia kwa watu wengine wakati wageni wakija hapa wanatucheka jinsi gani Watanzania sisi tulivyo wazembe katika kuangalia uhai wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala la lumbesa. Tunataka kuboresha hali za maisha ya Watanzania lakini kama kuna kitu kinawaongezea Watanzania umaskini hasa wale wakulima ni hili suala la lumbesa. Tumeweza

kupambana na majambazi, *RVF,* hebu Serikali ijikite katika kupambana na hawa wanaonunua mazao kwa wakulima kwa lumbesa. Kipimo cha kisheria kinachoruhusiwa ni kilo. Iweje leo tunashindwa kuwadhibiti watu ambao wanawaibia, wanawadhulumu wakulima chini ya neno la utandawazi? Naomba Serikali isilikubali jambo hili na Bunge lako Tukufu tukatae mkulima kuendelea kudhulumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula..

Mheshimiwa Spika, mimi nitakuwa na maeneo kama mawili tu au matatu ambayo nataka nichangie katika hoja hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nianzie na hoja ya kilimo cha umwagiliaji. Ninavyofahamu na kwa kadri Taifa linavyofahamu Rukwa ni miongoni mwa ile Mikoa minne inayozalisha chakula nchini. Mkoa wa Rukwa pia unayo mabonde kama yalivyo mabonde katika sehemu nyingine katika nchi hii. Lakini nilipokuwa naipitia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na hasa nikajikita katika majedwali yaliyoko huku mwisho. Nimeyarudia na kuyarudia sikuona hata Wilaya moja katika Mkoa wa Rukwa ambayo itapata skimu za umwagiliaji. Jambo hili linanifadhaisha na linawafadhaisha pia wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wao. Kwa sababu na wao wanatarajia waboreshe hali zao za maisha kwa kuongeza uzalishaji wa mazao kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nimeona katika kiambatanisho namba saba, skimu ya Uruira, hii inanitia hofu. Sijui ni skimu ambayo naifahamu mimi iliyopo katika Wilaya ya Mpanda au kweli ni skimu ambayo iko katika Wilaya ya Mbarali? Naomba Waziri anieleze hilo kama skimu hii ya Uruira inayokusudiwa ni ile ya Uruira ya Mpanda au ni Uruira hiyo ya Mbarali? Kama hivyo ndivyo itakuwa ni skimu moja ambayo tutakuwa tumepata miongoni mwa skimu kubwa tatu au nne ambazo tayari wananchi wenyewe walikuwa wameshaziibua katika mpango huu wa maendeleo ya kilimo katika Wilaya ya Mpanda. Kuna skimu ya Kakase, skimu la bonde la Karema, skimu la bonde la Mpimbwe, haya yote sijayaona humu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali pamoja na kwamba tunazalisha chakula cha kutosha katika Mkoa wa Rukwa kwa sababu tunamshukuru Mungu tunaendelea kupata mvua nzuri lakini bado wananchi wetu tunataka wabadilishe hali zao za maisha na kuongeza mazao ya kilimo katika miradi ya umwagiliaji. Napenda nipate maelezo kwa nini na ni vigezo vipi ambavyo vimetumika mpaka Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wake haumo kabisa katika mpango huu wa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda sasa nizungumzia suala ambalo limenifanya nisimame nalo ni zao la tumbaku. Hili ndilo zao pekee la biashara katika

Wilaya yangu ya Mpanda na matarajio ya Wizara ni kwamba lazima zao hili liongezeke kufikia tani 80,000 lakini zao la tumbaku lina matatizo mengi. Uzalishaji wa zao la tumbaku sasa hivi katika nchi yetu kwa sababu ya kutokupewa msukumo na msisitizo unaostahili bado haujaweza kubadilisha hali ya maisha ya wakulima wa tumbaku ambao wamekuwa wakilima tumbaku katika Wilaya ya Mpanda kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

Mheshimiwa Spika, Zimbabwe wanazalisha kati ya kilo 800-1300 kwa eka lakini wakulima wa Mpanda wanazalisha kati ya kilo 350-500. Uzalishaji huu duni umechangiwa na vitu vingi sana ukiwemo ukosefu wa Maafisa Ugani. Kwa mara ya mwisho nilipokuwa najaribu kufuatilia suala hili la zao la tumbaku nilikuta Afisa Ugani mmoja anahadumia kaya kati ya 1200-1800. Kwa hiyo, wakulima hawapati huduma inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi wakulima wetu wanachelewa kupata pembejeo katika muda muafaka. Msimu uliopita kwa mfano mbolea zilichelewa kufika. Lakini pia wakulima hawa wa tumbaku ni wakulima wa mikataba wana mikataba na makampuni ya tumbaku ambao ndio wanunuzi wa tumbaku inayozalishwa na wakulima wadogo wadogo.

Lakini makampuni haya hayana mikataba na mkulima mmoja mmoja yana mikataba na vyama vya msingi vya ushirika wa wakulima. Makampuni yameshindwa kuwafikishia wakulima pembejeo katika muda muafaka. Wakulima wamelima lakini mbolea imechelewa kufika, nguvu ya mkulima imepotea bure.

Wamepata pembejeo pungufu na pengine pembejeo imekuja kuwekwa katika kipindi cha mvua, *production* yake ikawa ndogo. Lakini kimsingi tayari nguvu ya mkulima huyu imeshatumika lakini hakuna mtu anayemwangalia, hasara anayopata mkulima huyu hakuna mtu anayemfidia pamoja na kwamba ni uzembe wa makampuni hayakufikisha mbolea katika muda unaotakiwa katika vijiji vyetu vya wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kisingizio wanachotoa hayo makampuni ni kwamba mvua zilikuwa nyingi, barabara zilikuwa hazipitiki, gari moshi haliendi ndio maana mbolea imechelewa kufika kwa wakulima. Lakini makampuni haya sio kwamba yanaanza kazi kwa msimu huu wa kwanza, yanafahamu ni kipindi gani tunapata mvua nyingi na barabara hazipitiki katika maeneo yetu lakini mpaka sasa wanashindwa kufikisha mbolea katika makao makuu ya Wilaya kwa muda unaotakiwa. Serikali inatizama tu haya makampuni wakati makampuni yanaendelea kuwakandamiza wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi ni bei. Napenda pia nipate kauli ya Serikali, fedha halali ya nchi hii ni fedha ya Kimarekani au ni shilingi ya Kitanzania? Kwa sababu soko la msimu huu wa tumbaku, tumbaku imenunuliwa kwa dola wakulima wetu wanalipwa kwa sarafu ya Kitanzania. Shilingi yetu ambayo inabadilikabadilika kama kinyonga, mkulima anayeuza leo kwa daraja fulani na mkulima atakayeuza siku ya pili

kwa daraja hilo hilo wanaweza wakajikuta wamepata malipo tofauti kwa sababu ya fedha yetu kutokuwa makini. Napenda nipate ufafanuzi wa Serikali kwamba kwa nini wamefikia mahali pa kukubaliana kwamba sasa tumbaku inunuliwe kwa dola badala ya shilingi ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, lingine mkulima huyu wa tumbaku bado hajanufaika na ruzuku inayotolewa na Serikali katika mbolea. Napenda kuipongeza Serikali katika kuwafikiria wakulima na kutoa ruzuku katika pembejeo na hasa wakulima wa tumbaku wakiwa miongoni mwao ambapo pia wanastahili kama wakulima wengine kupata hiyo mbolea ya ruzuku. Matokeo yake mkulima huyu kwa msimu uliopita amenunua mbolea ya tumbaku ghali zaidi kuliko msimu wa nyuma pamoja na kwamba mbolea inatolewa ruzuku, tatizo liko wapi? Au tunawadanganya wakulima kwamba ipo mbolea ya ruzuku wakati wanapokwenda kununua mbolea wanakuta ni ghali zaidi kuliko ilivyokuwa msimu uliopita? Makampuni haya ambayo ndio yamepewa uwakala wa kusambaza mbolea kwa wakulima ni tatizo, ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamejijengea utaratibu wa kupata faida kubwa kwa kuwatumia wakulima wa nchi hii, ni vema sasa serikali ikaangalia ni namna gani tutamsaidia mkulima huyu wa tumbaku ili anufaike na ruzuku inayotolewa na serikali katika pembejeo.

Mheshimiwa Spika, ukimtazama mkulima wa tumbaku mimi nadhani ataendelea palepale kama Serikali haitaweza kumsaidia kwa kuongeza Maafisa Ugani, kupata mbolea na madawa katika muda unaotakiwa lakini pia kumsaidia kuweza kuongeza uzalishaji wa tumbaku katika kila ekari.

Nilikuwa namtazama mkulima ambaye wao katika kijiji hicho walikuwa wanasema katika Chama changu cha Msingi cha Mpanda Kati, mkulima wa mfano alipata shilingi milioni 1,200,000/= kwa ekari moja ya tumbaku. Lakini nilipokaa naye na kuzungumza akaniambia kwamba yeye gharama zake zote ameziorodhesha zikafikia shilingi 5,035,000/= hivi. Nguvu kazi waliyotumia ni familia yake na mkewe na kijana wake yaani watu watu, gharama waliyotumia 5,035,000/= wakaja wakapata shilingi 1,200,000/= kazi ya mwaka mzima. Lakini ukija kutazama faida pale ni shilingi 7,000,000/=, ukiigawanya kwa mwezi ni mshahara wa shilingi 60,000/=. Lakini shilingi 7,000,000/= hii wanagawana watu watatu ambao walikuwa wanafanya kazi, yaani mume, mke na mtoto. Mtanzania na mkulima huyu wa tumbaku hatuwezi kumtoa katika umaskini, atabakia kuwa mfanyakazi wa makampuni ya tumbaku, ni lazima bei ya tumbaku iongezwe.

Nisimalizie muda wangu wote katika tumbaku pamoja na kwamba nilikuwa na mengi kuhusu suala la tumbaku inanikera sana lakini pia naomba Wizara itusaidie kuangalia ni namna gani tunaweza kuongeza uzalishaji wa kahawa kule Mwese. Mwese ni eneo zuri na kahawa inastawi lakini ni ghali sana kuwafikia wakulima kule na hakuna mkakati wowote wa makusudi wa kuweza kupanua mashamba ya Kahawa kule Mwesi.

Pia suala la pamba niliwahi kuongea na Mheshimiwa Waziri, napenda nipate maelezo kwamba wamefikia wapi na inaweza ikaanzishwa tena Mpanda au bado lile tishio la kufungwa kwa wakulima wa zao la pamba Mpanda mpaka sasa bado hali haijaboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Amour Arfi, baada ya Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka ambaye ndiye atakayefuata wajiandae Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe. Kwa hiyo, sasa Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, karibu!

**MHE. DR. OMARI MZERU NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara ya Kilimo ambayo ni Wizara muhimu sana sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Morogoro Mjini wakiwa pamoja na wanafunzi ambao leo hii wamejitokeza katika Bunge hili tukufu, nawashukuru sana. Lakini pia nawaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha, lakini nitajitahidi kuwatumikia kwa uwezo wangu wote na naomba Mwenyezi Mungu anisaidie. Pia naomba wasiwe na wasiwasi Mbunge wamempata na Mbunge ndiye mimi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nitoe rambirambi zangu kwa ndugu wa Marehemu kwa kifo cha aliyekuwa Mpendwa wetu, mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa. Pia na zile ajali mbaya zilizotokea muda mfupi huu katika nchi yetu hasa ile ajali ya Singida ambayo ilipoteza watu wengi lakini miongoni mwao walipotea vijana wawili ambao walikuwa ni wapiga kura wangu kwenye Manispaa ya Morogoro ambao ni vijana wa Bwana mdogo aitwaye Boniface Njohole. Mungu azilaze Mahali Pema Roho za Wapendwa wetu, Amin!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda sana nimpongeze Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake, ni hotuba ambayo inaleta matumaini sana kwa Watanzania. Napenda nitoe pongezi hizi pamoja na Naibu Mawaziri wake pamoja na Watendaji wao kwa umahiri wao na kwa jinsi ninavyofahamu ufuatiliaji wao wa mambo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimpongeze na kumshukuru sana kwa namna ya pekee, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mpendwa wetu, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuamua kwa makusudi kuuteua mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula la Taifa. Kwa kweli sisi wananchi wa Manispaa ya Morogoro tumeupokea mpango huu kwa mikono miwili kwa sababu ingawaje mashamba haya ambayo mradi huu utafanyika yapo katika Wilaya nyingine kama Wilaya ya Ulanga, Kilombero, Kilosa, Morogoro Vijijini na Mvomero, lakini tunaamini kwamba mazao yatakayopatikana hapa kwa vyovyote yataletwa sokoni na soko lipo Morogoro Mjini na sisi wananchi chakula

kinapokuwa kingi maana yake tunapata kwa bei nafuu, siyo watu wa Morogoro tu lakini kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kuuteua Mkoa wa Morogoro siyo kwamba ameupendelea, Mkoa wa Morogoro una sifa ambazo Mkoa mwingine hauna na ninaomba nitoe baadhi ya sifa hizo za Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro una rutuba ya kutosha ambayo haihitaji mbolea, una rutuba ya asili. Pili, Mkoa wa Morogoro una ardhi ya kutosha kabisa na mabonde mazuri sana ya kuzalisha chakula. Mkoa wa Morogoro una mvua ya kutosha ya wastani kwa mwaka mzima. Lakini mkoa wa Morogoro pia una mito 148 mikubwa ambayo haikauki kwa mwaka mzima hata wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro ni njia panda inayounganisha karibu robo tatu ya Mikoa ya Tanzania, maana yake ni rahisi kufikika. Lakini pia mkoa wa Morogoro uko karibu na Bandari Kuu ya Dar es Salaam kwa ajili ya kusafirisha mazao nchi za nje na uko karibu na uwanja mkuu wa ndege ambao ni rahisi kusafirisha mazao nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Mkoa wa Morogoro unavyo vyuo vitatu vya kilimo ukiongozwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ambacho kinatoa Maafisa Ugani wengi, mabingwa, Madaktari pamoja na Maprofesa. Sasa Mungu akupe nini! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi napata wasiwasi kidogo tu katika hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyouzungumzia mradi huu mkubwa wa Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula la Taifa kwa sababu ameuzungumzia kwa ufupi sana.

Katika kitabu chake Ukurasa wa 54 ametumia takriban mistari 13 tu, hii inanipa wasiwasi kwa sababu hakutuelezea programu nzima inakuwaje jinsi ya kuutekeleza mradi huu. Kwa mfano, vitendea kazi kwa maana ya matrekta, mashine za umwagiliaji, pembejeo kwa maana ya mbolea, madawa, wataalamu itakuwaje? Lakini pia jinsi ya utekelezaji wa kuimarisha barabara zinazotoka barabara kuu kuingia Wilayani ambako hayo mashamba ndipo yalipo. Kwa hiyo, huo ndiyo wasiwasi wangu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine linalonipa wasiwasi ni kwamba huko nyuma katika Mkoa wa Morogoro kulikuwa na miradi mingi ambayo tayari ilikwishabuniwa kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa chakula. Moja kati ya miradi hiyo ulikuwa ukiitwa Mpango wa Reli ya Uhuru ulioanzishwa enzi ya Dr. Chrisant Mzindakaya akiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Kwa kweli Dr. Chrisant Mzindakaya ni mtu ambaye watu wa Morogoro hawatamsahau kwa kipindi chake kwa sababu alisimamia sana kilimo na enzi yake tulikuwa tunapata mazao mengi na kwa bei nafuu katika soko kwa sababu kila mtu alikuwa anayo mazao. Alianzia mpango ulioitwa Mpango wa Nguvu Kazi, hivyo kila mtumishi wa Serikali ilikuwa lazima awe na

shamba lisilopungua ekari moja la chakula. Kwa hiyo, watu wote walikuwa na chakula katika Mkoa wa Morogoro. Tunamheshimu huyu Mzee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema haya maana yangu ni kwamba namwomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Wizara yake wajaribu kuuangalia mpango huu kwa jicho la karibu sana ili mpango huu uweze kufanikiwa. Mimi binafsi jinsi ninavyomfahamu mzee wangu Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ni mtu makini sana na mahiri sana hasa mwaka jana tulivyomwona jinsi alivyokuwa anasimamia Wizara ya Maji, kwa kweli nampongeza sana. Lakini pia amepata vijana wake wachapakazi wazuri, kama ni timu yeye ni Beki lakini yuko Dr. David Mathayo David *midfield* na Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza anamalizia kufunga magoli. Mimi nafikiri kutakuwa hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, bado mimi binafsi nakumbuka jinsi Mheshimiwa Waziri alivyolishughulikia suala la ununuzi wa mahindi kituo cha Morogoro mwaka jana kwa ajili ya kuhifadhi kwenye ghala la Taifa akisaidiana na Naibu Waziri , Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza. Nafikiri wakulima wangu pamoja na wafanyabiashara wadogo wadogo wa mahindi bado wanamkumbuka jinsi alivyosaidia kwa sababu ulifikia wakati walinunua mahindi pesa zikaisha na mahindi yalikuwa bado mengi sana. Mimi nikaenda kumwona na alifuatilia jambo hili kwa karibu sana na mpaka mahindi yote yakanunuliwa pamoja na nafaka nyingine ambazo zilikuwa zinanunuliwa Morogoro Mjini. Kwa hilo tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado naamini uongozi wa Mkoa wa Morogoro ukiongozwa na Jemedari Mkuu, Meja Jenerali Said Said Kalembo akisaidiana na Wakuu wa Wilaya wake ambao ni watu makini sana na wachapa kazi wazuri, naamini kwamba mradi huu kama watashirikiana kwa karibu kati ya Wizara ya Chakula, Kilimo na Ushirika na Uongozi wa Mkoa wa Morogoro basi nafikiri mpango huu utafanikiwa. Lakini kikubwa mno ni kwamba tuwatumie hawa wataalamu wetu niliowataja kutoka vyuo vyetu vitatu hasa Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuzungumza maneno mengi katika suala hili kwa sababu kwanza sina haja ya kupinga hasa kwa kuwa hotuba hii imezungumza vizuri, isipokuwa natoa angalizo dogo tu. Ni kwamba hili suala la upembuzi yakinifu *(feasibility Study)* lisije likachelewesha mradi wetu, kwa sababu gani? Kwa sababu nchi hii karibu kila sehemu inafahamika kwamba ni mazao gani yanafaa kulimwa na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amempatia *CD* karibu kila Mbunge katika Bunge hili jana, kwa maana ya kuonyesha kwamba mazao gani yanafaa wapi katika Wilaya mbalimbali.

Sasa sidhani kama *feasibility study* gani tena ingetaka ifanywe kuhusu suala hili labda kama ni kuangalia magonjwa na madawa ambayo yatafaa katika mazao hayo yatakayolimwa . Kwa kufanya hivyo maana yake mradi unaweza kuanza. Lakini *feasibility study* ya kuangalia magonjwa gani yatakayoathiri mazao hayo na madawa gani yatakayofaa kwenye mazao hayo yatakwenda sambamba pamoja na mradi utakaoanza. Kwa sababu tumekwishaona katika nchi hii haya masuala ya *feasibility*

*study* au upembuzi yakinifu unafanyika na unachukua miaka mingi mradi haufanyiki, wananchi wanasubiri kwa nguvu zao zote lakini hakuna kitu kinachofanyika. Kwa hiyo, naomba nitoe angalizo kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwamba isije ikawaharibia uwezo wao wa kufanya kazi kwa kutegemea wataalamu hawa ambao kwa kawaida utakuta mara leo wamesema hili na kesho hili, kwamba bado wanafanya uchunguzi na kadhalika. Naomba mradi uanze mara moja kwa sababu mradi huu ni ukombozi kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo kuwa Mkoa wa Morogoro una uwezo mkubwa sana, tukilima tutapata chakula cha kutosha, si kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro tu lakini kwa Tanzania nzima na pia kupata chakula cha ziada kwa ajili ya kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyotamka kuwa sikuwa na chochote cha kupinga hotuba hii, isipokuwa nataka kuiunga mkono pia kutoa angalizo na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na timu yake yote na Wizara ya Kilimo kwa jumla. Nawatakia heri waweze kufanikisha mradi huu kwa sababu hiki kitakuwa ni kipimo chao kikubwa sana, na kwa sababu Mheshimiwa Rais, ameuteua Mkoa wa Morogoro kwa kuwa anaufahamu sifa zilizoko katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Rais alipotaja mradi huu ufanyike Morogoro mimi binafsi nilifarijika sana kwa sababu mwaka jana katika Bunge lako hili Tukufu wakati nikichangia Wizara hii ya Kilimo wakati wa bajeti kama hii, nilitoa ushauri kwa aliyekuwa Waziri wa Kilimo wakati ule kwamba mkitaka kuzalisha mazao ya kilimo, Mkoa unaofaa kuzalisha ni Mkoa wa Morogoro, hivyo, Rais alipotangaza hivi nilijua kwamba inawezekana alinisikia kilio changu na akaniunga mkono na aliona kuna ukweli. Kwa hiyo, naomba mradi huu utekelezwe kikamilifu kwani mradi wa ukombozi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena niwashukuru wananchi wangu wa Mkoa wa Morogoro na naahidi kwamba nitawawakilisha kwa nguvu zangu zote na ninaomba Mwenyezi Mungu anisadie.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, bila kupoteza wakati naiunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka. Hebu niwataje wanne wanafuatia kwa mpangilio huu. Baada ya Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng’ong’o ambaye ndiye anafuatia, nitamwita na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe ambaye naye atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda na wa nne atakuwa ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto.

Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng’ong’o, Karibu!

**MHE. LEDIANA MAFURU MNG’ONG’O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba nami niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa pole kwa msiba mkubwa uliotupata, natoa pole kwa familia, ndugu na marafiki wa Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa. Pia natoa pole kwa wale wote waliofariki katika ajali mbalimbali na pia kwa familia za Wabunge wastaafu, Mheshimiwa Chubi na Mheshimiwa Stephen Kazi waliofarikia hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nami nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa kuandaa hotuba hii kwa makini na kwa umahiri wa hali ya juu. Nawashukuru sana. Nawapongeza pia watendaji wote, Maafisa Ugani wa Wizara hii wanaofanya kazi vijijini kwa kutumia nyenzo duni lakini wameendelea kutoa ushauri unaostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kwanza niipongeze Wizara kwa mpango mzuri waliouandaa hasa wa kuongeza wataalamu wa ugani. Tunaelewa kwamba kumekuwa na malalamiko makubwa kuhusu upungufu wa wataalamu wa kilimo huko vijijini. Lakini hotuba hii imekuja na mpango kabambe kabisa wa kuongeza wataalamu wa ugani na ifikapo 2011 iwe kila kijiji kiwe na mtaalamu wa kilimo. Hii ni hatua kubwa sana ya mabadiliko ya kilimo hapa nchini, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne. Lakini ningependa kutoa angalizo kwamba mageuzi haya yaendane na nyenzo mbalimbali kwa watalaamu hawa ikiwa ni pamoja na nyumba ili watakapokuwa huko vijijini basi kuwe na matayarisho mazuri yaliyofanyika ili waweze kuwa na nyumba na nyenzo za usafiri na ofisi za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la pembejeo. Naipongeza Wizara kwa kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo zitapatikana kila kijiji na Mheshimiwa Waziri ametumia neno kwamba zitapatikana kama soda ya *Coca Cola* inavyopatikana kijijini. Hii ni hatua kubwa sana na itahakikisha kwamba kunakuwa na ongezeko kubwa la mazao ya chakula na biashara huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni upatikanaji wa pembejeo hizi, hata kama zitakuwa vijijini sina uhakika kama utakuwepo utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kuzinunua. Kwa hiyo, napenda kushauri kwamba vituo au ushirika yaani *SACCOS* za vijiji au Kata zitumike kuhakikisha kwamba pembejeo hizi zinamfikia kila mwananchi na pia vikundi vya vijana pamoja na vikundi vya wanawake viweze kushirikishwa kikamilifu katika upatikanaji wa pembejeo.

Mazao yataongezeka, lakini hofu yangu ni soko hasa katika mazao ya chakula na hasa kwenye Mikoa kama Mkoa wa Iringa ambao tunategemea zao la mahindi kama la biashara lakini pia kama zao la chakula. Jana wenzangu walizungumzia kuhusu kuwa na bodi kwamba kuna mazao yale makubwa hapa nchini wana bodi kama Bodi ya Korosho, Tumbaku, Chai na hata Kahawa. Hivi kwa nini hatuanzishi bodi ya kusimamia mazao kama Mahindi na mazao mengine ya chakula ili kuhakikisha kwamba bei ya mkulima inalindwa?

Kwa mfano, Mkoa wa Iringa ulizalisha mahindi kwa wingi na mpaka sasa hivi kuna mahindi ya mwaka jana hawajauza, na mwaka huu wanakaribia kuvuna, kwa hiyo, matokeo yake yale mahindi wanayauza kwa bei ya hasara. Sasa mimi napenda kutoa ushauri kwamba Serikali iangalie kuwepo na Bodi itakayoangalia mazao ya chakula, tukiangalia kilimo na mazao mengine yale ya asili kama mihogo na viazi lakini viwe kwenye Bodi moja ili viweze kuangaliwa vizuri na kupangiwa bei. Sijawahi kuona kwamba tunazungumzia mazao ya biashara. Tunazungumzia habari ya bei lakini bei ya mahindi haizungumziwi, wakulima mpaka leo bado wanauza bei ya chini ambayo hailingani na gharama wanazotumia katika uzalishaji.

Kama kweli tunataka kuhakikisha kwamba kuna mageuzi ya kilimo ni lazima tuhakikishe kwamba mazao au bei ya mazao ya wakulima inalindwa na Serikali inasimamia vizuri zaidi. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba ile Mikoa minne inayotambulika katika uzalishaji wa mazao ya chakula hasa mahindi, tuhakikishe kwamba tunawalinda hawa watu la sivyo tutakuwa na pembejeo lakini hasara itatokea na wananchi watakata tamaa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika upatikanaji wa pembejeo ni kwamba labda tuanze kufikiria upangaji wa ardhi vijijini. Toka nianze kuangalia kilimo vijiji vingi kilimo chao ni kilekile, yaani shamba ni lilelile hakuna hata kulipumzisha. Mwaka huo huo mkulima anatumia pembejeo hizo hizo, kipande cha shamba ni kilekile! Sasa kama tunataka mageuzi ya kilimo ni lazima tuanze kuwafundisha wakulima kuyapumzisha mashamba, kwa maana hiyo ni kwamba mashamba ya kijiji yapimwe vizuri na yawepo maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo ili tuweze kupata mazao zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Vyuo vya Kilimo. Napenda niipongeze Wizara kwa kuangalia suala hili kwamba litaongeza wataalamu wa kilimo wakiwemo wataalamu wa ugani wataokwenda kuchukua mafunzo lakini pia na waalimu watakaofundisha vyuo hivi na kwamba kutakuwa na ukarabati wa vyuo. Napenda niipongeze Serikali kwa hatua hii, ni nzuri sana na itafanya pia fani hii ianze kupendwa na watu. Vijana wengi walianza kuiona kama fani hii si nzuri kwa sababu ilikuwa kama inaanza kusahaulika hivi. Kwa hiyo, napongeza kwa hatua hizo.

Pamoja na hayo natoa ushauri kwamba kwa wataalamu wengi wa kilimo vyuo vyao vingi vinatoa elimu hadi ya Diploma . Kwa sababu hiyo, napenda kushauri kwamba vyuo hivi sasa viangaliwe kutoa diploma za juu au digrii kwa sababu sijaona hata vyuo huria vinavyotoa fani za kilimo. Kwa hiyo, wataalamu wengi wa kilimo wamebaki kuishia palepale, aidha, kwenye ngazi ya diploma basi, na ndiyo wengi ambao wako vijijini, lakini wanapenda kujiendeleza.

Naomba Wizara hii ishirikiane na Chuo Kikuu Huria ili kiangalie pia digrii nyingine zinazoweza kutolewa katika fani ya kilimo. Lakini pia kuwa na digrii au diploma za juu katika vyuo vingine vya kilimo kama Chuo cha Ukiruguru, Nyegezi, Uyole na vingine ambavyo vinaweza kutoa digrii hizi ili kuhakikisha kwamba wataalamu wa kilimo wanakuwa na utalaamu na pia kuendana na soko la leo.

Pia napenda kutoa ushauri kwamba vyuo hivi au Wizara ya Kilimo pia iangalie mabadiliko yaliyopo duniani ili masomo yaendane na wakati, yaani zianze kubuniwa kozi nyingine tofauti ambazo ni za muda mfupi zitakazokuwa zinatolewa na kuwawezesha wananchi wengi kuweza kushiriki.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Ushirika. Maendeleo ya Kilimo yatakuja au maendeleo ya nchi hii yataletwa na ushirika na kwa kweli ushirika ndiyo toka zamani ulikuwa nyenzo ya kuleta maendeleo. Vyama vya Kuweka na Kukopa yaani *SACCOS* vipo vijijini na wananchi wengi wameitikia, lakini tatizo ni kwamba wataalamu wa ushirika ni wachache sana, hawakidhi mahitani makubwa yaliyopo.

Sasa kwa mpango huu wa kuwaongeza wataalamu nashauri Wizara pia iangalie kuongeza wataalamu wengi zaidi katika suala la ushirika. Pia mafunzo yatolewe kwa vyama hivi vya Kuweka na Kukopa. Mafunzo hayo ni pamoja na mafunzo ya kuchambua miradi, kwa mfano, mikopo inatolewa kikundi kinakwenda kuomba mkopo lakini upembuzi yakinifu wa miradi ile wanayotaka kufanya haifanyiki matokeo yake wanakopa na wengine wanashindwa kurejesha kwa sababu ule mradi haukupembuliwa vizuri kama ni faida au hasara. Kwa hiyo, ni jambo muhimu kabisa miradi ya wananchi ipembuliwe na nashauri kama wataalamu ni wachache Serikali iangalie uwezekano wa kushirikiana na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali zilizoko vijijini ili ziweze kusaidiana na Wataalamu wa ushirika kuweza kutoa mafunzo kwa vyama hivi vya Kuweka na Kukopa vikiwemo vyama vya Kuweka na Kukopa vya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha Umwagiliaji kinaweza kikafanya wananchi wakajitosheleza kwa chakula mwaka mzima na nimeona mfano wa kilimo cha chai kinacholimwa Wilaya ya Njombe kwa umwagiliaji mwaka mzima. Nafikiri tunahitaji tujifunze hapo kwamba tunaweza pia kulima mazao ya chakula na tukawa na uhakika wa chakula kwa mwaka mzima kama tutatumia mbinu za umwagiliaji.

Kuna mfereji wa umwagiliaji Malangali, Wilaya ya Iringa Vijijini ambao umetengenezwa vizuri sana, naishukuru Serikali. Lakini utaalamu unaotolewa pale, wananchi wanalima tu kama vile walivyokuwa wanalima zamani. Ninaomba Wizara itusaidie kuhakikisha kwamba kunakuwa na mtaalamu anayesimamia pale kuweza kuhakikisha kwamba kilimo hiki kinafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie uhakika wa chakula. Wizara kwa kweli imefanya kazi nzuri, kama nilivyosema imechanganua vizuri masuala yote yatakayotekelezwa na kwa kweli kama itatekelezwa kama ilivyoainisha kwenye hiki kitabu kutakuwa na mageuzi.

Lakini tumezungumzia kulima tu na kuhakikisha chakula kinakuwepo, sijaona mahali ambapo imezungumziwa ulaji wa chakula hiki. Maana yake suala la ulaji pia ni suala lingine, nilitegemea kwenye Wizara hii pia nione suala ambalo limezungumzia ulaji na kuhakikisha kwamba kila familia inapata chakula.

Upatikanaji wa chakula ni kitu kingine na ulaji wa chakula cha kutosha ni kitu kingine na naelewa kwamba nchi hii sasa hivi inakabiliwa na tatizo la utapiamlo, wananchi wengi wana lishe duni. Wizara imesemaje? Hakuna kitu chochote kilichoongelewa hapa!

Kuna Idara ya Lishe au sehemu ya Lishe katika Wizara ya Kilimo. Sikuona mahali ambapo wameongelewa watafanya kazi gani kuweza kuelimisha wananchi. Sasa hivi tuna matatizo makubwa, watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI wanalalamika kuhusiana na suala la chakula na tunasema vyakula vile vya asili. Nina uhakika kwamba Wizara ya Kilimo inaweza kufanya kazi hii. Sioni mahali ambapo kipengele hiki kimezungumziwa, ni nani atakayezungumzia hili kama vyakula vya asili vinatakiwa vitumike? Ninaomba Kitengo kile cha lishe kisaidiwe katika Wizara kiweze kufanya kazi yake vizuri na kuelimisha wananchi na kozi fupi pia ziwepo katika vyuo vya kilimo kuweza kuwaelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya ulaji wa chakula cha kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba nirudie tena kushukuru na kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa kazi hii nzuri aliyoifanya na nina uhakika kama haya na ambayo Wabunge tunashauri yakitekelezwa tutakuwa na mageuzi ya kilimo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe na Mheshimiwa Dr. Guido Gologolio Sigonda. Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

**MHE. CHACHA ZAKAYO WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Ningependa kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuona busara ya kumteua Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, baada ya kutambua kwamba kuna bongo ambazo ziko huku upinzani ambazo zinaweza zikasaidia nchi hii na sisi hatupungukiwi hata wakiendelea kuwachukua kwa sababu wengine watakuja. Kwamba mawazo sahihi ni lazima yatumike katika kuleta mabadiliko ya maendeleo katika nchi hii, sasa kile ambacho sijui ni kama Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David ambao ni vijana na wasomi, sijui kama hayo mawazo ambayo Waziri anayatumia ni yale ambayo tulikuwa tukizungumza naye tukiwa huku Upinzani. Kwa sababu alikuwa na mawazo mazuri sana, ameshakuwa Waziri wa Kilimo, siyo mara ya kwanza, hii ni mara ya pili, kwa hiyo, ameshawahi ku – *fail* mara moja.

Kwa hiyo anaweza akawa alijifunza kitu ambacho sasa anataka kuwaonyesha Watanzania. Mimi nampa moyo ajitahidi lakini kwa picha ninayoiona kuna makosa ya

msingi ambayo yamefanyika.  Sasa sisi huku tunaposimama kuikosoa  Serikali sio tunasema kwamba kila kitu kinachofanywa na Serikali ni kibaya, hapana!  Wanajitahidi sana, lakini sisi tunaangalia pale kwenye upungufu,  ndipo tunapolenga.  Kwa hiyo, sisi hatusimami kuwatukana, bali tunasimama kuwaeleza ili warekebishe na kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie suala la viwango kulingana na falsafa ya Spika wetu kwamba tunapungukiwa na viwango pale ambapo Wabunge wasomi wenye *experience* mbalimbali, Mbunge anaposimama dakika kumi na tano akizungumzia upungufu, halafu anarudi anasema yeye anaunga hiyo hoja mia kwa mia. Hilo linawatatiza sana wananchi, hata wananchi wa Tarime wamenituma niulize, hivi katika hiyo mia kwa mia amezungumzia upungufu dakika kumi na tano,  sasa hiyo mia kwa mia ule upungufu ni asilimia ngapi?   Watupe somo la hisabati ili kusudi wananchi wanapokuwa wanasikiliza kule wawe wanaelewa kwamba huyu Mbunge anazungumzia nini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda mbali na mimi pia kwa mara nyingine napenda kutoa rambirambi zangu kwa kuondokewa na Mheshimiwa mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa ambaye sisi tulikuwa karibu  naye kwa  kazi na msimamo wake niliokuwa naujua ni kwamba alikuwa anapenda ukweli na haki.  Kwa mtazamo wangu ni mwana-CCM ambaye ni *product* ya Mwalimu Nyerere, lazima awe na msimamo huo.  Yeye hakuwa mnafiki na alipenda  kukisema kile ambacho alikuwa anakiamini.  Kwa hiyo, nadhani Mungu atamweka mahali pema peponi, na hata vijana wengine Tanzania  ambao hawako humu Bungeni waweze kuja ili tutengeneze nchi yetu iweze kuwa ni nchi nzuri kama Mwalimu alivyotarajia.

Mheshimiwa Spika, kosa ambalo naliona kabisa la msingi ni katika *l*mfumo wa kumiliki ardhi *(land tenure)* kwa sababu tunapokuwa tunazungumzia kilimo, na Mheshimiwa Waziri anapozungumzia mapinduzi ya kilimo,  hili neno mapinduzi bado linanitatiza sana kuhusiana na CCM. Kwa sababu mimi nadhani mapinduzi yanajulikana dunia nzima kama yale yaliyofanyika Marekani mwaka 1777, yaliyofanyika Urusi mwaka 1917, Uchina mwaka 1949, Korea na mfano kama wa Korea Kaskazini ni mzuri sana kwa nchi za kijamaa kama hii yetu ilivyokuwa kwa sababu wao waliona waanzie na kilimo na hata siku walipoanza kutengeneza trekta lile la *Esking Sung,* marehemu alipokwenda kuangalia kile kiwanda alikuta ile trekta haiwezi kwenda mbele inarudi nyuma.  Lakini aliwasifu akasema kwamba huu ni mwanzo mzuri, tengeneza sasa itakayokwenda mbele.  Sasa hivi tungefuata ule mfano wa kijamaa tungekuwa mbali sana, kwa hiyo, kuna kitu kilikosewa hapa.  Mwalimu alijitahidi sana akasema ardhi ni mali ya umma, *access* ya ardhi ikapatikana kwa wananchi na akaweka  *principle*  ya ujamaa ambayo alijaribu kufanya hivyo vitu.  Alitoa mpaka ng'ombe na matrekta na kila kitu lakini ikafeli.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nadhani Mwalimu kilichomponza alikuwa mtu mwenye huruma sana.  Kwa hiyo, watu kama wale wafisadi yeye alikuwa anawaonea huruma, anawahamisha hapa anawapeleka pale, lakini kule China na nchi zingine wale walikuwa wanabanwa sana koo mpaka wanapigwa risasi  hata wakaacha.  Sisemi kwamba hii Serikali ifanye hivyo ila mimi nasema kwamba kwa sababu Rais

alikwishasema anawajua basi nadhani atawarekebisha kama alivyosema. Ila hilo ni tatizo kubwa lililoangusha *system* ya ujamaa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kumiliki ardhi sisi tunaangalia ardhi kama kitu cha hivi hivi. Ardhi ni kitu cha msingi *(fundamental)* katika maisha ya binadamu na katika *plan* zozote za uchumi zinazoweza kufanyika. Tunapozungumzia Amerika, tunazungumzia ardhi iliyoibiwa, watu wanatoka nchi nyingine wanakwenda wanaua watu nchi ile wanawamaliza, wanachukua ile ardhi. Kwa hiyo, utaona jinsi ardhi ilivyo kitu muhimu katika maisha. Tunapozungumzia Australia ile ni ardhi ambayo imeibiwa mpaka leo watu wa nchi ile wamebaki ni wachache na wanaendelea kudai haki zao, walinyang'anywa ardhi. Afrika nadhani mpango ulikuwa ni huo huo ila pia na sisi Mungu alitujalia tulikuwa na nguvu zaidi, waliweza kuvamia maeneo ya Kusini zaidi, lakini unaona mpaka leo mapambano yamefikia hatua ambayo bado Mwafrika anaweza kusimama pale na akasema ndio Rais wa nchi ile. Kwa hiyo, sisi bado tunayo *struggle*.

Mheshimiwa Spika, walishindwa kwenda Afrika Magharibi kwa sababu ya mbu, walikuwa wanakufa sana na malaria. Kuna mtu wa Nigeria aliandika kitabu akasema *Thank you mosquito* lakini Afrika Mashariki walikuja kwa hali ya hewa na bado wanataka kuja Tanzania na wanapofika hapa kitu cha kwanza wanachokamata ni ardhi. Wamekamata ardhi Zimbabwe, huo ndio mgogoro mpaka leo. Kwa hiyo, hili suala la *land tenure* tuliangalie sana kwamba sasa kama tunataka kufanya kilimo tunamilikishaje ardhi. Kama ni mfumo wa kijamaa basi *state* ichukue mamlaka ya kuwagawia watu ardhi, watu hawana haki hivi sasa ya kumiliki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa Muswada ule iliyoleta wa Sheria ya Ardhi (*Land Act*, 1999). Huo ulitoa haki kwa wananchi kwamba wanaweza kumiliki, kwamba ardhi ina thamani na inaweza kufidiwa kwa thamani hiyo. Sasa ambacho hatujaelewa ni kwamba ni kwa nini vijiji viendelee kumiliki ardhi wakati ambao vijiji siyo *entity animal*, unaposema kijiji sasa unamaanisha nani? Maana vijiji vya ujamaa vilikwisha, pale ni makao tu. Sasa kwa nini wale watu wasipewe ardhi, kila mtu kipande chake akithamini halafu akitumie? Hivi ndivyo Kenya walivyofanya na unaona kwamba mtu anaona ardhi ina thamani na anaweza kukopesha kutokana na ardhi aliyokuwa nayo. Hiyo ni hatua moja ambayo nafikiri Serikali inabidi iangalie kwa sababu nchi nyingine zinafanya hivyo hata Uganda.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kuangalia kama basi hatuendelei na *production* ya kijamaa, maana *production* zinafanana katika mifumo yote kwamba kuna ardhi, zile *factor* wanaita ni vitendea kazi muhimu. Katika mfumo wowote wa uzalishaji kuna *land* (ardhi), kuna *capital* (mtaji) na kuna *labour* (watu), wale hatupungukiwi. Kingine ambacho wale mabepari wanakiongeza, wao wanasema kwamba kuna *entrepreneur* yaani mfanyabiashara na naona kwamba hii nchi yetu sasa pamoja na kwamba inafanyika kimya kimya inaelekea sasa kuwa ni nchi ya wajasiriamali. Kwa hiyo, ningeshauri wale wa Chama cha Mapinduzi sasa ile nembo pale juu ibadilike tuondoe jembe na nyundo, tuweke alama fulani ya wajasiriamali kwa sababu siyo Chama cha wafanyakazi na wakulima tena, ni cha wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, basi kama ni ujasiriamali tuzungumzie kuhusu *large scale farms*. Sasa hayo mashamba makubwa kama tutaleta Wazungu waje kuyalima, hiyo ni shauri yetu. Lakini mimi nadhani kwamba watu wapo humu ambao wanaweza kupewa mashamba na wakapewa mitaji na wakafanya kilimo kama vile ninavyoona pale jirani Kenya. Wale walinyang'anywa ardhi lakini sasa hivi kuna *farmers* ambao ni Waafrika na wanazalisha kwa kiwango ambacho nchi ile inategemea hicho kilimo na ufugaji. Kwa hiyo, sasa tunapokuwa tunaruhusu watu wetu kukimbia vijijini na kuja mijini hasa vijana hawana ardhi kwa sababu waliopewa ardhi ni babu zao. Hata mimi kijijini kwangu aliyepewa ni baba, mimi sijapewa na tayari tunaendelea kuzaana na kuongezeka na matokeo yake wanaposikia kwamba watu Tarime wanapigana wanafikiri kwamba wale watu hawana shughuli nyingine ya kufanya ni kupigana, ni ardhi imepungua! Ardhi tuliyokuwa nayo sisi ni ile ambayo ilikuwa inaelekea mbuga ya Serengeti, lakini mbuga ya Serengeti imepanuka na kuchukua ardhi yetu kubwa hivi karibuni. Suala hilo nitaomba Serikali iliangalie kwa nini tunyang'anywe ardhi kiasi kile maana mpaka ulikuwa ni Mto Mara lakini sasa tumebanwa na ndiyo inasababisha kwamba tunakuwa hatuwezi kuendelea kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Ushirika. Ushirika nadhani Vyama vingine vya Ushirika viliweza ku-*survive* kwa sababu ya kupewa ruzuku kama *SHIRECU* na vyama vingine. Lakini mimi nashangaa kwa nini Mara *Cooperative Union* ambayo Mheshimiwa Waziri anaifahamu vizuri sana yenyewe haikupewa ruzuku yoyote na mpaka sasa hatuna Chama cha Ushirika na ndiyo kimesababisha kilimo chetu cha kahawa na pamba kudorora. Kwa hiyo, namwomba aangalie anawezaje kufufua kile Chama cha Mara *Cooperative Union* ama kingine ambacho kitakidhi hayo mahitaji. Na kama jinsi Mheshimiwa Cheyo alivyotushauri hapa, tusiangalie tu ushirika wa masoko, tuangalie ushirika yaani *producer cooperative* kama zile ambazo ziko katika nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, nchi ambazo zinaonyesha mfano mzuri ni kama *Norway, Sweden,* wamefanikiwa sana, *movement* hiyo, vuguvugu la *cooperative* ni la miaka mingi. Hakuna haja ya kugundua gurudumu upya, tuangalie wenzetu walifanyaje, na hiyo itatusaidia sana. Kwa hiyo, hili suala la *Land Tenure* tuangalie sana linaweza kutuletea vurugu katika nchi hii. Migogoro kama ya Rwanda na Burundi ni ardhi, na sisi sasa kama tulikuwa tunabadilisha mfumo wa kijamaa basi tungejifungia sehemu fulani hata mwaka mmoja *(close door policy)* halafu tuangalie tunapangaje mambo, halafu turudi tufungue *open door policy,* lakini sasa kama tumefungua wazi, watu wanakuja wa kila aina na wamelenga ardhi. Hiyo *movement* ya Mongiki unayoisikia Kenya ni watu ambao hawana ardhi lakini kwa bahati nzuri Tanzania hatujafikia hapo, tunaweza kujipanga na nchi yetu ikaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuzungumzia suala la Katiba, kwamba ardhi nayo pia umiliki wake uonekane kwenye Katiba. Sasa mmiliki wa ardhi ni nani? Serikali ilikwishajitoa katika biashara. Kwa hiyo, wananchi waimiliki, kila mtu amiliki kipande chake na sera iwe kwamba ni ya muuzaji au mnunuzi anayehiari *(willing buyer, willing seller)*. Ndio maana hii Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 inashindwa kutumika kule Vijijini, kwa mfano, makampuni ya nje yanakuja kuchukua kwa ajili ya uchimbaji, lakini nilipe sasa heka yangu ni shilingi ngapi, haijulikani ni shilingi ngapi, wanapewa

chochote, hali ambayo itawapa wananchi uwezo wa kumiliki ardhi na kuitumia. Kwa hiyo, hii bajeti ina asilimia tatu ambayo inapewa kwa wananchi. Sasa katika kuanzisha *an agricultural revolution* ambayo inazungumziwa na Mheshimiwa Waziri sidhani kama asilimia tatu ya bajeti inaweza kukidhi hiyo, ila kwa kuanzia nadhani tuanzie na *agrarian reform* yaani tuangalie kwamba umiliki wa ardhi uko vipi halafu ndiyo tuelekee kwenye *agrarian revolution*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningependa tuangalie lile bonde la *RUBADA*. Mwalimu aligundua kwamba lile bonde ni muhimu sana hapa Tanzania kama Wajerumani walivyokuwa wameona na Mheshimiwa Profesa Mtulya kutoka eneo hilo, alizungumza kwamba hili ni eneo ambalo lina hekari themanini za rutuba nzuri ambayo inazolewa kutoka maeneo yote ya nchi. Halafu hilo eneo pia lina maji, madini, linaweza kutengeneza *hydro power* na hata Wajerumani vita vyao vya mwisho pale ndipo walipokatalia mpaka hata meli yao ya mwisho ilizamishwa pale, kuna sehemu inaitwa *Stigler's Gorge*. Wajerumani tuwaangalie vilevile unaweza kujifunza kutoka kwa adui yako jinsi walivyo-*plan* nchi hii katika miaka ishirini na saba waliyokaa hapa na mambo waliyofanya, basi tuchukue yale mambo tuyasome, tuyaangalie, tunaweza kuyafanya sisi wenyewe. Kwa hiyo, hili bonde la Rufiji ni sehemu ambayo ni muhimu sana na kwa kuanzia tunaweza kuanzia hapa na umwagiliaji mito, maziwa tunayo, hatuwezi kupungukiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Naona niishie hapa, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa muda angalau nichangie machache kutokana na hotuba ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuwa mtu wa mwisho kuchangia kuna tatizo lake hasa kutokana ya yale ambayo wenzio wameyazungumza na hasa kufuatana na kanuni yetu kwamba si vyema ukazungumzia yale ambayo tayari yameshazungumzwa. Kwa hiyo, nilikuwa nimefikiri kwamba labda niache kabisa nisizungumze lakini bahati nzuri katika kupitia hiki kitabu nimeona kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo itanibidi kwa kweli nimkumbushe Mheshimiwa Waziri aliyetoa hotuba hii kwa sababu hayo mambo ameyasahau.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba niungane na wenzangu kwamba naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu unapounga mkono asilimia mia moja inatokana na kitendo kilichofanyika. Tukikumbuka tu kwamba ili kusudi tuwe katika utawala tulikuwa na utaratibu wa kuweka mfumo na huo mfumo ndio ambao unaelekeza ni nani atakayechukua uongozi, nani atakayeunda Serikali. Kwa hiyo, katika mfumo wa Vyama viwili ama Vyama Vingi tulikwenda kwenye majukwaa na bahati nzuri pale kwenye majukwaa kila mmoja alieleza sera yake na hatimaye Chama cha Mapinduzi ndicho ambacho kilipata nafasi ya kuweza kushinda katika ule mkakati wote wa uchaguzi.

Sasa baada ya kupata ushindi ni lazima Chama kijipangie utaratibu wake jinsi gani kitaendesha hii Serikali au nchi. Kwa hiyo, kimeweka sera katika mfumo wa Ilani. Sasa Ilani ndiyo ambayo inazungumzwa hapa, ni jinsi gani tunaendesha hii nchi. Ninaposema kwamba naunga mkono asilimia mia moja maana yake ni kwamba Mheshimiwa Waziri amezingatia na ametekeleza yale yote ambayo Chama cha Mapinduzi kilikuwa kimepanga katika Ilani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na uzuri wote wa hotuba yake, Chunya ameisahau. Mimi nitaendelea kila wakati ninapozungumza kuwakumbusha Waheshimiwa kwamba Chunya ni moja ya Wilaya katika Serikali ya Tanzania, tusifike mahali kuiona Chunya kama iko sehemu nyingine na nitaanza kuzungumza kwa kutoa mifano kwa baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa ni muhimu sana ayaingize.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na mazao ya biashara na kilimo. Kabla ya mwaka 1995 Wilaya ya Chunya hasa Jimbo langu la Songwe lilikuwa na mazao mawili makuu ya biashara. Zao la pamba na zao la tumbaku. Sasa kutokana na jiografia ya Jimbo langu la Songwe zao la pamba lilikuwa linalimwa bondeni na zao la tumbaku kwenye miinuko, ndiyo jiografia ambayo ipo. Lakini hiyo ni kabla ya mwaka 1995 na wananchi walikuwa wamefaidika sana lakini kutokana na athari ambayo ilijitokeza athari ambayo ilionekana kwamba inaweza kuathiri zao la pamba, kilimo cha pamba katika Jimbo la Songwe kilisitishwa baada ya kugundua kwamba kulikuwa na mdudu funza mwekundu na bado kimesitishwa toka wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nilitegemea ni kwamba Serikali angalau basi kwa sababu ndio lilikuwa zao pekee katika ukanda huu, basi ingefikiria ni jinsi gani ingechukuliwa kuwaendeleza hao wananchi katika upande wa zao la biashara.

Haikufanywa hivyo, matokeo yake ni kwamba zao sasa la biashara lilibadilishwa kuwa mazao ya chakula. Na mazao ya chakula kama tunavyofahamu wote na kutokana na hali ambayo Wilaya ya Chunya inasahaulika sana basi kilimo chenyewe ni duni kama wenzangu walivyozungumza. Kwa kweli maisha yakawa magumu sana.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho hata wananchi wa Jimboni kwangu wanajiuliza ni kwamba ni miaka kumi na mbili sasa tangu litolewe tamko la Serikali, tuliambiwa kwamba utafiti unafanywa kumjua huyo funza na jinsi ya kuweza kumdhibiti. Tunataka angalau Serikali ingefika mahali tuone kwamba imekamilisha utafiti.

Katika kufuatilia nimeelezwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwamba sasa hivi funza huyo, ndiyo anazidi kunenepeana, bado yupo. Sasa watu tunajiuliza, maana chakula chake kilikuwa ni pamba, sasa hivi huyo funza anakula nini, angalau wananchi wangeambiwa kwamba kuendelea kuwepo kwa huyo funza kunatokana na chakula kingine. Inawezekana pengine anakula mahindi, ndiyo maana hata mazao kule hayafikii katika kiwango kile. Kwa hiyo, hilo nalo tungependa tujue huyo mdudu lini atapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinazidi kuwapa unyonge ndugu zangu wa Jimbo la Songwe ni kwamba hata Malawi ambapo ni karibu kabisa pamba inalimwa, halafu katika Mikoa ya kati pamba inapolimwa, na sina uhakika kama Urambo inalimwa, lakini Kanda ya Kati pamba inalimwa.

Sasa wanajiuliza huyu mdudu ni pamba ile ya Chunya na mwenzangu wa Tunduru vilevile amesema kwamba alisitishwa kulima hiyo pamba. Ni katika eneo hili tu basi ndiyo huyo mdudu anastawi zaidi. Kwa hiyo, hilo ni swali mojawapo ambalo pengine tungeendelea kujiuliza na pengine Wizara ingejaribu kufikiria angalau kutoa majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya hali hiyo, Serikali haikuwa na mpango wowote wa kuweza kuwasaidia wale wananchi. Wananchi wameendelea kuvumilia, labda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Songwe kwa uvumilivu wao ambao wamekuwa nao katika kipindi cha miaka kumi na mbili lakini wana matarajio kwamba Serikali itafika mahali italipatia ufumbuzi suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa miinuko mmesema kwamba tumbaku ndiyo inalimwa. Pamoja na uharibifu wote wa kilimo cha tumbaku, wa mazingira, lakini zile barabara ndogo ambazo ndizo pengine tunazitegemea zinaharibiwa sana na haya magari makubwa ambayo yanakwenda kusomba hizo tumbaku katika yale maeneo.

Sasa upo utaratibu kwamba kuna *percentage* kidogo ambayo yale makampuni yanatoa kwenye Halmashauri. Nasema hiyo *percent* ni ndogo sana. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba Wizara ingefikiria ni jinsi gani wanaweza angalau wakaweka utaratibu uweze kusaidia kikubwa zaidi kuliko hivi sasa ili kusudi barabara zetu ziweze kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Katika kikao kilichopita niliahidiwa hapa katika Bonde la Songwe ambalo ni bonde zuri sana kwamba mipango ya umwagiliaji itafanyika. Nilikuwa nategemea kwamba katika mipango ambayo imeandaliwa na Wizara hilo suala lingekuwepo, bonde la Songwe lingekuwemo.

Kwa masikitiko makubwa hakuna, halikuonyeshwa mahali popote katika hiki kitabu! Nilikuwa naomba wajaribu kufikia kwa sababu tayari walishaniahidi kwamba watashughulikia, sasa sijui labda watakuwa na mpango mwingine, lakini nilitegemea kwamba katika mpango wao wangeweza kulionyesha. Mimi najaribu kukumbusha tu, kwa sababu hotuba kwa kweli ni nzuri sana.

Katika Mkutano wa Saba wa Bunge uliopita, niliahidiwa kwamba wale wadudu wasumbufu wa mimea kama panya watashughulikiwa. Katika bonde la Songwe kuna panya wengi sana lakini sijaona humu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia chochote. Nilikuwa nakumbusha wajaribu kufikiria hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wagani. Katika Jimbo langu lenye Kata kumi kuna wagani wawili tu wa kilimo. Pamoja na matatizo mengine lakini nilikuwa naomba nayo Wizara ifikirie. Katika Kata kumi zenye umbali kati ya kilomita arobaini unawaweka wagani kumi, bahati nzuri naishukuru Serikali wamewapa pikipiki, lakini zile pikipiki unakuta wakati mwingine unakwenda kumwomba msaada anakwambia sina mafuta. Sasa nilikuwa nafikiri kwamba vilevile hilo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nakumbusha tena katika vikao vilivyopita niliahidiwa kwamba yale madai ya wakulima wa pamba ambayo toka mwaka 1995 wamekuwa wakidai yatashughulikiwa, lakini mwaka jana hayajashughulikiwa. Mwaka huu nimeahidiwa vilevile yatashughulikiwa, yaani hivi sasa ninavyozungumza wananchi wangu wana mategemeo makubwa sana katika ahadi hiyo. Nilikuwa naomba tu kwamba hiyo ahadi ifikiriwe kwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono kwa mara ya pili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nami pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Wizara ambayo wote tunakubaliana kwamba ni Wizara muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu kwa sababu ndiyo inayofanya utaratibu mzima wa kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji, uwezo wa wananchi wa kawaida wa vijijini kuweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameiwasilisha jana na maombi ya fedha ambayo ameyatoa kwa ajili ya mwaka wa fedha wa 2007/2008. Lakini vilevile napenda kwa dhati kabisa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi nzuri sana ambayo imefanywa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusiana na Wizara hii ya Kilimo kiasi kwamba ameweza kueleza mikakati mbalimbali mbadala ambayo naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Wasira pamoja na Manaibu wake wawili wataweza kuifanyia kazi ili waweze kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakua.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nianze kuzungumzia suala zima ambalo Mheshimiwa aliyezungumza sasa amelizungumza na Mheshimiwa Chacha pia alilizungumzia. Mimi nadhani ni sawa kama sisi sote ni wanasiasa kufanya mjadala wa kina sana kuhusiana na ilani za vyama zinasema nini na kwamba Chama kinatekeleza Ilani yake. Lakini jambo la msingi ambalo ningependa kulizingatia sana ni kwamba tunapokwenda kwenye uchaguzi tunakwenda kuomba kazi kwa wananchi.

Ilani za Uchaguzi za Vyama ni barua za kuombea kazi. Ukishaomba kazi unapewa mkataba wa kazi, sasa ule mkataba wa kazi ndiyo maelekezo muhimu ya malengo, maelekezo ya kisera, mikakati ambayo tunatakiwa tuifanye.

Kwa hapa Tanzania malengo haya, mikakati hii na sera hizi tunakuwa tuna utaratibu wa kuzifanya mwaka hata mwaka, kwa maana kwamba hotuba za bajeti za

Wizara, sera mbalimbali ambazo zimetungwa na Serikali ambazo zina *cut across* na Vyama vyetu vya Siasa, ndiyo vinapaswa kuwa rejeo muhimu tofauti na kila siku Mawaziri hapa na Wabunge kuja kuimba ilani, ilani, ilani!

Kwangu mimi na Kambi nzima ya Upinzani, tunaamini kwamba ilani ni barua tu ya kuombea kazi na ndiyo maana ina orodha tu ya miradi, lakini siyo masuala ya kimkakati ya kiutekelezaji na kama kuna kitu ambacho kinaweza kuwa ni mwongozo wetu katika utendaji kingepaswa kuwa ni hotuba ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa mwaka 2005 wakati anazindua Bunge kwa sababu ile ndiyo ambayo ili-*search* kwamba tunataka tufike wapi kama nchi.

Kwa hiyo, suala hili ni vema kuendelea kuzungumza lakini Mheshimiwa Chacha juzi alisema hapa kwamba simba anapoingia kijijini hajisemi mimi simba, mimi simba, watu wanamwona ni simba na wanamkimbia.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo napenda kulizungumza baada ya hilo ni suala la bajeti ya Wizara ya Kilimo. Naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza. Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani katika Wizara ya Kilimo amelizungumza hili pia.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Wizara ya Kilimo wakati huo ikiwa chini ya Mheshimiwa Mungai ilikuja hapa Bungeni ikaomba tuwapitishie jumla ya shilingi bilioni 123. Miongoni mwa hizo shilingi milioni 45 ni fedha za maendeleo na zilizosalia takribani shilingi bilioni 78 hivi zilikuwa ni fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ambayo hotuba ya Waziri wa Kilimo wa sasa Mheshimiwa Wasira ametusomea hapa, si fedha zote ambazo Wizara ya Kilimo iliziomba, zilifika. Lakini fedha zilizoathirika zaidi ni fedha za miradi za maendeleo. Kwa maana kwamba fedha zile za mshahara, posho mbalimbali, na kadhalika zilikwenda kwenye Wizara bila athari kubwa kwa sababu zilikwenda kwa kiwango cha asilimia 94. Lakini fedha za miradi ya kilimo zilikuwa si chini ya robo tatu ambazo ziliombwa na fedha ambazo ziliathirika zaidi ni zile zilizotoka kwa wafadhili. Kwa hiyo, hii inaturudisha katika ile dhana ya kutaka kuendeleza kilimo chetu lakini tukitegemea zaidi miradi ya wafadhili. Sababu katika jumla ya shilingi bilioni 45 ambazo Waziri wa Kilimo aliziomba ni shilingi bilioni 5 tu ambazo zilitokana na fedha ambazo TRA inakusanya yaani fedha za ndani. Hii imeonyesha dhahiri kwamba kuna utegemezi mkubwa sana katika kuendeleza kilimo.

Kwa hiyo, hili naona ni *anormality* kubwa sana ambayo inabidi irekebishwe kwa sababu vinginevyo tutajikuta kwamba tunaimba kila siku wimbo wa kuendeleza kilimo, kuendeleza wakulima wetu lakini hatuwekezi katika shughuli hiyo, tunategemea wafadhili wafanye hivyo kwa niaba yetu. *Trend* hiyo imeendelea kwa mwaka huu kwamba sehemu kubwa ya fedha za maendeleo ya kilimo hazitokani na fedha zinatokana na fedha za wafadhili. Ina maana utegemezi wa zaidi ya asilimia 70 kwa sababu tuna uwezo wa kutoa fedha za ndani kwenye killimo kwa asilimia 28. Kwa hiyo, utegemezi wa zaidi ya asilimia 70 katika bajeti ya shilingi bilioni 60 ambazo Waziri anaziomba

hapa ni utegemezi mkubwa sana na ndio huo kupitia *ASDP, DASP* na miradi mingine ya kilimo. Kwa hili nilikuwa naomba Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi iweze kuangalia jambo hili, kwa sababu tukiendelea kuwategemea wafadhili yatatukuta yaliyotokea mwaka jana ambapo wafadhili watarajiwa watoe takribani shilingi bilioni 45 wakatoa shilingi bilioni 25 tu, na hiyo iko katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna tatizo na hili pia naamini Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameligusia. Tatizo kubwa tulilonalo ambalo ningependa pia Serikali iweze kuliangalia vizuri ni kwamba Waziri wa Fedha alituambia hapa kwamba bajeti ya Kilimo kwa ujumla wake takriban ni asilimia 6 ya bajeti nzima ya nchi. Bajeti iliyopitishwa hapa na Bunge lako Tukufu ya nchi ilikuwa ni jumla ya shilingi trilioni 6.06 na bajeti ambayo Waziri wa Kilimo ameomba fedha tumpatie akatekeleze kazi za kuendeleza kilimo ni shilingi bilioni 132 tu ambayo ukipiga hesabu ni asilimia 2.2 peke yake ndiyo fedha ambazo Wizara ya Kilimo inazipata katika Mfuko Mkuu wa Bajeti. Ni vizuri Waziri wa Kilimo atakapokuwa anatuelezea hapa aelezee hii asilimia 4 ambayo haionekani katika Wizara ya Kilimo iko wapi na inapatikana katika Wizara zipi na ni kwa nini fedha zote za kilimo zisiratibiwe na Wizara ya Kilimo. Maana yake inawezekana tumeambiwa kuna asilimia 6 lakini hali halisi sio asilimia 6 kwa sababu bajeti ambayo Wizara ya Kilimo inaomba ni shilingi bilioni 132; bajeti ambayo Bunge lako Tukufu limelipitisha ni shilingi trilioni 6. Sasa ukitafuta asilimia, ni asilimia 2.2. Sasa hizi asilimia 4 ambazo hazionekani katika Wizara ya Kilimo ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, la tatu ni uzalishaji katika kilimo. Tulizungumza wakati wa bajeti na Wabunge wengi walizungumza na mimi kama Waziri Kivuli wa Mipango nililizungumza kuwa tuna tatizo kubwa sana kwamba uzalishaji wa kilimo unashuka. Mchango wa Kilimo katika *(GDP*) pato la Taifa unashuka. Uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kiasi kikubwa unashuka. Mwaka jana tumeambiwa kwamba pamba ilishuka kwa takriban *negative* 65. Sasa haya mambo ni vyema Serikali ingekuja kuleta maelezo au Waziri alipotoa maelezo yake kuhusiana na kilimo, inakuwaje hawezi kutuambia kuna mikakati gani ya kuweza kuhakikisha kwamba uzalishaji katika kilimo unaongezeka. Kambi ya Upinzani imetoa mapendekezo yake kama jinsi ambavyo imeelezwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Kilimo. Lakini wanataka Serikali iyachukulie haya kwa uzito unaotakiwa kwa sababu ikitokea uzalishaji katika kilimo ukawa ama unadumaa au unashuka kama jinsi ilivyo sasa hivi maana yake ni kwamba nchi itashindwa kujitosheleza kwa chakula na vilevile nchi ikashindwa kupata ziada ya kuuza nje.

Katika hotuba ya Waziri inaonyesha kwamba mwaka huu tutaweza kujitosheleza kwa chakula kwamba kuna tani bilioni 11, kuna tani kama bilioni 2 za ziada ambazo tutaweza kujitosheleza. Lakini pia fungu ambalo limetengwa kwa ajili ya ununuzi wa chakula kuliweka kwenye ghala kuu la Taifa bado ni kidogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ajaribu kuangalia *very critical* mapendekezo ambayo tumeyatoa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uzalishaji katika kilimo unaongezeka. Tunatakiwa kuongeza uzalishaji kwa sababu moja kubwa. Sisi kama nchi maskini hatuna uwezo wa kudhibiti bei ya bidhaa ya kilimo hususan hizi ambazo tunauza nje katika soko la dunia, hatuna *control* ya *prices.* Lakini sisi tuna *control* na

uwezo wa kuzalisha *volume*. Kwa hiyo, lengo letu na mkakati wetu ni lazima uwe za kuzalisha zaidi tupate mazao mengi zaidi tuweze kuuza nje zaidi ili kuweza kuziba lile *gap* la *control* ya *prices* ambayo wenzetu wa nchi za magharibi wanayo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda kukizungumzia ni kwamba nilijaribu kupitia hotuba ya Waziri wa Kilimo ya mwaka jana na naona *some inconsistencies*. Kwamba mwaka jana tunasema hivi, mwaka huu hatupewi maendeleo yaliyofikiwa mwaka jana. Mwaka jana Wizara ya Kilimo ilikuwa imetarajia kutenda mambo makuu manne. La kwanza, ni kuhusiana na suala zima la ruzuku ambalo Waziri amelizungumzia, suala la *ASDP, ASDP of course* ni *ARV* na la nne ni suala zima la mageuzi yaani *modernisation* ya kilimo. Haya ndiyo masuala makuu manne ambayo Waziri wa Kilimo mwaka jana aliliambia Bunge.

Tulitarajia kwamba Waziri Wasira anapokuja kutoa hotuba yake na kutuomba fedha, sababu za msingi zinazomfanya hivyo, na Mawaziri wote wafahamu kwamba wanapokuja kutuomba fedha, wanaomba kutokana na mikakati ambayo wameiweka. Waziri Wassira hakuelezea kwa kina tumefikia wapi utekelezaji wa mambo ambayo Waziri Mungai aliliambia Bunge hili Tukufu juu ya mambo manne. Kwamba mambo ambayo tunakwenda kuyafanya sasa kwenye mwaka unaofuata ni yepi, na ni lazima yajengee kutoka pale ya mwaka jana yalivyowekwa. Sasa sijui kama ukibadilisha Waziri na mikakati inabadilika lakini mimi sijui! Ninachojua ni kwamba wataalamu ni wale wale. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri Waziri atakapokuwa anajibu aweze kulinganishia mambo manne ambayo Waziri Mungai alisema tunayatekeleza mwaka jana, yametekelezwa namna gani na tunayaendeleza vipi ili kuweza kufikia ukuaji wa kilimo wa malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho nataka kuzungumzia ni la wataalamu. Serikali inapanga kuajiri wataalamu wa kilimo 2,500 wakiwemo wahitimu wa kutoka Chuo cha *SUA* takriban 500. Waziri Kivuli wa Kilimo amezungumzia tatizo lililotokea mwaka jana ambapo Waziri wa Elimu ya Juu kinyume cha Sheria ya Bodi ya Mikopo akatangaza taratibu mpya za jinsi wanafunzi kupata mikopo. Mambo ya asilimia 40 na mambo ya *Division One* na *Two*. *SUA* walikuwa wamedahili wanafunzi 800 kuingia *SUA* ambayo ndiyo *capacity* yao. Kutokana na masharti mapya ambayo Waziri wa Elimu ya Juu aliyatoa *SUA* ilidahili wanafunzi chini ya 200 mwaka jana. Leo Waziri wa Kilimo anataka kwenda kuajiri wanafunzi wa *SUA* 500 na mwakani wengine na mwaka unaofuata wengine, wanafunzi ambao tayari Waziri wa Elimu ya Juu amewanyima elimu. Nashindwa kuelewa, tuna Serikali moja au kila Waziri anajipangia anavyotaka!

Kwa hiyo, nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atufahamishe atawatoa wapi hawa wataalamu ambao Waziri mwenzake amewazuia wasisome? Kwa nini pasiwe na mkakati maalumu wa kuhakikisha kwamba kwa kuwa tunataka kuimarisha kilimo chetu kwa ku-*modernised* kilimo, wanaosomea kilimo mikopo yao iwe ni *grant* na pasiwe na masharti kama jinsi ambavyo vyuo vingine wanapewa masharti ili tuweze kuwa na wataalamu wa kutosha wa kilimo waweze kutusaidia wakulima vijijini kuweza kuendeleza nchi yetu?

Hayo ndiyo mambo ambayo nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri aweze kutupatia ufafanuzi hasa hasa hili suala la mwisho ambalo tumelizungumzia la *SUA* ambalo Msemaji wa Upinzani alisema na nimelizungumzia. Tunataka tupate maelezo kwa sababu mwaka jana tumepoteza zaidi ya wanafunzi 600 ambao walikuwa waingie *SUA,* hawakuingia kwa sababu ya maamuzi ya Waziri ambayo hayakuzingatia sheria ya mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na naamini kabisa kwamba changamoto ambazo tumezitoa, mawazo ambayo tumeyatoa Serikali iliyoko madarakani sasa hivi itayafanyia kazi kwa sababu lengo letu ni moja kuhakikisha kwamba Watanzania wanaendelea. Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia juu ya hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Manyoni Magharibi tunatoa pole kwa wenzetu waliotangulia mbele ya haki na tunazitakia familia zao afueni ili waweze kusonga mbele katika maisha.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kukupongeza kwa jinsi unavyotuongoza, kwa kweli naona una-*balance* mambo vizuri, panapostahili sifa lazima tutoe, panapostahili lawama nazo tuzitoe ili tuweze kwenda vizuri. Haiwezekani tusimame hapa tusifu tu, tunajua Serikali inafanya mambo mazuri na yale ambayo inafanya mambo mazuri tuyasifu na yale ambayo yanakwenda mrama basi Serikali ikubali lawama.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli mbiu yake mpya ya hongera kwa kazi ina *stick sense of duty* kwa watu. Kwa hiyo, naona ni kauli mbiu mpya sisi tulikuwa tumezoea tunasema pole kwa kazi, aah hongera! Hongera kwa Serikali, hongera kwako Spika kwa kazi nzuri nadhani tunasonga mbele haturudi nyuma, hiyo ndege nadhani imetake *off* vizuri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza Serikali kwa suala la chakula. Tulikukuwa na njaa mwaka ule uliopita na kwa kweli nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitaipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri iliyoifanya. Ninaona kweli timu hiyo iliyoko mbele hapo imejipanga vizuri ina *combination* ya uzoefu na utaalamu na suala la njaa lilishughulikiwa vizuri sana hasa kwenye maeneo yangu. Chakula kilifika japokuwa kulikuwa na tatizo la zabuni ni nani asafirishe hicho chakula mpaka kuwafikia watu. Lakini bahati nzuri chakula kilifika hakuna aliyekufa kwa njaa ila ninaomba warekebishe kwa hilo kwamba siku za usoni likitokea hilo tatizo basi wenzetu walirekebishe vizuri kwa sababu wazabuni walipewa bei ndogo sana katika kusambaza hicho chakula. Matokeo yake ni kwamba amepatikana mmoja tu, ni kama vile akawa anaitikia wito wa Serikali kwa uzalendo. Sasa *over straight* ya chakula sehemu zingine chakula kikachelewa, ikafika mvua ikawa sehemu zingine hazipitiki lakini watu walipata chakula kwa baiskeli, walipata chakula kwa punda basi mradi watu walibahatisha. Sasa tunaomba siku za usoni tunavyokwenda tuone kwamba chakula hiki kinasambazwa mapema na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ninalizungumzia hilo kwa sababu Wilaya yangu ni kati ya Wilaya ambazo zinaathirika sana wakati mvua zinaponyesha. Suala la miundombinu la barabara ni suala mtambuka. Chakula hakiwezi kutoka sehemu fulani kwenda sehemu fulani. Mimi nadhani wenzetu nao wangeliangalia hilo ili chakula kiweze kufika maeneo ambayo hakuna chakula. Tumeambiwa kwamba mikoa kadhaa inakuwa na chakula kingi, imetajwa hapa karibu mikoa sita au saba, chakula cha kutosha na ziada. Na mikoa mingine kama hiyo nayo itakuwa na chakula lakini haitakuwa na ziada. Sasa ikatajwa na mikoa mingine ambayo ina upungufu wa chakula. Tani milioni 11 zilivunwa, mahitaji ni tani milioni 10, kuna ziada. Lakini sasa hayo maeneo yenye chakula, chakula hicho kinafikaje katika maeneo ambayo chakula ni pungufu. Tatizo lipo hapo, chakula kipo Rukwa, miaka mingi Rukwa wanazalisha chakula kingi lakini namna ya kufika maeneo mengine ni tatizo. Sasa sijui tuna *balance* vipi hilo! Barabara zetu zote za mkoa, wilaya hazipitiki wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala lile liangaliwe kwa makini kwa maana kwamba barabara zetu ziweze kupewa kipaumbele ili tuweze kuhakikisha kwamba chakula kinasambazwa ipasavyo, vinginevyo tutaendelea na tatizo la ku-*import* chakula kama tulivyoona na kama tunaendelea kuona wakati chakula kipo nchini cha kutosha. Chakula chetu ni kizuri kuliko vyakula hivi tunavyoagiza vya kutoka nje hata *treatment* yake hatujui ni vipi lakini tunalalamika tunaagiza chakula kingi kutoka nje lakini chakula kilichopo ndani kinaoza au watu wanatumia njia zingine za kuweza kutoa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda kusisitiza jambo la pili kwamba tunasahau kwamba mkombozi wa kilimo ni jembe la plau. Tumepewa takwimu hapa kwamba asilimia 70 ya watu wetu wanategemea jembe la mkono. Asilimia 20 wanategemea jembe la plau na asilimia 10 wanategemea trekta. Sasa tatizo letu ni kwamba tunataka hawa watu asilimia 70 watoke hapo waende kwenye kilimo cha trekta. Miaka ya nyuma kilimo cha plau kilitiliwa mkazo sana. Katika maeneo ninayotoka mimi kuna tofauti kubwa ya watu wanaotumia jembe la plau na wanaotumia jembe la mkono. Mfano tunaotaka kuuweka ni sawa na mtu ambaye anatumia baiskeli sasa anataka kununua gari badala ya kununua pikipiki. Mimi nilifikiri ingekuwa *rational* huyu mtu anatoa baiskeli kama amefaulu ku-*save* basi ananunua pikipiki anakwenda ananunua gari. Hali kadhalika tungefikiria hivyo kwamba mtu anatoka kwenye jembe la mkono anakwenda jembe la plau, haina gharama wala *service*. Lakini trekta unahitaji *service, u*nahitaji mafuta, *repair*. Mbuga zetu wengine kule trekta mara nyingine inashindwa lakini tunahitaji dozi mbili tatu, za plau za ng'ombe unalima vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda kusisitiza kwamba Wizara ije na mkakati huo na kwa kweli hizi shilingi bilioni moja za kila mkoa kwamba zingelielekezwa huko watu wakakopeshwa kwa ajili ya kununua plau na maksai, wangetukomboa. Mfano uko wazi kwangu watu wanatajirika kwa sababu ya mifugo, wanaitumia vizuri. Ningelipenda mkakati huo uweze kuangaliwa tuweze kuona kama tunaweza tukasonga mbele, vinginevyo tutaendelea kuagiza chakula kila mwaka. Tumetumia shilingi bilioni 225 mwaka 2003, tukatumia shilingi bilioni 237 mwaka 2004, tukatumia tena shilingi bilioni 234 mwaka 2005 na sijui mwaka huu tutatumia shilingi ngapi. Lakini tunavyosisitiza

kwamba tuwe na chakula cha kutosha lakini cha ndani pia tukitumie vizuri katika kukiokoa na kukisambaza.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza pia kwamba tulikuwa na utaratibu mzuri sana hapo siku za nyuma wa wataalamu wa ugani. Lakini sasa hivi labda mmoja utamkuta kwenye Kata na tena huyu unamkuta ana-*combine* mifugo na kilimo. Lakini vijiji vyetu tuliendelea sana, wakati fulani walikuwepo Mabwana shamba; walikuwepo watu wanaotoa ushauri kuhusu mbegu, kuhusu upandaji kwa mistari na mambo kama hayo, lakini bahati mbaya nadhani imesoma mahali hapa kwamba Wizara imekuja na mkakati huo mimi nafikiri nichukue nafasi hiyo kama imefanya hivyo basi tuwapongeze kwa hilo wafanye vizuri ili watu waweze kupata ushauri wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya mazao hasa haya mazao ya mchanganyiko bado kitendawili. Katika maeneo yetu suala la *specilisation* tunashindwa tulime zao gani hasa. Mtu a-*specialised* , alime zao gani? Maana yake kila tunapojaribu *ku-specialised* mkulima anakuta anapata kwa wingi lakini bei inampiga chenga. Akilima alizeti soko hakuna, pili, kutokana na shida za mkulima mazao yananunuliwa pale mashambani hata kabla ya kuvunwa. Sasa anashindwa alizeti, mwakani analima dengu na dengu wanamuwahi huko huko nyumbani. Sisi dengu watu wananunua shilingi 80,000 kwa gunia, lakini sasa kweli hiyo ni bei halali kwa sababu yeye anakwenda kuuza kwa shilingi ngapi. Ni bei nzuri lakini watu watakimbilia kule nako kukawa na matatizo ya bei na bei nayo ikaanguka sasa wakakimbilia ufuta. Ningeliomba kwamba Wizara ije na mkakati mzuri wa kuweza kutuokoa kwenye suala hilo ili tuweze kuona, tuwe na uhakika tunalima hasa zao gani, eneo moja linalima zao na eneo lingine linalima zao gani. Kwa sababu watu wanafanya kama vile kubahatisha. Tulishukuru katika ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alituahidi kwamba tulime kwa wingi alizeti, ufuta na dengu, kwamba soko safari hii linaweza likawa zuri, tunaomba Serikali iweze kutupatia soko na ni matumaini yangu kwamba ahadi hii itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tulijitokeza kwa wingi sana kuitikia wito wa Serikali kulima zao la mtama. Watu walijitokeza kwa wingi kuitikia wito wa Serikali ili kujihami na tatizo la njaa na kweli mtama husitawi, lakini kama nilivyowahi kusema huko nyuma ni kwamba ndege *queleaquelea* likawa tatizo kubwa. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri yeye ni Mwenyekiti wa hiyo *Locust Commission* inayoshughulikia masuala hayo ya nzige na ndege lakini tulijionea wenyewe. Maana ndege yenyewe sijui ni moja au ngapi, kama Serikali haiwezi kuja na mkakati huo basi watu wamekata tamaa. Mimi mwenyewe Mheshimiwa Spika, nililima mtama vizuri sana lakini bahati mbaya ilibidi tugawane na ndege. Inakuwa adha kubwa, inakuja kugeuka *suddenly* sasa inakuwa *intensive* kwa maana ya kwamba sasa unashinda shambani kutupa makombora huku yanapiga miluzi na kadhalika, ni ghasia. Kijiji kizima ni miluzi lakini ndege ile ni *very effective* japokuwa ilichelewa ilipofika maeneo hayo na kunyunyuza ikawa *very effective*. Inaonekana kwamba kuna ufumbuzi wa suala hilo. Kwa hiyo, tunaomba msimu huu unapokuja tutakapokuwa tunatoka kulima tena mtama na uwele tungeiomba Wizara inayohusika iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka eneo la tumbaku. Gando wanalima tumbaku vizuri sana, lakini basi wakulima hao wawe *rewarded.* Mazao hayo yamelimwa kwa wakati sio ucheleweshaji tena wa malipo. Tani 80,000 zinatarajiwa kuvunwa hapa nchi nzima lakini Gandu ina *-contribute a lot of tobacco.* Sasa watu wawe *rewarded* kwa jasho lao mapema walipwe na wasisumbuliwe. Ningeliomba pia fedha za miradi ya kilimo katika Wilaya ya Manyoni, Wilaya ya Manyoni ni kubwa sana, fedha hizi zinazokuja ni kidogo na nyingi zinaelekezwa kwenye upande wa Bonde la ufa ambako rutuba hakuna. Sasa sehemu yenye rutuba kule hatupati fedha kabisa, ningeliomba suala hili liweze kuangaliwa ili tuweze kutusaidia. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii.

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Lwanji, namwita sasa Mheshimiwa Fuya Kimbita. Lakini kabla hujaanza kuongea nimeletewa ujumbe hapa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge mmoja ambaye mkoa wake sipendi kuutaja, anatoa ushauri kwa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda kwamba tatizo la panya wanamshangaa kwa sababu kwenye mkoa huo wa yule Mbunge mwingine panya ni kitoweo. Kwa hiyo, waambie watu wako Chunya, Songwe wachangamkie kidogo. *(Kicheko)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii tena ili niweze kuchangia katika Wizara yetu muhimu sana ya Kilimo. Mimi kwa kuunga mkono kwa ujumbe ulioupata basi tukaribishe hao ndugu zetu wanaofanya kitoweo cha panya kwa sababu tuliathirika sana na mapanya ya msimu huu kule kwetu hai Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza na ukiwa wa mwisho kweli mambo mengi yanakuwa yamekwishazungumzwa mimi nitagusia machache na yale mengine ambayo yamekuwa yameshazungumziwa. Niungane pamoja na wenzangu kutoa salamu za rambirambi, pole kwa misiba ambayo imeendelea kutukumba ikizingatia zaidi na Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hapa Marehemu Amina Chifupa, tunamwombea Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi kwani ni katika zile *digital*. Sasa mojawapo ya *digital* imeondoka na hivyo tunazidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo ni muhimu sana kama wenzangu walivyotangulia kuisemea. Sina wasi wasi na uongozi uliopo, Serikali imejipanga vizuri, yupo Mheshimiwa Waziri pale na Manaibu wake anayefahamu vizuri sana kilimo cha umwagiliaji kule kwangu Hai. Kwa hiyo, awali ya yote niunge mkono hoja hii na kuiombea kila la heri ili Mwenyezi Mungu atujalie tuweze kuendelea vizuri kwani mwelekeo ni mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwa ufupi ningeshauri tuachane na kilimo cha mazoea nikimaanisha kwamba tumezoea kulima kwa kutegemea msimu wa kilimo bila ya kuzingatia utaalamu. Ni muhimu sana kuzingatia utaalamu hasa kwa sisi ambao tuna maeneo madogo utaalamu ni muhimu sana. Wenzangu wamezungumzia sana mambo ya matrektra ni *mechanisatio,* nadhani pale Wizara ya Kilimo iko Idara nzuri sana inayoshughulikia *mechanisation.* Tukiwawezesha hawa wenzetu kwa maana ya kutoa

ule utaalamu wao kutoka kwenye vichwa vyao na kwenye vitabu ili ukapelekwa kwa wakulima wetu, kilimo kitabadilika sana hapa nchini. Ningependekeza basi kwa makusudi mazima kuwa Serikali ifungue vituo vya kukodisha matrekta maeneo mbalimbali nchini ili kwa wale wananchi ambao hawana uwezo wa kwenda kukopa au kununua trekta waweze kwenda kulimiwa na hivi vituo vidogo vidogo. Aidha, kwa kuwawezesha watu binafsi ambao wataweza kuwa na uwezo zaidi kwa ajili ya kwenda kuwalimia wakulima wenzao.

Hilo ningeomba tulizingatie ili tuweze kuinua hicho kilimo tunachokizungumzia. Upande huo huo wa *mechanisation* tunahitaji utaalamu. Nilikuwa nazungumza jana jioni na watalamu wengine wa kilimo, kumbe sio kila mahali unaweza ukapitisha ile *disc plough* kwamba kilimo unachokifanya ili kiwe kizuri, kuna utaalamu pia. Kuna mahali pa kuweka *disc plough* na kuna mahali pa kutumia zile *chisel* kwa maana ya kuhifadhi maji zaidi ardhini kwamba uhaba wa mvua unapotokea ile mimea itaweza kuendelela vizuri.

Kwa hiyo, utaalamu ni kitu muhimu sana na nikizungumzia humo humo kwenye huo utaalamu kuna mambo ya *crop population* ndani ya eneo la ardhi. Ni muhimu pia tukizingatia na wale wataalamu wetu basi tunaowatarajia waweze kuja kuelimisha wananchi wetu tukishirikiana nao kwa maana ya kupata *yeild* nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kilimo cha Umwagiliaji ni kilimo chenye manufaa zaid na wataalamu wanatuambia kwamba kilimo cha umwagiliaji madhara ya magonjwa ni pungufu zaidi ya kile kilimo kinachotegemea mvua. Kwamba magonjwa yanakuwa yamepungua zaidi wakati tunapolima, si wakati wa mvua. Sasa kwenye kilimo cha umwagiliaji tunashukuru *scheme* mbalimbali tumeziona, lakini tulibahatika kuona kule kwa wenzetu China. Kule kuna umwagiliaji wa kuweza kusafirisha maji labda unayapitisha mahali ambapo kuna magadi. Si lazima sana kujenga hizi *structure* za *concrete,* kuna kutumia hata hizi *polythine bets* kiasi cha kuweka udongo na kutayarisha vizuri maji yanapita tu kwenye zile *polythine layers.* Badala ya kutegemea sana kwamba tuweze kuwa na uwezo mkubwa sana wa kujenga *concrete structures* ambazo wataalamu wetu wa kilimo upande wa umwagiliaji nafahamu wanafahamu vizuri, ni kuwapa fursa tu wakaweza kutoa hayo mambo kwa wananchi wetu ili waweze kutumia hiyo njia nyepesi lakini kwamba itakuwa na matunda mazuri sana mbele ya safari yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kilimo tumesisitiza kilimo kwa nchi nzima, mazao mbalimbali, lakini linakuja tatizo kubwa sana la soko. Soko linakwamisha sana wakulima wetu, mimi ningependekeza tuwe na Bodi kama wenzangu walivyotangulia kusema ya kushughulika na mazao ya nafaka ili kulinda bei za wakulima wetu. Pia nishauri kwamba itokeapo mikoa ya mipakani inapojaliwa kuvuna zaidi, tusiwazuie kuuza, wauze kwa sababu kwa wenzetu wakiuza wanapa pesa nzuri zaidi ili waweze kujiandaa kwa kilimo kikubwa zaidi kwa msimu unaofuata. Hapo nitatoa mfano wa kule Jimboni kwangu Hai. Mwaka juzi tulijaliwa kuvuna lakini kutokana na taratibu zilizokuwepo hatukuweza kuuza na wakulima wengi sana walibakiwa na kiasi kikubwa sana cha mahindi ndani ya majumba yao na mengine yaliharibika. Bahati mbaya mwaka huu huenda mavuno yasiwe mazuri sana kiasi kwamba wangekuwa wamejaliwa kuuza

wangekuwa na kiasi kikubwa cha akiba ya fedha ambayo ingewasaidia kununua mazao ya chakula.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na katika kuuza kwa wenzetu ni hesabu za kibiashara tu. Tunapouza nje ya nchi kwa bei kubwa zaidi lakini tungekuwa tunahitaji chakula sisi, endapo tutaagiza ina *bulk* tutaagiza kwa bei ndogo zaidi. Kwa hiyo, mimi sioni sababu ya kuwazuia wakulima wetu wakati tunaweza tukaagiza nje in *bulk* kwa bei rahisi zaidi wakati sisi tunauza kwa bei ya juu zaidi. Kwa hiyo, ningeomba kwamba tusiwazuie wananchi wetu kuuza pale ambapo wanajaliwa kuvuna ziada. Ni muhimu tuwaeleza umuhimu wa akiba ya chakula ili tusikumbwe na njaa, hilo naomba tulizingatie. Pia niombe kwamba, kwa sababu nimeulizia kuhusu hii akiba ya chakula tunayokuwa nayo hapa nchini, nikaambiwa ni Sheria iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, ningeomba basi tulete Sheria ambayo itatusaidia kuongeza kiasi cha hifadhi ya chakula hapa nchini. Kwamba tuwe na tani nyingi zaidi za hifadhi ya chakula ili kwamba tunapopata hii shida ya chakula tusibabaike sana, tuwe na akiba ya kutosha. Wenzangu wamezungumzia na mimi ningeomba nisisitize hilo kwamba tulete ile sheria ili tuweze kubadilisha hiyo sheria na tuwe na hifadhi kubwa zaidi ya chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo ni hayo, pamoja na ya wenzangu wale waliyoyazungumza ningeomba yazingatiwe. Nikija kwa upande wa Ushirika, Tanzania tulianza na ushirika mzuri sana. Tumekuwa chimbuko la Ushirika hapa Afrika Mashariki na Kati, enzi na enzi, nadhani na nchi jirani wakawa wanakuja kujifunza hapa, kuna mahali tukatetereka kidogo Ushirika wetu ukafa. Sasa sisi ndiyo tunaenda kujifunza tena kwa wenzetu ambao walijifunza hapa kwetu. Tulipokwenda kombo kidogo naomba tujirekebishe ili tuweze kuwa na ushirika mzuri ambao utaweza kuleta manufaa na tija kwa wananchi wetu. Lakini ningeomba tuwe wakali zaidi, kwa sababu ushirika umewakatisha sana tamaa watu wengine kwa sababu ya ubadhirifu. Kulikuwepo na baadhi ya viongozi kwenye vyama vyetu vya ushirika waliougeuza ule ushirika kama mali binafsi, kampuni binfasi. Wamekula wameshiba kwa maana ya kuiba lakini tunachelea sana kuwachukulia hatua. Ningependekeza basi wale ambao watagundulika kwamba wamefilisi ushirika lakini mali wanazo tuzichukue zile mali pamoja na kuwashitaki. Sheria iwe kali kabisa ili tusiendelee kukatisha tamaa wananchi wetu juu ya ushirika kwani ushirika ndiyo mkombozi wa wakulima. Awe mkubwa au mdogo bila kuwa na ushirika mkulima atayumba sana. (*Makofi*)

Sasa hii elimu ya ushirika, wenzangu wamezungumzia kuhusu wataalamu wa ushirika kuwa ni wachache. Pamoja na uchache huo tumesikia vizuri sana Mheshimiwa Waziiri anavyokusudia kuongeza hawa wataalamu wa ugani, nadhani na ushirika nao wataongezwa lakini pia basi niombe pia na sisi Waheshimiwa Wabunge tujumuike pamoja na wenzetu kwenda kuelimisha wananchi wetu na kuwashawishi na kueleza umuhimu wa ushirika. Pale ambapo elimu ni ndogo tuweke jitihada zaidi tuweze kufufua ushirika na kwa maana ya kuunda hizi *SACCOS* ambazo zinasaidia sana wananchi pale ambapo zimekwishaanzishwa. Kwa hiyo, ningeomba hii elimu tushiriki pamoja na sisi na kuomba ubadhirifu ndani ya vyama vya ushirika udhibitiwe kwa nguvu zote vinginevyo tutakuwa tunazungumza tu ushirika watu watajineemesha pasipo kuchukuliwa hatua ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia hayo ya jumla, sasa nijikite kule Jimboni kwangu Hai ambapo nawashukuru sana wale wananchi kwa kunichagua na kuchagua Chama cha Mapinduzi. Ukweli ni kwamba wanakiri mabadiliko yamekuwepo baada ya kuwa kwenye vipindi viwili vya upinzani. Sasa hivi muda mfupi sana tangu uongozi wa CCM uchukue madaraka katika Awamu hii, wananchi wanaona mabadiliko makubwa sana, na mimi napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwao na kuendelea kuahidi kwamba tutashirikiana pamoja ili kuleta yale maendeleo. Hata hivi tunavyoenda kuunda Halmashauri nyingine baada ya wenzetu Siha watakavyokuwa na Halmashauri yao sasa tutakuwa na Halmashauri yetu pekee ya Hai, tutaendelea kujipanga vizuri kwa ajili ya kuwahudumia vizuri sana na kuhakikisha kuwa kila kile kinachokwenda kwa ajili ya mwananchi kinamfikia mwananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika kule Wilayani Hai kuna jiografia aina mbili kwa maana ya maeneo ya miinuko na tambarare. Kule milimani tunalima kahawa, migomba, mboga mboga na kuna matunda wanaita maparachichi na ma-*ovacardo*. Sasa hiki kilimo cha kahawa ambacho kimesaidia sana uchumi wa nchi tangu hapo tulipopata uhuru wetu, nimekuwa nikizidi kuomba siku zote tuzidi kuimarisha taasisi yetu ya *TACRI* kwa maana ya kwamba iwezeshwe zaidi kufungua bustani mama katika kila kijiji ili ile miche iweze kupatikana kwa wingi zaidi.

Kuna utaalamu pia tuendelee kufundisha wale wananchi wetu waache kilimo cha mazoea. Siku hizi kuna mashine ambapo unamenya ila kahawa bila hata kuivundika ili uioshe moja kwa moja, unakwenda kuianika na kuweza kupata *quality* ya juu zaidi. Kama tunavyofahamu kwamba kwenye kahawa vitu vichache sana vinaweza vikaharibu ubora wa kahawa, vumbi, moshi labda na harufu nyinginezo ambazo zinashusa *quality* ya kawaha. Kwa hiyo, naomba wataalamu wetu wazidi kuja kwa wakulima wetu kwenda kuwafundisha zaidi ili tuachane na kilimo cha mazoea kwamba kuna utaalamu zaidi wa kufanya hicho kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maeneo yetu kule maeneo ya tambarare tunategemea zaidi pia na kilimo cha umwagiliaji ambacho pia nashukuru tulitembelea na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna *scheme* kule kwa Musa, Mheshimiwa Chiza anazifahamu sana. Tukiziimarisha zile *scheme* ni kwamba Hai tunaweza kujitosheleza kwa chakula na kuhudumia majirani zetu na kupata hata ziada ya kuuza nje ya nchi. Sasa mwaka jana tulitengewa pesa kwa ajili ya banio la Mijongweni, lakini lile banio pesa zilitumika kwenda kufanya kazi nyingine kutokana na hali iliyotukumba ki-nchi. Nimezungumza na Mheshimiwa Chiza kanihakikishia kwamba mwaka huu banio litapata fedha, nashukuru sana. Kwa hiyo, nakumbushia tu kwamba tusije tukalisahau lile banio la Mijongweni, ni muhimu sana kwa ajili ya umwagiliaji wa upande ule wa tambarare ambapo tunalima mazao mchanganyiko, mahindi na mazao mengine kwamba umwagiliaji kule unatuwezesha kulima mara tatu kwa mwaka.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kengele ya pili haijalia, ningependa nizungumzie ushirika pale Hai. Tunakwenda vizuri lakini kuna matatizo madogo madogo. Kuna matatizo kwenye vyama vyetu vya msingi, baadhi havifanyi vizuri, baadhi vinafanya

vizuri sana kushiriki pamoja katika kazi za wananchi. Kuna migogoro ya mikataba ambayo wenzetu waliingia na hao tunawaita wawekezaji. Tumeomba tuipitie ili mikataba kwa manufaa ya wananchi au wanachama wa vyama vile vya msingi. Kwa mfano, mgogoro wa *KCU* na chama cha msingi cha Lyamungo. Nimeandika pia kwa maandishi, tumefika mahali kwenye mazungumzo, lakini ningeomba basi na Wizara itusaidie tuweze kumaliza ule mgogoro kwa sababu wananchi wa Lyamungo wanalihitaji lile shamba kwa ajili ya shughuli zao za maendeleo. Nadhani halina mjadala sana kwa sababu haki ipo kwa ajili ya wale wananchi ambao ni wananchi wa kile chama cha msingi ambapo ningetegemea tulimalize hili suala haraka iwezekanavyo ili wananchi waweze kutumia lile shamba kwa makusudio yaliyopo kwenye mawazo yao.

Mheshimiwa Spika nisingependa kutumia muda mwingi zaidi kwa sababu mengi zaidi wenzangu wamekwisha yazungumzia. Lakini tuna fursa ya kipekee pale Hai, *Airport* tuliyonayo ya *KIA* ambapo tunaweza tukasafirisha sana mazao nje ya nchi ikiwa ni mboga, maua na kilimo cha mazao madogo madogo, kwa sababu tunayo fursa ya kuwa na barabara, maji umeme na *Airport* nzuri kabisa ambapo sioni sababu kwa nini tu-*export* maua yetu kupitia Nairobi na wakati *Airport* iko pale, ni kiasi cha kujipanga vizuri ili tuweze kuitumia vizuri ile *airport* kwa maana ya kuinua uchumi wa kanda nzima ya pale Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi naiunga mkono hoja hii. Mwenyezi Mungu awabariki sana na ninavyoona ni kwamba tunakwenda vizuri maadamu tutekeleze yale yaliyoandikwa humu yasibaki kwenye maandishi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA**: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ya kuchangia kama mchangiaji wa mwisho kama ulivyosema. Pili, niendelee kuwashukuru wananchi, wapiga kura wangu wa Jimbo la Singida Kusini kwa kunipa ushirikiano katika awamu hii ya pili. Naahidi kuwa tutaendelea kushirikiana kutekeleza malengo tuliyojiwekea. Tatu, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Manaibu wake wote wawili kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Ni matumaini yangu kwamba Wizara imepata Waziri na Naibu Mawaziri, na sio Mawaziri wamepata kazi isipokuwa Wizara imepata Waziri na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wangu, Mheshimiwa Parseko Kone kwa ushirikiano mzuri anaotupa sisi Wabunge wa Mkoa wa Singida. Tangu amekuja, amefanya kazi nzuri, naomba aendelee kushirikiana naye na kwa kweli anafanya kazi nzuri katika maeneo yote ya kilimo, elimu na kadhalika, nampongeza sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole na rambirambi kwa misiba yote iliyotokea kule Singida pamoja na Arusha na maeneo mengine yote yaliyotokea, naomba niwape pole wafiwa na niwaombee heri na subira kwa Mwenyezi Mungu. Ulinipa nafasi ya kuongoza msafara kwenda kwenye mazishi ya mwenzetu, marehemu Amina Chifupa, tuliifanya kazi hiyo kwa niaba yako na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa

naomba niwasilishe salamu na shukrani za mzazi wa marehemu Amina Chifupa Mpakanjia kwamba anashukuru sana Bunge, anakushukuru wewe, anaishukuru Serikali kwa ushirikiano na msaada mlioutoa katika kipindi kigumu cha kuomboleza msiba wa mtoto wake, naomba kuwasilisha salamu hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa niaba ya wenzangu niwashukuru sana viongozi tulishirikiana nao kule Mkoa wa Iringa Wakuu wa Wilaya wote na kadhalika. Wamefanya kazi nzuri wametusaidia vizuri na pongezi na shukrani za pekee zimfikie *DC* wetu wa pale Njombe, Mama yetu Rwegasira na vilevile *DC* mwenzetu tuliyekuwa naye hapa ndugu yetu Gembe ambaye ni *DC* wa Makete, kwa kweli walitupa ushirikiano mkubwa sana naomba niwashukuru kupitia kwako wapokee shukrani zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijikite katika kuchangia hotuba hoja tuliyonayo mbele yetu na mimi nataka nijielekeze sana kwenye Jimbo kwa sababu mambo ya jumla yameshazungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi na mimi sitaki kuyarudia sana. Kimsingi, Mkoa wa Singida unajilisha pale ambapo tunapata mvua ya kutosha ingawa tunapata mvua mara moja kwa mwaka lakini kama tutapata mvua ya kutosha Mkoa wa Singida sisi hatuombi chakula, sana sana tunawasaidia majirani zetu kuja kupata chakula. Ni pale tunapoathirika kwa njia moja au nyingine, ukame, mvua nyingi kama ilivyokuwa mwaka jana ndiyo tunapata matatizo ya chakula. Nashukuru kwa Serikali ilitusaidia chakula.

Lakini kutokana na mvua nyingi ambayo ilitokea mwaka jana yapo maeneo ambayo yameathirika sana na hayakupata mazao ya chakula kama inavyotegemewa wakati wote. Naomba kutaarifu hapa kwamba maeneo kama ya Kata ya Sepuka, Mgungila, Mwaru, Isuna na Kata ya Ikumbi, ni baadhi ya maeneo ambayo yameathirika kwa chakula, na ningeomba Serikali ifanye utaratibu wa kutusaidia na kwa kweli yameathirika kama nilivyosema kwa sababu mvua ilikuwa kubwa, ndiyo maana imeathiri jitihada ambazo zilikuwa zimefanywa na wakulima wetu. Lakini nasema kama si matatizo hayo sisi Singida tunajitosheleza.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kusema kwamba ukiacha habari ya mvua iliyokuwa nyingi lakini wakulima wameathirika sana na matatizo makubwa matatu. Tatizo la kwanza ni ndege waharibifu. Yupo Mbunge mwenzangu mmoja amezungumzia kuhusu habari ya ndege waharibifu. Sisi tunaathirika sana na ndege waharibifu na hili nilishawahi kulisema hata katika Bunge wakati ule wa awamu ya pili. Kwamba kwa kweli ni vizuri Serikali ikajua kwamba hili ni eneo ambalo linaathiri jitihada za wananchi na wakulima wetu Mkoani Singida, vijiji vya Ihombwe, Mwaru, Ihanja na maeneo mengi tu. Kwa hiyo, ndege ni wengi sana na kwamba kama Serikali haikuchukua hatua ya kuleta ndege kuja kunyunyiza zile dawa tutaendelea kuathirika.

Nishukuru kwamba mwaka huu ndege ya kunyunyiza dawa ililetwa lakini imechelewa. Mwezi wa nne mazao yameshaathirika tayari na mimi nilisema katika awamu iliyopita kwamba hili liwe ni zoezi la kudumu katika Wizara ya Kilimo, wanajua sisi tunaanza kulima mwezi wa kumi na moja au wa kumi. Hawana sababu ya kusubiri

mpaka tuwaambie jamani huku tumeathirika, wako wataalamu wamejipanga, kwanini wangojee mpaka wananchi walalamike.

Kwa nini wao wasielewe kwamba lipo tatizo pale. Ikifika mwezi wa kwanza au wa pili wawe wanajua kwamba Singida ni moja ya eneo ambalo linaathirika kwa ndege, wapeleke ndege zile kwenda kuangamiza ili kuokoa jitihada za wakulima. Vinginevyo wakulima wanaona kama vile hatufikishi malalamiko yao, hatuwasaidii wakulima juu ya jambo hilo, na kwa kweli inakwamisha na mnawataka walime lakini wanaathirika na ndege waharibifu. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara iweke katika mipango yake kwamba hili ni zoezi la kudumu, wasingojee kuambiwa wala kupewa taarifa, ikifika ni mawasiliano kati ya Wizara na Uongozi wa Mkoa au Wilaya yetu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo wako wanyama wakali, yupo simba kule, tembo hao mnaowaita ndovu. Wapo wanyama wakali kwa maana ya simba, tembo kwa lugha ya hapa ni ndovu, wanasumbua sana hawa wanyama. Licha ya kwamba wanaua wananchi, wako wananchi kadhaa ambao wamepoteza maisha yao kwa sababu ya simba au ndovu na Serikali inajua na Serikali ya Mkoa inajua. Ni kweli Serikali ya Mkoa imepeleka wale maafisa wake kwenda kuifanya hiyo kazi lakini tayari athari imeshatokea. Kwa hiyo, ninachosema licha ya kwamba tunapoteza maisa ya wananchi wetu kwa sababu ya simba na tembo katika maeneo hayo ya Ihombwe, Mwaru, Ihanja Isuna na kadhalika, lakini vilevile wanaharibu sana mazao yanaathirika sana. Kwa hiyo, wanakwamisha jitihada hizi ambazo zinafanywa na wananchi. Naiomba Serikali hili nalo waliangalie namna ya kufanya. Wananchi wanalalamika sana habari ya kufidia kutokana na hao tembo au ndovu, lakini mpaka sasa kumekuwa na kigugumizi kwenye Serikali kuwafidia wananchi wale wanaouawa au kufidia mazao yanayoharibiwa na hao wanyama. Mimi nadhani iko haja kwa Serikali kuliangalia hili vinginevyo kwa kweli wananchi watakata tamaa.(*Makofi*)

Maana yake wameanza kusema, “tunalima, ndege wanakula, tunalima, ndovu wanaharibu, kuna sababu ya kuendelea kulima!” Mimi ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho jambo hili aliangalie vizuri tuone kwamba tunapata maelezo ya kutosha na wananchi wasikie jambo linalofanyika.

Mheshimiwa Spika, yako maelekezo kwamba kwenye maeneo kama ya kwetu, tulime sana mtama tusilime mahindi kwa sababu tunapata mvua kwa uchache. Lakini wakinamama watu wazima hawa wakongwe na wazee wanasema, sisi kazi ya kulinda ndege hatuiwezi na nyie tukiwaambia leteni ndege yenu haiji kwa wakati unaotakiwa.

Kwa hiyo, sisi mnapotuambia tulime mtama tunapenda lakini hatuwezi hivyo tutaendelea kulima mahindi. Kama kweli Serikali ina nia kwamba tulime mtama zaidi basi ni vizuri isaidie ndege ije ili akinamama hawa wasiendelee kulalamika kwa sababu uwezo hawana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 , Serikali ilitoa ahadi kwamba limepatikana soko la mtama mweupe kule Italia na kwamba sasa fursa hiyo ipo na kwamba wananchi walime na sisi tumekwenda kuwatangazia wananchi walime mtama

mweupe. Sasa wanalima sana mtama mweupe lakini habari ya soko la Italia halipo, hakuna kitu! Lakini nasema Serikali mnatuweka mahali pagumu sisi Wabunge. Haya mnayoyasema hapa sisi tunayachukua tunakwenda kuwaambia wananchi. Yasipotekelezwa mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na mwaka wa tatu, tunapata kigugumizi katika kujibu limefikia wapi!

Ningependa nipate maelezo hapa leo wakati wa kufanya majumuisho ya Wizara hii ili kusudi wananchi wasikie na mimi pia nisikie nikawaambie soko la mtama mweupe ambao liliahidiwa na Serikali mwaka 2003/2004 na wananchi wa Singida sasa wanalima, umejaa mtama unaharibika , sasa soko lake limefikia wapi? Tusiwe na utaratibu wa kuahidi vitu wakati hatuna uwezo wa kuvitekeleza, mnatupa kazi ngumu sisi Wabunge kwenda kutoa maelezo ambayo hatunayo.

Mheshimiwa Spika, Ushirika ni jambo muhimu, ni nyenzo nzuri ya kumkomboa mwananchi. Lakini kwa Jimbo langu na Singida kwa ujumla, kwa kweli vyama vya Ushirika na *SACCOS* ni vigumu kuundwa. Kwa sababu pale kwenye Halmashauri yangu wapo maafisa wawili wa ushirika. Sasa hawa maafisa wawili wa ushirika kwa Wilaya kubwa kama ile ambayo kila siku tunaomba muigawe na nyinyi hamtaki kuigawa sijui kwa sababu gani, tunaambiwa yapo maombi mengi! Maombi mengi yanatoka wapi? Sisi Mkoa wa Singida ndiyo mkoa peke yake ambao haujaguswa. Mikoa mingine yote imeshaguswa, msitulinganishe na mikoa mingine.

Mkoa wetu ndiyo Mkoa peke yake ambao haujaguswa katika kugawiwa, mnapotulinganisha na Mikoa mingine ambayo imegawiwa sisi hatuwaelewi. Sasa nasema katika suala la ushirika maafisa wawili hawatoshi. Naomba Wizara hii ifanye utaratibu wa kutusaidia maafisa ushirika wengine ili kweli vyama vya ushirika viundwe, *SACCOS* ziundwe vinginevyo hata habari hii ya kwamba kuna fedha za JK shilingi bilioni moja wataishia kupata watu wa mjini, watu wa vijijini hawawezi kupata kwa sababu hakuna *SACCOS* wala hakuna vyama vya ushirika.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeshatenganishwa siku nyingi sana na Wizara ya Mifugo lakini mpaka leo unaambiwa Afisa Kilimo, Afisa Mifugo wanachukua *role* zote mbili. Mimi nadhani wakati umefika sasa maadamu Wizara ya Kilimo ipo peke yake na Mifugo ipo peke yake hawa nao watenganishwe.

Pawepo Afisa Mifugo na Afisa Kilimo ili kila mtu awajibike katika eneo lake na ataweza kufanya vizuri zaidi na ufanisi utapatikana vizuri zaidi kuliko kuchanganya Afisa Kilimo na Afisa Mifugo kwa wakati mmoja. Maadam Wizara zimeshatenganishwa naomba na huku chini nako watenganishe ili kuwe na ufanisi mzuri hawa *extension officers* katika sehemu zetu mbalimbali wanazozishughulikia.

Mheshimiwa Spika, sisi tunapata mvua mara moja kwa hiyo tunapozungumzia suala la umwagiliaji mimi nadhani maeneo yale ambayo yanapata mvua mara moja ndiyo maeneo ambayo yanastahili kufikiriwa zaidi kuliko maeneo mengine. Kwa hiyo, *scheme* zilizoko Mkoa wa Singida maeneo ya umwagiliaji ambayo yapo kule Mkoa wa Singida

kama kule Mang'onyi, Puma, Ihanja, yapo maeneo mazuri ambayo yanastahili kupata umwagiliaji kupata msaada na vifaa kwa ajili ya umwagiliaji.

Niiombe Wizara hii kusaidia sana Mkoa kama wa Singida ambao unapata mvua mara moja, upate afueni kwa sababu ya kutumia kilimo hicho cha umwagiliaji katika sehemu zile ambazo zinafaa kwa ajili ya umwagiliaji kama ambavyo nimetaja.

Nashukuru Mang'onyi wameendelea kutusaidia, matumaini yangu ni kwamba mwaka huu wataendelea kutusaidia ili *scheme* ile imalizike na wananchi wale ambao walikuwa wanapata manufaa na ile *scheme* waweze kufaidika na *scheme* hiyo. Lakini nasema ni vizuri tushirikiane kwa kweli ili tubainishe sehemu hizo na tumebainisha, na sisi tuweze kufaidika. Vinginevyo tutaendelea kupata mvua mara moja na kama mvua haikupatikana tutaendelea kuomba chakula na mnasema sisi watu wa Singida tunaendelea kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zao la alizeti ndiyo zao ambalo linastawi. Mimi nashawishika na maoni ya mtaalamu fulani alisema kuwa wakati umefika Tanzania sasa tuanze kufanya *specialization* ya kilimo. Singida alizeti inastawi, karanga zinastawi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Missanga ,ahsante sana. Nadhani Singida Kusini wamekusikia vizuri. Waheshimiwa Wabunge muda umebakia takriban dakika nne ambao haututoshi kuendelea na shughuli yoyote. Naomba nitangaze kwamba tutakaporejea saa kumi na moja nitawaomba Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara hii kuchangia. Mpangilio kwamba saa kumi na moja kamili Mheshimiwa Chiza ataanza, baada ya hapo atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David halafu mtoa hoja atamalizia kuanzia saa kumi na moja na nusu kwa muda wa saa moja. Kwa hiyo, saa kumi na mbili na nusu tutaingia katika Kamati ya Matumizi.

Nachukua fursa hii pia kuwakumbusheni Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia Jumatatu wiki ijayo tuna hizi Wizara ambazo ni za siku mbili mbili. Jumatatu tarehe 9 na tarehe 10 ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Tarehe 11 na 12 ni Wizara ya Miundombinu na tarehe 13 ambayo ni Ijumaa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwa hiyo, itaendelea hadi tarehe 16 Jumatatu ni Wizara ya Nishati na Madini. Nawatamkia hivi kwa sababu Saba Saba imefika sasa, msitokomee moja kwa moja mkasahau tena kwamba kuna Wizara kama hizi zinakuja. Baada ya kusema hayo naomba sasa kutangaza kusitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera kwa Bajeti nzuri ambayo inalenga kumkomboa mwananchi kutoka katika umaskini. Pamoja na mafanikio hayo naomba kutoa ushauri kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu usambazaji wa pembejeo. Naomba Maafisa Kilimo waandae semina na mafunzo mafupi kwa ngazi ya vijiji ili kuwaelimisha zaidi juu ya umuhimu wa matumizi wa kutumia mbegu bora na za kisasa, mbolea na dawa mbalimbali za kutibu mimea.

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo kwa kutumia zana za kisasa ndicho kitakachomkomboa mkulima. Wizara itafute matrekta ya bei ndogo badala ya haya yanayouzwa shilingi 35,000,000 si rahisi wananchi kumudu gharama zake. Nashauri Wizara ikopeshe matrekta kwa vijiji ambavyo vitakuwa vimeandaa mpango kazi au andiko ili ifahamike rasmi namna gani watarudisha fedha hizo. Kwa kufanya hivyo kilimo kitakuwa muhimu na kwamba hata vijana watapenda kulima kwa sababu watatumia muda mfupi na kuelekeza nguvu na muda mwingine katika shughuli zingine za maendeleo kama vile ujenzi wa shule, zahanati ama barabara. Bila zana za kisasa kilimo kwa kutumia jembe la mkono ni kuendelea kuchapa miguu badala ya kutembea mbele.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu kilimo cha mabondeni. Wizara imeonesha nia njema katika hili. Nashauri mikopo midogo itolewe hasa kwa vijana ili waanzishe kilimo cha mboga mboga, mpunga na mazao mengine. Pia naomba tuangalie zaidi namna ya kuwawezesha vijana wapate hamasa ya kupenda kilimo hasa cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, Shirika la Utafiti wa Miwa *(Sugar Research)* kwa jina la zamani Kibaha, kuna matatizo, kuna watu waliokuwa wanafanya kazi kwenye shirika hilo. Wafanyakazi hao walikuwa wanafanya kazi ya ulinzi kwa takribani miaka kumi na kumi na mbili, wafanyakazi hawa miaka yote hiyo walikuwa wanafanya kazi kama vibarua. Kwa miaka yote hiyo hawajawahi kusimamishwa kazi. Kwa bahati mbaya au kwenye mazingira ya kutatanisha walinzi hawa wamefukuzwa kazi bila ya kulipwa chochote. Wafanyakazi hao ni Samwel Shija, Saidi Kujumu, Said Onja, Rajabu Saidi na Ahmed Kiepele.

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo vielelezo vyote anavyo Naibu Waziri. Taarifa nyingine alipofika Waziri Mkuu pale Kibaha mwezi wa tano, malalamiko hayo yalijitokeza. Naomba Waziri aniambie jambo hili linashughulikiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri, matokeo ya utafiti unaofanywa wa mbegu yasiwekwe kwenye *library* za *Research Institute* tu. Nashauri kuwe na mashamba ya Serikali au watu binafsi ya mbegu. Hii itasaidia mbegu zilizozalishwa kwenye *Research Institute* zitapelekwa kwenye mashamba ya kuzalisha mbegu. Mbegu zitakazozalishwa zitasambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara itutangazie bei ya fidia ya miti kwa mfano, minazi, mikorosho, miembe na kadhalika. Kama ikikatwa kwa mfano kutengeneza barabara. Pia nashauri ili tuwasaidie wakulima wetu kwa kuwaiga wakulima wa Bangladesh. Bangladesh kuna ushirika wa watu wanafanya shughuli zinazofana, mfano, mkulima anapewa mkopo wa pembejeo. Ndani ya ushirika huo kuna wataalamu wa kilimo. Mkulima katika kupewa mkopo anapewa mkopo na kumlipia mtaalamu. Ndani ya ushirika huo pia kuna wanunuzi, wanakopeshwa pesa za kununua mazao na kukopeshwa mashine ndogo ndogo za ku-*process* na kupaki mazao hayo na kwenda kuuza. Kwa hiyo, ushirika mmoja unakuwa na wakulima wanakopeshwa kutokana na mahitaji yao, kunakuwa na wataalamu wa kilimo kuwapa ushauri wakulima. Wanaweza kukopeshwa pikipiki, baskeli kwa mfano kwa kuwafikia wakulima. Pia kunakuwa na wanunuzi wa mazao ambao hukopeshwa pesa za kununulia mazao au mashine ya kupandisha thamani ya mazao walizonunulia. Kwa mfano, matunda. Wanunuzi wanakopeshwa mashine ndogo ndogo za kutengeneza *juice* na ku-*pack*.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika aliyoitoa Bungeni siku ya tarehe 5 Julai, 2007.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imelenga sana kuinua kilimo hapa nchini. Kutokana na Serikali kuweka mkazo juu ya kilimo na mkazo mkubwa unatakiwa ili kuhakikisha kuwa fedha hizi zinazopelekwa Wilayani zinatumika katika malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nianzie na suala zima la pembejeo za kilimo hasa *sulphur* kwa ajili ya kupulizia mikorosho. Ni kweli kwamba mwaka 2006, Serikali ilitoa ruzuku kwa ajili ya *sulphur* na dawa nyingine ambazo zinahusiana na kupulizia mikorosho.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembejeo hiyo yenye ruzuku ya Serikali ilisaidia sana kupunguza ukali wa bei. Tatizo kubwa ni kuwa pembejeo hizo zilifika katika maeneo yale ya barabarani (Miji) na kusahaulika maeneo ya vijijini. Aidha, wakulima wadogo wadogo iliwawia vigumu kuweza kupata pembejeo hizo zenye ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, naiomba Serikali itoe maelekezo ya kutosha kwa mawakala kuwa pembejeo hizo ni kwa ajili ya wakulima wote wakubwa na wadogo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya suala la ununuzi wa korosho. Kwa miaka mitatu mfululizo ununuzi wa korosho katika Wilaya ya Rufiji umekuwa na utata mkubwa na hali ilikuwa mbaya zaidi mwaka jana ambapo kiasi kilichonunuliwa ni kidogo mno na kusababisha maelfu ya tani kubaki kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ni kweli korosho hazikuwa nzuri kutokana na mvua kuanza kunyesha mapema kabla ya korosho kukomaa, lakini si kweli kwamba korosho zilikuwa

mbaya. Ushauri wangu ni kwamba ni vizuri kwa Serikali kuendelea kushinikiza wanunuzi waweze kununua korosho hizi hata kama ni ghafi kwa bei inayolingana na hali halisi ya korosho. Kitendo cha kuwaachia wakulima kuhodhi korosho hizi ghafi kunawakatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Spika, aidha, naiomba Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa korosho inanunuliwa kila mwaka, kwa utaratibu unaofaa ambao utawahimiza wakulima kuendelea kulima korosho na si kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa hotuba yake nzuri. Vile vile niwapongeze Naibu Mawaziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Wizara nzima kwa jumla kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi napenda nianze mchango wangu kwenye sekta hii ya kilimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo katika mchango wangu nitaigawa katika makundi mawili ambayo ni moja, kilimo cha mazao ya chakula na pili ni kilimo cha mazao ya biashara. Sekta hii inawezekana kabisa kuwa mkombozi katika kuinua uchumi wa nchi na pia kuondoa umaskini kwa wananchi wengi hususan wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana endapo yafuatayo yatatiliwa maanani, matumizi mazuri kwa wataalamu wa kilimo, elimu ya kilimo kwa wakulima wadogo, kuanzisha benki za maendeleo zitakazokuwa na viwango vya riba nafuu na marejesho ya muda mrefu na kutotegemea kilimo cha mvua, badala yake juhudi ziwe kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha mazao ya chakula, Jimbo la Korogwe Vijijini limebahatika kuwa na mabonde yenye rutuba ambayo kama yatatumika ipasavyo kwa kilimo cha umwagiliaji basi Korogwe haitakuwa na shida ya chakula kabisa. Matumizi bora ya mabonde haya yanaweza kuzalisha chakula cha kutosheleza Mkoa mzima wa Tanga na hata nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Korogwe Vijijini wanaishukuru Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kuahidi kujenga lambo katika Kijiji cha Mapangoni kwa nia ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo katika kipindi cha mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu sasa Serikali imeahidi kujenga bwawa kubwa katika Kijiji cha Manga Mikocheni, Kata ya Mkomazi kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Mkomazi/Mazinde/Mombo/Cheke/Makuyuni. Wananchi wa Korogwe Vijijini wanaiomba Serikali iharakishe taratibu za ujenzi wa mradi huu. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha wananchi katika maeneo hayo kulima mpunga, mahindi, maharage na mboga katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo cha umwagiliaji kiwe cha tija kwa mkulima na Taifa kwa jumla, ni lazima kiandamane na upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo na sio jembe la mkono. Bila shaka umefika wakati muafaka kuwawezesha wakulima wadogo kupata mikopo ya pembejeo na zana kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha mazao ya biashara. Korogwe Vijijini kuna mazao makuu matano ya biashara ambayo ni katani, chai, kahawa, korosho na pamba. Napenda nichangie kwenye zao la Mkonge. Hili ni zao ambalo halitegemei hali ya hewa. Zao hili limepokelewa vizuri sana katika Wilaya ya Korogwe hususan Jimbo la Korogwe Vijijini. Zao la mkonge wengi wamezoea kuwa ni zao la mabepari wa Kizungu au wakulima wakubwa. Wakulima wa Korogwe tumeifuta zana hii kwani zao hili hulimwa na wakulima wadogo wadogo katika mashamba yao wenyewe au katika vitalu vidogo vidogo wanavyogawiwa kutoka kwenye mashamba makubwa yaliyokuwa yanalimwa na *Katani Limited*.

Mheshimiwa Spika, mkonge ni mali ghafi ya bidhaa mbalimbali duniani kama vile karatasi, mbolea, dawa, pombe, mazulia, gesi, umeme na bidhaa mbalimbali za kuundia magari. Zao hili linaweza kwa kiasi kikubwa kuliongezea Taifa fedha za kigeni. Wakulima wa zao hili wanaiomba sana Serikali iwaunge mkono kwa kuwasaidia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ardhi wanayotumia ipimwe ili wapate hati za kumiliki na kuweza kupata mikopo, pili, kupatiwa mikopo ya riba nafuu na ya marejesho ya muda mrefu, tatu, zao hili huhitaji sio chini ya miaka mitatu ili uvunaji uanze na nne, Serikali isaidie katika uanzishaji wa viwanda vya kutengeneza bidhaa za mkonge kama vile gesi na umeme, mbolea, karatasi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali isikae pembeni na kuacha kusaidia ufufuaji wa mkonge na hasa kuwawezesha Wazalendo ambao wamejitokeza kwa wingi kulima mkonge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Peramiho nachukua nafasi ya pekee kumpongeza Waziri na timu yake na hasa Katibu Mkuu kwa ushirikiano wa dhati katika shughuli za maendeleo ya kilimo Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mkurugenzi wa Mfuko wa Pembejeo na *SCCULT* kwa ukombozi waliowapa wakulima wa Jimbo la Peramiho mkopo wa pembejeo. *SACCOS* zifuatazo zimeshukuru sana ni *SACCOS* Kata ya Tanga, *SACCOS* Kata ya Magagura, *SACCOS* Kata ya Likumbo, *SACCOS* Kata ya Ndongosi, *SACCOS* Kata ya Mpitimbi, *SACCOS* Kata ya Gumbiro, *SACCOS* Wanawake na *SACCOS* Vijana.

Mheshimiwa Spika, mchango wa fedha ya mkopo toka mfuko umesaidia kuleta mageuzi ya kilimo. Mkopo umerejeshwa vizuri tunaomba mtufikirie tena.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Akiba na Mikopo. Vyama hivyo vinatoa mchango mkubwa ingawa ni vichanga. Vimekuwa na mahangaiko makubwa ya kuviimarisha. Vinaweza kuwa njia bora ya mageuzi ya kilimo kwa kutoa huduma zifuatazo, masoko, zana bora za uzalishaji, pembejeo na kadhalika. Tatizo lililopo ni kwamba vyama hivi havina muungano unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kwa kuwa mwaka 2005 Wizara ya Ushirika na Masoko wakati ule ilipeleka timu mahsusi kuja kujifunza namna bora ya kujenga muungano wa vyama hivyo. Tungeomba ripoti hiyo itoke ili tupate njia muafaka ya kuvijengea uwezo vyama vyetu. Ripoti ilikuwa inatoa ushauri bora wa kuimarisha *SCCULT* ili itoe huduma bora ya kuvijenga vyama hivyo. Kwa sasa yako makampuni yamefunga mikataba na vyama vyetu na kuvifanya vyama hivyo kutoka na sauti ya kujipanua zaidi. Kwa sasa *SCCULT* ina mahusiano na vyama vikubwa kuanzia Afrika Mashariki - Afrika na dunia na kwa kazi kubwa iliyofanywa na *SCCULT* ni budi sasa Serikali tukaamua kuipa nguvu *SCCULT* ikasaidia kuviwezesha vyama vyetu.

Mheshimiwa Spika, maswali. Swali la kwanza, kiasi gani cha fedha kilichotengwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya mfuko wa pembejeo na kati ya kiasi hicho ni kiasi gani kitatumika kwa ajili ya ukopeshaji wa matrekta na zana nyingine bora za uzalishaji kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, *Vote 43* - Kifungu kidogo 4456 ni miradi mingapi katika kifungu hicho itatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea? Pia 4486.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba mwaka jana Serikali ilijitahidi kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweka mkakati maalumu wa mikutano ya wadau wa mazao kuweka malengo ya masoko na uzalishaji. Tunaomba taarifa ya mrejesho ya kutuwezesha kupima utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu pia ni kwamba bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa mbolea ya ruzuku. Tunaomba Serikali sasa itusaidie kufanya majadiliano ya namna bora ambayo wakulima watapata mbolea kwa bei ya ruzuku hasa vijijini na kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, nina ombi, tunaomba *SGR* waongeze vituo vya kukusanya na kuuzia mazao katika Jimbo la Peramiho katika maeneo yafuatayo, Wino katika Kata ya Wino ni karibu tu na barabara kuu ya lami ya Songea - Makambako; Gumbiro katika Kijiji cha Ngadinda, pia barabara kuu na Mpitimbi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ni kwamba ruhusa ya kuuza mahindi nje ya mipaka ya nchi iwe inatolewa kwa wakati ili kusaidia wananchi kujipatia mapato kwa wakati. Hiyo iendane na kutangaza mapema kiasi cha ununuzi kupitia *SGR.*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nitoe mchango katika hotuba nzuri ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza, niunge mkono hotuba nzuri iliyotoa ufafanuzi mzuri wa utendaji wa mwaka jana na hali ya mwaka ujao, naomba waendelee na juhudi waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie skimu za umwagiliaji kazi zinavyoendelea kujengwa katika Wilaya ya Misungwi ni ya kutia matumaini. Ushauri wangu ni kwamba ni vema Serikali ikawa karibu na wakandarasi ili ujenzi ukamilike kwa kiwango kilichotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umwagiliaji Mbarika ulioanzishwa na vifaa vikanunuliwa visivyokidhi uwezo, naomba Serikali ieleze ni mkakati gani uliopo kwa sasa kuhusu mradi huo kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya dawa za pamba ambayo bei yake ni kubwa, wakulima wamekuwa hawamudu gharama ya dawa kwani si rahisi kununua kwa bei iliyopo ukiwemo utaratibu wa kuyapata. Ni vema Vyama vya Ushirika vikahusishwa katika uuzaji wa pembejeo kama ilivyokuwa mwanzo, cha muhimu kuimarisha usimamizi tu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la maji kwa Kituo cha Utafiti Ukiriguru, ahadi ya Serikali ina zaidi ya miaka mitatu sasa naomba Serikali ifuatilie kwa karibu tatizo hilo liishe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maabara na huduma yake, watafiti wamekuwa wakilalamikia Bajeti wanayopewa ni ndogo. Serikali iliangalie suala hili kwa umakini kwani ni gharama kubwa kuanza utafiti upya wakati kuendeleza ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri juu ya Ushirika Kazi unavyoendelea, ni mzuri lakini juhudi zaidi ielekezwe vyama vya msingi ili viweze kujiendesha kwani kwa sasa baadhi ya vyama vya msingi vilishakufa. Ni bora sasa kuainisha vyama na wanachama hai waliopo. Vyama hivyo vitajenga *union* imara, naomba Serikali ifanye kazi hiyo ya kuviimarisha vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watumishi wa Ushirika, naomba waongezwe ili waweze kuwafikia kwa urahisi wanachama vijijini.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Idara ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao kwa kusikia kilio cha wana Misungwi kuhusu ndege waharibifu aina ya Kwelea kwelea. Watendaji wa Wizara waliwahi mapema na kuwadhibiti. Ahsante sana. Naomba Serikali iendelee na maandalizi ya kuwa tayari kwa mlipuko wowote unapotokea.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na mpango wa Serikali wa awali wa upembuzi yakinifu wa mmwaka 2007/2008 utakaochukua eneo la *(Ha)* 78,950 Misungwi ikiwa na eneo la *(Ha)* 4,450, hatua hii ni ya kutia moyo kwani Misungwi ni kame ana. Matunda ya skimu tumeyaona kwa Mradi wa Igongwa (Mabulei). Hivyo tunaahidi ushirikiano na wataalamu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie zao la pamba. Napenda kutoa ushauri kwa Bodi ya Pamba kusimamia ushindani uwe wa haki ili mkulima asipunjwe, mambo ya kuzingatia ni mizani zihakikiwe zisipunje wakulima, maghala ya kutunzia pamba yasakafiwe ili pamba iwe na ubora (usafi), wanunuzi watoe stakabadhi kuepuka malalamiko ya kuibiwa wakulima, wanunuzi au wale watakaopewa jukumu la kugawa mbegu wasambaze mapema wakati wakulima wana pesa za kununua na elimu itolewe kwa dawa kama ni zana mpya kwa kutumia sinema na vipeperushi. Hayo ni sehemu tu ya uboreshaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, sina budi pia kutoa salamu zangu za rambirambi kwa misiba ambayo ilitufikia katika Bunge hili. Kwanza kwa mpendwa wetu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia na wote waliofariki katika ajali za magari. Mwenyezi Mungu awarehemu kwa kuwapokea na kuwasamehe makosa yao. *Inshallah* awaweke mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, hoja iliyo mbele yetu ni ya kilimo. Katika sekta hii, mtazamo wangu pamoja na kuiona Wizara hii kama ni Wizara mama katika Wizara zote, iliyojaa wataalamu wenye sifa za kutosha, yenye Katibu Mkuu mahiri, ndugu Peniel Lyimo, nadhani wakijipanga vizuri mimi sina wasiwasi nchi yetu itaitwa ghala la Afrika kama vile ilivyokuwa Zimbwabwe miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii mipango yote ambayo wanaiandaa basi itekelezwe kama vile ilivyokusudiwa. Kwa mantiki hii, uwasilisho wa hotuba hii ya leo tutaihifadhi kwa kufuatilia utekelezaji wake mwakani katika Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha kilimo cha kujitegemea, wazo langu ni kwamba ungeandaliwa mpango maalumu wa kugawa kwa wakulima ekari zaidi ya mia tano na kukopeshwa matrekta ili iwe *pilot project* ya uzalishaji katika zao watakalopangiwa. Hii pia ingeweza kutoa ajira.

Mheshimiwa Spika, Balozi wa Japan aliyepita Bis Sato alisema: “Tanzania mtakamatana uchawi wa uchumi wenu na maendeleo yenu msipozingatia kilimo.” Hili alilizungumza Morogoro katika uzinduzi wa mradi wa mfano katika shamba la mpunga.

Mheshimiwa Spika, umeshafika wakati kwa Watanzania kupunguza maneno ya kujiliwaza na kujipa moyo wa kupiga hatua kwa kufanyakazi. Mimi ningefurahi sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika angeshauri Wabunge kila mwenye shamba la ekari elfu moja na kuonyesha hati angempatia trekta moja la mkopo. Mheshimiwa Waziri na watalaamu wake wabuni na kuonyesha njia katika ushawishi wa kilimo ili kipendwe.

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki litakuja tu pamoja na kwamba sio leo. Lakini lazima tujiandae na umiliki mkubwa wa mashamba kabla ya wageni kuja kufanya vitu vyao na wenyeji (sisi) kufanywa manamba. Hili nalo tulione na tujiandae nalo.

Mheshimiwa Spika, suala la kumsema vibaya Mtanzania kwa sababu ana ardhi kubwa ya kulima tuliache kabisa na badala yake tumpongeze na hatimaye tumuwezeshe aweze kuzalisha na kuajiri katika lengo la kuzalisha kwa ziada.

Waziri amesema ataandaa vijana wa kuja kuwa maafisa wa kuajiriwa kusaidia wakulima. Sina hakika vigezo vya vijana hao lakini naogopa kama watakuwa wamepitia vyuo vya kilimo au la.

Mheshimiwa Spika, kilimo kilikuwa kikipambwa kwa jina la uti wa mgongo, kipaumbele, mkombozi lakini bado *impact* yake ni ndogo na mvuto haupo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, atoe mfano kwa kutoa jina jipya la Wasira na hasira katika mageuzi ya kilimo na hili linawezekana kabisa, *it can be done, play our part.*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kilimo yaende pamoja na mipango mizuri, mbolea, dawa za kunyunyuzia wadudu, maandalizi ya helikopta kwa dharura na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lazima Wizara hii pia iombe ushirikiano wa mambo tofauti na *IFAD* ambayo naamini itasaidia sana kwenda na kasi ya hasira za kubadili kilimo kuwa mfano katika Wizara zote.

Mwisho, nashauri Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Naibu Mawaziri waizunguke Tanzania kwa maelekezo na kuona shughuli za kilimo zinahitaji nini.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naunga tena mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mlalo, upo mradi wa umwagiliaji wa Kitivo. Mradi huu umetelekezwa pamoja na kwamba Serikali na wafadhili walitumia fedha nyingi kuuanzisha na kuupatia vifaa vya thamani kubwa ili kuuhudumia. Utelekezaji huu ulianza pale ambapo bwawa lililokuwa likihifadhi maji kwa ajili ya mrdi huu lilipobomolewa na mvua kubwa zilizonyesha.

Mheshimiwa Spika, tangu hapo, huduma zilizokuwa zikitolewa zilianza kufifia, sehemu kubwa ya vifaa kama matrekta na kadhalika vikaondolewa na wakulima wadogo wadogo (wanaushirika) wakaachwa bila huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, nimeangalia kwa makini na kubaini kuwa mradi wa umwagiliaji wa Kitivo katika Jimbo la Mlalo haupo katika mpango wa Wizara na wala hautajiwi mahali popote.

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi wananchi wa Mlalo tunahisi kuwa Serikali kwa makusudi imeamua kuutelekeza mradi huu. Kwa dhati kabisa, ningependa Waziri atoe maelezo ya kutosheleza kwa wananchi wa Mlalo, ni nini hatma ya mradi wa umwagiliaji wa Kitivo uliopo Bonde la Umba katika Jimbo la Mlalo.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Wizara hii kwa hotuba ya Bajeti iliyoleta matumaini ya kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, napenda kuwasilisha hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Katika Jimbo langu nashukuru tunazo skimu saba za umwagiliaji ambazo ni Uwalaka, Savunda, Msemembo, Udimaa, Nyamagogo, Mtiwe na Ngaiti. Lakini skimu zote hizi hufanya kazi wakati wa msimu wa mvua kwa vile hakuna bwawa lolote la kuvuna maji ili yatumike wakati wa kiangazi. Eneo letu ni kame sana lakini wakati wa mvua maji mengi hupotea bila ya kuvunwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana mabwawa ya kusaidia skimu hizi yajengwe hatua kwa hatua. Hatua hii itaondoa kabisa tatizo la njaa linaloikumba eneo letu mara kwa mara na pia itaondoa umaskini kwa kuwa wakulima watavuna mara mbili au zaidi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu kilimo cha mtama. Eneo letu tangu miaka ya zamani tunalima mtama kutokana na hali ya udongo na uchache wa mvua. Lakini miaka ya karibuni kilimo cha mtama kimeachwa na kilimo cha mahindi kimeshamiri. Tatizo la kilimo cha mtama ni ukosefu wa mbegu bora, tatizo la Kwelea kwelea, ukosefu wa soko na kadhalika. Tunaomba Wizara isaidie kuondoa vikwazo hivyo na viongozi wa eneo hilo tutafanya uhamasishaji wa zao hili hususani mtama mfupi.

Mheshimiwa Spika, tatu kuhusu zana za kilimo. Katika Jimbo langu 90% ya kilimo kinatekelezwa kwa zana duni ya jembe la mkono. Eneo hili la zana linahitaji mapinduzi ya haraka. Jembe la kukokotwa na ng'ombe (plau) lingekuwa hatua ya awali ya mapinduzi hayo. Kupitia *ASDP* tunaomba wakulima wakopeshwe plau kwa masharti nafuu ili waachane na jembe la mkono. Aidha, uanzishaji wa kituo cha matrekta pia itawasaidia wakulima wengi uwezo wa kukodi matrekta. Ni mradi unaoweza kujiendesha wenyewe kwani huduma hii italipiwa. Katika Jimbo hili kuna matrekta matano tu. Hayakidhi mahitaji hata kidogo ya kuleta mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa *(SACCOS).* Wananchi wameitikia wito wa kuanzisha *SACCOS* kwa sababu ya kujikomboa na umaskini. Lakini Maafisa Ushirika hawana usafiri wa kuzifikia *SACCOS* na kuzishauri/kuzielekeza. Mbaya zaidi wakaguzi wa ushirika *(COASCO)* wana uzembe na ukiritimba wa hali ya juu. Vitabu vya *SACCOS* vikipelekwa *COASCO* huchukua hadi miezi sita bila kurudishiwa matokeo ya ukaguzi. Naomba dosari hii irekebishwe.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri binafsi pamoja na Wizara yake kwa hotuba yao nzuri ya Bajeti ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo inaleta matumaini makubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Sika, pamoja na mengi uliyoyasema kwenye hotuba yake, naomba kuongezea machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wadogo wadogo wa kilimo bado ni tatizo kubwa. Hii inatokana kwa kuwa ardhi ni mali ya wananchi, inakuwa ni vigumu sana wao kutoa ardhi kwa ajili ya kilimo. Hivyo nashauri kila kijiji kitenge maeneo ya ardhi kwa wakulima na nyingine kwa wawekezaji wengine ili waweze kulima.

Mheshimiwa Spika, pili, wakulima wetu wakati wa mavuno, wote huvuna kwa pamoja na hii husababisha bei kushuka na kusababisha kuuza mazao yao chini ya gharama halisi za uzalishaji. Kwa kuwa kila Wilaya ilishachagua mazao ya aina mbili zao la biashara na chakula, nashauri utaratibu wa stakabadhi za mazao uwepo nchi nzima au utaratibu mwingine wa kumsaidia mwananchi aweze kuuza mazao yake kwa faida kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukuarifu kwamba Mkoa wa Mara tunayo maeneo mengi ya kilimo ambayo ni mazuri ila yanahitaji malambo na makinga maji toka mito mbalimbali. Tunaomba mtusaidie katika Bajeti ijayo nasi tuweze kufaidika na mpango huo mzuri wa Serikali wa kusaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze wewe, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Spika, kutegemea misaada kutoka kwa wahisani kunaweza kuleta athari kubwa kwa kilimo na sekta nyingine mbalimbali za maendeleo. Hii inatokana na kuchelewa kupatikana kwa misaada hiyo na hata inawezekana kukosekana kabisa. Kwa

hivyo, ni vema kutegemea zaidi mapato ya ndani kutokana na vyanzo mbalimbai hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya kilimo yanaweza kufanikiwa kutokana na sera na dhamira ya kweli ya kukifanya kilimo kuwa ni kipaumbele katika nchi yetu. Kwa kuwa Tanzania ina mito mingi na mabonde makubwa kama vile bonde la Mto Rufiji, Kilombero, Ruvu na kadhalika kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji kunaweza kusaidia kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo na hivyo kuwa na uhakika wa chakula na kuongeza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mbolea inawafikia wakulima kwa bei mbaya, bei kubwa ambayo ni kinyume na matarajio yao. Jambo ambalo kwa namna moja au nyingine linadhoofisha wakulima na kilimo chenyewe. Je, Serikali kwa sasa ina mpango gani mzuri zaidi utakaohakikisha kwamba mbolea inawafikia wakulima kwa wakati na kwa bei nafuu iliyopangwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa asilimia kubwa ya wakulima katika nchi yetu wanaishi vijijini, je, Serikali haioni kuwa wakati umefika sasa kuwa na mtandao mzuri wa barabara hadi vijijini ili wakulima waweze kusafirisha pembejeo pamoja na mazao yao kwa haraka na kwa bei nafuu zaidi? Vile vile kuwaondolea au kuwapunguzia kodi katika baadhi ya mazao yao ili iwe ni motisha na hivyo kuwafanya wakulima waweze kuzalisha zaidi kwa maslahi yao na Taifa kwa jumla. Ahsante.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na timu yake kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika niliposoma katika hotuba yake ukurasa 44 Ibara ya 66 hadi 68 kuwa Wizara imebaini haja ya kuweka mkazo katika eneo la ugani. Eneo hili likifanyiwa juhudi, tutaweza kupiga hatua kwa kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Sika, hata hivyo, naomba sana Wizara iangalie umuhimu wa kupeleka watumishi wa ugani katika eneo la mwambao wa Ziwa katika Jimbo la Kigoma Kusini. Eneo hili ni maarufu kwa kilimo cha mpunga, mahindi, muhoga na matunda ya aina mbalimbali. Eneo hili katika shughuli za kilimo inaonekana uzalishaji ungekuwa maradufu kuliko ilivyo sasa kama wangekuwepo wataalamu wa ugani. Hivyo naomba Wizara itoe upendeleo wa binafsi na wa makusudi kupeleka watalaamu hao katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 52 umezungumzia zana za kilimo. Mara nyingi zana za kilimo zimekuwa zinadhaniwa kuwa ni matrekta tu. Nashukuru kwa *CARMATEC* kupewa jukumu la kubaini mahitaji. Ni vema mkazo uwekwe sana kwenye majembe ya kukokotwa na wanyama ambayo yana unafuu kuliko matrekta. Kutoka hapo wakulima wataongeza vipato na hatimaye kufikiria kununua matrekta.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kuondoa riba kwenye matrekta ili kilimo kipate sura halisi ya kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na kupata fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii nyeti katika nchi yetu kwa mwaka huu wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Christopher Chiza na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David. Hali kadhalika niwape hongera kwa kazi nzuri Katibu Mkuu wa watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara kidogo. Lakini ni ukweli ulio wazi kwamba zaidi ya asilimia 80 ni wakulima ambao wengi wa wakulima hawa ni wakazi wa maeneo ya vijijini na ni ukweli usiopingika kwamba kilimo kinachotumika ni kilimo duni cha kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri na ukweli usiopingika kwamba tegemeo na Pato la Taifa linaitegemea sana sekta hii ya kilimo. Wananchi walio wengi hawana shughuli mbadala isipokuwa wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2006/2007, sekta hii kupitia Bajeti ilielezwa kukua kwa 5.8% mwaka 2004, 5.2% mwaka 2005, kadhalika sekta ndogo ya mazao ilikua kwa asilimia 6.0 na asilimia 5.2 katika kipindi hicho na ilielezwa kwamba kasi hiyo ilikuwa ndogo katika kuchangia kuondoa umaskini na sababu kubwa zilielezwa ni kutokana na kuathiriwa na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama tunahitaji kuondokana na tatizo la njaa au kuongeza pato kwa mazao ya biashara ni lazima basi juhudi za makusudi zielekezwe juu ya ukulima wa kisasa, kutumia zana bora na kutotegemea mvua.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ikubali juu ya kuwekeza nguvu zake katika kilimo cha umwagiliaji. Serikali ihimize kilimo cha umwagiliaji kwa hatua za kutoa elimu kwa wakulima ili kutumia maji ya kuvuna yanayotokana na mvua ndogo tunazozipata.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kugawa miradi ya kilimo kwenye Mikoa, Wilaya hadi vijijini bado hauridhishi kabisa kwani miradi mingi inaelekezwa mahali ambapo pengine hapastahili. Maeneo ya Mikoa yenye ukame kama ilivyo kwa Singida, Dodoma, Shinyanga na Tabora, Mikoa hii ingepewa kipaumbele hasa kwa kupatiwa miradi ya umwagiliaji. Mikoa/Wilaya iwezeshwe na Serikali kwa kuchimbiwa malambo ambayo yatawezesha kuvuna maji yanayopatikana kwa mvua ndogo zinazopatikana katika msimu wa masika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara ilifanya upembuzi yakinifu na kusanifiwa kwa skimu zipatazo 62. Hakuna skimu yoyote katika Mkoa wa Singida likiwemo Jimbo langu la Iramba Magharibi. Kadhalika skimu saba zilitekelezwa chini ya *PIDP* lakini Singida wala Iramba hazimo na skimu za *DADPs* ni miradi mitatu tu ya Singida Mjini, vijijini na Iramba lakini Jimbo langu hakuna.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo za kisasa na kwa kutumia wakala ili wakulima waweze kukopa hazipo, bado wakulima wanategemea juhudi binafsi.

Mheshimiwa Spika, mazao ya biashara hayatiliwi mkazo zao kama alizeti, pamba, vitunguu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani hawatoshi, Wizara iajiri Maafisa Ugani hadi ngazi za vijiji na Kata.

Mheshimiwa Spika, Wizara ione uwezekano wa kusaidia chakula vijiji vya Jimbo langu ambavyo ndege waharibifu waliharibu mtama na hivyo kukabiliwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri na uwasilishaji mzuri. Skimu za umwagiliaji, Kiambatisho Namba 3 nadhani namba 9 na 10 zimechanganywa. Mapogoro iko Ileje, sisi hatuna Iyendwe Mbozi Kiambatisho Namba 4 ni skimu ya Mbebe ambayo iko Ileje. Mradi huu haujakamilika, unahitaji fedha za nyongeza kama shilingi 130,000,000 ili ukamilishwe pamoja na miundombinu yake. Nadhani nilimdokeza kwenye kikao Dar es Salaam. Mkandarasi anaendelea na kazi, kiambatisho namba 7, nashukuru kwa skimu ya Chitete iliyoko Ileje.

Mheshimiwa Spika, *intake* ya skimu hii ilibomoka mwaka jana na kuna haja ya kujenga *intake* mpya ili shughuli za umwagiliaji ziweze kuendelea vizuri. Natanguliza shukrani kwa ushirikiano wako.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika hongera, *you presented your budget very well.*

Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie tu kuwapa wakulima matumaini zaidi ili walime zaidi mwaka huu, bei ya pamba isikatwe. Pia kuna haja ya kuangalia *climate* changa *vs data* za kupanda. Wapewe *need to consider November* kama tarehe za kupanda. Nilisahau hili kwenye hotuba yangu. Ahsante.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu,

Naibu Katibu Mkuu na watengaji wote wa Wizara hii kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kule jimboni Mbozi Magharibi katika Kata ya Chitete, Tarafa ya Msangano, tarehe 24 Desemba, 2006 mradi wa umwagiliaji wa Naming'ango uliharibiwa na mafuriko makubwa. Baada ya hapo Wizara hii ilifanya tathmini ya gharama za hasara iliyotokea na kukisia kuwa ukarabati wake ungegharimu karibu shilingi 480,000,000.

Kwa kuwa mradi huu uliharibika siku sita kabla ya muda wa matazamio kumalizika, je, Serikali imemchukulia hatua gani mkandarasi ambaye kwa hakika hakuwa makini kuhakikisha kuwa nguzo za daraja la mradi huo zinakita kwenye mwaka; badala yake akaacha zinaning'inia kwenye mchanga. Je, ni lini mradi huu wa umwagiliaji utakarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa vile sasa pale ambapo daraja la mradi wa sasa lipo, kutokana na mto kutengeneza njia yake mpya ambayo ni pana kuliko daraja lenyewe, paachwe na kutengeneza daraja jipya na mabano sehemu iliyopo umbali wa mita 200 tu toka hapo. Hii ni kwa sababu mahali ninaposhauri pana upana mdogo na mwaka upo juu juu tu na ndipo toka enzi za mababu wananchi walikuwa wakitengeneza madaraja ya miti ambayo ilidumu muda wote bila kuharibiwa na mafuriko. Kwa taarifa yako mahali hapa ndipo wananchi waliwashauri wataalamu waliokwenda kusanifu mradi huu mara ya kwanza lakini wao wakapuuza na matokeo yake yakawa mradi mzima kusombwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia masuala yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, Wilaya ya Mpwapwa ina mabonde mengi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Bonde la Chamkoroma, Manghweta, Tubugwe (Kongwa), Bonde la Mlembule, Mwenzele, Nana, Tambi, Mbori (Matomobo) Inzomvu, Godegode, Lumuma, Malolo, Mbuga, mradi haujakamilika hadi sasa, utakamilika lini? Bonde la Lufusi katika Wilaya ya Mpwapwa, je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwa fedha na utaalam?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla unalima sana mazao ya biashara, karanga, ufuta na alizeti. Serikali iliahidi kuunda Bodi ya Mazao mchanganyiko lakini Bodi hiyo haijaundwa hadi sasa je, ni lini bodi hiyo itaundwa ili kusaidia wananchi wanaolima mazao hayo kupata soko la uhakika

la kuuza mazao yao. Kama karanga, ufuta, alizeti, mahindi, mtama na kadhalika. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoani Kigoma wananchi wake hawapati njaa misimu yote kwa sababu wana ardhi kubwa na yenye rutuba lakini kumekuwa na uhaba wa watumishi wa kilimo, Afisa Kilimo hasa vijijini, nilikuwa naiomba Serikali iweze kutupatia wataalamu mapema iwezekanavyo ili tuweze kulima na kupanda kiutaalamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna vijiji vingine ambavyo viko karibu na mto mkubwa ambao ni Mto Luiche. Wananchi wanaokaa karibu na mto huo ni Kamala, Simbo, Mwakizega, Kaseke na kadhalika. Je, ni lini Serikali itatuletea kilimo cha umwagiliaji? Ahsante.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri hata hivyo nnaomba nichangie maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo nchini kinakabiliwa na matatizo mengi sana. Tatizo moja linalokabiliwa na kilimo nchini ni upungufu wa watumishi. Kutokana na hali hii kilimo kina tija duni sana. Kanuni bora za kilimo hazizingatiwi katika mazao yote. Serikali haina budi kufundisha na kusambaza wataalamu wa kilimo katika vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine katika kilimo nchini ni zana duni zinatumika. Asilimia zaidi ya tisini ya wakulima wanatumia jembe la mkono katika kilimo chao. Kuendelea kutumia jembe la mkono ni kudumaza kilimo. Serikali ichukue hatua thabiti kuondoa jembe la mkono katika kilimo nchini na badala yake kuingiza zana za kisasa zikiwemo majembe ya kukokotwa na wanyama na matrekta madogo na makubwa.

Serikali isimamie uainishaji wa vituo vya zana bora za kilimo nchini zikiwemo matrekta madogo na makubwa ya kukodisha kwa lengo la kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kutegemea mvua pia ni tatizo kubwa katika kilimo cha nchi yetu. Asilimia kubwa ya wakulima wetu huathirika sana miaka inayokabiliwa na ukame. Njaa za mara kwa mara zinazosababishwa na ukame, wakati umefika wa Serikali kuelekeza rasilimali nyingi katika kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu ina maji mengi yakiwepo ya mvua, Mito na Maziwa. Aidha, nchi yetu imejaaliwa mabonde mengi na mazuri sana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa mfano bonde la Mto Bubu Wilayani Kondoa ni moja ya mabonde mazuri yaliyofanyiwa utafiti na kubainika kuwa ni eneo zuri sana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma ni kame sana tunaomba Serikali itumie utafiti huo kuanzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika bonde hilo.

Mkoa wa Dodoma ni moja ya mikoa ambayo hayana zao kuu la biashara. Hata hivyo wakulima wa Dodoma wameanza kulima mazao ya mbegu za mafuta kama karanga, ufuta na alizeti kama mazao ya biashara pamoja na kulima mazao haya lakini hawana utaalamu wa kuyaendeleza hivyo Serikali inaombwa kuwasaidia wakulima hawa utaalamu na masoko ya mazao haya. Aidha, Serikali inaombwa iwahamasishe wawekezaji kujenga viwanda vya kusindika mafuta mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma hauna chama kikuu cha ushirika. Tunaomba Wizara isimamie uzinduzi wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache naunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, *export levy* kwa wakulima wa korosho ipo vipi? Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa ununuzi wa zao la korosho hususan katika jimbo la Kilwa Kaskazini?

Mheshimiwa Spika, je, kuna mpango wowote wa kuanzisha Bodi ya Mazao yasiyo makuu kama ufuta, nazi, machungwa, ndizi na kadhalika?

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheishmiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nikaweza kuandika maoni yangu kuhusu hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kwamba kilimo ndio sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni dhahiri kwamba kilimo kinachangia asilimia zaidi ya 44 ya uchumi wa nchi. Hivyo, kwa mantiki hiyo, ni lazima itoe kipaumbele wa kipekee cha kuweza kukikuza kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo kiweze kukua na kiwe endelevu ni lazima Serikali itilie maanani yafuatayo, kilimo cha umwagiliaji, mazao ya chakula, mazao ya biashara, utafiti wa mazao, mfuko wa pembejeo, huduma za ugani, ruzuku ya mbolea na maendeleo ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, nchi yetu imebarikiwa sana kwa kuwa na mito mingi ambayo baadhi yake kama Ruvuma, Matandu, Rufiji, Ruvu, Wami na kadhalika haikauki hata wakati wa ukame. Lililobaki hapa ni umakini wa Serikali kutumia rasilimali hii ya mito kufanikisha kilimo cha umwagiliaji katika skimu walizoziandaa lakini hata kuongeza zaidi kwani Tanzania ina maeneo mengi na makubwa ambayo yanaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji ambacho ndicho kilimo cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, mazao ya chakula kama suala la umwagiliaji utatekelezwa kwa umakini mkubwa na taaluma inayohusiana nayo itatolewa kwa wakulima hata wale wadogo wadogo, basi uwezekano wa nchi hii kuweza kujitegemea angalau kwa chakula ungepatikana na hivyo tukaondokana na uwagizaji wa chakula tukabaki tu na uagizaji wa vifaa vya utendaji ambayo kwa kawaida havitengenezwi hapa nchini. Kwa hiyo, mkazo

uwekwe katika kufanikisha hili kwa manufaa ya kuzalisha chakula cha mahitaji hasa ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya biashara, mazao ya biashara ambayo yanaipatia nchi yetu pato ni pamoja na korosho, lakini tuone ni kiasi gani Serikali inashughulikia matatizo yanayolikumba zao hili la korosho. Miongoni mwa matatizo yanayoikumba mikorosho ni kama kukosekana huduma za ugani, kuchakaa kwa mikorosho, hakuna ruzuku ya dawa lakini kubwa na baya ni kwa hata hicho kidogo kinachozalishwa hakina soko la uhakika. Ni hivi juzi tu hapa Bungeni tumeelezwa kwamba wanunuzi wa korosho wananunua kwa bei ya shilingi 280/= lakini stakabadhi huandikwa shilingi 410/= au zaidi. Tunaitaka Serikali isimamie kero hizi kwa manufaa ya kukuza zao hili na kipato cha wakulima.

Mheshimiwa Spika, mazao mengine ni chai, kahawa, tumbaku, pareto, mkonge, pamba na kadhalika. Mazao haya yanayo matatizo mengi katika kuimarika kwake na kutoa mchango katika Pato la Taifa. Tunaitaka Serikali isimamie na itoe kipaumbele maalumu kama huduma za ugani, pembejeo, upatikanaji wa mbegu bora na kadhalika kwani wakulima wengi hawana kipato cha kufanikisha uzalishaji wa mazao hayo. Pia Serikali iangalie uwezekano kwa kueneza zao kama la pamba kwa maeneo mengi zaidi hapa nchini ili kuinua kipato cha wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti wa mazao, kwa kuwa mazingira yanabadilika kila leo hivyo hivyo sayansi na teknolojia, tunaitaka Serikali iendane na wakati katika suala hili la utafiti wa mazao kwa mujibu wa kubadilika kwa hali ya hewa, mazingira, sayansi na teknolojia. Vituo vya utafiti viongezewe fedha kwenye Bajeti, vituo vya utafiti viongezwe nchini, wataalamu wapatikane zaidi, lakini cha muhimu zaidi ni kwamba uwepo utaratibu mahususi wa kusambaza matokeo ya tafiti hizo nchini kwa manufaa ya kuongeza uzalishaji wa mazao husika.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani kama ilivyo ruzuku ya pembejeo ikiwemo mbolea, dawa na hata miche bora, inalalamikiwa sana karibu maeneo mengi nchini. Ni vyema Serikali iwe makini zaidi na kuona ni kwa namna gani itaweza kulipatia ufumbuzi. Lakini pamoja na kuongeza maofisa ugani, lakini maofisa wenyewe wawe tayari kufanya kazi kizalendo na hili la ruzuku nalo ni vyema Serikali ipitie utaratibu wake upya, ili ukubaliane na mahitaji halisi ya nchi kwa muda muafaka. Nakushukuru na ahsante sana.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa kueleza machache juu ya hoja hii na nichukue fursa hii kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake iliyotoa mwanga katika kuleta mageuzi ya kilimo kwa lengo la kuongeza kasi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 60,061,912,600 ni kidogo lakini wasiwasi wangu kuwa maendeleo yanayotakiwa hayawezi kufikiwa kwa asilimia zaidi ya 80 ya fedha za maendeleo ni fedha za nje,

zinazotegemea wafadhili na tukijua fika kwamba mara nyingi wafadhili wanachelewa kutupatia fedha hizo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa Bajeti ya Maendeleo tujibane na tulichonacho na tutumie fedha za ndani, kwani lengo lililokusudiwa linaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha maua bado hakijaeleweka vizuri katika jamii kubwa ya Watanzania ambapo kikitekelezwa vizuri kinaweza kukuza kipato cha wakulima na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Serikali ifanye jitihada za makusudi ya kuwawezesha wakulima kulima kilimo cha maua sambamba na kupatikana kwa soko lililo na uhakika. Uvunaji wa maji ya mvua, bado haujatekelezwa vizuri na wakulima katika maeneo mengi. Elimu juu ya uvunaji wa maji unapaswa kuboreshwa lakini ushauri wangu ni kwamba Serikali iwapatie nyenzo wakulima zitakazopelekea uvunaji wa maji ya mvua sambamba na matumizi bora ya maji hayo.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa kilimo, hauna budi kupewa nafasi kubwa ili kuweza kuibua mbegu bora ili kukuza kasi ya uzalishaji na kupelekea tija kwa wakulima kuongeza kipato. Vituo vya utafiti Mlingano, Uyole, Ukiruguru na Selian vizidi kuimarishwa na wataalamu wa utafiti wawezeshwe ili wawe na nafasi nzuri zaidi kutenda wajibu wao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya hali ya hewa ni jambo la kawaida, hivyo nashauri Serikali iwahamasishe wakulima kulima mazao yanayostahamili ukame kama mihogo, mtama, uwele na kadhalika, ili hata ukame ukiibuka basi hatuwezi kuwa na upungufu wa chakula, hivyo naishauri Serikali kufuatilia hali ya unyeshaji wa mvua zilivyo kwa tahadhari zaidi.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani ni jambo muhimu katika suala zima ya mageuzi ya kilimo. Maafisa Ugani ni kidogo ni vyema waongezwe, sambamba na kupatiwa vyenzo za usafiri kama magari na pikipiki ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi maafisa hao.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni vipi Serikali imeangalia Halmashauri zenye udhaifu wa kutumia fedha kupitia miradi ya *ASDP, DASIP* na *PADEP.* Nashauri Serikali kupeleka wahasibu wenye sifa kwenye Halmashauri kuepukana na uzembe na upotevu wa fedha za Serikali. Ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nipongeze Wizara kwa kazi nzuri sana ambayo imefanya katika sekta hii muhimu ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo kinachangia asilimia 40 ya Pato la Taifa letu, nguvu kazi kubwa ya kilimo ipo vijijini ambako ni 75% ya walioko vijijini ni wanawake na kuna hali ngumu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haioni haja ya kutafakari na kushirikiana na sekta ya kilimo na miundombinu ili kujenga miundombinu sehemu ambazo kuna uzalishaji mkubwa wa kilimo?

Mheshimiwa Spika, kilimo ni sekta muhimu sana lakini bado ina changamoto kadhaa kama ifuatavyo:-

Kwanza eneo kubwa la wakulima bado wanatumia jembe la mkono pamoja na kuwa na mfano wa pembejeo, nasikitika kusema kuwa mfano huo bado haujakidhi lengo la kuundwa kwake mfuko huo, watu wakiandika barua hawajibu, juzi nilikuwa na swali kujua Mkoa wa Iringa wamekopesha matrekta mangapi? Takwimu zilionyesha ni wananchi 17 tu. Mkoa wa Iringa una Wilaya saba nazo ni Ludewa, Makete, Nyombe, Mufindi, Iringa na Kilolo na wakazi wapato milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni masoko, mazao mengi tunauza katika hali ya *raw* sio *finished goods*. Sisi wananchi wa Iringa tunaomba wawekezaji wa mazao ya viazi tunalima sana viazi na viwanda vya *juice*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo, mwaka jana pembejeo zimepatikana kila kata lakini vibali vilikuwa vinapatikana makao makuu ya Wilaya hiyo kupelekea mwananchi kusafiri sana kutafuta vibali. Hilo tunaomba liboreshwe.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Waziri Mkuu kwa uwezo wao wa kuja kununua mahindi mkoa wa Iringa kupitia *SGR* Makambako. Aidha, wananchi wa Iringa (Ludewa) tunaomba kituo cha *SGR* kiwepo Ludewa, pia ununuzi wa mazao kwa stakabadhi tunaomba wataalamu waje wafundishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya changamoto hizo kuzingatiwa kwa niaba ya wananchi wa Iringa naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawiziri na watendaji wote kuanzia Katibu Mkuu kwa kazi nzuri, japo ngumu.

Mheshimiwa Spika, maombi, kilimo cha kahawa bado ni tegemeo katika jimbo la Moshi Vijijini. Naomba Wizara inisaidie kuanzisha vitalu vya miche ya kahawa katika maeneo ya *Old Moshi,* Uru na Kibosho ili wananchi wapate miche kwa upesi na kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, *vanilla* ni zao mbadala ambalo naomba msaada wa Wizara wa kulieneza jimboni kwangu kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushirika, Chama cha Msingi cha Kirima - Boro kimekuwa na mgogoro wa karibu mwaka sasa, baada ya wana ushirika kuwatuhumu viongozi wao kwa ubadhirifu. Baada ya ukaguzi kufanyika na msajili msaidizi mkoa wa Kilimanjaro, tuhuma hizi zilithibitishwa, uongozi ukasimamishwa na kuamriwa wakabidhi ofisi na mali zote za chama kwa Kamati maalumu iliyoundwa chini ya usimamizi wa msajili msaidizi. Hadi leo uongozi huu umekataa kukabidhi ofisi na kuna tuhuma kwamba unaendelea kuingia mikataba na wawekezaji wa nje ya mkoa kwa ghiliba ili mali za ushirika zisiweze kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote.

Naomba msukumo wa Wizara ili maamuzi yaliyofikiwa yatekelezwe, ofisi na mali za Chama cha Ushirika vikabidhiwe kwa Kamati teule.

Mheshimiwa Spika, tanbihi, haya ni maombi tu na Mheshimiwa Waziri hana haja kuyazungumzia wakati wa majumuisho, ila akitaja jina langu kama mchangiaji kwa maandishi itapendeza.

**MHE. ALHAJI DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa asilimia mia moja. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, kamilifu na ya kina na yenye kujitosheleza. Hotuba hii kwa mara ya kwanza inaelekea kwenye mapinduzi ya kijani *(Green Revolution).* Nayasema haya kwa dhati kama bwana shamba *(Agronomist)* niliyoanzia *rank and file* kama *Assistant Field Officer* hadi *Agricultural/Research Officer* na *Regional Agricultural Officer*, natambua umuhimu wa kilimo kama chanzo cha chakula, lishe na kipato cha wananchi wetu na hatimaye kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo mwelekeo wa hotuba ya Waziri kuhusu pembejeo za kilimo, mbolea, mbegu bora na zana za kisasa za kilimo pamoja na matrekta, mkazo katika kilimo cha umwagiliaji ukitilia msisitizo umwagiliaji wa *scheme* ndogo, kati hadi kubwa ni jambo sahihi na naliunga mkono. Lazima sasa tuwe na mkakati wa makusudi wa kuwa na lengo la kuongeza eneo linalomwagiwa kila mwaka. Mathalani hekta laki mbili za umwagiliaji kila mwaka kwa mgawanyo wa *scheme* ndogo na za kati na mashamba makubwa. Pia tuwe na mkakati wa kuingiza matrekta kwa miaka mitatu hadi 2010/2011 ambao huingiza matrekta si chini ya elfu moja kwa mwaka wa kwanza na kuongezeka kila baada ya mwaka uliopita. Kilimo cha umwagilijai na matrekta ndio mapinduzi ya kilimo yenyewe. Ugani na utafiti wa kilimo ni masuala muhimu pia.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba *focus* ya umwagiliaji ielekezwe mkoa wa Morogoro hasa katika Bonde la Kilombero, Ruaha na Wami. Naona mkazo katika *scheme* za umwagiliaji mkoani Morogoro ni sahihi. Endelea hivyo, kwani agizo la Mheshimiwa Rais la kuifanya Morogoro kuwa ghala ya Taifa ni sahihi na tuliunge mkono.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa hotuba yake ambayo imeeleze mipango iliyotekelezwa mwaka 2006/2007 kwa ufanisi mkubwa. Hali kadhalika mpangilio wa malengo na mipango ya kuinua ubora wa kilimo kwa mwaka 2007/2008 umeandaliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo na mipango iliyopo, bado tatizo la mipango mahsusi iliyoandaliwa na Serikali ya kumkomboa mkulima au wakulima wadogo, kuondokana na kutumia jembe la mkono, haiko bayana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alieleze Bunge lako Tukufu hatua *practically* yaani mambo ambayo wakulima hawa wadogo, wenye vishamba vingi, lakini vidogo, wanatakiwa kuyafanya ili wapate kutumia *power tillers* au wanyama kazi ili waondokanae na kutumia nguvu nyingi mno kwa kulima pasipo tija.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kodi ya *VAT* wanayotozwa wakulima wadogo wa miwa inayouzwa katika viwanda vya sukari vya Kilombero na Mtibwa. Zao la miwa limesamehewa tozo la *VAT* katika *schedule* ya *TRA*. Lakini *VAT* inatozwa kwa miwa ya mkulima inapovunwa kwa kukatwa, inapopakiwa katika magari na inaposafirishwa kwenda kiwandani. Huu ni mzigo mkubwa wa gharama kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, kwa nini *VAT* itozwe kwa wakulima wadogo tu wakati wakulima wakubwa hawatozwi au wakitozwa kwa kuwa wao ni *VAT Registered Agents* wanadai kisheria kurejeshewa makato. Huu ni upungufu mkubwa wa utaratibu mzima wa *VAT* katika suala hili. Naiomba Serikali ilishughulikie suala hili lililoendelea kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni ushauri kwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwamba majengo ya hifadhi za mazao yanayolimwa katika Wilaya za Mkoa wa Morogoro zianze kujengwa katika kila Makao Makuu ya Wilaya mapema iwezekanavyo. Hatua hii itawahamisha ipasavyo wakulima wengi kuwa na uhakika wa soko kwa mazao yao kwa kuitikia wito uliotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuufanya Mkoa huu kuwa ghala la chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango nilioutoa, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, wakurugenzi na watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuongelea uendelezaji wa fani ya lishe. Fani hii ni muhimu sana lakini Wizara sasa inaonekana kutoipa uzito unaostahili wananchi wanakabiliwa na lishe duni wakiwemo watoto. Wilaya nyingine nchini ikiwemo Wilaya ya Makete pamoja na matatizo yake yote haina afisa lishe hata mmoja. Wizara iangalie hili, ili itoe mafunzo kwa wataalamu wa ugani na Kitengo cha Chakula na Lishe Wizarani kipewe rasilimali kama vitengo vingine Wizarani. Wizara pia ianzishe kozi za muda mfupi kuhusu masuala ya lishe. Kama tunahitaji kuwezesha wananchi kiuchumi ni

muhimu sana wananchi kupata mafunzo ya namna ya kuendesha *SACCOS* zao, lakini haya yafanyike kwa ufanisi kwa sababu Maafisa Ushirika ni wachache sana Wilayani hivyo kuongeza ukiritimba na urasimu kwa wananchi wanachama katika Vyama vya Kuweka na Kukopa. Hivyo ni muhimu fedha ziongezwe kwenye idara hizi ili waweze kuwahudumia wananchi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, suala la pembejeo za kilimo, ni vizuri sasa tuangalie kuwapatia wananchi pembejeo kupitia *SACCOS* zao zikiwemo *SACCOS* za wanawake ambao kilimo chao kimeendelea kuwa cha jembe la mkono na bila pembejeo. Naomba mfuko wa pembejeo uangalie pia suala la jinsia kwa kuhakikisha kwamba *SACCOS* au vikundi vya wanawake wanaohitaji mikopo ya pembejeo wapewe umuhimu.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa ugani wapo pia wanaofanya kazi katika mazingira magumu (maeneo ya mazingira magumu) wengi hawana nyumba za kuishi. Nyumba za wataalamu wa ugani zijengewe kabla ya mtaalamu hajapelekwa kijijini ili kumwezesha kutekeleza majukumu yake kwa moyo mmoja ili asikate tamaa. Mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia kwa mia moja.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Mawaziri wote wawili, Makatibu Wakuu na wataalamu wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo naomba nichangie na Mheshimiwa Waziri azingatie ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza Chuo cha Utafiti Tumbi ambacho kimetelekezwa kwa muda mrefu bila kupewa fedha za kutosha kuendeshea shughuli za utafiti;

(ii) Kutenga fedha za kutosha kwenye vyuo vyote vya utafiti hapa nchini kwani bila utafiti hakuna kilimo bora;

(iii) Vyuo vipewe vitendea kazi, kama vile gari, pikipiki, kompyuta za kisasa ili kutumia utaalamu wa kisasa;

(iv) Kuvifanyia ukarabati vyuo vyote hasa majengo ambayo ni ya muda mrefu ili kuwapa moyo wafanyakazi hao;

(v) Kuendeleza kilimo kwenye shamba kubwa la kilimo Uyole kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambavyo kilikuwa chuo cha kuigwa.

(vi) Kutoa elimu kwa wakulima wa tumbaku hapa nchini kwa kupata matumizi mbadala ya ukaushaji wa zao la tumbaku ili kuondoa usumbufu kwa wakulima kutokana na Sera za Mazingira au hali ya machafuko hao nchini na duniani kwa jumla.

(vii) Kuwepo na soko huria kwa wanunuzi wa tumbaku kama ilivyokuwa miaka ya nyuma 1998/1999 kulikuwa na Makampuni mengi ambayo kwa ujanja yaliungana kumkandamiza mkulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, Serikali iweke vipengele kwa wanunuzi kutoa fungu kidogo kutengeneza barabara zitokazo kwenye maeneo ya uzalishaji wa zao la tumbaku/pamba. Kuhusu pamba, Serikali iangalie suala la soko hasa wakulima wanapotaka kuuza kwenye masoko hayo, hupata usumbufu mkubwa hasa kwa wakulima wadogo wadogo.

Kuhusu elimu, ningeshauri elimu itolewe kwa wakulima wa zao la pamba ili waweze kuviamini Vyama vya Ushirika ambavyo vilisababisha wakulima kupata hasara ya madeni mbalimbali na kushuka kwa zao hilo na kutoa elimu kwa mbegu mpya za kisasa ili ziweze kutumika kwa wakulima wengi nchini ambao hawana imani na mbegu mpya, bado hutumia mbegu za asili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, kwa kuwa kulikuwa na Kiwanda cha Chuma cha Nkola, Igunga, kilifanya kazi nzuri kwa miaka ya nyuma na kufanya wakulima wa zao hili wa Igunga kuwa na wakulima wengi wa pamba, baada ya kuona kwamba mbegu zao hazina mahali pa kuuza hiyo ilichangia kushuka zao hili kwa Wilaya ya Igunga.

Nashauri, Bodi ya Pamba ishauriwe kufungua Kiwanda hicho hata kama kuna mikopo ili kiweze kuendeshwa; Bodi ya Pamba ifanye mkakati wa makusudi kama walivyofanya kwenye zao la korosho ili wakulima wawe na uhakika na soko; Bodi ya Pamba isaidie kusimamia Vyama vya Ushirika wasile tena fedha za mikopo kwa manufaa yao, mara ikigundulika mara moja kuchukuliwa hatua sio kulindana na Kamati ndogo ndogo za wakulima wa mazao haya ziwe na wasomi ili angalau waweze kuangalia hesabu zao, wakati wa kuuza na zile za mikopo, ili kuondoa mzigo wa madeni kwa wakulima. Naunga mkono tena hoja mkono.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa 34 Kifungu cha 51 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika amesema Wizara bado iliendelea na uendelezaji wa mradi wa *PADEP* ukiwemo Mkoa wa Kusini Pemba. Ninachotaka kukifahamu katika Mkoa wa Kusini Pemba ni miradi gani iliyotekelezwa na katika Wilaya zipi au ipi na vijiji gani na miradi hiyo au mradi huo imegharimu kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, uzito wa sekta ya kilimo kwa maendeleo ya nchi umetambuliwa zamani sana katika nchi yetu katika mwaka 1971 kilimo kauli mbiu ilikuwa siasa ni kilimo, leo kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Inakuwaje kwa uzito huo nilioueleza bado nchi yetu itegemee fedha kutoka nje kwa asilimia 88.75 kwa kuendeleza kilimo. Je, Serikali imekuwa makini katika maamuzi hayo. Endapo wafadhili hawakutoa fedha hizo Wizara itachukua hatua gani ili kukinusuru kilimo?

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri na kwa kweli hata ya mwaka jana au tuseme Bajeti iliyopita hotuba ilikuwa nzuri vile vile, lakini baada ya kumalizika mwaka huwa kuna malalamiko mengi kwa Wabunge kwa mfano ruzuku ya mbolea na kadhalika. Nadhani ipo haya uzuri wa hotuba uambatane na utekelezaji. Wizara ninaishauri iwe kali kwa watendaji ambao hawatekelezi wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa kutoka kwa Wabunge juu ya kutomalizika kwa mabwawa ya umwagiliaji na Wizara haikutenga fedha ya kuyamaliza. Sanjari na hilo Wizara imeanzisha ujenzi wa mabwawa mapya. Haioni Wizara ingeyamaliza yale ambayo hayajamalizwa. Naishauri Wizara katika kujenga miundombinu ya umwagiliaji tuanzie mabonde makubwa na miundombinu ikamilike ndio yaelekezwe mabonde mengine.

Mheshimiwa Spika, kivutio kikubwa cha kukuza kilimo ni bei nzuri na ya uhakika vinginevyo juhudi zote zinazochukuliwa hazitazaa matunda makubwa. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa na mikakati madhubuti ya suala hilo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo David na Mheshimiwa Mhandisi Christopher Chiza, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma umejitahidi sana kuendeleza kilimo hasa cha mazao ya chakula lakini jambo la kusikitisha ni kwamba wakulima hao wanajikuta kila mwaka wanazalisha hasara ya shilingi 25,000/= kwa heka ya mahindi na shilingi 17,000/= kwa heka ya maharage. Aidha, bei hizo zinazidi kuwa mbaya kwa mazao hayo hayasindikwi na pia *SGR* kushindwa kununua mazao hayo na kuwaachia walanguzi. Wakati huo huo Serikali imepiga marufuku kuuza mazao hayo nje kwa jirani zetu kama Malawi na Msumbiji. Je, ni lini Serikali itafungua amri hiyo ili kuwezesha watu wetu kuuza mazao yao popote wanapotaka kama Serikali haiwezi kuwasaidia kuwapa soko lenye bei nzuri?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani ili kuhakikisha inanunua ziada ya mazao hayo badala ya kuwaachia wanunuzi wakandamizaji? Wananchi wanazidi kuchakaa na watoto wao wameshindwa kusoma na akinamama ndio wanaumia zaidi.

Mheshimiwa Spika, chonde, Ukanda wa Ziwa Nyasa hauna zao maalumu la biashara. Naomba jicho lako la huruma lituone. Naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto haina viwanda. Wakazi wake wanategemea kilimo cha mboga na matunda kwa kumwagilia kienyeji kwa ufanisi

mdogo. Ibara ya 46 – 48 na vitambatisho vyote (1-11). Wilaya ya Lushoto imeachwa kabisa. Naomba anieleweshe sisi wa Lushoto tumeandaliwa miradi ipi ya umwagiliaji. Ahsante.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa wazima na salama na vile vile napenda kuwapongeza Mheshimiwa Spika na Naibu wako, Mheshimiwa Anne Makinda kwa namna mnavyojitahidi kuongoza Bunge.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia naanzia na zao la korosho. Nimesoma hotuba lakini naona Mheshimiwa Waziri anazungumzia zaidi kulima lakini hataji soko ambalo ndilo tatizo sugu la zao hili muhimu kwa mikoa yote ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuwa wananchi wa Kusini wanategemea sana zao hili na halina soko la uhakika kwani wananchi zao hili ndilo wanalolitegemea kwa kila hali sasa linapokosa soko la uhakika ndio wananchi wa mikoa hii wanazidi kuwa maskini zaidi. Hivyo ninaiomba Serikali iwahakikishie wananchi hawa soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni tuliridhia Mkataba wa Kimataifa juu ya matumizi ya tumbaku sasa naona tunahimiza kilimo hiki cha tumbaku sasa huko si kuwa ndumilakuwili, kuwa huku tunaridhia na wakati huo huo tunaimarisha.

Mheshimiwa Spika, Waziri kuhusu hili unasema nini?

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa naunga hoja mkono.

Pili, natoa pongezi za dhati kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai kwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote Wizarani kwani kwa muda mfupi sana mabadiliko yapo na yanaonekana na mipango ya hapo baadaye inaleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo machache; kwa kuanzia napendekeza umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji kwa ujumla wake kwani kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani ni hatari zaidi kutegemea kilimo cha mvua. Kwa kule kwetu Hai kilimo cha umwagiliaji kimeonyesha mafanikio makubwa sana kuanzia kule Mlimani kupitia *PADEP* ambapo mifereji imekarabatiwa na hivyo kuwezesha upatikanaji wa maji ya uhakika zaidi na kupunguza migogoro baina wananchi kwenye zamu za umwagiliaji, hivyo ninaomba sana kwa vile vijiji ambavyo havijapata pesa *PADEP* vipatiwe kwa sababu mafanikio ni makubwa sana na kilimo cha mazao madogomadogo na mbogamboga kimeanza kushamiri sana hadi kule vijiji vya ukanda wa tambarare *PADEP* bado ingesaidia sana.

Kwa ukanda wa tambarare zile sehemu za umwagiliaji naomba zikamilike ambazo Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher Chiza anazifahamu vizuri sana na

kukumbushia ahadi yake ya kujenga lile banio la Mijengweni ambalo lilishatengewa pesa lakini zikatumika wakati wa dharura ya njaa. Kwa ujumla kwa upande wa Hai tukiimarisha kilimo cha umwagiliaji hatutakuwa na uhaba wa chakula hata kidogo na badala yake tutaweza kuzalisha zaidi na ziada kwa ajili ya nje ya Hai hata kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napongeza ruzuku kwenye miche ya kahawa mpya kwani tumeshaeneza elimu sana na hivyo wakulima wengi kushawishika sana kuotesha kahawa mpya lakini shida kubwa ni upatikanaji wa miche mipya. Hivyo nashauri tuzidishe juhudi kwa upande wa uzalishaji wa miche mipya ili kila kijiji kiweze kuwa na bustani mama. Pamoja na kusisitiza ubora wa kahawa tunayovuna kwa ajili ya bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya nafaka kwa mfano mahindi na maharagwe naomba tusiwazuie wakulima wetu pale wanapokuwa wamejaliwa kuzalisha ziada kuuza nchi jirani kwani huko wanapata bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirika nashauri kuuangalia sana kwani ushirika mzuri ndio ukombozi wa wakulima. Inafahamika dhahiri kuwa kule kwetu Hai na Kilimanjaro kwa ujumla wake, ushirika ulikuwepo siku nyingi na uliweza kuwaletea maendeleo ya haraka sana wananchi wa Kilimanjaro hapo siku za nyuma. Sasa shida kubwa ni pale ambapo tumekuja kuwa na viongozi wa ushirika wasiokuwa waaminifu kiasi cha kusababisha wakulima/wanaushirika kutokuwa na imani nzuri na ushirika. Kumekuwepo na matatizo makubwa sana kwenye baadhi ya Vyama vya Msingi vinavyounda *KNCU* ya ubadhirifu wa pesa ya wakulima pamoja na mali nyingine za ushirika ikiwa ni pamoja na mashamba, majengo na magari.

Mheshimiwa Spika, kuna mikataba ambayo Vyama vya Msingi iliingia na wawekezaji katika mashamba ambayo siyo mizuri kwa iliyo mingi; napendekeza na kushauri kwa nia ya kuimarisha ushirika Hai na Kilimanjaro kwa ujumla wake kuiangalia upya kwa maana ya kurekebisha mapungufu yaliyopo kwani malalamiko kutoka kwa wananchi ni mengi sana na yakiachwa yaendelee uhai wa ushirika uko kwenye mashaka makubwa sana. Kwa maneno mengine nashauri tusibembelezane na watu wanaothibitika kuhujumu ushirika nchi mzima.

Mheshimiwa Spika, tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu ili mipango iliyopo iweze kutekelezwa kwani mabadiliko yatakuwa ni makubwa sana kwa nchi nzima.

Nimemalizia kwa kutoa mfano hai ambao utasababisha ushirika Mkoani Kilimanjaro kuvunjika. Chama cha Msingi Lyamungo kinachomilikiwa na vijiji vitatu yaani Lyamungo Kilaya, Lyamungo Kati ya Lyamugo Sinde wanalo shamba linaitwa Uremi ambalo chama kikuu *KNCU* wameng'ang'ania hati ya hilo shamba kwa miaka mingi na kuna taarifa kwamba *KNCU* walikusudia kuliuza. Nashauri kwa msisitizo mkubwa, Wizara iingilie kati na hilo shamba lirudishwe kwa Chama cha Msingi cha Lyamungo kwani wananchi wanalihitaji kwa shughuli za maendeleo kwa miaka mingi sana.

Naunga hoja mkono na kumwomba Mwenyezi Mungu awatangilie nyota na sote.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kutoa pongezi kwa hotuba nzuri ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, na mimi nimeona angalau nichangie katika hotuba hii. Japo kwa maandishi. Katika Jimbo langu la uchaguzi la Gairo Wilaya ya Kilosa toka niwe Mbunge katika ziara zangu za Kata na Vijiji sijawahi kuona Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu ukiulizia kwa Afisa Kilimo wa Wilaya utaambiwa wapo na wamepeleka ripoti nzuri za vijiji vyao Wilayani; na ukiuliza wananchi katika katika vijiji hivyo hivyo wanatakwambia hawamjui wala hajawahi kumuona Afisa Ugani katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano huo tu pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuongeza Maafisa Ugani lisipoangaliwa na usimamizi wa uhakika nia nzuri ya Serikali haitaonekana. Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iwe makini na kuchunguza Maafisa wake Vijijini wanafanyakazi ambazo Wizara inakusudia. Sivyo tutaja wataalamu watalii sio wa kilimo na hasa katika Jimbo la Gairo wa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, katika kilimo hasa wa Chakula katika Mkoa wa Morogoro. Jimbo la Gairo limekuwa siku zote linafahamika kwa kuzalisha mahindi, viazi vitamu, kwa wingi na hata wakulima wengi katika Wilaya za Kiteto na Kongwa ni kutoka katika Jimbo la Gairo.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi za nchi yetu Kilimo cha Chakula wanatumia mbolea tofauti na wananchi wa Wilaya ya Kilosa ambao hawatumii mbolea kutokana na ardhi yao bado ina rutuba. Cha ajabu sehemu zingine zinafaidika na ruzuku ya mbolea na mambo mengine. Lakini katika Jimbo la Gairo na Wilaya ya Kilosa hakuna ruzuku ya aina yoyote na hasa ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, na hata katika mfuko wa pembejeo sielewi ni vigezo gani vinatumika kuwanyima mikopo ya matrekta wananchi wa Gairo pamoja na kutimiza masharti na kuwa na sifa hizo mfuko huo haujamfaidisha mwanachi hata mmoja wa Gairo sijui kama kuna wajanja ambao wamefaidika kutumia jina la Gairo kujifaidisha, lakini kama mwakilishi mfuko huu hauna msaada wowote katika Jimbo la Gairo ambalo linajulikana kwa kilimo mahiri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika bila kuchukua hatua za haraka kuangalia kwa makini kitengo cha pembejeo. Kisiwe na urasimu na kutoa mkopo kwa watu maarufu na wasio na sifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuamini kwa kazi nzuri na nia yake ya kweli Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Naibu Mawaziri wake nategemea watabadilisha

hali hii na kusafisha kitengo hicho ili wawepo watu mahiri wanaothamini matakwa ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nategemea majibu ya kutosha na naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yenye kuleta matumaini ya mapinduzi ya kilimo na kuwa na mikakati ya kuboresha ushirika katika Mikoa mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Mtwara ambao una matatizo makubwa katika kilimo, hotuba hii inaleta matumaini ya kuwa na maisha bora kwa wakulima wetu.

Pili, nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kuwa na mikakati mizuri ya kuungana na Serikali katika kuboresha ushirika na kujishughulisha sana katika sekta ya kilimo ili kujipatia chakula na biashara ili kujiondolea umaskini na kuongeza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia akinamama wa Mkoa wa Mtwara walio mstari wa mbele katika shughuli za kilimo na kushiriki kikamilifu katika ubanguaji wa korosho kupitia vikundi mbalimbali kama sera ya CCM inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mkoa wetu kuwa na zao kubwa la korosho ambalo ni la biashara, bado wakulima hawa wanajishughulisha na kilimo cha mazao mchanganyiko kama mahindi, Mpunga, Mihogo, Ufuta, Mbaazi, Karanga na kadhalika. Kwa miaka ya nyuma mazao haya yalikuwa yakilimwa kwa wingi na masoko yalikuwa na uhakika. Lakini wanunuzi wakubwa wamepunguza kwa kiasi kikubwa hivyo kupelekea uzalishaji wa mazao haya na wanunuzi kuelemea katika ununuzi wa korosho ambao pia wananunua kwa bei ya chini hali ambayo ari ya wananchi hupungua kabisa katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba wakulima wa Mkoa wa Mtwara bado wapi katika lindi kubwa la umaskini unaosababishwa kutokuwa na uhakika wa masoko ya mazao yao, ingawa Serikali inatuhimiza kuwa na mazao mbadala, Mkoa wetu tayari tunayo mazao mbalimbali ambayo kama Serikali itasaidia kutafuta wananunuzi wa kudumu wa mazao mchanganyiko basi mkulima wa Mkoa wa Mtwara atanufaika na kujiongezea kipato, ili kumudu kuendesha maisha yao hatimaye kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara tunayo mabonde mazuri ya kilimo kama eneo la Kitere lililoko Mtwara Vijijini, Bonde la Mto Ruvuma lililopo Tandahimba, Newala, Masasi na Nanyumbu ambako pia kuwa Bonde nzuri la Nangaramo. Hadi hivi sasa mabonde haya yanatumika kwa kiwango kidogo sana kutokana na vifaa duni vinavyotumika vya kilimo. Hivyo tunaiomba Serikali ianze kuweka mipango madhubuti na endelevu juu ya matumizi ya mabonde haya kwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuitumia vema rasilimali hii ya ardhi kwa kumwezesha mkulima kupata pembejeo za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yanayowakabilia wakulima wa Mtwara. Nichukue nafasi hii katika kusisitiza kuiomba Serikali kuviwezesha vyombo vyetu vya ushirika kuweza kukopesheka katika mabenki ili nao waweze kuingia katika ushindani wa kibiashara ili waweze kununua mazao kutoka kwa wakulima na kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya ubanguaji korosho.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuishukuru Wizara pamoja na Mfuko wa Pembejeo kwa mwaka huu wa 2007 kwa kuwafikiria wakulima wachache wa Mkoa wa Mtwara na kuweza kuwakopesha matrekta ili kusaidia kuanza kilimo cha kisiasa, tunaiomba hizi zilizoanza basi mikopo ya matrekta madogo vikopeshwe Vyama vya Ushirika ili yaweze kusambaa katika maeneo mbalimbali na kuweza kuleta mapinduzi ya kilimo katika Mkoa wetu, ili kuleta pato zuri kwa wananchi na uchumi kwa nchi yetu.

Mwisho, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Mipango ya ugani, mapinduzi ya kijani ya kilimo, umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo inatia moyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza zao la korosho, limepata mtazamo mpya. Huko nyuma zao la korosho liliachwa kujihudumia lenyewe. Mwanzo huu wa kulisaidia zao la korosho ni nzuri, tunaahidi kuunga mkono juhudi hii. Mimi binafsi nitazidi kuongeza miche mipya ya korosho mwaka huu. Msimu uliopita nilipanda miche 1,000 mwaka huu nitapanda miche 5,000 ili kuunga mkono mtazamo huu mpya wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ya namna Halmashauri za Wilaya zinazolima korosho zitakavyopata *export levy* ya zao la korosho zilizozalishwa na kuuzwa nje. Mkoa wa Mtwara una vyama vya ushirika lege lege. Moja ya sababu kubwa ni pamoja na maafisa ushirika kuwa mawakala wa wanunuzi wa korosho. Uongozi wa Mkoa wa Mtwara uliomba Wizara kusaidia ushirika wa *MAMCU* kupata Mtendaji Mkuu wa kuazimwa hadi hapo ushirika utakapotengemaa. Serikali imeanza kuchukua hatua za kuwapangua baadhi ya maafisa ushirika, lakini tunaomba hatua hizo ziharakishwe.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa matatizo yaliyotokea katika ununuzi wa korosho msimu uliopita hayatajirudia tena. Narudia kumpa pongezi za dhati Mheshimiwa Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara. Aidha, naomba kuipongeza Bodi ya Korosho kwa kazi nzuri. Ila masikitiko yangu ni Mwenyekiti wa Bodi ambaye haonyeshi nia ya kuendeleza Bodi pamoja na zao la korosho. Hivi hamjui jinsi anavyotumia vikao vya Bodi kwa malumbano zaidi kuliko maendeleo ya zao la korosho?

Mheshimiwa Spika, badala ya Mtendaji wa Bodi kufanya kazi anatumia muda mwingi kujihami na kujibu tuhuma zisizo na msingi. Hata hivyo naishukuru Wizara na hasa Waziri mwenyewe kwa masimamo wake imara kuhusu Meneja Mkuu.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. Kazi yenu ni nzuri. Nimekuwa nikiuliza utaratibu wa kuleta wawekezaji kuhusu matunda. Geita ina matunda mengi sana kiasi ambacho wakulima wanakosa soko, matunda yanaoza ovyo. Tafadhali sana nakuomba Waziri tembelea Geita uone, nanasi, embe, tikiti maji, uone jinsi yasivyo na soko. Geita inazalisha *first class* za nanasi zinazopatikana ulimwenguni kwa utamu. Hii imeathibitishwa na wataalamu wa uchimbaji ambao walipeleka *sample South Africa. Juice* yake haihitaji kuongezwa utamu. Hivyo tukianzisha kiwanda cha kusindika mazao tutapata faida na tunaweza na sisi kuongeza mazao ya kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikieleza hoja hii nzuri sipati majibu naomba nipewe majibu leo. Maeneo yanayoweza kuongezewa uzalishaji katika kiwanda ni matunda kutoka Geita, Sengerema, Ukerewe, Biharamulo, Lushoto, Morogoro na sehemu nyingine zenye matunda kama Tabora.

Mheshimiwa Spika, ninaimani kiwanda kikijengwa Geita tija itapatikana ya kutosha. Naunga hoja mkono.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Spika, tunashukuru Mungu Tanzania ina ardhi kubwa na nzuri kwa kilimo, ufugaji, iliyojaa madini ya aina zote pamoja na maji tele. Kwa vile uti wa mgongo wa Tanzania ni ardhi safi ya kilimo na asilimia 80 ya wananchi ni wakulima na wafugaji, naomba Serikali kujikita ndani ya sekta hiyo. Pia Serikali inapaswa kujipanga kwa makusudi ili iweze kuchochea maendeleo ndani ya kilimo ili kuleta tija ya chakula na kunyanyua hali za wakulima na wafugaji. Kuzaliwa kwa viwanda vikubwa nchini husababishwa na wizi wa mazao ya wakulia.

Mheshimiwa Spika, kwa kupata ufanisi ndani ya sekta ya kilimo nchi inahitajika kufanya mapinduzi makubwa ya kilimo kwa makusudi na kwa nia ya kunyanyua uchumi wa Tanzania. Serikali isiogope kuwa na uamuzi wa kutaka kilimo kiwe cha kisasa kwa kutafuta nchi kama China ikaombwa kututengenezea matrekta ili yaweze kugawiwa matrekta matano kila Wilaya ya Tanzania pamoja na kuwakopesha wananchi ng'ombe wawili wa maksai pamoja na plau za kukokotwa na ng'ombe. Hili ndani ya kipindi cha Ilani ya Uchaguzi lazima utatoa jibu zuri tu; pale ndani ya mapinduzi hayo yatakaposhirikishwa na huduma pamoja na taaluma kadhaa.

Mheshimiwa Spika, yapatikane matrekta matano kila Wilaya na kila ndani ya kipindi cha Ilani ya Uchaguzi ya kipindi cha miaka mitano, pamoja na kuwakopesha wakulima plau pamoja na maksai wawili. Hili litaleta mapinduzi makubwa ya kilimo ndani ya kipindi hicho. Pia Serikali ipangilie vizuri maeneo ya kilimo kwa mazao mbalimbali, maksai kupitia Maafisa Ugani kwa kila kijiji na afisa huyo huyo apewe jukumu la kuwapatia pembejeo za aina zote hadi kuhakikisha kiasi cha mavuno kwa kila wakulima, jambo litakalomuwezesha mkulima kulipa deni lake.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa maksudi ianzishe Kituo cha Utabiri wa Hali ya Hewa upande wa kilimo. Kituo ndiyo kitakachotoa maelekezo yote ya mwongozo na

chanzo cha wakulima kuanza kushughulikia mashamba yao kwa utaalamu zaidi, Serikali pia kwa makusudi ianzishe *SGR* ndogo kwa kila Wilaya ili mavuno yaweze kununuliwa kwa wakati kwa manufaa ya wakulima na Serikali ikusudie kujenga viwanda vya kusindika nafaka kufuatana na ya sekta ya mazao husika. Pia juhudi za makusudi zifanyike kuanzisha viwanda vya kusindika matunda nchini. Serikali iweze angalau kujenga kiwanda kila ndani ya kipindi cha miaka mitano ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji kisimamiwe na wataalamu ili kiweze kuendeshwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nia na maana ya kuchangia ni kutoa mawazo ya matayarisho ya Mapinduzi ya Kilimo ndani ya Tanzania. Serikali kwa makusudi iombe mkopo mkubwa tu wa matrekta,ili kunyanyua kilimo na kuongeza wingi wa mavuno ili Tanzania iweze kujitegemea kwa chakula cha Taifa lake. Serikali isiogope kubeba deni kubwa juu ya kilimo, lazima tuthubutu juu ya mapinduzi ya kilimo Tanzania. Ahsante sana.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake iliyofafanua vizuri masuala ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mpango wa *ASDP* ambao unasaidia kuboresha maisha ya mkulima katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri limejitokeza suala la kupungua uzalishaji wa mazao ya kilimo kutokana na ukame na hivyo Wizara kuonyesha jitihada za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Lakini kwa upande mwingine mvua nyingi nazo huchangia kupunguza uzalishaji kwa baadhi ya mazao yasiyohitaji mvua nyingi na pengine hata uzalishaji kwa ujumla kupungua kutokana na mazao kusombwa na maji. Ningependa kujua Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uharibifu utokanao na mvua nyingi? Je, ule mpango wa kuvuna maji ya mvua zinazozidi na kuyatumia kwa umwagiliaji wa kipindi cha ukame umeshaanza?

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la uwezeshaji wa maafisa ushirika katika maendeleo ya vyama vya kuweka na kukopa *SACCOS.* Kwa hali halisi ilivyo maafisa ushirika wameonekana kushindwa kufanya kazi ya uhamasishaji na uanzishaji wa *SACCOS* kwa ufanisi kutokana na mapungufu katika vitendea kazi. Hawa wanalipwa mishahara lakini mara nyingi wamekuwa ni watu wa ofisini kwani ukizungumzia suala la kwenda vijijini majibu yale ni kwamba hakuna usafiri wala mafuta.

Mheshimiwa Spika, kama wateja wengi wa maafisa ushirika wako vijijini na wakati huo huo maafisa hawa hawawezi kufika kwa wateja. Je, Serikali haioni kuwa inapoteza rasilimali za Taifa kwa kuwalipa maafisa pasipokufanya kazi iliyokusudiwa? Naiomba Serikali iwawezeshe maafisa ushirika kufanya kazi kwa kuwapa vitendea kazi. Serikali iangalie pia hali ya taaluma yao ya kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika maeneo mbalimbali ili waweze kutoa maelekezo yanayostahili kwa walengwa wa aina

tofauti. Ukweli ni kwamba wengine elimu ya *SACCOS* waliyonayo ni ndogo na inahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa korosho wanalia, wanapunjwa sana na wanunuzi wa korosho ghafi kwa bei ya hasara. Takwimu katika hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji zinaonyesha kuwa bei ya korosho katika soko la dunia inashuka tangu mwaka 2004 hadi 2006. Kumekuwa na hisia miongoni mwa wakulima kuwa bei hii kushuka si kweli bali ni ujanja ujanja wa wafanyabiashara ili kuendeleza unyonyaji kwa wakulima. Ningependa kujua kama suala la bei ya korosho kushuka ni kweli na wakulima waeleweshwe sababu za kushuka huku. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hili? Je, mbali na mkakati wa kuongeza thamani kwa njia ya ubanguaji wakulima wanatakiwa wafanye nini zaidi?

Kwa kuwa mkakati wa ubanguaji utachukua muda mrefu hautaweza kuleta matokeo kwa mwaka huu, naishauri Serikali ifanye ufuatiliaji wa karibu zaidi kuhusu bei ya soko la dunia ili mwaka huu katika msimu ujao korosho bei isishuke bali ipande. Ninalizungumza hili kwa uchungu kwani kwa wakulima gharama za uzalishaji zinapanda kila mwaka ukianzia mbegu bora, dawa za mazao na wadudu, gharama za palizi na nyinginezo. Serikali iliangalie kwa ukaribu hili suala.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kutoa *CD* ya ramani ya mazao katika nchi yetu. Pamoja na *CD* hii yapo maeneo ambayo yamekuwa yakistawisha mazao ya aina mbalimbali kwa mfano, ulezi, uwele, pamba, soya muhogo lakini baadae ukulima kupungua au kuachwa kabisa kutokana na sababu tofauti tofauti. Kwa mfano, kuzuka kwa magonjwa na wadudu waharibifu, ukosefu wa masoko, bei inayoshuka bila kutabirika, kupungua kwa rutuba ya ardhi, mabadiliko ya hali ya hewa na mvua zisizoaminika mabadiliko katika tabia ya ulaji. Je, Serikali imejiandaa vipi kukubaliana na sababu hizi? Kwa mfano mdogo tu soya ilikuwa ikistawi Mkoani Mtwara lakini uzalishaji umepungua kutokana na ukosefu wa soko. Hivyo naiomba Serikali kupitia mpango wa *ASDP* na wadau mbalimbali ijitahidi kuondoa vikwazo hivi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, *CD* hii ikifanyiwa kazi vizuri na kwa ushirikiano mzuri na maafisa ugani watakaoajiriwa kila kijiji kilimo kitaimarika na hali ya wakulima itaboreshwa. Naomba kuwasilisha na naunga hoja mkono. Ahsante.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na pia kumpongeza sana yeye binafsi na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayofanya ikiwa ni pamoja na juhudi kubwa za kufufua na kuimarisha ushirika nchini, hususan *Nyanza Cooperative Union 1984 Limited.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitoe salaam za rambirambi kwa familia za Marehemu Stepehen Kazi, Marehemu Hezron Ndonbo na Marehemu William Kasubhi, ambao walifariki dunia tarehe 24 Juni, 2007 katika ajali ya gari wakiwa safarini kuja Dodoma kushughulikia ufufuaji wa *NCU (1984) Limited* ili iweze kuanza tena

biashara. Wanaushirika wana deni kubwa kwa mashujaa hawa watatu wa Ushirika ambao tutawaenzi ipasavyo kwa juhudi zaidi za kuimarisha ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, ushirika nchini kwa uhakika bado una nafasi ya kufanya vizuri zaidi hasa katika uwezo wa watendaji wake. Mimi binafsi naamini misingi ya kupata watendaji wazuri katika Ushirika upo katika kuhuisha sheria yenyewe kwa kuruhusu kuwa na ulazima wa kuajiri wataalamu, kuanzia katika safu za watendaji wa ngazi ya Vyama vya Msingi vya Ushirika hadi katika ngazi ya *Union* na hasa katika Bodi zenyewe za *Union.*

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa ukosefu wa taaluma katika utendaji wa kila siku wa vyama vingi vya ushirika ndiyo kimekuwa chanzo kikubwa cha matatizo makubwa ya uendeshaji wa utawala wa fedha. Ni matumaini yangu kuwa Wizara italingalia suala hili kwa mapana zaidi na kwa nia ya kupata uendelevu.

Mheshimiwa Spika, napenda nieleze masikitiko yangu kwa *KACU* ambayo bado inadaiwa kiasi cha shilingi 45,000,000/= na wakulima wa pamba wa Jimbo la Tabora Kaskazini tangu msimu wa mwaka 2003/2004. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata fedha hizo za wakulima hawa waliovuja jasho kubwa wakipambana na umaskini. Naomba juhudi za Serikali sasa zizae matunda na wananchi hawa walipwe.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa kupeleka ruzuku kwa wakulima kupitia pembejeo unaonyesha kwamba lengo halijafanikiwa kwa kiwango kilichotarajiwa. Tatizo kubwa na njia gani itumike ili mlengwa afikiwe na kufaidika. Sisi tutaendelea kuunga mkono Serikali katika juhudi zake za kutafuta njia hiyo bora ya kumfikia mkulima. Muhimu tunaloliomba ni kuwepo kwa mazungumzo shirikishi ambapo mkulima pia atashirikishwa katika kutambua namna bora zaidi ya kumfikishia ruzuku.

Nataka niamini kuwa Serikali itakuwa *flexible* na kuzingatia *circumstances* pamoja na aina ya zao na jiografia ya maeneo ambako wako hawa wakulima, katika kupata namna ya kumfikishia ruzuku huyo mkulima. Hii inamaanisha kuwa inawezekana utaratibu wa kufikisha ruzuku ukatofautiana kutoka eneo hadi eneo, zao hadi zao. Muhimu ni usawa katika kiwango cha ruzuku ambayo tunataka kumfikishia mkulima.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara katika mikakati yake ya kufikia mapinduzi ya kijani ambapo kilimo cha aina zote na mazao ya aina zote kitahuishwa, ikiwa ni pamoja na *mechanization* na upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuongeza nguvu na ubora wa huduma za ugani nchini, ni muhimu pia kumjenga vizuri zaidi huyu mkulima tunayetaka alete mapinduzi ya kijani kwa kumuongezea maarifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua zetu za msimu, mkulima hubakia akiwa hana kazi kwa karibu miezi sita katika msimu. Ingekuwa vizuri mkulima huyo akapata

mafunzo ya kina katika kipindi hicho pia. Wakulima hawa wanahitaji kusaidiwa katika kupanua uelewa wao wa hali ya hewa na namna ya kuitumia ipasavyo katika shughuli zao, namna ya kufikia mikopo ambayo itasaidia katika kupanua na kuboresha kilimo chao na pia kuongeza thamani ya mazao yao na kuyafikisha katika masoko yanayolipa vizuri na katika muda muafaka. Wakulima hawa wanatakiwa kufundishwa na kuzielewa sheria mbalimbali zinazotawala shughuli za kilimo pamoja na biashara ya mazao na bidhaa za kilimo. Wanahitaji kujazwa maarifa hawa.

Mimi naamini kuwa katika hatua hii ya maendeleo, Serikali haiwezi kuketi kando na kumwachia mkulima peke yake na kibaya zaidi kuyaachia makampuni hasa yanayonunua mazao ya wakulima, yafanye kazi hii ya kumwelimisha mkulima. Serikali inapaswa kuongoza shughuli hii ya kumwelimisha mkulima ili pia kuwa na uhakika wa usahihi wa elimu anayopewa huyu mkulima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya yote nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Stephen Wasira, pamoja na Naibu Mawaziri wake wakisaidiwa na Katibu Mkuu, Ndugu Peniel Lyimo mwenye uzoefu kwa kila fani ya kilimo. Naunga mkono hoja hii nzuri na yenye matumaini kwa wengi wetu kama kweli tutasimamia vizuri mipango iliyoandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, *Green Revolution* inahitaji uhakika wa maji, mbolea, mbegu, dawa na wataalamu wanaojituma kutekeleza azma hiyo ya Serikali. Wataalamu wetu wa sasa ambao wengine wamejiunga na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kukosa *choice* yao ya awali, lazima tuwe nao kwa uangalifu zaidi. Wengine wanaona kilimo kama kazi isiyo na hadhi, kazi ya kushinda mashambani bila hata ya mkaguzi anayewauliza wanafanya nini, kazi ambayo imewafanya wengine washinde kwenye vilabu vya pombe tu.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kulisema hilo kwa sababu, kweli sehemu nyingi za vijiji vyetu, mabwana shamba wanaonekana kwa nadra sana shambani kwa wanavijiji, sheria, kanuni za kilimo bora haziangaliwi wakati wahusika wapo na hawachukuliwi hatua yoyote, ni kwa msingi huo mimi nashauri yafuatayo:-

Moja, *recruitment* ya vijana wa *Form IV* kwa ajili ya mabwana shamba, uanzie kwenye Serikali za vijiji. Tuwapate vijana wengi kutoka maeneo hayo ili hata tukiwafundisha waweze kurejea katika maeneo yao waliyoyazoea na kulingana na mazao yanayolimwa maeneo hayo. Siyo vizuri kumchukua kijana wa Kagera akashughulikie zao la korosho Mtwara *(misuse of manpower).*

Mheshimiwa Spika, pili, tuanze kuwatafuta wakulima wazuri wa mifano ili tuwasaidie kutuzalishia mbegu nzuri za mazao tunayalima katika maeneo mbalimbali. Kazi hii isiachiwe mashamba makubwa tu kuzalisha, *outgrowers* waongezeke.

Tatu, tuhamasishe wawekezaji wa nje na ndani, hata baadhi ya *graduates* wa kilimo wajiunge kuanzisha mashamba makubwa na tuwape kila aina ya msaada wa mikipo ili kilimo kisiendelee kuwa cha watu wasio na kisomo. Dunia imebadilika, tajiri wa hivi sasa anatakiwa kuwa mkulima kuliko mtumishi wa ofisini ili akiendesha kilimo kisayansi. Ni kwa msingi huo je, wazo la kuwakopesha watalaamu wanaostaafu au wenye nia ya kuacha kazi ya ajira ya Serikali na kuanzisha kilimo na ufugaji wa kisasa, umeishia wapi? Nchi za *NORDIC* zilizowahi kukubali kuanzisha mpango huo mwaka 1997 kwa *U$D* milioni mbili ili wataalamu wa kilimo wawezeshwe kulima kuliko kuajiriwa, hii ni pamoja na wataalamu wa mifugo kuanzisha mashamba ya mifugo *(Vouches).*

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kuhusu kuendelea kutegemea sana miradi mingi ya kilimo kupata fedha za nje; bila kuwa na mpango wetu wenyewe wa *Phasing in and phasing out,* yaani kujiandaa kila mwaka kuongeza mchango wetu wa ndani ili mwaka wa mwisho tuwe tumeongeza kiwango staili kwa mradi husika, mara nyingi fedha za nje zikifikia mwaka wa mwisho, huwa sisi hatuna za kuendelea na mradi husika na hivyo miradi mingi kufa kifo cha mende, kama waswahili wanavyosema, tutajifunza mpaka lini? Miradi mingi ambayo ilikuwa *funded* toka *external account* haipo tena. *Programmes* nyingi za umwagiliaji na hata za utafiti mara nyingi zimeendelea kubakia kama watoto yatima baada ya wahisani kujitoa. Hii ndiyo hali inayojitokeza hivi sasa kuwa na miradi zaidi ya asilimia 94 zinaendelea kwa fedha za nje na sisi tukiwa na chini ya asilimia sita. Hata makubaliano ya nchi za *SADC* hatujayafikia ya asilimia 10 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, waangalie utaratibu mpya wa kuagiza mbolea kwa kutumia *TFC* na soya kuachia wafanyabiashara mmoja mmoja aagize. *Stockists* waendelee kuwa wasambazaji. Mtindo wa kuagiza mbolea za nje kwa wingi itatupunguzia sana bei na hata umuhimu wa kuwa na ruzuku hautakuwepo. Mfano, *Urea 46% N* ukiagiza zaidi ya tani 12,500 bei kwa mfuko. *F.O.B* haizidi shilingi 10,000/= kwa mfuko wa kilo 50. Kwa nini utaratibu huu tusiujaribu?

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufanikiwa na nia ya Serikali kuagiza na kusambaza zana za kisasa za kilimo bila kuwa na *Tractor Service Centre* nchini. Makosa ya nyuma tusikubali yakajirudia. Kampuni binafsi zaweza kuhimizwa ili zitekeleze majukumu yake ya kuanzisha *Mechanized Service Centres.*

Je, mipango ya kuanzisha tafiti za mazao mbalimbali kikanda kwa kujengea mifuko yake yenyewe ili tuweze hapo baadaye kujitegemea, imefikia wapi ili badala ya kuendelea kuomba kila mara wahisani watusaidie kuendeleza tafiti zetu. Hii itatuwezesha tufanye kila tunachokitaka badala ya kuwaachia wao waamua nini tufanye.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kuendeleza suala nzima la Maonyesho ya Kilimo kwa kila Kanda. Kwa zaidi ya miaka saba sasa, ni miji ya Arusha, Mbeya na Morogoro peke yake ndiyo inayoendesha Nane Nane kila wakati. Hivyo, nini Sera ya

Maonyesho haya? Nini uamuzi wa Wizara kuhusu *future* ya maonyesho haya Kitaifa? Je, ni kuendeleza maonyesho kwa miji hii peke yake au ni pamoja na miji mingine?

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Wizara kuongeza wataalamu wa ushirika kwa Mikoa ambayo imekuwa ikiogopa kuanzisha hata *SACCOS* kwa kuogopa matatizo ya wizi wa fedha za ushirika katika Mkoa wa Rukwa. Tunaomba waletwe wataalamu wengi wa kufanya kazi hii muhimu . Hatuna watumishi!

Mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri na timu yake waone namna ya kufanya Mkoa kuwa mfano wa Mikoa mingine kwa kilimo cha maksai kwa kutumia zana mbalimbali. Vituo hivyo vya maksai viwe vya kisasa na viwe na zana zote muhimu za kukokotwa na ng'ombe. Hatua ya pili, tunaomba, matumizi ya matrekta na zana za kisasa zaidi zipewe kipaumbele kwa Mkoa hu wa Rukwa. Mheshimiwa Rais amekwishaombwa na wana Rukwa alipotembelea Rukwa mwezi Juni, 2007.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote. Naona kwa sasa kilimo kimepata wenyewe.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda nami nichukue nafasi hii kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo wa kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo. Pamoja na pongezi hizo bado nina maoni ambayo nadhani yanaweza kusaidia katika kuboresha sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni msingi mkubwa wa maendeleo, maafisa kilimo wapelekwe vijijini kwa wingi, maafisa kilimo wawekewe mazingira mazuri ya kuifanya kazi yao kwa kupatiwa usafiri (pikipiki), nyumba nzuri ya kuishi, mshahara mzuri, motisha kwa kila atakayefanya vizuri kwenye eneo lake na mafunzo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, pia kutoa ripoti kwa maendeleo ya sehemu yake, zana za kilimo ziwe ya kisasa ili kukuza na kuongeza maeneo ambayo yanastahili kulimwa, kuchukua hatua za makusudi ya kuwahamasisha wananchi kuchangia ununuzi wa trekta la kijiji au kata kwani kama tunaweza kuhimiza wananchi wakajenga shule na zahanati iweje washindwe kununua trekta lao ambalo Serikali isaidie au maafisa kilimo watoe mwongozo wa namna ya kutunza trekta hilo. Hapo tutakuwa tumeongeza pato la mazao. Lakini pia Serikali ifute *VAT* katika zana za kilimo za majembe ya kukokotwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe inaweka utaratibu wa kuwawezesha wakulima waweze kufikia uzalishaji wa mazao yetu kwa kiwango cha ubora wa Kimataifa ili kufikia au kuingia katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea, wananchi wengi hawana uwezo wa kununua mbolea ya kutosha, hivyo wapewe mbolea kwanza kwa mkopo na baada ya mavuno walipe deni hilo. Maeneo yenye maji au mito isiyokauka, Serikali iwasaidie wananchi kwa kuwatengenezea *system* ambayo wananchi watatumia na kisha baada kuanza utaratibu huo, waweke mfumo mzuri wa kuanza kulipa deni lao.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini Serikali haikuweka utaratibu wa tahadhari kwa kuvuna maji mengi yaliyomwagika kipindi cha masika yaliyokuwa na mvua nyingi? Ni kwa nini tuyaachie maji yaende tu hivi na wakati tunayahitaji? Ushauri, Serikali iweke mikakati ya kuanza kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kuliko kuyaacha maji yote yaende baharini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirika, naomba Wizara iwe karibu na Mkoa wa Singida, ili kuusaidia kuanzisha Chama cha Ushirika kwa kuwapa fedha za kutisha ili kuupa mkoa huo unaosemwa uko mwisho kiuchumi upate nafuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na nampongeza Waziri pamoja wasaidizi wake na watendaji wote kwa hotuba iliyopangika kwa umahiri na yenye uelekeo mzuri hivyo naipongeza kwa asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mengi yameshazungumzwa na yameshachangiwa mimi nina mapendekezo yafuatayo, kama tuanavyojua kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu kwa hiyo, kizidi kuimarishwa na kuwaelimisha wananchi juu ya kilimo cha kisasa cha sayansi na teknolojia. Pia mabwana shamba wazidi kusambazwa katika sehemu zote. Kuanzia tarafa, kata hadi vijiji na wawezeshwe kwa kupewa nyenzo ili wazidi kuelimisha wakulima wetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka zamani katika shule, vyuo, magereza na kadhalika, sehemu hizi zote zilikua zikijitegemea kwa kulima na kupata chakula chao kwa hiyo, wakiweza kujikimu kwa chakula chao na watalaamu walikuwa wakitembelea sehemu hizo kwa kuwapa miongozo, elimu na maelekezo na yaliyofanikiwa vizuri sana, hivyo suala hili kama halipo naomba lirudishwe kwani lilileta mafanikio sana.

Mheshimiwa Spika, pia vyama vya ushirika viimarishwe na wale mawakala warudishwe ili wayanunue mazao kule kule shambani, badala ya kuwaachia walanguzi wanaokwenda kuwalangua kwa bei ndogo, matokeo wakulima hawapati tija, wanabaki na umaskini, lakini hivyo vyombo vikiimarishwa tutaweza kuwakomboa wakulima wetu kiuchumi. Naitakia mafanikio kwa yote yaliyopangwa yatekelezeke.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia kwa mia moja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Lakini hata hivyo nina machache naomba yazingatiwe. Napongeza Serikali kwa jumla na nakubaliana na vipaumbele vya kutekelezwa vilivyowekwa na Serikali kwa maana ya elimu, miundombinu, maji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo sikubaliani na asilimia 6.2 iliyogawiwa kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kutokana na Pato la Taifa hasa ukizingatia kilimo

kwa ujumla wake ndiyo tegemeo kubwa kwa Watanzania yaani kinatoa ajira kubwa zaidi ya asilimia 75 na inachangia zaidi ya asilimia 44.

Mheshimiwa Spika, kama hilo nalo halitoshi basi kilimo ni muhimili kwa Taifa hili kwani bila ya kilimo hakuna chakula na bila ya chakula hapatakuwa na utulivu na bila utulivu Uhuru wa nchi hii utachangiwa. Kwa hiyo, basi nashauri Bajeti ijayo ya mwaka 2008/2009 kilimo kipatiwe angalau asilimia 10 ya gawio la Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa wanazozichukua lakini kwa sasa kuna jambo muhimu lilotatiza wananchi na wakulima, mfano mbolea, dawa, ugani na masoko.

Mheshimiwa Spika, bila ya mambo manne ya hapo juu niliyotaja bado tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, kukosekana maji kati ya hayo basi hatutaweza kuendeleza hoja za kilimo na hakutakuwa na lolote litakalofanikiwa. Wakati tunaimarisha hayo tujipange kwa siku za baadae tujiandae tena kuhimiza au kusimamia kilimo cha umwagiliaji, hili kwa kweli ndiyo ajenda inayofuatia baada ya kukaa nyuma katika miundombinu na kwa maana hiyo basi ndiyo maana nakubaliana na maji kupewa kipaumbele cha tatu kwani najua bila ya maji hakuna kilimo wala mifugo basi dhana ya kuimarisha mtandao wa maji itoe jibu kwa upanuaji wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Taifa hili bila ya chakula litanyanyasika na chakula ni kilimo, kilimo ni ajira, kilimo ni uhai, kilimo ni ukombozi, kilimo ni viwanda na viwanda ni maendeleo. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara kwa kuandaa Bajeti na hotuba hii. Niseme kweli nia na madhumuni ya Serikali katika kuinua kilimo na maisha ya Watanzania ni nzuri sana. Kwa kuwa tumeona jinsi nchi inavyoshindwa kujitosheleza kwa chakula na kusababisha upungufu wa chakula yaani njaa inayoendelea kuonekana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii Watanzania waishio vijijini wanaendelea kuishi katika maisha duni wakati mwingine chini ya dola moja kwa siku. Baada ya maelezo hayo naomba nizungumzie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo ni dhahiri mfuko huu ni msaada kwa wakulima, tatizo ni mdhamana katika baadhi ya maeneo. Napenda kuishauri Serikali iruhusu Halmashauri zetu zikope vifaa vya kulimia mfano matrekta makubwa na madogo, majembe ya kukokotwa na ng'ombe ili Halmashauri kwa niaba ya mfuko wa pembejeo ili isimamie. Naomba Serikali iniambie kwa nini mfuko huu hauthamini udhamini wa Halmashauri kwa wakulima wetu?

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu yapo maeneo mengine mfano Bukombe wananchi wake hawana hatimiliki aidha za mashamba au viwanja vyao.

Mheshimiwa Spika, pembejeo pamoja na kuwa na Shinyanga inaongoza kuzalisha zao la pamba bado wananchi wake ni maskini sana. Tunafahamu zaidi ya 60% ya zao la pamba inatoka Shinyanga. Katika Wilaya ya Bukombe karibu 79% ya wananchi wanaishi kwa kiwango cha chini ya dola moja za Kimarekani, wakati huo zaidi ya 90% ya wakazi ni wakulima. Wakulima hawa wanapata shida sana katika mustakabali wa pembejeo. Pembejeo hawazipati kwa wakati, dawa hawazijui, mbolea haiwafikii wakulima kwa wakati na hata kutopata kabisa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali yafuatayo, dawa za pamba na mbolea waruhusiwe wafanyabiashara binafsi/wabinafsishe ili kuwe na ushindani wa soko. Kwa kufanya hivyo wakulima watapata dawa, mbolea kwa wakati, watapata  dawa nzuri. Ili kuondoa usumbufu wanaopata wakulima hawa Serikali ihamasishe yafuatayo:-

Kwanza, wakulima wawasilishe vitabu vyao kwa makarani wakati wa mazao ili takwimu za mauzo yao zirekodiwe. Wanunuzi watoe takwimu sahihi za ununuzi, makarani waandike takwimu sahihi katika *passbook,* majina ya wakulima wa pamba yaorodheshwe mapema ili kazi za kuhakiki vitabu vya akiba *(passbook)* iweze kufanyika kwa wakati. Kwa kufanya hivyo tutaboresha maisha ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji, nashukuru Serikali kwa hatua waliyoamua kutekeleza kilimo cha umwagiliaji Mkoani Shinyanga, hata hivyo naomba Serikali iniambie kwa nini Bukombe hamuitengei fedha za kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, *DADPs* naomba Serikali itusaidie kujua takwimu za fedha zinazopelekwa Wilayani kwenye Halmashauri zetu. Kwani kwa kufanya hivyo itatusaidia kujua na kusaidia maamuzi ya matumizi ya fedha za *DADPs*.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishukuru Serikali kwa maamuzi ya kutoa ajira kwani hapa ndiyo sekta hii itaboreshwa. Madeni ya wakulima kupitia *KACU* na *SHIRECU* Serikali iyalipe. Naomba nijui ni lini wakulima waliokopwa na vyama hivi vya ushirika watalipwa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja mkono.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mipango ya kukuza sekta ya kilimo ni pamoja na kuimarisha mikakati ya kuongeza idadi ya wawekezaji binafsi. Hili ni jambo jema na hasa ukizingatia katika ulimwengu huu wa utandawazi ni dhahiri kwamba sekta binafsi ndiyo ambayo inatarajiwa kukuza uchumi wa nchi. Hata hivyo ni vyema tukafahamu ya kwamba tuwafikirie zaidi wawekezaji binafsi ambao ni wazawa na wazalendo wa nchi hii. Katika hili tunapaswa kuwawezesha ipasavyo Watanzania ili waweze kumudu ushindani katika soko la ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, ni vema basi Serikali ikaandaa utaratibu wa kuwakusanya vijana wahitimu wa vyuo mbalimbali wakashajiishwa kuunda makampuni ya kilimo. Kwa upande wake Serikali ihakikishe ya kwamba kampuni hizo zinapewa mikopo ya matrekta, pembejeo zote zinazostahili pamoja na ardhi ambayo tayari imeshawekwa

miundombinu ya msingi, maji, umeme na kadhalika. Mikopo hiyo ni lazima itoze riba nafuu na yenye kulipwa kwa muda mrefu. Kwa kufanya hivyo vijana wengi na hasa waliomaliza vyuo vikuu hawatapoteza muda kusubiri ajira, bali watajiunga pamoja ili kuanzisha miradi ya kilimo ikiwemo ufugaji.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umefanikiwa sana nchini Misri. Ni vema basi tukaiga kwani una manufaa makubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeazimia kusomesha na hatimaye kuongeza idadi ya maafisa ugavi kufikia 11,703 ifikapo mwaka 2010/2011. Aidha, Serikali imepanga kuwapatia usafiri iwe wa baiskeli au pikipiki ili mradi kuwawezesha kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, idadi hii ya maafisa ugani ni kubwa na bila shaka uajiri wao utashuka mpaka ngazi ya kijiji. Mimi napatwa na shaka moja kubwa nalo ni kwamba maafisa ugani hawa wameandaliwa makazi huko ambako watapelekwa kufanya kazi? Haitoshi tu afisa ugavi kumpatia usafiri lakini akawa nyumba ya kulala hana. Hili litakuwa ni tatizo kubwa na linahitaji kufikiriwa na mapema, vinginevyo ule ufanisi ambao tunautarajia kwa wagani, kamwe hautopatikana. Ni vema basi pakaandaliwa utaratibu wa kuwapatia mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao za kuishi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la msingi na ambalo linahitaji kuzingatiwa ni *specialities* za maafisa ugani ambazo wanatarajiwa kuajiriwa kwao. Ili tuondokane na mpango uliopo kazi za kila aina yaani mazao ya chakula mazao ya biashara, mifugo na kadhalika, hali hii haitotufikisha mbali. Ni vema basi maafisa ugani wakapewa kazi *specific.* Kwa mfano mifugo pekee mazao ya nafaka, mazao ya mizizi, mboga mboga, katani, korosho, pamba na kadhalika, tukifanya hivyo Afisa Ugavi atakuwa na nafasi na muda wa kutosha kushughulikia zao lake na kwa hivyo tija itaweza kuonekana kwa kipindi kifupi. Ikiwa hiyo itakuwa ngumu basi kwa kuanzia tuwagawe wagani katika fani zifuatazo:-

Mifugo uzalishaji, mifugo tiba, mazao ya mboga mboga, mazao ya biashara na kadhalika mpaka hapo baadae tukaweza kufikia kiwango cha *crop specific* au *specific field.*

**MHE. GEOFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha maisha ya wakulima. Hata hivyo napenda kuchangia kidogo kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani, kwanza napenda niishukuru sana Wizara kwa kufanya uchambuzi wa hali halisi ya huduma za ugani nchini. Uchambuzi unaonyesha kwamba mahitaji ni makubwa sana. Hata hivyo napenda niishauri Wizara iwe na mkakati wa makudusi wa kabisa wa kupeleka maafisa ugani katika maeneo ambayo yanazalisha mazao ya biashara kwa mfano, kahawa, pamba, chai, korosho na kadhalika, tukisubiri mpango wa miaka mitano wa kukabili upungufu huo kuanzia mwaka 2007/2008 tutakuwa tumechelewa sana.

Mheshimiwa Spika, ombi maalumu, sasa hivi zao la kahawa, mibuni inashambuliwa na magonjwa zaidi ya matano. Ili kukabiliana na hali hiyo naomba Wilaya ya Mbozi na hususani jimbo la Mbozi Mashariki ambalo hulima sana zao hilo ipewe watalaamu maafisa ugani wa kutosha mapema inavyowekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo za kilimo, kwanza napenda nieleze masikitiko yangu kwamba mwaka 2006/2007 Mkoa wa Mbeya ulipata mbolea kiasi kidogo tani karibu 18,000 kati ya mahitaji halisi tani karibu 70,000. Wilaya ya Mbozi ilipata karibu tani 64,000 kati ya mahitaji halisi ya tani 18,000. Pamoja na hayo bado mbolea hizo za ruzuku ya Serikali zilikuwa zinauzwa kwa bei kubwa kati ya shilingi 20,000 hadi 35,000 ni wakulima wachache sana ambao waliweza kununuliwa mbolea hizo. Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa kama tunataka kauli mbiu hiyo iwe na maana basi ni vizuri Serikali ihakikishe kwamba mbolea na mbegu za ruzuku zinakuwa za kutosha ziwafikie wakulima mapema na kwa bei ambazo wananchi wakulima wengi wanazimudu.

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya kilimo yatakuwa ni ndoto ya mchana kama mkulima hataangaliwa kipekee. Waziri Mkuu alipowasilisha hotuba yake alisema kiwango cha mbolea na mbegu za ruzuku ya Serikali kitaongezeka sina hakika kwa sababu mbolea ya ruzuku ilikuwa tani 108 tu, lakini kwenye hotuba ya Waziri Mkuu inaonesha mbolea ya ruzuku ya Serikali itakuwa karibu tano 80,000 kwa mwaka 2007/2008, Sasa hapa ongezeko liko wapi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha mfuko huo lakini maafisa wa mfuko huo wanawazungusha wakopaji sana. Baadhi ya watu waliokopa kutoka jimboni kwangu Mbozi Mashariki wamekuja kunilalamikia kwamba bila ya kutoa kitu chochote (rushwa) ni vigumu sana kupata mkopo. Aidha, maafisa wa mfuko wanapoenda Wilayani kuhakiki yale waliyoandika kwenye fomu zao pia hudai baadhi ya gharama. Napenda niishauri Wizara ifuatilie malalamiko ya wakulima/wakopaji hao. Mikopo ya mbolea na matrekta siyo zawadi hivyo pale mkopaji anapombwa rushwa na akatoa tunategemea atalipaje deni hilo?

Mheshimiwa Spika, nia ya kujenga kiwanda cha mbolea Mbeya. Baada ya kuona kwamba mahitaji ya mbolea ni makubwa nchini na hayatoshelezi wananchi wa Mkoa wa Mbeya kupitia Wabunge, Mheshimiwa Richard Nyaulawa wameamua kujenga kiwanda cha mbolea katika Mkoa wa Mbeya, chakato wa uanzishwaji wa kiwanda hicho unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nia ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya ni kwa manufaa ya wananchi wote nchini na kwa kuwa azma ya wananchi hao ni kuwapunguzia wananchi (wakulima) wa Nyanda za Juu, shida ya upatikanaji mbolea nchini, basi tunaomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ituunge mkono sisi wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kutusaidia kutafuta wawekezaji kwenye vyombo vya habari azma hiyo, itusaidie pia kuwahamasisha Watanzania wengi zaidi ili wajiunge nasi.

Mfuko tayari umeshasajiliwa kwa jina la *Mfuko wa Pembejeo Tanzania limited* na mfuko unaendelea kuuza hisa.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. Ahsante sana.

**MHE. JOB. Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilihimiza sana wananchi wa Kongwa kulima Mtama na Mahindi mwaka jana. Wananchi wameitikia wito na wamevuna sana mwaka huu. Wanauliza, wauze wapi? Soko hakuna! Tunataka *SGR* iruhusiwe kununua Kongwa.

Mheshimiwa Spika, bei ya mazao ya mtama na mahindi ni ndogo mno. Wananchi wanauliza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mnahimiza tu kilimo, mbona bei ya mazo haishughulikiwi ili iwe bora zaidi?

Mheshimiwa Spika, tunahitaji Bodi ya Mazao mchanganyiko haraka! Ninaunga mkono hoja.

**MHE. ADAM K.A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitambue kazi nzuri sana inayofanywa na Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Aidha, nawapongeza sana Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Christopher Chiza na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David. Pia, nataka nitambue kazi nzuri inayofanywa na Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo na watendaji na wataalamu wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Lakini pamoja na hayo, naomba niseme yafutayo:-

Kwanza Watanzania walio wengi ni wakulima wadogo wenye uwezo mdogo, ni watu maskini. Wataondokana na umaskini kwa kuzalisha zaidi kwa mazao wanayolima, pili, naomba nipate maelezo ya Serikali kuhusu mkakati wa *Rural Finance* ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimekuwa nazungumzia sana suala la fedha katika kilimo kama njia kuu mojawapo ya kumwezesha mkulima, siyo kumpa bure ili kumkopesha kwa namna ambayo ataweza kulipa kwa kuzingatia mazingira maalumu ya kilimo. Ni imani yangu kwamba ni lazima pawe na utaratibu wa kitaalamu *(coordination)* baina ya Idara Kuu husika za Serikali na kwamba jambo kubwa muhimu kama hili haliwezi kuwa jambo la Wizara moja peke yake. Lazima kuwa na njia kamili kabisa na ushirikiano wa taaluma na rasilimali wa fedha (Hazina), Mipango na Uchumi, Kilimo, TAMISEMI na kadhalika.

Tatu, lazima tufanye tathmini ya teknolojia. Mazao mengi ya wakulima *(family household level)* watagongana na tekinolojia kwa kupokea mbegu bora, mbolea nzuri, mafunzo ya kutosha na kadhalika, hawana ndoto ya kununua trekta, isipokuwa kama mikakati ya *Rural Finance* ikikamilika, basi nyumba hiyo ya mkulima mdogo inaweza ikapanga mikakati ya kuongeza uzalishaji wa kaya yao kama watapata uhakika kwa fedha za ziada kwa njia ya mikopo ruzuku.

Mheshimiwa Spika, mimi naendelea kuwa na wasi wasi mkubwa juu ya pesa zinazozidi kupelekwa kwenye ngazi za Halmashauri. Naamini kwamba taaluma iliyokuwepo ya usimamizi haitoshi, matokeo yake ni kwamba tunatengeneza bila kukusudia mazingira yanayosababisha kuwepo kwa pesa zinazobakia kwenye mifuko na hivyo kutengeneza tamaa za kula kwa upande wa wataalamu. Mfano wa hilo ni miradi ya umwagiliaji maji jimboni kwangu ya Yawayawa na Bupu. Miradi hiyo imechukua pesa nyingi, imezua matarajio makubwa ya mafanikio kwa wakulima na hakuna kilichopatikana. Matumizi makubwa, matokeo sifuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la uwekezaji kwenye kilimo lazima kipatiwe ufumbuzi. Matumizi yote ya fedha lazima yawe na malengo ya uzalishaji kwa thamani na idadi.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo *ASDP* na *DADPs* kwa shilingi bilioni 82 zilizokadiriwa baada ya miaka mitatu ya utekelezaji kama Taifa, Tanzania itakuwa imenufaika vipi kwa matumizi haya ndani ya sekta ya kilimo. Naomba *evaluation (assesment)* ya nini kinachotarajiwa kwa kulingania na malengo ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mzee wangu Mheshimiwa Stephen Wasira na namtakia kila la kheri. Naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii. Nitachangia maeneo machache nikianzia na Mkoani kwangu Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya biashara, kwa kuwa wakulima wanahimizwa kuongeza juhudi kwenye mazao ya biashara ikiwemo kahawa ya *Arabica* inayostawi Kilimanjaro na kwa kuwa mashamba ya wakulima hao ni finyu sana kati ya nusu ekari mpaka ekari tatu na kwa kuwa kilimo cha biashara kinaanzia hekta 20 na kuendelea; je, Serikali ina mpango gani wa kuwagawia wananchi yale maeneo yaliyokaa wazi yakingojea kilimo cha mahindi kwa msimu, mfano, mashamba ya *Primary Societies,* mfano shamba la *Machine Tools* na mengineyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu katani, je, Serikali ina mpango gani na mwekezaji aliyechukua mashamba ya katani huko Same na anasuasua kuyaendeleza? Je, mazao gani mbadala yaliyofanyiwa utafiti ambayo yatalimwa kwenye maeneo yenye uhaba wa ardhi kama Mkoa wa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie motisha kwa wakulima wa nafaka. Wakulima wengi Kilimanjaro takribani 80% ni wakulima wa nafaka kwa msimu yakiwemo mahindi. Serikali inasisitiza kilimo chenye tija, tatizo ninaloliona hapa ni gharama kubwa za kilimo na mvua za wasi wasi. Pamoja na hayo yote, wakulima hawaachi kuandaa mashamba mwaka hadi mwaka na kuotesha hata kama mwaka uliotangulia hawakufanikiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kuiomba Serikali sasa ipange bei ya chini ya kilo/gunia la mahindi ili wananchi waweze kupanga gaharama za kilimo. Mkulima

atakapojua bei rasmi ya gunia la mahindi, atahamasika kulima kwa nguvu zote na atakuwa na matarajio ya uhakika ya kurejesha gharama zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umwagiliaji wa matone kwa zao la kahawa, kwa kuwa sasa wakulima wakubwa wa kahawa na chai wanatudhihirishia kuwa ili mazao haya mawili yashamiri, yanahitaji maji kwa kiasi mfululizo. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuchangia utaalamu huu wa *drip irrigation* kwa wakulima a kawaida?

Mheshimiwa Spika, uvumi kuhusu madhara ya dawa za kahawa, hivi karibuni kumekuwepo na shida kubwa ya kupata wachumaji wa kahawa kwenye mashamba makubwa ya wawekezaji kutokana na uvumi kuwa dawa zinazotumika zinaua. Jambo hili limetokea huko kwenye mashamba ya *Tchiba Estate* huko Moshi. Kwa kuwa utafiti huwa unafanyika kabla dawa kutumika, naomba Serikali iwahakikishie wananchi kuwa dawa hizo ni salama kwa afya za wanadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa mbegu bora, hapa naiomba Serikali itoe tamko kuhusu ushiriki wake katika kusaidia wakulima wadogo wanaozalisha mbegu bora hususan zile za mahindi. Mpaka hivi sasa mbegu nyingi zinaagizwa kutoka nje. Ni lini basi tutajikomboa kwa hilo? Naomba jibu kwenye majumuisho.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili nami kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba niweze kuchangia katika hotuba hii.

Aidha, natumia fursa hii kutoa salaam za pole kwa familia za Marehemu Amina Chifupa, Stephen Kazi, Mzee Ndonho na Mzee Kasubi waliopoteza maisha hivi karibuni kutokana na vifo vilivyotokana na sababu mbalimbali. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hawa na wale wote wa ajali za magari barabarani katika mikoa ya Singida, Arusha, Mbeya na kwingine kote hapa nchini, mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninayo maeneo machache tu. Eneo la kwanza ni kuhusu upatikanaji wa chakula. Naipongeza Serikali kwa tathimini hiyo inayotoa matarajio na matumaini makubwa ya kutokuwa na njaa. Tahadhari, katika maeneo ya Kwimba walikopata mavuno mazuri ya mpunga maeneo hayo ndiyo maeneo yanayotegemea Pamba kama zao la biashara. Mvua zilizosababisha mpunga kupatikana kwa wingi ndizo zilizofanya Pamba isipatikane kwa wingi. Hivyo, tathimini inaweza kuonyesha kuwa maeneo haya yana chakula lakini kumbe wananchi wamegeuza baadhi ya mazao yaliyofikiriwa kuwa ni ya chakula tu kuwa ni ya biashara kutokana na zao lao la Pamba kutopatikana. Ushauri wangu, Serikali isiache kutoa tahadhari kwa wananchi kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha angalau kwa mwaka mzima. Kila usemapo hilo, useme vile

vile ni kiasi gani kinahitajika kwa mtu mmoja kwa mchanganuo wa nafaka na maharage/choroko/kunde.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kama Pamba, Serikali ielekeze/iielekeze Bodi ya Pamba kupitia mfuko wake wa kuendeleza Pamba *(CDF)*, iwe inatenga kiasi cha fedha kurekebisha bei ya Pamba hasa bei ya Pamba inaposhuka sana katika soko la dunia ili wananchi wasikate tamaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za mwaka 2006/2007, naipongeza sana Serikali kwa mipango yake ya kipindi hicho na kiwango cha utekelezaji kilichofikiwa. Naamini yalikuwa mandalizi mazuri kwa kuiwezesha sekta hii kuanza kuendelea kwa kasi kubwa na ulikuwa ni msingi wa mambo yajayo. Napongeza sana!

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa mwaka 2007/2008, naipongeza Serikali na kuunga mkono mipango hiyo hasa ile inayolenga kuendeleza sekta ya kilimo hususan huduma za ugani. Kilimo ni taaluma na taaluma haina budi kufundishwa, tena kwa vitendo. Wananchi wetu wengi hawana taaluma hiyo, wamekuwa wakilima kwa kutumia uzoefu tu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa makusudi wa kuongeza wataalamu wa ugani. Hawa ndio watakuwa walimu wa wakulima wetu. Ni muhimu wataalamu hao kwanza waende vijijini si kwa nia ya kupanua mashamba, bali kwa nia ya kuongea tija. Pia, waende vijijini si kama wataalamu, bali kama washauri kwa wakulima walioko tayari vijijini wanaolenga kupata zaidi kwa hekta. Lengo ni kuwafanya wakubalike. Wasiende kama viongozi, wasiende kama wakaguzi waende kama washiriki. Wakikosea mahali pa kuingilia, zoezi zima litakuwa bure. Waende vijijini wakiwa na mabega yanayolingana na ya wananchi watakaowakuta huko. Wasipande sana wakawaacha mbali wananchi na wasishuke sana kudhalilisha taaluma na sababu iliyosababisha wapelekwe huko ninaamini kwa kuwaheshimu watu na kutanguliza uzalenda sekta hii itaenda haraka.

Mheshimiwa Spika, wataalam hao tunawahitaji sana Kwimba kwa kuwa kati ya vijiji 187 ni vijiji 37 tu vilivyo na wataalamu hao. Hata hawa walioko huko vijijini kwa sababu moja au nyingine wengi nao hawatekelezi shughuli iliyowapeleka huko, wamebaki kuwa ni waajiriwa tu (hawana-*impact).* Wilaya hii iwe ya kwanza kufikiriwa kupelekewa wataalamu hao kwa vile walioko huko tayari wamezidiwa na kazi na wamekata tamaa. Kwa hali waliyonayo sasa hawawezi tena kuleta mapinduzi yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, maandalizi kwa ajili ya mapinduzi ya kijani, mipango naipongeza na kuiunga mkono. Hata hivyo hapa nina machache ya kuboresha. Matumizi ya mbolea yaangaliwe sana kwa vile matumizi mabaya yanaweza kuwa na matokeo mabaya na yenye gharama kubwa kurekebisha. Sambamba na matumizi ya mbolea ya chumvichumvi kuangaliwa kwa uangalifu mkubwa, bila elimu ya kutosha matumizi ya matrekta nao yaangaliwe sana. Hoja isije ikawa kupanua mashamba tu bali kuzalisha

zaidi kwa hekta. Hivyo, matrekta yapelekwe tu kule yanakohitajika yasipelekwe si tu kwa kuwa kuna fedha bali ni kwa kuwa yanahitajika kweli.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, mfuko wa kukopesha wakulima uanzishwe. Pili, tulenge kuongeza pato kwa hekta na akiba ya chakula ya kutosha kutokana na hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naunga mkono asilimia mia kwa mia na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na wahusika wote.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa kwamba hali ya kilimo hususani uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hairidhishi wala haikidhi mahitaji halisi ya Watanzania ya chakula na mauzo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba sekta ya kilimo inakua kwa kiwango cha asilimia tano kwa mwaka kiasi ambacho ni kidogo mno. Mchango wa Pato la Taifa *(GDP)* wa 50% ni mdogo mno hasa ikizingatiwa ya kwamba asilimia 80 ya Watanzania wote hutegemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa kiwango kidogo katika sekta hii, Taifa limekuwa halijitoshelezi kwa chakula na kulazimika kuagiza chakula toka nje kwa fedha zetu adimu za kigeni na hata kuomba misaada toka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya mazao nchi za nje yamepungua na kubaki chini ya 55% ya mauzo yote. Mapato ya wakulima kwa ujumla yameshuka na kusababisha umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hali hii mbaya ya kilimo na uzalishaji wa mazao imeathiri pia mipango ya kimaendeleo na uchumi. Kwa ujumla mipango mikubwa ya MKUKUTA na *Millenium Development Goals* iko mashakani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii mbaya ni dhahiri Serikali ikaangalia upya namna ya kukuza kilimo chetu. Ni lazima kufanya mkakati wa kuongeza ekari au maeneo yenye mkakati wa kuongeza ekari au maeneo yanayolimwa na kupandwa mazao kwenye ngazi za vijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa. Ipo haja ya ku-*mobilize* wataalamu wote wa kilimo na viongozi wa siasa waende vijijini kusimamia malengo yote yaliyopangwa katika mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuangalia upya sera ya ndani ya Taifa *(Domestic Policy)* ya Azimio la Iringa la mwaka 1972 kuhusu Siasa ni Kilimo. Ni lazima Serikali ihimize katika kuondoa kilimo cha viraka viraka (vishamba vidogo vidogo) na badala yake mashamba yapimwe na kuyaweka katika *blocks* ili kurahisisha utoaji huduma kwa wakulima kupitia maofisa ugani.

Mheshimiwa Spika, lazima kuwepo na mkakati wa kuhakikisha kila mkulima anapata pembejeo na zana anazohitaji kabla ya msimu haujaanza na kila kijiji au kata

kiwe na mfuko wa pembejeo na zana za kilimo ambazo utasimamiwa na Kamati teule za vijiji au Kata.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuongeza Maafisa Ugani ili kuongeza ufanisi na Maafisa Ugani *(Extension Officers)* hawa wapewe *package* nzima ya utaalamu wa kilimo ili kutoa huduma bora. Pia ni vema Maafisa hawa wakapatiwa *either* baiskeli au pikipiki ili kuwawezesha kuwafikia wakulima.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwe na mkakati maalumu wa kuondoa jembe la mkono kwani kwa kutumia zana hii hafifu hatutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ishirikiane na ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili kuhakikisha vyanzo vya maji haviharibiwi na hivyo kutumika vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuimarisha maeneo mbalimbali nchini yenye ardhi nzuri na mabonde kando kando ya mito mikubwa ni wa muhimu sana. Uwepo mkakati wa kukaribisha mara kwa mara wawekezaji wakubwa ili waweze kuyaendeleza mabonde hayo kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri uwepo mkakati wa kuwapa wakulima hususani wale wadogo wadogo mikopo kwa ajili ya kilimo. Pia ipo haja ya kuanzisha Benki ya Wakulima hususani wakulima wadogo wadogo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali ni lazima iweke na kuimarisha huduma na utafiti wa mazao *(research services)* ambazo zimezorota mno. Japo ni kweli kwamba kuna hazina kubwa ya matokeo ya utafiti wa kilimo yaliyokwishapatikana lakini inaonekana dhahiri kwamba kiwango kikubwa cha matokeo hayo hakijafika kwa wakulima na kutumika kuendeleza kilimo chao.

Kwa hiyo, mkakati wa kuimarisha huduma za utafiti wa kilimo ziende sambamba na ufufuaji na uimarishaji wa huduma za ugani. Serikali ihakikishe kiungo hiki kinaimarishwa na kuwa chenye matokeo yaliyokusudiwa *(result oriented)* ya kuwezesha matokeo ya utafiti kuwafikia walengwa na kutumika ipasavyo ili yainue kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kulitazama kwa jicho la kipekee suala zima la kuimarisha na kuendeleza kilimo cha mazao ya biashara nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera pamoja na Mikoa mingine ina mazao ya biashara ambayo ni kama jadi ya wananchi. Mfano, Kagera ni wakulima au wazalishaji

wazuri wa buni/kahawa. Lakini sasa zao la buni/kahawa limekosa soko baada ya bei kuwa haitabiriki, hata wakulima wamepunguza ukubwa wa mashamba na hivyo kuathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie upya kulifufua zao la buni. Mashamba yafufuliwe pia yapanuliwe. Hii itawezekana iwapo tu wakulima watakuwa na uhakika wa bei kuaw nzuri. Naishauri Serikali itafute masoko ya buni/kahawa.

Mheshimiwa Spika, wakulima wafundishwe kulima mashamba yanayoleta tija yaani yawe bora. Izingatiwe kiasi kinachozalishwa kile ekari. Wakulima wapatiwe mbegu bora na hasa naomba yawepo mashamba/vitalu vya miche bora. Miche ipelekwe kwa wakulima ili tuinue zao hili la biashara.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa ugani pia ni muhimu, wawepo na wapewe malengo ya kazi, ili wapimwe kwa kushindana na malengo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, wakulima sasa wapewe elimu wao wenyewe katika vijiji vyao badala ya kuwaelimisha wataalamu wa ugani na viongozi wa Kiserikali tu. Mara nyingi hawa wataalamu na viongozi wa Kiserikali hawafikishi ujumbe unaotakiwa kwa walengwa, ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, ushirika ni njia pia itakayoinua Taifa letu. Serikali ibuni mkakati wa kuhakikisha wakulima wanajiunga katika ushirika wao ili kwa pamoja waweze kufikiwa na wataalamu na huduma zingine muhimu. Naishauri Serikali itilie maanani kurudisha moyo wa ushirika ili tupate mazao kwa wingi, hali itakayoinua Taifa letu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutuletea *STABEX*. Sisi Mkoa wa Kagera na hasa Jimbo la Muleba Kaskazini, tulinufaika na barabara nzuri na bora.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali isiache barabara hizo kuharibika tena, iendelee kutenga pesa za kukarabati barabara hizi. Aidha, wananchi kule vijijini wajifunze na kufuata utunzaji wa barabara zetu ambazo tayari tumezipata.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kutayarisha hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo: Moja, uhaba wa Maofisa Ushirika ni kikwazo kikubwa katika kuhamasisha wananchi kuelewa umuhimu na manufaa ya Ushirika na Akiba na Mikopo. Kwa sababu hiyo Wizara iongeze watendaji wa Ushirika kwa kila Kata ili iwe rahisi kiutekelezaji.

Pili, Maofisa Ushirika wa Wilaya wapatiwe usafiri (magari) ili iwe rahisi kwao kuwafikia wananchi na kuharakisha maendeleo.

Tatu, Serikali kupitia Wizara husika iwe na vipindi maalumu vya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kwa njia ya televisheni, redio, vijarida na pia kuwa na utaratibu wa kuelimisha wananchi vijijini kwa njia ya *projector.*

Nne, kwa kuwa Tanzania ina eneo kubwa sana kwa kilimo imefika wakati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wapewe maeneo kwa ajili ya kilimo ili waoneshe mfano kwa Watanzania na walime mazao yatakayouzwa ndani na hata nje nchi.

Hali hiyo itahamasisha wananchi wengi zaidi kuitikia kilimo cha kisasa. Kila Mbunge alime si chini ya ekari 50; na zao la alizeti na zabibu lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, Bonde la Rufiji lina nafasi kubwa sana kwenye suala la kilimo hasa mpunga, sikuona mkakati wowote kwenye Bajeti hii, hivi hawa wataalamu hawalioni hili?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilipata bahati ya kuzungumza na *Deputy Speaker* wa Vietnam, mfanikio yao kwenye kilimo yametokana na kuboresha maslahi ya mabwana shamba kwenye maeneo ya mashamba. Je, sisi tutafanya hivyo au wataendelea kukaa ofisini?

Mheshimiwa Spika, zao la korosho Serikali sasa iwaunganishe wakulima hao na makampuni ya China, sio kuruhusu watu toka India. Ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba nzuri na iliyosomwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Naibu Mawaziri wote wawili, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi na Watendaji kwa kuandaa Bajeti hii ya Wizara vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendeleza na kuboresha vyama vya ushirika. Katika mwaka 2006/2007 ni *SACCOS* zaidi ya 1,400 zimefunguliwa na ni 25 tu zimepewa mafunzo. Ili *SACCOS* kama vyama vya ushirika viweze kukua, kupata faida na kuendeshwa kisayansi inabidi wanachama na viongozi wapate elimu juu ya uendeshaji wa *SACCOS* kibiashara na elimu ya juu ya ujasiriamali. Hii itasaidia kuwafanya wananchi wajue umuhimu wa kujiwekea akiba mara kwa mara na kwa kutumia *SACCOS* watapata mitaji ya biashara na shughuli zao za kuwaletea kipato, kwa masharti nafuu. Wasiwasi wangu ni kuwa fedha za Serikali za mfuko wa uwezeshaji zinazotolewa *SACCOS,* zinaweza zisilete matokeo tarajiwa kama suala la mafunzo lisipotiliwa mkazo.

Mheshimiwa Spika,  wote tunatambua umuhimu wa vyanma vya ushirika vya mazao. Tangu vyuma watu  wamepata maendeleo, uchumi wao ulikuwa na waliweza kuwapeleka watoto wao shule kwa kupitia vyama vya ushirika. Vingi vya vyama hivi vimekufa au vinachechemea kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo madeni makubwa.

Mheshimiwa Spika, ili vyama  hivi kama *KNCU* na *KDCU* vya Mkoani Kagera, viweze  kutoa huduma kwa wananchi/wanachama  ipasavyo ninaomba Serikali iweke mpango wa kuvilipia madeni yote ili waweze kuendesha shughuli  zao  kwa ufanisi zaidi.

Vile vile kuna viwanda kama *BUKOP,* kiwanda cha kukoboa kahawa kilicho Mjini Bukoba lakini kinahudumia mkoa mzima visaidiwe. *BUKOP* ni kiwanda cha zamani, kimechakaa, hivyo kinaongeza gharama za uendeshaji na kiwanda kinafanya kazi kwa hasara. Hasara hii inachangia bei ya kahawa inayotolewa na vyama vya ushirika kwa wakulima kuwa ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba katika kufufua ushirika Serikali itenge fedha zisaidie kufufua kiwanda cha *BUKOP* ili  kuupunguzia mzigo na kuongeza bei ya kahawa ya mkulima.

Mheshimiwa Spika, dunia inaendelea na Tanzania tunaendelea hivyo hatuwezi kuendelea kukumbatia mazao tuliyoaoea kama *traditional crops* tu kama kahawa, pamba na kadhalika wakati umefika sasa  wa kuweka mikakati ya  kuinua mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa wa Kagera, tangu bei ya kahawa iliposhuka kwenye soko la dunia watu wengi wamezidi kuwa maskini kwani kipato kimeshuka. Lakini Mkoani Kagera hali ya  hewa ni nzuri, watu wanaweza kulima na kuvuna hata mara mbili kwa mwaka. Mazao yanayoweza kulimwa  na kuleta faida kwa wananchi kuliko hata kahawa ni kama mahindi, maharage, *vanilla* na karanga.

Mheshimiwa Spika, tatizo lilipo ni kukosa chombo maalumu cha kununua mazao hayo (soko la uhakika). Hii inasababisha Watanzania  hawa waachwe kwa walanguzi ambao hununua kilo ya mahindi hadi kwa shilingi 150, kiasi hiki ni kidogo sana, hakiwezi kutosheleza hata gharama za mkulima.  Lakin ihawa walanguzi wanauza karanga kwa shilingi 800 kwa kilo, Maharage shilingi 450 kwa kilo na mahindi shilingi 400 kwa kilo, je, Serikali ina mipango gani ya kuweka chombo au soko la uhakika kusudi wakulima hawa wasilanguliwe na wapate fedha za kutosha na wahamasike  kulima zaidi?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika  na wote walinaomsaidia katika kazi hii ngumu, kwani kama tujuavyo kilimo ndio kila kitu, bila ya chakula  hakuna maendeleo yoyote kwani mazao yakiwa mazuri  huleta hata fedha za kigeni kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na kilimo, nchi yetu inategemea sana kilimo na tunamshukuru Mwenye Enzi kwa kutupa ardhi iliyo nzuri na inayofaa kwa mazao ya aina yote.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie sana kutoa elimu kwa vijana ili tupate mabwana shamba wenye ujuzi wa kujua ardhi ipi ni nzuri kwa zao lipi, pili, ugonjwa wa zao lolote unapozuka wawe wepesi wa kuhcukua hatua ya kutoa matibabu kwenye zao husika, tatu, wawe karibu sana na wakulima bila ya kujali mkulima mdogo au mkubwa, nne, awe mkweli wa kuwashauri wakulima kuhusu mbolea gani inayofaa kwa wakati gani na fedha ipi na pia kuwa na ujuzi wa kugundua mbolea iliyokwisha wakati au iliyoharibika.

Mheshimiwa Spika, mabwana shamba wakiwa wengi na kusambaa maeneo yote ya kilimo sio kung'ang'ania kukaa ofisini au mijini basi matunda yataonekana.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa sana kuona zao la pamba na sukari kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 limeshuka nikijiuliza kwa nini napata jibu ya kuona kwamba labda wakulima wamekata tamaa, hii si vuziri ni bora kurudi nyuma na kufufua kwa nguvu zote kilimo hicho hasa cha pamba, kuwapatia wakulima mbegu nzuri na ushauri wa kufana ili zao la pamba lipande maradufu. Kama ilivyotiliwa maanani chai na kuongezwa kwa mashamba ya ziada na kupatikana mbegu bora kama alivyoeleza Waziri ukurasa wa 12 na 13 wa kitabu basi ni hivyo tufanye kwa mazao mengine ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kama ikigundulika kwamba wafanyakazi mashambani au wanaoishi karibu na mashamba husika wamefanya ubadhilifu au uharibifu wa mashine au kuunguza mashamba kama walivyofanya wa *TPC*, Moshi wasiachwe hivi hivi kwa kufukuzwa hii kazi bali hatua kali za kisheria wachukuliwe na ikiwekana hukumu ziwe kali, kwani wanapoachishwa tu kazi, haiwi ni fundisho kwa waliobaki, adui yupo popote kama wametumwa na maadui wa maendeleo ya nchi yetu basi wakitoka pale watapata kazi eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kugawa mbolea uzingatie sana usimamizi wa Mheshimiwa Mbunge kwenye eneo husika, mbolea igaiwe kwenye maeneo ya mashamba ambayo hasa yana ushirika wa vyama kama *SACCOS* ambapo Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na bwana kilimo wa Wilaya wasimamie ugawaji wa mbolea hivyo, kuhakikisha inawafikia wakulima kwa bei halali na marejesho yanapokelewa kwa wakati muafaka. Kabla ya ugawaji wa mbolea hiyo uchunguzi ufanyike kwa kuhakiki mbolea aina gani inatakiwa eneo hilo na kwa kiasi gani bwana shamba wa eneo ashirikiane na ofisi ya Wilaya wafanye kazi ya kupata mbolea husika, pembejeo na mbegu kwa wakati wake; usimamizi wa kutosha ufanyike sio maagizo tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana. Vijana wengi wamesambaa mijini na wazurura hovyo bila ya kazi maalum. Vijana hawa wakusanywe na Wizara maalumu inayoshughulikia vijana baada ya kupata takwimu sahihi ya vijana waliotayari kujihusisha na kilimo Wizara ya Ardhi ihusishwe kutoa eneo la ardhi na bwana shamba apatikane, vijana hawa wapelekwe kwenye maeneo ya shamba, Serikali ikiwa

tayari kupata fedha ya kusaidia vijana hawa kwa mwaka mmoja tu, vijana hawa wapatiwe, ardhi, mbegu, pembajeo na matrekta na bwana shamba waelekezwe kwenye kilimo kwa kutegemea ardhi waliyopewa ni nzuri kwa zao gani, aidha, matunda, mahindi, mpunga na zao gani hasa wawe wanapata chakula kwa wao wenyewe kuzalisha na hapo hapo waelekeze nguvu zao kwenye kilimo cha zao la biashara kwa kuuza nje ya nchi na hata ndani. Wasimamiwe katika kupata soko na njia ya kufikisha mazao yao kwenye soko husika.

Mheshimiwa Spika, vijana wakikusanywa na kupatiwa ushauri na kuunganishwa kwa kuundiwa ushirika wao, nina hakika wimbi la hatari lililosambaa bila ya kazi maalumu ambapo ninavyoona mwisho si mzuri, tutakuwa tumepata angalau ufumbuzi kilimo ni umaskini wetu walivyo bila kilimo ni utajiri mkubwa, kinachohitajika ni usimamizi wa nguvu moja.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ni kilimo kibaya ila kinachohitajika kukusanya maji yaliyo mengi wakati mvua zinaponyesha, nchini kwetu mvua huwa zinanyesha kwa wingi wakati zinapamua kunyesha tutoe ushauri wa kukusanya maji haya na Serikali iwe tayari kukabiliana na matumizi ya kujenga mabwawa ya kukusanya maji, wakulima eneo la pembezoni mwa mabwawa husika wasimamiwe na kutumia ardhi na maji husika kwa kilimo kama ilivyo kwenye pembe za mifereji ya maji ya *TPC* na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, vyama vya ushirika vipewe kipaumbele kwa kupatiwa wanaushirika wenye elimu ya kutosha kusimamia vyama hivyo na na wenye ukweli na uaminifu, wasiwe wachovu kwani wanapokuwa machovu huchangia kuiba na kushirikiana na walanguzi kuuuza mazao kwa bei kubwa lakini hapo hapo mkulima akipatiwa sumni ya bei hiyo bei za mazao zisimamiwe kikamilifu na maafisa wa kilimo Wilayani na mnunuzi yeyote anayekuja kununua mazao awe anatambulika na Wilaya husika kabla hajaenda kwa mkulima kununua mazao, Serikali Wilayani isiache tu wanunuzi kiholela kwenda kuwadanganya wakulima na kununua mazao yao kwa bei wanayopanga wao. Mkulima ashirikishwe kupanga bei ya mazao yake kwani yeye ndiye anayejua hasara na gharama aliyotumia kwenye mazao yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali kuweka macho kwenye kilimo na vyama vya ushirika na kuhakikisha mkulima ajione siyo maskini bali ni tajiri. Kupunguza vijana kukimbilia mijini. Ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayokwamisha kilimo nchini na ambavyo ni lazima Wizara iyafanyie kazi ni Wizara ya Kilimo ichukue jukumu la kuwapa elimu wananchi ili kuwapa ushauri wa kulima mazao yanayokwenda sambamba na hali ya hewa, kilimo kinacholimwa kiende sambamba na utabiri wa hali ya hewa, upungufu wa *Extension Officers* pamoja na wao pia kutokuwa na nyenzo za usafiri ili kuwawezesha kuwasikia wananchi, pembejeo na hasa mbolea kutokuwafikia wakulima katika kipindi

kinachotakiwa. Hii ina kwenda sambamba na kuwatumia wazabuni wa mbolea ambao wanawapandishia bei wananchi kinyume na bei iliyopangwa na Serikali, fedha zinazotengwa kwa ajili ya kitengo cha utafiti wa mazao ya kilimo kimekuwa kikitengewa fedha kidogo, Wizara itilie mkazo *research centres* zote za kilimo kwa kuwapatia fedha za kutosha za uendeshaji, Wizara isimamie kilimo cha viraka viraka ili wakulima waweze kufikiwa kwa urahisi na mikopo ya matrekta itolewe kwa wananchi ili kupunguza adha ya kilimo cha mikono kinachotumika katika maeneo yaliyo mengi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninapenda kushauri ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali ifungue vyuo vyote ambavyo vilikuwa vinatoa mafunzo ya *certificate* ya kilimo na kuwawezesha kupata hao *extension officers* ambao ndiyo wanaowafikia wakulima zaidi ya wote wanaotoka na *Diploma* na kwenda kufanya kazi maofisini.

Pili, kiwango cha 6.2% kilichotolewa kwa wakulima ni kidogo mno. Nashauri Bajeti ya mwaka mwingine wa fedha upandishwe (iongezwe). Kilimo ni uti wa mgongo kinachotoa ajira kwa wananchi kwa 80%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Kilimo na Naibu Mawaziri wote wawili kwa jinsi wanavyojitahidi kutafuta kila mbinu ya kuboresha kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu lililonisukuma kuchangia Wizara hii ni kilimo cha zao la tangawizi jimboni kwangu Same Mashariki. Zaidi ya asilimia 60 ya wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki wanaishi milimani sawa na na tarafa mbili na sawa na kata kumi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wa Same Mashariki milimani wanategemea kilimo cha tangawizi, hili ndilo zao maarufu Same mlimani. Zao hili ni zao adimu sana. Nikuhakikishie kabisa asilimia kubwa ya tangawizi inayotumika Tanzania inatoka katika milima ya Same Mashariki na Magharibi.

Mheshimiwa Spika, zao la tangawizi ni zao linalostawi vema iwapo litapata maji ya kutosha. Linapokosa maji ya kutosha halistawi kabisa. Tarehe 10 Februari, 2006 niliandika barua Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuiomba Wizara itume wataalamu wake ili kwanza Serikali ione ni kiasi gani wananchi wangu wanajitahidi kulima tangawizi na pia Wizara ione umuhimu wa kuwasaidia wananchi wangu njia ya kuhifadhi maji ili upatikanaji wa maji uwe wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ninayo nakala ya barua hiyo ambayo nina uhakika kabisa Serikali waliipata lakini sikujibiwa chochote hata kwa njia ya mdomo. Kutokujibu barua kunaashiria nini? Ninaiomba Serikali isiwe inapuuza mambo muhimu yanayogusa uhai wa wananchi waliotuchagua kuwawakilisha.

Mheshimiwa Spika, kilio changu tangu nilipoandika barua ni kuiomba Serikali ikaone kilimo cha tangawizi kilivyoshamiri Same Mashariki ili Serikali itoe utaalamu zaidi. Pili niiombe Serikali sasa bila kuchelea itume wataalamu wake ili ikatupatie njia nyingine mbadala ya kuhifadhi maji kwani wananchi wakipatiwa mabwawa ya kuhifadhi maji wataweza kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nina imani kabisa kama wataalamu wa kilimo au Waziri mwenyewe angefika kuona kilimo kile cha tangawizi na matatizo yanayowakabili wananchi wangu kutokupata maji ya kutosha basi leo hii wananchi wangu wangepata japo mabwawa madogo machache ya kuboresha kilimo cha tangawizi.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anafunga mjadala huu anijibu kwamba kwa sababu barua niliyowapelekea kuhusu matatizo ya kilimo cha tangawizi ambayo nakala ninayo haikujibiwa na wala Serikali haikutoa msaada wowote tangu tarehe 10 Februari, 2006 sasa hivi Serikali inawasaidiaje wananchi wangu ili waboreshe kilimo cha tangawizi na kuboresha maisha yao.

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kutumia fursa hii adhimu uliyonipa kuwapa pole wazazi wa Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, aliyekuwa Mbunge, Viti Maalum, Vijana. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Pepon, *Amin!*

Mheshimiwa Spika naomba kuchangia yafuatayo katika Bajeti ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kutilia mkazo utafiti katika nyanja mbalimbali za kilimo kulingana na mahitaji ya uzalishaji endelevu. Siku zote kutakuwa na mahitaji ya mbegu za mazao mbalimbali zitakazohimili mabadiliko ya hali ya hewa, udongo na mahitaji ya ulaji wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na upendeleo maalumu wa kuongeza eneo la umwagiliaji maji, hili liambatane na elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya maji kwa uzalishaji bora zaidi na wenye tima zaidi. Hii ina maana mazao ya kumwagilia yaendane na pamoja na tija ya kubwa kwa mazao husika, Wizara ya Kilimo, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wawe na mkakati maalumu wa kutoa elimu ya ufundi *(VETA)* kwa mahitaji ya wakulima wa vijijini *(appropriate technology).* Hili litasaidia sana katika kutatua matatizo ya kiufundi yanayotoka mashambani. Elimu ya ufindi vijijini ikiambana na na viwanda vidogo vidogo vijijini pamoja na upatikanaji wa *prime movers* huko huko itasaidia sana maendeleo ya kilimo vijijini.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembajeo mbalimbali za kilimo bado ni tatizo kwa vile zinahodhiwa *(monopoly)* ya wachache. Tatizo kubwa hasa kwa baadhi ya

pembejeo za dawa *(agrochemical)* zinatolewa zabuni kwa kutumia *trade name* badala ya *fabric name*. Hili limewapa udhibiti mfanyabiashara mmoja na wengine wanaoleta bidhaa ili ile yenye ubora wa kemikali ile ile wanakataliwa kwa sababu ya jina tu. Mfano hai ni ule wa *Sulphur* ya ajili ya korosho.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani kupewa mafunzo ya mara kwa mara kulingana na matokeo mapya ya utafiti sambamba na hili, maafisa hao wafikiriwe kupatiwa usafiri wa kuaminika.

Mheshimiwa Spika, pia kuwepo na msukumo maalumu wa kutumia mashine ndogo ndogo kwa wakulima kulingana na ukubwa wa kilimo chao. Siyo wakulima wote wanaweza kutumia matrekta *economically power tillers, ox-draft implements, portable irrigation equipment* vinaweza vikawa na tija zaidi kwa wakulima wenye uwezo mdogo. Ni wakulima kama hawa ndiyo wapatiwe mikopo midogo midogo kulingana na mahitaji ya kilimo cha eneo dogo na la kati.

Kuhusu mikopo kwa ajili ya pembajeo ya muda mfupi na muda wa kati ni muhimu sana kwa wakulima wadogo na wa kati. Hili litiliwe mkazo. *Afro-processing* ipewe kipaumbele, hili liambatane na mtumiaji wa teknolojia mbadala mashambani ili kupata umeme kwa maendeleo ya kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, biashara ni asubuhi, naomba nianze kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda mfupi nilionao, salamu za rambirambi zote alizokwishazitoa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika katika hotuba, naomba na mimi zichuliwe kwamba zinatoka kwa dhati kwenye sakafu ya moyo wangu. Naomba wapendwa wote waliotangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu, alaze roho zao mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa ufupi tu, waajiri wangu walioko kule Buyungu na jirani wa Muhambwe wanaonisikia na kuniona, nawatakia kazi njema, nazidi kuwaombea na Bwana awabariki sana huko waliko.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kuchangia hoja hii katika eneo moja tu, eneo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, maana mengine nina hakika Mheshimiwa Waziri atayagusia. Yapo mambo kadhaa ambayo Wabunge takriban 37 wamechangia katika eneo hili la kilimo cha umwagiliaji. Sitaweza kujibu hoja zote moja moja, nimeweza kuziweka kwenye *clusters*, lakini ziko chache ambazo nitazifafanua.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ujumla naomba nitaje yale ambayo naona kwamba Waheshimiwa Wabunge wanahitaji aidha kujikumbusha au kuyafahamu. Kwanza, ni mikakati ya kilimo cha umwagiliaji tunayoitumia, maana kila mara tunarudia rudia tukija hapa tunaulizana maswali *almost* yale yale.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza, nitaje kwamba tunao Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani wa mwaka 2002 na mpango huu umekwishasambazwa katika Halmashauri zote za Wilaya katika Tanzania Bara. Sasa, ningependa Wabunge kama wapo ambao hawajapata nakala hii au hawajui waipate wapi, basi wawasiliane na Halmashauri zao na wale ambao hawajaweza kabisa kupata kule, wawasiliane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa sababu hapa kwenye Mpango Kamambe *(National Irrigation Master Plan),* ndio mahali pa kuanzia mipango yote ya Kilimo cha Umwagiliaji. Yawezekana pia ukisoma ile *Master Plan*, usione *scheme* yako, kwa sababu ile ni *study* imefanywa na inaweza isiwe *very exhaustive* na ndio maana tunaendelea kui-*up-date*. Lakini, naamini kabisa kwa kiwango kikubwa inakupa *picture* ya uwekezaji katika Wilaya yako, ukitaka kufanya uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji ufanye nini.

Mheshimiwa Spika, pili, Wabunge wengine wamekuwa wakiuliza kwamba hii mipango hata *National Irrigation Master Plan* haina *time frame*. Siyo kweli, hii *National Irrigation Master Plan* inatoa mwelekeo ukitaka kuwekeza ufanye nini. Lakini, programu ya kutekeleza ipo *ASDP,* ambayo ina *time frame* ya miaka saba kama atakavyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, tatu, nimesikia kwamba tunafanya uwekezaji katika umwagiliaji pasipokuwa na dira yoyote wala sera. Hii vilevile naweza nikasema kiasi fulani ni kweli. Aidha, si kwamba baada ya kuwa hatujawa na sera ya umwagiliaji, tumesimama hapo, la hasha! Kama watakavyokuwa wameona Waheshimiwa Wabunge katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mwaka huu tunaandaa Sera ya Kilimo cha Umwagiliaji na hii sera itakapokuwa tayari, italetwa Bungeni hapa na sheria ya umwagiliaji itatungwa baadaye. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba kilimo cha umwagiliaji ni kilimo ambacho kina *discipline* ya hali ya juu, kinahitaji utaalam ambao kwa kweli lazima usimamiwe kwa sheria, maana tunatumia pia rasilimali ambazo zinatumiwa na watu wengine; tunatumia maji ambayo yanatumiwa kwa matumizi mengine, tunatumia ardhi, kwa hiyo, lazima kuwe na sheria ambayo itakuwa inatawala kilimo hiki ili tuweze kufikia malengo yetu. Kwa hiyo, mwaka huu tunatarajia sera itakuwa tayari na baadaye sheria itakayosimamia utaratibu wa kilimo itakuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niende kwenye suala lingine ambalo naona linaleta utata hapa mara nyingi tunapojibu maswali ya Bungeni na hoja za Wabunge; suala la takwimu. Inabidi takwimu tuziweke sawa, vinginevyo tunaweza kuwa tunataja takwimu, lakini mwingine akaelewa vingine na ikawa-*mislead* watu wengine. Sasa, naomba niende kwa haraka haraka nitaje takwimu chache tu ambazo zinagusa kilimo na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, eneo linalofaa kwa kilimo hapa Tanzania ni hekta milioni 44. Sasa, jana tulisikia nafikiri alikuwa Mheshimiwa Khamis alisema wakulima milioni 4.8 wanalima hekta milioni 44, maana yake wanalima eneo lote la Tanzania ambayo haijafikia! Pia jana simkumbuki Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema *square kilometre 44 million*, maana yake ni kwamba, unalima *size* ya Tanzania, haiwezekani! Kwa hiyo, hizi *data* ni vizuri wanapozichukua wawe wanazihakiki na kama wanataka data hizi,

*source* yao ya *information proper* itakuwa ni Serikali; Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla. Ukipata data *REPOA* na kwingineko, basi *verify* na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo linalolimwa hivi sasa ni hekta 10,100,000 na katika hiyo, eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, siyo linalolimwa ni jumla ya hekta 29,400,000. Katika hiyo, hekta milioni 2.3 ndio zile tulizosema zinafaa kabisa kwa umwagiliaji, yaani zinafaa sana *(High Irrigation Development Potential)*, hekta 4,800,000 zenyewe zina *Medium Irrigation Development Potential* na hekta 22,300,000 zina uwezekano. Sasa, jumla yake ni hekta 29,400,000 na sasa hivi baada ya Mheshimiwa Waziri kusoma hotuba, tumeona eneo limeongezeka kwa takriban hekta 9,000 na zaidi kidogo. Hivi sasa eneo linalomwagiliwa Tanzania ni hekta 273,425.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kwa nini hatufanyi hivi, kwa nini hatufanyi hivi? Kwanza, nizungumzie ni mbinu zipi tunazitumia katika ku-*approach* suala hili la umwagiliaji. Hatuwezi kufanya kila kitu, lakini tumesema kwanza, tuangalie wale wakulima zaidi ya asilimia 80 ambao ndio wamejikita kwenye kilimo hiki.

Kwa hiyo, tunachofanya ni kukarabati na hii ndiyo namba moja, kukarabati na kuboresha *scheme* zilizochakaa huko zamani. *Scheme* hizi kama za Kalenga huko kwa Mheshimiwa Stephen Galinoma, Cherehani, Mkoga na nyingine, zile ambazo zimechakaa. Lakini pia kama mtakumbuka juzi nikiwa najibu swali hapa la Mheshimiwa Mgana Msindai, nilitaja kwamba mafuriko yaliyopita yamevunja au yameharibu *scheme* 50 ambazo zinahitaji bilioni tano kuzikarabati na kuzirudisha katika hali yake. Kwa hiyo, *scheme* za namna hii nazo lazima tuzikarabati hata kama zilikuwa ni mpya lakini zimechakaa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunafanya mkakati mwingine ni kujenga *scheme* mpya. Sasa, *scheme* mpya au mradi mpya unapoanza kuujenga, lazima ufanye utafiti, ufanye *design*, ufanye *bill of quantities*, ndio maana tukasema basi, tutakuwa na upembuzi yakinifu japo Wabunge wengi wameuliza upembuzi huu utatupeleka wapi? Huwezi ukaenda kuanza kujenga mradi mpya pasipokuwa na *survey, design* na *bill of quantities*, huyo mkandarasi utampa nini? Kwa hiyo, katika taarifa zetu hizi tumeonesha kwamba, kutakuwa na miradi 62 ambayo itafanyiwa upembuzi yakinifu mwaka huu. Naomba Waheshimiwa Wabunge, watuvumilie tunaposema suala la kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, liko eneo lingine ambalo tumeamua kwa makusudi kabisa kwamba, tuliangalie katika jumla hii ya miradi mipya, ni eneo la Maziwa, ili tuweze kutumia rasilimali maji iliyopo katika Maziwa. Tunataka kutengeneza Ukanda wa Kijani katika Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa. Ziwa Tanganyika hatujaligusa sana kwa sababu maji yake yako *very deep* na ninyi mnajua. Lakini, kule kunakowezekana chini chini kabisa kuelekea kule kwa Mheshimiwa Abdallah Sumry, mjomba wangu, kama alivyosema mwenyewe jana, kule inawezekana. Tunataka tufanye hivyo kwa sababu maeneo haya hasa Ziwa Victoria, ukiangalia yanayo *potential* kubwa sana ambayo ni ya

usafirishaji, kuna Ziwa, kuna Kiwanja cha Ndege, kuna Reli, kuna Barabara. Sasa, wananchi wakiweza kutumia maji yale yaliyoko katika Ziwa Victoria wakalima mazao yao, wataweza kuyasafirisha *across* na kuyapeleka katika masoko hata nje ya nchi ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, naenda haraka haraka, nataka nizungumzie uzito katika uwekezaji kifedha. *National Irrigation Master Plan* inatuonesha kwamba ili tuweze ku-*break heaven*, tunahitaji kulima hekta 405,000 kwa umwagiliaji, ili hizi ziweze kutoa mchango wake vizuri, tutahitaji kufanya uwekezaji wa kekta 30,000 kila mwaka na Serikali itatakiwa kuwekeza takriban bilioni 30 kila mwaka. Hizi ni fedha nyingi, kwa hiyo, mara nyingine Waheshimiwa Wabunge wanapoona fedha zimekuwa ngumu, basi waelewe kwamba suala la kuwekeza katika umwagiliaji nalo lina matatizo yake. Lakini pamoja na hayo tunataka pia tuweze kutafuta katika vyanzo vingine. Viko vyanzo mbalimbali ambavyo mnaweza muweke hata katika Miradi ya *TASAF, NGOs* mbalimbali na hata kwa Madhehebu na Vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa haraka haraka nigusie hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge walionesha kwamba, wanakerwa na wanahitaji majibu ya haraka. Mheshimiwa Said Arfi alisema katika kiambatanisho namba 7, mradi ule alikuwa hana hakika. Nataka nimhakikishie kwamba, Mradi ule wa Uruwira ni wa kwake kule Mpanda na siyo Mabarali, ile ilikuwa ni *typing error*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, naomba nimhakikishie kwamba, Mradi wa Kitivo tayari umepata fedha za *DADPS* milioni 52 na utatekelezwa katika mwaka 2007/2008. Aidha, kule Pawaga nako ukarabati unaendelea baada ya mafuriko yaliyotokea na Serikali imeshatoa shilingi milioni 169 na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, kuhusu Lubada, nataka nimhakikishie kwamba baada ya Kihoko kushindwa, waliojitokeza sasa ni makampuni ya *Armtan* ya Marekani na *Infoenergy* ya UK, ambao wanataka kulima mazao hasa michikichi kwa ajili ya *Bio-Fuel*. Kwa hiyo, utaratibu bado unaendelea na si kwamba Lubada sasa imetelekezwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yameshaanza kutekelezwa kule Mang'ora, yeye mwenyewe ni shahidi, kazi ya *design* imefanywa na hivi sasa hata barabara ile ya Mang'ora – Oldeani ambayo waliahidiwa, tayari imekabidhiwa kwa *TANROADS* ili iweze kuijenga. Kwa hiyo, nafirkiri utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Balai ambalo ndio litahusika na masoko, inaendelea kutekelezwa. Kuhusu soko la vitunguu pia nimeshaongea na Kampuni ya Burton ambao wameahidi kwenda kule kuwatafutia au kusaidia wakulima kuingiza vitunguu vyeupe ambavyo vina soko zuri sana huko Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Anne Kilango, naomba nimshakikishie kabisa kwamba, Wizara iko pamoja naye katika haya mazao na mimi mwenyewe nimekwenda mpaka huko, Mamba Miamba, Ndolwa. Tumeona kilimo cha tangawizi na hivi sasa Tanzania *Organic Movement* imeanza kushirikiana na wakulima wale kwa ajili ya kuendeleza Zao la Tangawizi. Pia tumewaelekeza wataalam wa *irrigation* waende kuangalia namna ya ku-*up-scale* matumizi ya Ndiva kwa ajili ya ku-*support* Zao la Tangawizi na mazao mengine ambayo yanalimwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgana Msindai, alizungumzia kuhusu kazi ya Ilunda. Nataka nimhakikishie kwamba, Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Ilunda na mimi ningeomba kwamba kama kuna upungufu katika utekelezaji wa mradi huu, tutatuma wataalam wa umwagiliaji (wahandisi waliobobea), watakwenda kukagua. Tukikuta kuna ubadhirifu au kuna matatizo, Serikali itachukua hatua. Lakini naomba nimhakikishie kwamba, mimi niko tayari kwenda naye, ili tuweze kuuangalia mradi huu ambao yeye mwenyewe uko katika Jimbo lake. Nimkumbushe kwamba, yeye kama Mbunge, anao wajibu wala sio wa kuombwa wa kuhakikisha anajua miradi iliyomo katika Jimbo lake na kuifuatilia, kwa sababu hakuna anayemzuia kuingia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kumekuwa na shauku kuhusu wageni walioko hivi sasa pale *Speaker's Gallery*. Ninafurahi kutambua uwepo wa Balozi wa Uingereza Nchini, Mheshimiwa Philip Perum na mgeni mwingine kutoka Uingereza Bw. Chris Macabe**,** ambaye ni *Political Director* kuhusu *Northern Ireland* kule Uingereza. *(Makofi)*

*Honourable Philip, we are delighted to have you with us and it is always a pleasure when we welcome a diplomat representing one of our most important development partners with whom we have a very long history. Thanks very much.*

*I also intend to start the honour of the freedom of the Speaker's Gallery and once that is accepted by the Steering Committee, I am sure you are one of the leading contestants. Thank you. (Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kwamba muda ni mdogo, lakini ningependa nichukue nafasi hii kwa mara nyingine, kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya kijana mwenzetu, Mbunge mwenzetu Marehemu Amina Chifupa, aliyefariki tarehe 26 Juni, 2007, pamoja na Wajumbe wetu wa Bodi ya *Nyanza Coorperative Union*; Marehemu Hezron Ndono, Marehemu Stephen Kazi na Marehemu William Kasubi, ambao walifariki wakiwa kazini. Mwenyezi Mungu, azilae roho zao wote mahali pema peponi, *amen*.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja kwa kuwa muda ni mdogo sana, niende kwenye baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na mimi nichangie kidogo. Najua sitaweza kusoma majina yao, lakini Mheshimiwa Waziri atasoma majina yao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu suala la masharti magumu ya kupata mikopo chini ya Mfuko wa Pembejeo. Labda niseme tu kwamba, masharti magumu wakati mwingine yanatokana na wakopaji, wao ndio wanasababisha masharti yawe magumu kwa kutofuata taratibu za kukopa. Sasa kwa kifupi nashauri tu kwamba, kwa sababu tatizo kubwa ambalo limezungumziwa ni ukosefu wa dhamana, nawashauri wananchi kujiunga na Vyama vya *SACCOS*. Wajiunge na *SACCOS* zitawadhamini, zitakuwa kama dhamana zao na wataweza kukopa ama matrekta au pembejeo za kilimo. Maombi haya yapitishiwe kwenye Halmashauri za Wilaya, ambapo *SACCOS* hizi zipo.

Lazima *DED* apitishiwe pamoja na Afisa Kilimo wa Wilaya au Bwana Shamba wa Wilaya. Waambatanishe pia na vielelezo vifuatavyo: Nakala ya hati miliki ya dhamana ambayo anayo, ankala kifani za pembejeo *(Pro-forma Invoice)*, wawe na andiko linaloonesha mapato na matumizi ya mkopo huo ambao wanataka kukopa. Kwa wale wanaotaka kukopa pembejeo, wawe na leseni za biashara, pamoja na uzoefu wao katika biashara hiyo uwe ni kuanzia miaka miwili na kwa yule anayekopa trekta, shamba liwe angalau linafikia hekari 50. Sasa, usipotekeleza masharti haya, ndiyo yanayosababisha useme unacheleweshewa mkopo. Ni kwa sababu hujatimiza na kwa kuwa ni mkopo, lazima taratibu zote zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, tangu Mfuko huu wa Taifa wa Pembejeo uanzishwe mwaka 2003/2004, hadi tarehe 30 Juni, 2007, umetoa mikopo ifuatayo: Matrekta 191 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.88; Imekarabati Matrekta 254 yenye thamani ya shilingi milioni 872; Matrekta madogo *(power tillers)* 52 yenye thamani ya shilingi milioni 255, pia vimekopeshwa kwa wakulima; na pembejeo za kilimo na mifugo zenye thamani ya shilingi bilioni 15 nazo zimekopeshwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha wa 2007/2008, Mfuko huu umetenga shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya mikopo katika mpangilio ufuatao: shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya mikopo ya matrekta na zana nyingine za kilimo. Katika suala hili la mikopo, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mwantumu Mahiza, ameshauri kwamba, Wizara itafute matrekta ya bei ndogo tofauti na haya ambayo yanauzwa kwa shilingi milioni 35 kwa trekta. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu kwamba, Wizara imeshafanya mchanganuo na kujua matrekta ya bei nzuri kutoka India, Pakistan na China. Matrekta haya tayari yameshafanyiwa *testing*, wameyaangalia wakakuta kwamba yanakidhi mazingira ya Tanzania. Kwa sababu tuna kituo chetu kile cha *CAMARTEC* kule Arusha, ndicho kimeshachunguza na kimegundua kwamba yapo matrekta mazuri sana, yanayofaa kwa mazingira yetu ya Tanzania yenye *Horse Power 60 – 80*. Matrekta haya yana bei kuanzia shilingi milioni 17 mpaka milioni 26. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu, ambao tunapenda kusema kwamba, vitu vinavyotoka China au vitu vinavyotoka India au Pakistan, vina viwango vya chini. Napenda kuwajulisha kwamba,

wenzetu wale wa India, Pakistan na China, sasa hivi ni tishio katika uchumi wa dunia katika kilimo. Kwa kutumia vyombo hivyo hivyo, kwa kutumia matrekta hayo hayo, kwa kutumia *power tillers* hizi hizi ambazo tunasema zina *standard* ya chini, ndizo hizo hizo wanazozitumia katika kuendeleza kilimo. Kwa hiyo, nawashauri Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wananchi wanaonisikiliza kwamba, siyo kila kitu kinachotoka India, kina *standard* ya chini, maana tunavyougua mioyo yetu hapa, tunakwenda India kutibiwa; kwa nini tusione kwamba India wanaweza pia wakazalisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa nikimbie nizungumzie suala la Ushirika kidogo. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kuhusu upungufu wa Maafisa Ushirika na vitendea kazi katika Wilaya. Napenda kuwahakikishieni kwamba, Wizara yangu pamoja na TAMISEMI, tunashirikiana katika kuhakikisha kwamba, tunapeleka Maafisa Ushirika katika Wilaya na katika Mikoa ili waweze kutosha katika kufanya kazi ya *modernization* ya Ushirika nchini. Hii ni pamoja na kupeleka vitendea kazi kama pikipiki, baiskeli na magari.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa pia kwamba Viongozi wa Vyama vya Ushirika wapo wasio na uaminifu na wapo ambao hatimaye wanasababisha baadhi ya Vyama vya Ushirika kufa kabisa ama kushindwa kujiendeleza. Napenda kuzungumza kwamba, Serikali inasaidia katika kusimamia uchaguzi wa Viongozi wa Ushirika ili tuweze kupata viongozi ambao wanaujua ushirika, lakini pia ambao wanajali maslahi ya wana-Ushirika wao. Serikali inasaidiana na Vyama hivi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha Ushirika, niseme tu kwamba, wananchi hasa ndio wanaohusika na Ushirika, lakini Serikali itakuwa inaweka changamoto katika kuhakikisha kwamba, taratibu na Sheria za Ushirika zinafuatwa. Kuhusu wabadhirifu katika Vyama vya Ushirika, wameanza kuchukuliwa hatua za kisheria. Kwa mfano, Viongozi wa Vyama vya Ushirika vya *Mwika North*, Marangu *SACCOS* na Watendaji Wakuu wa *ACU*, wameanza kuchukuliwa hatua. Aidha, Viongozi wa *SHIRECU* na Nyanza walioondolewa kwenye uongozi, taratibu za kisheria sasa hivi zimeshaanza ili waweze kuchukukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa James Msekela, amezungumzia kuhusu madai ya *KNCU,* ambayo inadaiwa na wakulima wa Pamba. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ilishafuta madeni mwaka 2006/2007 na katika madeni hayo, yapo hayo ya *KNCU* ambayo yatalipwa pamoja na Vyama vingine vya Ushirika nchini. Niseme tu kwamba, katika bajeti ya mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni tatu zitatumika kulipa *baadhi* ya madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Cheyo, amesema kuwepo na Vyama vya Ushirika vya Wazalishaji *(Producer's Cooperatives)*. Mimi nadhani, kazi ya Serikali ni kuhamasisha, wenye Ushirika ni Wananchi wenyewe na Serikali haiwezi kusema anzisheni Ushirika, lazima wanaoanzisha Ushirika wawe na nia moja kwamba, tunaanzisha Ushirika wa kitu fulani. Wanasema sisi tunaanzisha Ushirika wa Wazalishaji wa Mihogo, Ushirika wa Wakulima wa Pamba, Ushirika wa Wavuvi. Kwa hiyo,

wananchi wenye nia moja ndio wanaweza wakaanzisha Ushirika na Serikali ikasaidia kuhakikisha kwamba, wanafuata taratibu za kiushirika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, amezungumzia Serikali kuviwezesha Vyama hivi kukopa ili viweze kujiendeleza. Nadhani kama nilivyozungumza awali ni kwamba tumesaidia katika masuala ya uchaguzi ili kuweze kupatikana viongozi wazuri. Lakini pia, Serikali itasaidia kutoa viongozi ambao wataenda kuimarisha *management* kwa maana ya utendaji kusudi Vyama hivi viweze kukopesheka. Kwa kuanzia tu ni kwamba, Chama cha *MAMCU* kule Kusini, kiko kwenye mchakato wa kuwasilisha maombi yao ya mkopo *CRDB,* wenye thamani ya shilingi bilioni tatu. Halafu *TANECU* nao wako kwenye mchakato huo huo wa kiasi cha shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, pia ameshauri Bodi ya Pamba isimamie Ushirika ili wale Viongozi wa Ushirika wasile zile fedha za mikopo. Labda niseme tu kwamba, Bodi ya Pamba ipo pale kwa niaba ya Serikali. Jukumu la Bodi ni kusimamia na kuhamasisha uendelezaji wa mazao husika, liwe ni Zao la Pamba, Zao la Korosho ama Zao la Tumbaku. Jukumu la kusimamia Vyama vya Ushirika ni la wana-Ushirika wenyewe, wachague viongozi waaminifu na wenye sifa za kuwaendeleza wao wenyewe. Sheria ya Vyama vya Ushirika, inazingatia uchaguzi wa viongozi wenye sifa, hilo tunawapa tu mwongozo, lakini Serikali haiwezi tena ikaanza kusimamia Ushirika. Ushirika utasimamiwa na wana-Ushirika wenyewe. Wakiona viongozi ni wabovu, wanawang'oa, wanachagua viongozi wengine ambao wana sifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma H. Killimba, amesema hakuna pembejeo za kisasa kwa ajili ya wakulima. Napenda kumhakikishia kwamba, Wizara yangu pamoja na *Rock Feller Foundation* na *Bill & Melinda Gates Foundation*, tunashirikiana kuandaa mpango wa kuanzisha mawakala wa kilimo *(Rural Agro Dealers),* ambao watapatiwa mafunzo pamoja na kupewa mikopo ya kuweza kuwakopesha wakulima.

Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, amesema kwamba mbolea haikufika kule kwake Mbozi. Napenda kusema kwamba, mwaka 2006 Mkoa wa Mbeya ulitengewa tani 19,318 na tani 18,282 ndizo zilizonunuliwa kwa maana kuna *balance* ya tani 1,000 ambazo hazikununuliwa. Mbozi ilipewa asilimia 80 ya mbolea hiyo na maeneo mengine yalipewa asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka, mbolea ya ruzuku mwaka 2006 vilikuwepo vituo 24 na vingi vilikuwa kwenye ngazi ya Mkoa. Mwaka huu wa 2007/2008, mbolea ya ruzuku itasambazwa Mikoa ile ambayo inalima mahindi na tumbaku kwa wingi kwa maana ya *big four;* Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa na maeneo ya Manyara, Kilimanjaro na Arusha, ambayo yanalima mahindi kwa wingi ndiyo yanapata mbolea kwa ajili ya mahindi.

Lakini pia maeneo ya tumbaku; Tabora, Ruvuma, Kigoma na maeneo mengine yanayolima tumbaku yatapelekewa mbolea ya ruzuku ya tumbaku. Pamba itapatiwa ruzuku ya madawa, korosho itapatiwa ruzuku ya madawa, kahawa itapatiwa ruzuku ya

miche, imetengenewa shilingi milioni 500, chai shilingi milioni 500 kwa ajili ya miche na mahindi na mtama mbegu pia zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla kengele haijalia, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha Bungeni jana. Katika kuhitimisha kwanza, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Manaibu Waziri kwa mchango wao mkubwa katika kujibu hoja ambazo zinahusu maeneo makubwa katika maeneo ya ushirika, pembejeo na umwagiliaji. Kazi yangu imekuwa rahisi kutokana na mchango wao wa nusu saa, lakini maelezo ya kuhitimisha hoja hii nitayagawa katika sehemu tatu. Kwanza ningependa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wote walioshiriki katika mjadala huu, uwe umesema au hukusema, uwe umeandika au hukuandika, nawashukuruni sana kwa kutuunga mkono. *(Makofi)*

Kazi hii, tunayoifanya inahitaji kuungwa mkono ili tupate moyo wa kuifanya kwa sababu ni ya kuleta mageuzi makubwa kwa maisha ya asilimia 80 ya watu wa nchi yetu. Huwezi kuifanya kama huungwi mkono. Kwa hiyo, ukiungwa mkono unapata usingizi mzuri, unaota namna ya kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitambue kwa majina Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia. Wabunge 29 wamechangia katika mjadala kwa kuongea hapa Bungeni na hawa walioongea ni Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, akiwa anawakilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mbunge wa Mkuranga, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, Mbunge wa Mpanda Magharibi, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero Magharibi, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Dr. Idris A. Mtulia, Mbunge wa Rufiji na Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Yona S. Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Fuya G.

Kimbita, Mbunge wa Hai na Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini. Hao ndiyo wale waliochangia kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuwatambua Wabunge waliochangia kwa maandishi ambao wako 64, nao ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Lucas J. Siyame, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Maulida Anna M. Komu, Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Musa A. Zungu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Anne K. Malecela na Mheshimiwa Martha M. Mlata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Clemence D. Lyamba, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Alhaji Dr. Juma A. Ngasongwa na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji. *(Makofi)*

Wengine waliochangia lakini nilishawashukuru ni Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza na Mheshimiwa Dr. David M. David. Vilevile napenda kuwatambua wafuatao, waliochangia Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini walizungumzia masuala yanayohusu kilimo: Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Teddy Kasella- Bantu, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa Clemence B. Lyamba. *(Makofi)*

Ukijumlisha wote ambao wametoa mchango wao, utaona idadi ni kubwa sana kulingana na sekta hii ya kilimo. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana wote na napenda niwahakikishie kwamba, kwa muda uliopo hapa ni vigumu sana kuweza kujibu hoja moja moja, tukifanya hivyo sidhani kama tutamaliza. Kwa hiyo, napenda kuwaahidi kwamba, tutasoma kila mtu alichoandika na kila mtu alichosema na kama kuna jambo ambalo linahitaji kumwandikia kwa maandishi, tutamwandikia kila mtu aliyechangia ili aweze kujua tunavyoshughulikia jambo alilolisema. Tutafanya hivyo kwa sababu huo ndiyo wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua wote waliochangia, sasa kabla ya kujaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza, napenda niseme mambo ya jumla. Kwanza, tumesema katika hotuba na tunatambua kwamba kilimo chetu bado kiko nyuma sana. Lazima ukubali hilo kwamba, kilimo chetu bado kiko nyuma sana, kilimo chetu ni cha wakulima wadogo, wanalima mashamba madogo, wakulima wetu hawatumii mbolea wala hawatumii sana kanuni za kilimo bora, kwa sehemu wakubwa wako maeneo machache ambayo wanatumia. Maeneo yale ukienda utaona maendeleo ni makubwa zaidi kuliko kule ambako hawatumii kabisa, hicho ndicho kilimo chetu na hiyo ndiyo hali ya kilimo cha Tanzania. Lakini ni kilimo hicho hicho ambacho kimetufikisha hapa na ndicho kinachochangia asilimia 45 ya Pato la Taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani Waheshimiwa Wabunge, mtakumbaliana nami, mkitumia fursa hii kuwapongeza wakulima wote Tanzania kwamba hicho ndicho kilimo chao, teknolojia yao ni jembe la mkono, hawawezi kutumia mbolea, hawana mbegu za kisasa katika maeneo mengi, lakini wamelima na kila mwaka wanalima na wanachangia kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa Tanzania. Ukikataa hilo utakuwa unakataa ukweli kwa sababu hata Bunge hili linaendeshwa na wakulima wa jembe la mkono, huo ndiyo ukweli, ndiyo wanaogharamia. *(Makofi)*

Pamoja na uzuri wote wa Bunge hili, wale wakulima wa jembe la mkono ndiyo wanaotugharamia sisi hapa, wanastahili pongezi zetu sisi sote. Lakini hiyo haitoshi kukubali kwamba, kilimo chetu kiko nyuma, haitoshi kukubali kwamba wanafanya kazi ngumu na katika mazingira magumu, inabidi tuchukue hatua za kuboresha kilimo chetu. Hiyo ndiyo kazi ambayo tunaifanya hapo. Kwa kweli huo ndiyo msingi wa hotuba niliyoiwasilisha hapa jana. Tunasema kilimo chetu kiko nyuma, lakini tuna wajibu wa kukisaidia ili kipige hatua kiwe cha kibiashara, kiache kuwa kilimo cha kujikimu. Kila tulilolisema hapa msingi wake ni huo. Sasa kwa muda mrefu tumesema hatuwekezi vya kutosha katika kilimo chetu. Lakini ili tujaribu kujibu hoja ya uwekezaji, tumeanzisha programu inayoitwa *ASDP*. Mpango wa miaka saba ambao tutakuwa tunawekeza kila mwaka, lakini kuwekeza lazima uwe na mpango, huwezi kuwekeza tu. *(Makofi)*

Sasa tunasema kwa kuwa wakulima wako vijijini na Serikali iliyo karibu na wao ni Serikali za Mitaa, kwa hiyo, kilimo chetu kitaendeshwa vijijini na uwekezaji kupitia *ASDP* itabidi tuuelekeze vijijini. Lakini ili tuweze kufikisha kiwango chochote cha uwekezaji katika kilimo, lazima wakulima katika vijiji wawezeshwe kuibua na kuwa na mpango. Mpango huo unaitwa *Village Agricultural Development Plan*. Mahali ambapo kijiji kipo na mpango upo, tukipeleka uwezeshaji wa namna yoyote, tunachukua hatua ya

kuwasogeza wakulima kutoka kwenye *substance* kwenda kilimo kinachowalipa. Hiyo inawezekana kwa kila namna. Nimelisema hili kwa sababu katika mjadala wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamehoji sana na wengine wamesema kuna mazao fulani hayamo kwenye hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema hakuona alizeti. Rafiki yangu Mheshimiwa George B. Simbawane, alisema hakuna zabibu, anataka niseme zabibu niliisahau. Mimi sijasahau zao hata moja, lakini hotuba ile lazima iwe na kurasa 60, hakiwezi kuwa kitabu kikubwa sana. Ninachotaka kusema ni kwamba, mazao yetu ni mengi kinachotakiwa ni kuamua ni zao gani, linalimwa wapi na mpango wetu wa *DADPs* katika ngazi ya Wilaya na kijiji, uzingatie zao linalostawi hapo. Fedha hiyo, kupitia *Local Government* tunaipeleka isaidie kukuza mazao hayo na kilimo cha mazao hayo katika eneo linalotokea.

Kwa hiyo, kama Dodoma zao lao kuu ni zabibu, basi Mpango wa Maendeleo ya Wilaya za Dodoma, utazingatia haja ya kuzalisha zabibu, *ASDP* itakuwa ina-*support* zabibu. Kama zao la chakula la Dodoma ni mtama, basi *ASDP* ita-*support* mtama kama zao la chakula Dodoma. Vivyo hivyo kule Lushoto kwa Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, alikuwa anazungumzia juu ya matunda na mazao mengine ya mbogamboga kwa sababu uchumi wa watu wa Lushoto unategemea matunda yale na mbogamboga. Kazi yetu kule ni kutengeneza mpango ili tusaidie uzalishaji wa matunda na mbogamboga kama njia ya kusaidia kuinua kipato cha wananchi wa Lushoto. Hiyo unaweza ukasema mazao yote mnayoweza kuyafikiria.

Kwa kweli tunao mkakati mahususi kwa mfano wa kujaribu kusaidia mazao ya mafuta kama alizeti au ufuta na karanga kwa ajili ya chakula na kwa ajili ya kuuza nje. Kwa sababu tuna viwanda hapa vinatengeneza mafuta, viwanda vyetu hivi vinategemea mafuta *crude* kutoka nje, mwaka 2006 tuliyawekea kodi ndogo kwa ajili ya kutaka wananchi hapa wa-*promote* mazao ya mafuta. Nadhani wakati ni mzuri sasa kuwekeza ili tuweze kuzalisha mazao haya kwa wingi ili viwanda vyetu viweze kutengeneza mafuta ya kula hapa hapa nchini, kwa kutumia malighafi iliyopo hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Mpango huu wa *ASDP* unajibu matatizo yetu ya namna zote ambazo unaweza ukafikiri katika Sekta ya Kilimo. Wenzangu hapa wamezungumzia masuala ya ushirika, wamezungumzia masuala ya umwagiliaji, yote yako *covered*. Kwa mfano, mwaka huu katika bajeti maana kuna hoja moja imeulizwa hapa, nadhani alikuwa anauliza Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, aliuliza na mjukuu wangu, anasema mimi mjukuu wake na wakati yeye ndiyo mjukuu wangu anaitwa Mheshimiwa Juma H. Killimbah na wengine wote waliouliza kwamba, Waziri wa Fedha alisema Sekta ya Kilimo imepewa asilimia 6.3 mbona Wizara ya Kilimo ina shilingi 131,000,000 ambayo ni asilimia 2.2? *(Makofi)*

Waziri wa Fedha alikuwa anazungumzia Sekta ya Kilimo, alikuwa hazungumzii Wizara ya Kilimo. Sekta ya Kilimo inajumuisha vitu vingi kweli; kilimo, chakula na ushirika ni sehemu tu ya sekta ya kilimo. Lakini kuna Wizara ya mifugo ambayo imepewa fedha kama sehemu ya kilimo, kuna barabara za vijijini ambazo zimepewa

fedha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa kweli nyingine mmeshazipitisha ambazo ni Sekta ya Kilimo, kwa sababu huwezi ukalima halafu ukabaki na mazao yako huko huko kijijini kama hakuna barabara. Kwa hiyo, wanaotengeneza barabara ni muhimu sana kwa Sekta ya Kilimo. Vinginevyo kinakuna ni kilimo cha kulima na kula huko huko unakoishi maana huna mawasiliano na soko. Halafu kuna fedha nyingine ambazo nimezisoma humu katika bajeti ya kilimo shilingi 58 bilioni hazimo zinakwenda kuhudumia *DADPs* kupitia Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya. Zote ukizijumlisha kwa pamoja ndiyo unakutana na ile 6.3, nadhani hesabu inakubali hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, siyo kuona Wizara moja akasema mbona hazifiki, unajua ukijibiwa halafu usikubali na huku umejibiwa sawa sawa, kukubali ni hiari yako. Haiwezekani anayekujibu akulazimishe kukubali, yeye anakupa jibu halafu unaamua kama umekubali au hukubali basi unaendelea, lakini hilo ndilo jibu sahihi na ndiyo ukweli wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ukweli wa mambo ambayo tunakwenda nayo kwa sasa. Sasa baada ya maelezo hayo ya jumla na kwa kweli niseme kabla ya kumaliza lile la jumla, tunapozungumza juu ya *Green Revolution*, tunazungumza juu ya habari ya kumwezesha mkulima huyu kwa kumpa huduma za lazima ambazo kwa sasa hana. *(Makofi)*

Anahitaji pembejeo tunamfikishia, kama ni mbolea tunamfikishia, kama ni mbegu iliyokuwa *improved (improved seeds)* tunamfikishia, madawa ya mimea tutamfikishia na kadhalika ili aweze kuzalisha. Unaweza ukampelekea mbolea, madawa na kila kitu lakini akawa hajui kuyatumia. Tunampelekea mtaalam mpaka kijijini kwake, amwelekeze namna ya kutumia. Kwa hiyo, *agricultural revolution* ni *package* ya pembejeo inayokwenda sambamba na utalaam unaomwezesha mkulima yule kujua cha kufanya na akijua ana-*improve,* mapato yake yanaongezeka na maisha yake yanakuwa bora kuliko jana na huo ndiyo msingi wa maisha bora kwa kila Mtanzania. Hiyo ndiyo tunayoiita *Green Revolution*. *(Makofi)*

Sasa rafiki yangu Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, anasema Mheshimiwa Joseph J. Mungai mwaka 2006 alisema mambo manne, mimi nimeanzisha ya kwangu hapana, tena akayataja vizuri nikawa ninayasikiliza. Anasema alisema juu ya pembejeo na ruzuku, ruzuku iko palepale kama Mheshimiwa Joseph Mungai alivyoianza mwaka 2006 na sisi tunaiendeleza. Anazungumzia juu ya *ASDP, ASDP* ni mpango mkubwa hata Mheshimiwa Joseph Mungai hawezi kuondoka nao hata mimi siondoki nao. Ule unabaki palepale na sisi wote tunauendeleza, anazungumza mambo hayo lakini nadhani alikuwa hajasoma tu kile kitabu vizuri maana angelikisoma vizuri, asingeyasema hayo maana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ni mtaalamu halafu ni mtafiti mzuri, hawezi kusema mambo tu halafu akawa anajisemea. Ukimkuta amesema mambo tu hayana uzito, ujue ni bahati mbaya siku hiyo labda hakuamka vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hatukubadili kitu kwa kweli tunaendeleza ile *green revolution* niliyoisema leo Mheshimiwa Joseph Mungai, aliisema mwaka jana na mwaka alikuwa anasema kwamba amehudhuria mkutano Abuja, Nigeria na Afrika tukakubaliana

kwamba sasa wakati umefika wa kuweka msukumo katika *green revolution.* Nilichofanya mimi ni kuwafuata wale watu ambao wameanzisha *AGRA, AGRA* ni *Alliance for Green Revolution in Africa*, nimewafuata mpaka *New York* na *Washington* nimezungumza nao tumekubaliana kwamba, *time has come now* tuanze kwenda mbele badala ya kuendelea kuzungumza. Sasa tunaanza na tunaendeleza kazi aliyoianza Mheshimiwa Joseph J. Mungai na hiyo ni *continuity,* ndiyo Serikali hakuna mtu mmoja anayekuja na anaanzisha Serikali yake mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nina kazi ya kujibu baadhi ya hoja. Kwa bahati nzuri hoja ya kwanza nitakayoijibu itakuwa ni ya Kamati ya Ardhi. Kamati ya Ardhi kwa kweli ni watu ambao tunasaidiana sana kila mara tunaonana, kila mara sisi tunachota maarifa kutoka kwao na wanaboresha sana mipango ya Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, ninachoweza kusema kwa Kamati ya Ardhi ni kwamba, tunakubaliana na ushauri wote waliotupa tutauzingatia kama ambavyo tumekuwa tunazingatia ushauri wao wakati wote na bahati nzuri Waziri Kivuli wa Upinzani ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, nikiipongeza na yeye yumo katika wale ninaowapongeza. Halafu pia ni rafiki yangu sana na tunaheshimiana sana. Jana wakati anasoma yale mambo nikamwuliza lakini haya ya kwako au kuna mtu kakukosesha? Akasema ya kwangu bwana lakini ya Kambi, nikamwambia aaaah! Bwana usiwe unakubalikubali mambo namna hii. Kwa sababu amesema humu mambo nikawa nashangaa, lakini ninamheshimu sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kweli anaweza kuandika maneno haya, nikamwuliza mara mbilimbili hata leo tena nimemwuliza tulikuwa naye hapa, ana takwimu ambazo zimekosewa kabisa ndizo hizi Mheshimiwa Christopher K. Chiza alikuwa anajaribu kuzielezea. Anasema kuna wakulima 4,800,000, siyo kweli kuna familia milioni 4.9 *actually* ambazo jumla ya wakulima ni 12 milioni, wanaoishi katika familia hizo za wakulima, hiyo ni takwimu sahihi. Halafu si kweli kwamba, wanalima hekta 44 milioni, wangezilima nchi hii ingekuwa haina matatizo tena kwa sababu hekta milioni 44 ndizo hekta zote zinazofaa kwa kilimo Tanzania. Tungekuwa tumelima zote kungekuwa hakuna tatizo la kazi, hii *ASDP* ya nini maana wote tungekuwa tunalima, lakini takwimu hizi kwa bahati mbaya siyo sahihi. *(Kicheko/Makofi)*

Halafu Mheshimiwa amezungumzia sana mambo ya utekelezaji na akaupa *percentage* sasa nikasema lakini tulikuwa wote kwenye Kamati na utekelezaji ule mimi niliu-*present* pale na wote tukaukubali pamoja naye; sasa tena hizi takwimu zinatoka wapi? Kwa hiyo, huruma yangu kwake ilikuwa na msingi huo tu kwamba, kwa kweli walimkosesha na watu wa kumkosesha inawezekana wapo hapa lakini sasa wamenyamaza. Lazima kuna watu wamemkosesha haiwezekani akasema maneno hayo, tunamjua sana sisi ni mtu anayeheshimika sana halafu ni msomi mzuri tu. Sasa amesema vitu vingi sana takwimu asilimia ngapi na sijui tumetekeleza asilimia tano, asilimia tano inatokea wapi? *ASDP* ina *programs*, ina *PADPs,* ina mpango unaoitwa *ASPS,* tena huu mpango huu wa *PADPs* unatekelezwa mpaka Pemba na Unguja halafu yote hiyo *part* ya *ASDP* sasa asilimia tano hii lazima hii Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, siyo ya kwako. *(Kicheko)*

Halafu kuna maneno alisema yanashangaza kidogo, tumeseme pamba imeshuka kwa asilimia 66 akasema ni kukosa dhamira ndiyo ilishuka. Bwana mimi natoka kwenye kilimo cha pamba, mwaka 2005 wakulima wa pamba walipanda lakini mvua ilikosekana. Hata ukiwa na dhamira pamba ikakataa kuota, dhamira yako haiwezi kugeuka pamba. Haiwezekani, *this is the fact of life* kwamba umepanda. Anachosema hapa Mheshimiwa Salim Hemed Khamis ni kwa sababu hatuzingatii sana *irrigation,* sisi tumeweka asilimia 75 ya bajeti kwa *irrigation* na tumesema tunataka kufanya *irrigation* kadri tunavyoweza lakini hakuna nchi duniani ambayo inaweza ikategemea *irrigation* kwa kilimo chake chote. *(Makofi)*

Hata ukii-*irrigate* yote ikitokea *drought* chanzo chako kinakauka, sasa uta-*irrigate* na nini? Kwa hiyo, ikitokea *drought* hata Amerika *productivity* bado inashuka. Nafikiri tuendelee tutafika tu. Kwa hiyo, kwa sababu ya kuheshimiana sana na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, wala sitaki kusema zaidi. Nilitaka kumsaidia ili aweke zile takwimu sawa tu. Kwa sababu nina hakika anatuunga mkono kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nianze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, namsifu Mheshimiwa John M. Cheyo, alisema mambo ya kiutu uzima jana. Alisema kuwa mpinzani maana yake si kupinga kila kitu. *(Makofi)*

Kwa sababu upinzani *I mean* ni sura mbili za shilingi tu kwamba wewe upo upande mmoja na mwingine, lakini mna nia ile ile ya kujenga nchi yenu. Kule Uingereza tulikotoa huu mfumo, kuna kitu wanakiita *the royal government*. Halafu upinzani wanauita *the royal opposition. Royal government and royal opposition.* Sasa hiyo *royal opposition* ya hapa eti ya kupinga tuuu! Sasa Mheshimiwa Cheyo akasema hii *wrong.* Na mimi nakubaliana na wewe mzee. Safi sana, mambo namna hii lazima kufundisha vijana, hasa akina Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, wana damu inachemka lazima kuwaambia. Hapana kupinga pinga kila kitu, lazima kukubali mambo ya kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa John M. Cheyo pale alikuwa anasema wakulima wanakatwa shilingi 20 ya pamba. Sasa tunatoa ruzuku, mimi namwambia ile ya shilingi 20 itaendelea. Kwa sababu ile ni *system,* inawawezesha wakulima kuweka akiba ili ukifika msimu wa kilimo waweze kununua pembejeo kwa sababu wakulima huwa wanakula hela yao ikifika msimu hazipo. Kwa hiyo, wanawawekea akiba tu. Ukifika wakati wa kilimo, wakiwa hawana hela wanatumia pesa zao wananunua dawa. *That is a very good system,* ukiiondoa hiyo pamba itashuka. Lakini pamoja na hiyo kwamba tunajua bei ya zile pembejeo iko juu, ndiyo maana tumeweka ruzuku ya pamba ili bei zile za pembejeo ziwe nafuu, zimwezeshe mkulima huyu badala ya kupiga mara moja tu angalau apige mara mbili.

Kwa hiyo, *effect* itakuwa ni kwenye bei kwamba, huyu sasa anaweza kupata ile dawa kwa bei nafuu na hasa kwa sababu dawa yenyewe inaagizwa na Bodi. Kwa hiyo, uwezekano wa ku-*control* bei upo na ku-*control* bei ni pamoja na kuishusha kwa sababu

Bodi itakuwa imepata *subvention* kutoka Serikalini. Hicho ndiyo kitu ambacho tulikuwa tunakisema. Nadhani hili Mheshimiwa John M. Cheyo, hana matatizo nalo. Suala la mbegu tunalishughulikia, Ukiriguru karibu wanaanza kutoa *UK 91* na *research* kwa ajili ya mbegu inaendelea, na vile vile tunaka kuanzisha kitu kinaitwa *delinting* ili tupate mbegu ambayo haina nyuzi ili tuanze kufanya utafiti wake halafu iwe inapandwa na kuota kwa haraka. *Germination* inakuwa nzuri zaidi, inampunguzia mkulima kupanda mbegu nyingi sana katika eneo badala yake awe anapanda mbegu chache.

Mheshimiwa John M. Cheyo, pia alikuwa anasema ingawa pamba bei yake iko juu lakini kuna watu wanataka kuishusha kwa kuweka Mfuko wa Elimu. Mimi hili kwa kweli sitaki kulitolea kauli, kwa sababu mambo haya ya mifuko yana utaratibu wake. Kama mtu anataka kukata wakulima bei, kuna Ofisi ya Wizara ya Kilimo, kuna Waziri Mkuu, mpaka kwanza walete tu-*study* tuone kama kweli hiyo haitamwathiri mkulima. Lakini vilevile hatuwezi kuwazuia wakulima hawa kukaa wao wenyewe wakaamua mambo yao halafu Serikali ukawaambia hakuna kabisa kabisa, hiyo kwa kweli itakuwa ni *problem.* Tuwaachie uhuru wa kuamua lakini wailetee Serikali ili tuweze kuona *effect* ya hilo itakuwaje.

Kilimo cha mashamba makubwa tunakitilia mkazo na tunawaita watu wote wa ndani na nje wanaopenda kuwekeza na ziko taratibu ambazo zinafanywa za kuwa na ardhi iliyopimwa ili waweze kufanya. Mheshimiwa John M. Cheyo alisema *KNCU* ile tunapoteza muda wa kuisaidia tuiache ife, kwanza ilikwishakufa siku nyingi. Mimi nasema hapana, kwa sababu *KNCU* ile ina mali za wakulima za tangu *Victoria Federation.* Thamani ya mali zile ni shilingi bilioni 12 na madeni yao ni kama shilingi bilioni sita. Kwa hiyo, kwa kweli hawajafilisika. Kinachokosekana pale ni *management* sasa wakati tunajaribu kujenga ushirika kutoka chini, mali yao ile lazima ihakikishwe inalindwa ili ushirika ule uje urithi haki zao zile. Sisi ni Serikali ya watu hao hao, kwa hiyo, lazima tusaidiane nao katika kutafuta *solution*. Kwa hiyo, kusema tuiache ife, mimi sikubaliani na hilo. Bahati mbaya hilo hatukubaliani, lakini mengi sana tunakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Adamu K. A. Malima, alizungumzia kwamba tufanye tathmini ili tuone hizo fedha tunazopeleka kwenye *ASDP* kama kweli zitakuja kutupa matokeo mazuri. Mimi nadhani *study* ya huu mpango imefanywa, nia ni kuongeza tija na kama tija itaongezeka lazima tutakuwa *better off* kuliko tulivyokuwa kabla hatujaanza mpango huu.

Alizungumzia Halmashauri za Wilaya kwamba, hazina uwezo wa ku-*handle* fedha hizi. Sisi tunaendelea kujenga uwezo kwa kushirikiana na TAMISEMI, kuijengea uwezo na vilevile tunaweka utaratibu wa tathmini, sio kuacha tu mpaka mwaka uishe, tutakuwa tunakwenda kuona utekelezaji kuwa na hakika kwamba kweli fedha ile inatumika kwa kazi iliyokusudiwa. Lakini ningependa niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, hii pesa ya Serikali na sisi tuna majimbo yetu na kero ya umaskini inatuhusu wote, kwa hiyo, fedha hii kama inakwenda kule sisi tuwe ni sehemu ili tuwe na uhakika kwamba fedha hii inatumika kwa manufaa ya wananchi tunaowawakilisha. Mimi nadhani hiyo itatusaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya viwanda vya korosho, vipo viwanda vina matatizo bado kwa mfano, Kusini ule umeme haujafika kila mahali. Kwa hiyo, ubanguaji kwa mwaka huu utakuwa na *problem* lakini shabaha ni kubangua korosho zote ili tuachane kabisa na hiki kitu kinachoitwa kuuza korosho ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, alizungumzia juu ya huduma za ugani na pembejeo. Alisema asilimia 80 ya mbolea iliyokwenda huko, haikuuzwa Mkoani wala Wilayani; ilienda wapi sasa? Lakini hii ndiyo moja ya sababu iliyofanya tuwe s*pecific* kwamba, sasa badala ya kupeleka mbolea tu kila mahali, kabla hata hatujawaandaa wakulima kuitumia kwanza, tupeleke kule inakotumika halafu kule ambako haijatumika, tupeleke ruzuku ya kitu kingine ambacho kinatakiwa kwa wakati huo. Hiyo itatusaidia kidogo.

Mheshimiwa Vita R. Kawawa, amezungumzia *SGR* na akataka tutangaze bei na kwamba hakuna dawa za mikorosho ambazo zimekwisha fika huko, hiyo kazi itafanyika. Kwa sasa Namtumbo tutajaribu kadri tunavyoweza, kuweza kuona ya kwamba zinafika kwanza, kuna mawakala wengi tumewapeleka huko tutawafuatilia.

Mheshimiwa George B. Simbachawene, nadhani nimekwisha mhakikishia kwamba, lile tatizo la zabibu litakuwa *taken care of* na vilevile suala la mbolea na mgogoro wa upatikanaji wa mbolea, tutautazama nilikwisha zungumza naye. Inaonekana kwamba, kulikuwa na kutokuelewana kidogo. Lakini tutaweka utaratibu ambao sasa mbolea itaweza kufika kwa wakulima bila ubishi wala haihitaji tena kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Kilimo. Tumeshatoa majibu kwamba tutajihidi kuwaongeza Maafisa Ushirika na kuwasambaza.

Mheshimiwa Castor R. Ligallama, alikuwa anazungumzia uwekezaji katika shamba lile la *KOTACO.* Tutazungumza naye tuone hawa wawekezaji ni wapi na uwezo ni upi ili tuweze kujiridhisha kabla hatujawapa, maana unaweza ukawapa watu tena wakashindwa. Masuala yote yanayohusiana na umwagiliaji yanatakiwa yaanzie chini kwenye *DAPs* na mradi unaokuwa mkubwa zaidi kuliko uwezo wa *DAPs* ule unaweza sasa ukaletwa rufani yake ili tuone utaalam gani unaweza ukasaidia.

Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, alikuwa anazungumzia Chama Kikuu cha Ushirika na Menejimenti, Meneja Mkuu wa Chama cha Tunduru ameshateuliwa, yuko njiani anakwenda kule. Vyama vingine vyote vya Mtwara vile vinavyolima korosho, tumekwisha vipatia Mameneja, wako njiani wanakwenda kule. Wanakwenda kuanzisha Ofisi na kuviimarisha hivyo vyama kabla ya msimu wa korosho haujaanza mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, alisema sana juu ya matrekta Rufiji. Nadhani mambo ya matrekta haya tatizo letu la matrekta ambayo nafikiri tutakuja kupata ufumbuzi kidogo tutakapotisha sheria ile inayoruhusu *leasing,* hapo ndipo tutaweza kukopa kweli. Lakini kwa sasa, waagizaji wa matrekta hawaingizi matrekta hapa kwa sababu hakuna soko la uhakika. Ndiyo maana ule mfuko tunaupa shilingi 3.5 bilioni, utakopesha matrekta mangapi kupitia mfuko ule? Kwa hiyo, lazima iwepo *system*

nyingine ambayo itawawezesha watu kukopa matrekta, tutakapoanza hiyo *leasing system,* nina hakika watu wengi zaidi wanaweza kunufaika kwa kukopa matrekta.

Lakini kama alivyosema mmoja wa Wabunge wenzetu hapa, hata hivyo ni vigumu sana kutegemea matrekta ya-*solve* kilimo chetu chote. Kama watu wetu asilimia 70 wanatumia jembe la mkono, *graduation* yao lazima iwe kwenda kwenye wanyama kazi kwanza kuliko kusema wote wataenda. Kwa sababu hata hivyo, kuna maeneo mengine matrekta hayawezi kulima. Kama yale ya milimani ya Brigadia pale hayawezi kwenda. Kuna maeneo mengine hayana ardhi, sasa hivi teknolojia ya kule ni kupeleka utaalam na pembejeo ili *productivity* iongezeke. Ndiyo maana kwa mfano, kwa wakulima wa kahawa tumeamua kuwapa *subsidy* ya miche ili waweze kuongeza zaidi uzalishaji kwa kupanda miche mipya ambayo inazalisha zaidi na inakinzana na magonjwa. Kwa hiyo, nadhani kila mahali itabidi pawe na aina fulani ya *system* yake.

Suala lingine lililoongelewa na Mheshimiwa Yono S. Kevela, ilikuwa ni Kituo cha Makambako hakiisaidii sana Njombe wanakonunua *SGR,* nashangaa kidogo. Kwa sababu Makambako iko Njombe lakini sasa Rudewa watafaidika vipi na Makambako kabla ya Njombe. Nitazungumza naye Mheshimiwa Yono S. Kevela, tuelewe *problem* hasa ipo wapi ili tusaidiane ku-*solve.*

Mheshimiwa Festus B. Limbu, alitoa ushauri mzuri tu tuweke mkazo katika *Agro Processing* na mimi nakubaliana naye. Hatuwezi kuwa na *modern economy* kama mazao yetu yote yanauzwa *raw* kusema ukweli. Kwa hiyo, kwa kweli wote tujaribu ku-*promote* kila linalowezekana ili watu wanaotaka kuwekeza hapa sasa waanze kuingia katika *Agro Processing.*

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyosemwa hapa ni mengi na kwa kweli ni vigumu sana yote nikayasema, lakini nimetoa ahadi mapema tu ya kusema mambo yote tuliyoyasema yameandikwa yote na ushahidi wake ninao hapa. Wako watu wamezungumzia umwagiliaji, wapo 36 wote tunao. Wapo watu 13 wamezungumzia masuala ya Sera na wapo watu saba wamezungumzia Bodi za Mazao na bajeti zao ndogo, wote tunao.

Wapo watu tisa wamezungumzia usalama na uhifadhi wa chakula, wote habari zao zimeandikwa. Wapo watu 12 wamezungumzia utafiti na mafunzo, wote tumewaorodhesha. Wapo watu 14 wamezungumzia, wote tumewaorodhesha. Wapo watu 13 wamezungumzia zana za kilimo, wote tunao.

Wapo watu 13 wamezungumzia huduma za ughani. Watu 23 wamezungumzia maendeleo ya ushirika ili mradi kila mtu aliyesema tumemnukuu mambo aliyoyasema na sisi tutafuatilia kwa umakini kabisa. Sasa isingelifaa tena na mimi mtoa hoja nipigiwe kengele hata ya kwanza, maana mambo ni hayo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ninaloweza kusema ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge, hii kazi ni yetu sote, kama kuna Mbunge yeyote ana jambo *serious* anaona hatukulisema hapa, tunaweza kulizungumza nje ya Bunge na tukalifanyia kazi na

ufumbuzi ukapatikana. Kwa sababu hapa siyo mwisho ni kwamba kazi yetu ni *continuous.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wote na kusema ya kwamba, Wizara yetu iko *open,* Waheshimiwa Wabunge ni *colleagues,* njooni tuzungumze mahali ambapo *problem* ipo ili tusaidiane. Yapo mambo mengine kama yaliyosemwa kule Singida, wanasema kuna kwelea kwelea ni vizuri ikitokea hali hiyo hata ukampigia Waziri moja kwa moja na mimi ukinipia ndege itakwenda ku-*deal* na kwelea kwelea. *(Makofi)*

Hata jana mimi nilipigiwa simu kutoka Bunda kwamba panya wamekuwa wengi na kwa sababu kule hatuli panya, sasa imekuwa ni p*roblem.* Kwa hiyo, imebidi sasa tutume watu kwenda kupambana nao, lakini kama kuna mtu yeyote anayedhani kuwa panya ni bidhaa, tunamkaribisha pale Bunda. *Samaki nchanga*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1001 – *Administration and General* ................ Sh.2,836,147,400.00

**MWENYEKITI:** Kaeni tu mtapata nafasi. Tunawaandika kwanza, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Hemed Salim Khamis, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Charles M. Kajege na Mheshimiwa Juma H. Killimbah. Nitoe tu tahadhari, kama unachukua mnachoita mshahara wa Waziri, halafu unatafuta mradi mdogo wa umwagiliaji, nitakuzima hapo hapo. Kwa sababu siyo kazi yake, kama unachukua mshahara wa Waziri kwa mujibu wa kanuni zetu, utazungumzia suala la Sera. Haya tuendelee.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ninashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hiyo Semina imeingia kwa Waheshimiwa Wabunge. Programu Namba 10, *Sub-Vote 1001,* kipengele kidogo 250100, *Basic Salary* ya Mheshimiwa Waziri kwenye *policy issues.*

Kwanza, namshukuru kwa kukubaliana na mimi kwa vitu vingine. Wakati nachangia nimezungumzia juu ya *issue* ya pembejeo na ninamshukuru kwamba kuna lita milioni 1.2, alivyoileta zana ya kukatwa shilingi 20 kwa pamba kama ni dhana ya kuweka akiba, sina matatizo nayo. Lakini Mheshimiwa Waziri anajua kabla hajawa Waziri, yeye mwenyewe tulikuwa tunawiana kile kitabu ambacho wakulima wanaandikwa mle fedha zao, kitabu hiki kinagawika kila mwaka na kinakwenda *balance* iliyobaki humu. Kitabu hiki ikifika wakati wa pembejeo zile takwimu zinageuka, sasa hiyo dhana ya kuweka inatoka wapi? Kwa hiyo, kama akisema dhana itakuwa ya kuweka, kwa sababu yeye ni Waziri na anajua tatizo la kitabu hicho ambacho wakulima wanaandikwa, mimi nitakubaliana naye lakini anihakikishie kwamba, atahakikisha iwe dhana ya kuweka. Kama mkulima hajapewa pembejeo zote kwa msimu huu, basi hizo fedha zionekane kwa msimu unaokuja. Hiyo sina matatizo nayo, lakini Waziri awe mkweli. Anajua wazi kabisa kwamba, huo sio utaratibu kwa hivi sasa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tukubali kwamba vitabu hivi tunavyotumia, *are not used friendly,* yaani havitoi takwimu zote zile ambazo tunaona katika vitabu mbalimbali vya bajeti. Hili linaweza kuwa ni tatizo la Serikali nzima, lakini tumetumia hii kuulizia kwa Wizara hii ya Kilimo, tunapoambiwa kwamba tumetoa shilingi bilioni 379 kufuatana na bajeti ya Serikali halafu ukija kuongeza unakuta anazoomba Mbunge ni shilingi bilioni 131. Kwa hiyo, ni wazi lazima tuanze kuuliza kwamba zile shilingi bilioni 200 ziko wapi. Sasa anaposema ziko kwenye *livestock,* ukiangalia kwenye *livestock* unakuta shilingi bilioni 12 tu. Ziko kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia *Vote* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, unakuta kuna shilingi bilioni 33 tu. Sasa ndiyo kusema basi Serikali nzima ikae vizuri ili vitabu hivi ukisema nina trilioni moja kwa ajili ya elimu na hili nitalikuta hivyo hivyo kwa elimu. Utasema shilingi trilioni moja kwa elimu unakuta kuna shilingi bilioni 265. Kwa hiyo, nataka maelezo ya kina. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kukubaliana na Mheshimiwa John M. Cheyo, juu ya suala lile la *pass book,* anasema tulikuwa tunakubaliana na mpaka sasa tunakubaliana. Tunakubaliana kwamba kama mkulima anakatwa shilingi zake 20 na kama zanaandikwa kwenye *pass book* na kama fedha anayowekeza humo ndani ni nyingi kuliko thamani ya pembejeo atakayochukua ile ni benki akaunti. Kwa hiyo, lazima iwe *reflected* kwenye akaunti yake ya mwaka unaofuata. Huo ndiyo msimamo wangu ulivyokuwa na ndivyo ulivyo hivi sasa. Tofauti yake ni kwamba, sasa nasimamia ili uwe. *(Kicheko/Makofi)*

La pili, nilichosema na bado nakirudia, alichosema Waziri wa Fedha ni kwamba, Sekta ya Elimu kwa mfano, imepewa 18%, alikuwa hazungumzii Wizara ya Elimu alikuwa anazungumzia kuanzia chekechea mpaka elimu ya chuo kikuu. Sasa kwenye kilimo alikuwa anasema Sekta ya Kilimo. Ukichukua *ASDP* kwa mfano, ambayo inaunganisha sekta zote za kilimo, sisi ni *lead Ministry,* lakini *ASDP* ina-*involve* TAMISEMI, ambao ndiyo wasimamizi wa watekelezaji kule chini halafu inawahusisha Wizara ya Mifugo na Sekta ya Barabara hasa barabara za vijijini. Halafu inahusisha vilevile Masoko. Kwa hiyo, hizi zote ukiziweka pamoja, ndiyo zinaitwa Sekta ya Kilimo. Lakini Sekta ya Kilimo hiyo inahudumiwa na Wizara mbalimbali. Sasa ukisema Sekta ya Kilimo halafu ukataka zote 300 ziwe chini ya Wizara ya Kilimo kwa sababu

inaitwa Wizara ya Kilimo, kwa kweli itakuwa *unfair* lakini Wizara ya Kilimo hata katika *context* ya sekta hata kwa *definition* ya dunia ni pana zaidi. Inahusisha hata misitu ya kupanda, samaki na hata nyuki ni Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama umejumlisha zote hizo bado hazikufika 300, sasa mimi kwa kweli sijui namna ya kusaidia. Lakini mimi nilichokuwa naeleza ni *concept.* Hapa sina hesabu ya sekta zote, lakini *concept* iliyo na maana ya Sekta ya Kilimo ndiyo hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John M. Cheyo, naona umesimama tena. Hebu kaa nitoe tahadhari nyingine.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** *Okay!*

**MWENYEKITI:** Madhumuni ya Kamati ya Matumizi ni kupata ufafanuzi na siyo kumtosheleza anayehoji apate anachotaka yeye. Kwa mfano, kwa Sera za *UDP*, sekta maana yake itawekwa yote kama ni kilimo yatapelekwa kwenye vitabu vya kilimo. Hivyo ndivyo unavyotaka wewe, siyo lazima hawa sasa wanaosimamia Serikali ya CCM, wakutosheleze kwenye hilo. Nadhani tukiendeleza ubishi kwamba Serikali inayotawala itekeleze yale unayotaka kwa mfumo unaoutaka, sasa hakuna hata maana ya kuwa na Ilani za Uchaguzi. Kwa hiyo, ukitikisa kichwa nitakuzima moja kwa moja, uwezo huo ninao, kwa sababu huko ni kukosa nidhamu kwa Kiti na kanuni ipo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, zungumza ukiwa umetulia, usiwe na jazba. Sema unalotaka kusema lakini hakuna hoja yoyote ya kuitaka Serikali ya CCM ifanye vile unavyotaka wewe.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayezungumza juu ya Sera ya Chama hapa. Tunachosema ni *simple* kwamba, wewe umekuja kutuomba pesa, wewe umekuja kusema nitatoa pesa kiasi hiki kwa sekta hii. Sasa mimi nafikiri kama jambo hili ni gumu kwa Waziri anayehusika kulijibu, labda wewe kama Mwenyekiti wetu ungelichukua kama hoja ikafanyiwe utafiti ni vipi vitabu hivi vitaoanisha pesa tunazoambiwa zipo na kweli pesa zinazoonekana zipo na hili pia linahusisha hata uwajibikaji. Tutakapokuja kumhoji mtu anayehusika na hela hizi, wewe ulikuwa *allocated; where is this money?* Hana habari, ziko huku au ziko wapi?

Kwa hiyo, nasema kama vitabu hivi haviwezi kuonesha hali halisi, basi *they are not within the ink, they are printed on.* Ni vizuri basi tutafute njia ya kupata vitabu vitakavyoonesha vitu bayana. *That is what I am trying to say. I have nothing to do with a Party. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri usiwe na shida na hilo. Wakati makadirio ya bajeti ya yakipitishwa na Bunge kwenye mchango mmoja ilibidi nisimame, nieleze jitihada ambazo Ofisi yangu itafanya kuvifanya vitabu hivi viwe *more user friendly,* hilo nilikwisha lisema. Kwa hiyo, hakuna haja ya kulirudia rudia. Utakumbuka siku ile kulikuwa na sehemu ambazo baadhi yenu mlikuwa mnasema zinajirudia rudia na

hazieleweki. Sasa hayo ni mambo mepesi tu ni *technical,* tutakaa Kamati ya Uongozi na Serikali, tutayaweka vizuri.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilidhani labda Mheshimiwa John M. Cheyo anaendelea, nikaonekana nimetulia ukawa umenishitukiza lakini nitajitahidi kuweka mambo sawa sawa. Mimi nina mambo mawili. La kwanza ni suala la samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 43*, kifungu cha 1001, mshahara wa Waziri. Hili suala ni la kisera kama jinsi ambavyo umetushauri.

Wakati nachangia nimezungumzia hotuba ya Waziri aliyepita, kwa maana ya mipango ya mwaka 2006 na mipango ya mwaka huu na nimejaribu kuonesha jinsi ambavyo hakuna *consistency* kwamba, hatu-*build on* kitu ambacho tulikifanya mwaka 2006. Nitawapa mfano, ukurasa wa 85 wa Hotuba ya Mheshimiwa Joseph J. Mungai, hata sijui kama wanayo hapo, mnaweza kuangalia. Imezungumzia suala zima la uwekezaji na mikopo katika kilimo na kuna *bullets* takribani 12, ambazo zinazungumzia kwenye mwaka wa fedha 2006/2007 kuna mambo ambayo tutayafanya kupelekea kilimo chetu kiweze kukua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Stephen M. Wasira, suala la uwekezaji na mikopo kama jinsi ambavyo mipango ilikuwa imeandikwa, hakuna hata sentensi moja, mbona tukizungumza kwamba Mawaziri wanakuja wanasahau kama mwaka 2006 walituambia kitu fulani, mwaka huu wanakuja na vitu vipya na *ASDP* kwa mfano ni miaka saba, kwa hiyo ni lazima tu-*build on* mwaka 2006 tumefanya nini, tumefikia wapi na Bunge lifahamishwe kwamba matatizo yalikuwa ni moja, mbili, tatu, nne na mwaka huu tunataka kufanya nini. Kwa hiyo, ni mfano mmoja tu ambao nimejaribu kuonesha jinsi gani ambavyo mwaka 2006 Waziri alituambia hivi na mwaka huu Waziri ametuambia hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sikuridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri na suala la kusoma au kutokusoma, unaweza ukani-*accuse* kwa mambo mengine yote, lakini siwezi kuja Bungeni kuzungumza bila kuwa nimesoma na nimekuonesha *exactly* ukurasa na jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wa sasa ameshindwa ku-*build on* na Waziri aliyepita. Kwa hiyo, nataka nipate maelezo, ile mipango yote katika eneo hilo la uwekezaji na mikopo. Mheshimiwa Waziri aliliambia Bunge mwaka 2006, mmetekeleza kwa kiasi gani na mwaka huu wa fedha mtafanya nini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilimsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, wakati anaongea, alisema kwamba, alitaja mambo manne ambayo ndiyo angeyashughulikia na yangeshughulikiwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007, aliyataja kuwa ni ruzuku na pembejeo ya ruzuku, *ASDP* na mapinduzi ya kijani, hayo ndiyo mambo aliyoyataja na mimi nilimnukuu. Sasa nilichokuwa namjibu ni kwamba, yale mambo ambayo aliyasema, ndiyo tunayoyatekeleza sasa. Ndiyo hayo hayo kwa sababu ruzuku na pembejeo ya ruzuku ipo na tunaendelea kutekeleza mwaka huu kama ilivyokuwa mwaka 2006, isipokuwa tuna-*improve on.* Tulichobadilisha mwaka huu ni kwamba, tuna ruzuku

ya pamba, madawa, tunatoa ruzuku ya miche ya kahawa na miche ya chai. Lakini ruzuku ile bahati nzuri fedha iliyotengwa mwaka ule na ya mwaka huu inalingana, shilingi 19.5 bilioni, hiyo ndiyo nilikuwa najaribu kumfafanulia.

Ya pili, *ASDP* ni programu ya miaka saba na mwaka wa 2006 huu tunaoumaliza sasa ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa hiyo programu na katika kitabu changu cha hotuba nimetumia kurasa nyingi kueleza tulichofanya katika mwaka uliopita, hata Mheshimiwa Joseph J. Mungai, wakati anasema mwaka 2006 alikuwa anasema kazi ya kwanza itakuwa ni kuziandaa Halmashauri, kuandaa jamii ambayo itatekeleza mpango huu, hiyo ndiyo kazi tuliyofanya. Tumefanya katika *districts* zote, tumejaribu kufundisha, tumewezesha *district councils* kuanzisha *DADEPS*. Hiyo ndiyo kazi tuliyofanya na ina-*build up* kutoka ile ya mwaka 2006, sasa nisichokielewa kwa Mheshimiwa Zitto ni mikopo gani ambayo anasema hatukuisema, kwa sababu mkopo pekee tunaousimamia katika Wizara ya Kilimo ni kupitia Mfuko wa Pembejeo.

Mfuko wa Pembejeo umeendelea kutoa mkopo na mwaka huu tumeripoti kwamba, mwaka 2006 tumekopesha matrekta 81 na yapo yote katika hotuba, sasa nisingeweza kukopesha kitu ambacho sina, lakini nadhani maelezo niliyompa yanalingana kabisa na swali alilohoji na utekelezaji wa mwaka 2006 umeelezwa vizuri tena kwa kurasa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani majibu niliyonayo ndiyo hayo.

**MWENYEKITI:** Nadhani ameridhika lakini hili la uwekezaji labda mlitazame, sijui Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto alikuwa na maana gani, lakini labda baada ya hapa kwa sababu sasa umeridhika, mnaweza kuendelea kushauriana kuhusu huo ukurasa wa 85 wa hotuba ya mwaka 2006.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi. Napenda kuuliza jambo ambalo nililigusia wakati nachangia ...

**MWENYEKITI:** Kasma ipi?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kasma ni *Vote 43*, programu ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu cha 250100, ambayo ni *basic salaries,* mshahara wake na nazungumzia *administration* ambayo nafikiri inahusu Chama cha Ushirika cha Mara, ambacho kama wilaya nyingine, kiliyumba na hatimaye hakikuwahi kupewa ruzuku tena na hata baada ya kuweka katika *receivership* mali zake bado zinashikiliwa. Wakulima wa pamba na kahawa Tarime bado wanakidai hicho chama lakini hata katika mpango wa sasa, naona vinazungumziwa vyama vingine vya maeneo mengine vinavyokuwa *stabilized*, lakini hiki chama kimesahaulika. Nakumbuka ya kwamba wakati kinayumba na kufa au kulemaa, Mheshimiwa Waziri alikuwa Mkuu wa Mkoa katika mkoa ule na kwa hiyo anakifahamu vizuri. Napenda kujua ana mikakati gani katika kukifufua na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao kwa madai waliyonayo?

La pili, napenda kuzungumzia Shirika la Uaguzi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO).* Hili ni shirika ambalo lina malengo ya ukaguzi ya vyama vyote vya ushirika na hili shirika limeshindwa kufikia malengo ya ukaguzi kwa sababu ya utawala mbovu, ambao umesababisha watumishi waliostaafu, waliofukuzwa na kuachishwa kazi au kupunguzwa kazi, wameshindwa kuelewana na uongozi uliopo hadi kwenda kufungua kesi nyingi zipatazo 12 na wanalidai shirika hili zaidi ya shilingi milioni 150 na kwa ubishi wa uongozi, kesi zinaendelea, pamoja na kwamba fedha za Serikali ambazo inaweka katika shirika hilo pamoja na mishahara minono, magari ya kufanyia kazi kila ofisi na vilevile fedha za kuajiri wataalam, kuna zaidi ya *CPA* 15 pale lakini halijaweza kufikia malengo wala kutatua mgogoro na hawa wafanyakazi.

Fedha hizo zinatumika zaidi kwa kufanya kesi, kesi nyingine ziko mbali hata mpaka huko Rukwa, gari linakwenda huko linakaa wiki tatu. Haya ndiyo ningependa nijue ya kwamba ana mpango gani ikiwa ni pamoja na kutazama uhalali wa ofisi kuu hiyo kuhamishiwa Dar es Salaam? Kuna mpango wa kuihamisha kwenda Dar es Salaam na huo mpango umesimamiwa na Viongozi Wakuu wa Shirika hilo, ambao ni pamoja na Mhasibu Mkuu, Mkuu wa Idara ya Utawala na Mkurugenzi wa Utawala, ambao tangu waajiriwe familia zao zinaishi Dar es Salaam, hilo pia tungependa tupate ufafanuzi.

La tatuna la mwisho ni pale ambapo…

**MWENYEKITI**: Sasa Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, naona unaogelea tu, unatafuta matatizo yote uliyonayo uulizie hapa, sio utaratibu kikanuni ni kutafuta ufafanuzi katika jambo, sasa wewe unachangia.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi anijibu hayo mawili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuweka rekodi sahihi kwamba, wakati *Mara Cooperative Union* inakufa, mimi sikuwa Mkuu wa Mkoa nilikuwa raia tu, nilishaacha kuwa Mkuu wa Mkoa. Lakini nilishuhudia ikifa, kwa sababu nilikuwepo kama raia, kitu ambacho naweza kusema tunasaidia vyama vilivyopo sasa kwa mfano, Nyaza ipo haijafutwa ni chama, *SHIRECU* au hivi vyama tunavyovisaidia vya korosho, vipo lakini *Mara Cooperative Union* ulifutwa kwenye daftari la vyama. Kwa hiyo, kwa kweli kisheria *Mara Cooperative Union* haipo.

Lakini sisi kama Wizara inayosimamia ushirika, tungependa washirika wa Mkoa wa Mara wawe na chama cha ushirika cha mkoa au cha wilaya, kadri watakavyopenda wenyewe. Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kuwahakikishia wakulima wa Mara kwamba, Wizara yangu iko mbioni kwenda kushirikiana nao na kwa kweli tumeshapeleka wataalamu kule kufanya *ground work* ili hatimaye waanzishe Chama Kikuu cha Ushirika. Tumeshafanya uchaguzi katika vyama vya msingi, sasa tunashughulika na chama cha ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo kwa wakulima wengine wa maeneo mengine, tutatazama uwezo wa Serikali ili kuweza kuwalipa wakulima waliokuwa wanaidai *Mara Cooperative Union,* shilingi mia mbili na arobaini na moja milioni kama walivyo wakulima wa Chunya na wakulima wa maeneo mengine. Fedha za bajeti hii zikitosha huenda tutaweza kuwalipa wakulima. Tungependa kuwapa wakulima motisha.

La pili, hii *COASCO* kwanza hakuna mtu aliyeagiza *COASCO* ihamie Dar es Salaam, *COASCO* iko Dodoma hapa na itaendelea kuwa hapa. Kwa sababu *COASCO* ni chombo cha ukaguzi, kikiwa hapa kinakagua nchi hii kwa urahisi zaidi kutokea hapa kuliko Dar es Salaam. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Wangwe, hakuwa amepata *information* kamili, kwa sababu wakati mwingine kuna watu waliofukuzwa kazi *COASCO,* sasa wanatembea kila mahali wanaandika kwenye magazeti na wanatumia kila njia ili *message* ifike. Sisi hatukatai kuwasilikiza, wengine nimewahi kuonana nao, lakini wana kesi ziko mahakamani, ukishakwenda mahakamani unaiachia mahakama iamue.

Sasa mimi Waziri siwezi kuiambia mahakama isisikilize maana nimeshaamua, zile kesi ziko mahakamani, *COASCO* haikuwatuma kwenda mahakamani, wao wenyewe walienda. Kwa hiyo, mahakama ikiamua kesi hizo zitakuwa zimeamliwa lakini mashirika yote yana matatizo ya hapa na pale lakini huwezi kusema kwa sababu ya tatizo hili basi *COASCO* imeshindwa kazi yake. *COASCO* inafanya kazi ya kufundisha kwa kushirikiana na Idara ya Ushirika. Sasa hivi kazi kubwa wanayoifanya ni kufundisha wataalamu wa vyama vya ushirika, kwa sababu watamkagua nani kama hamna zana? Kwa hiyo, tumewaambia wafanye kazi ya kufundisha ili wapate vyama imara ambavyo wanaweza kuvikagua. Kazi hiyo wanafanya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, pamoja na Idara ya Ushirika ya Wizara yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote* 43, programu ya 10, *sub-vote* 1001, mshahara wa Waziri. Nataka nimhakikishie Waziri wangu kwamba, mimi ninamheshimu sana kwa sababu hata katika *speech* nimempongeza yeye na Manaibu wake wawili na watendaji wake wote. Wakati tuko Dar es Salaam, tunajadili hizi bajeti kwenye Kamati, ilipitishwa bajeti ya Wizara ya Kilimo, lakini tulipofika hapa mara tu baada ya bajeti ya Wizara ya Fedha kusomwa, tumepewa vitabu hivi vya *public expenditure* na *development votes,* hizi takwimu zao ni tofauti kabisa. Sasa inawezekana vilevile upande wa takwimu hizi kukawa kuna makosa huku na huku, lakini si ambacho nataka kukisema. Nataka kusema kwamba, najua kuna mambo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri atayajibu, lakini napenda kupata ufafanuzi wa mambo machache:-

La kwanza, niuliza kuhusu madeni ya ushirika, nilisema kwamba mwaka 2006 nilipouliza swali hili niliambiwa kwamba, waliofanya ubadhirifu wa ushirika kutumia Sheria ya Ushirika Na. 20, walichukuliwa hatua za kisheria hata kufikishwa mahakamani. Lakini hapa nimekuta kuwa badala ya kuchukuliwa hatua za kisheria, Wizara imejiandaa kulipa fedha za ushirika. Kwa hiyo, napenda kupata ufafanuzi hapa, ilikuwaje sasa tulisema tutachukua hatua kule watalipa hizo pesa, lakini sasa Wizara inalipa fedha hizo?

La pili, habari ya benki ya wakulima, tulisema kwamba katika bajeti ya Waziri wa Fedha, alizungumzia kwamba kutakuwa na *Investment Bank* ambayo mwaka 2006

alisema kwamba, ilihitaji kuongezwa shilingi bilioni 50, lakini mwaka huu alisema kwamba itaongezwa mtaji kidogo. Sasa nataka ufafanuzi, huo mtaji kidogo ni kiasi gani? Kwa sababu kwanza tulikuwa hatuamini kama *Investment Bank,* inaweza kuwahudumia vizuri wakulima, kwa sababu mazingira ya wakulima ni tofauti kabisa. Hili ni jambo japokuwa alilizungumza Waziri wa Fedha, lakini kwa sababu Mheshimiwa Waziri, kagusia wakulima, atakuwa analifahamu vizuri.

La tatu, nataka nipate ufafanuzi juu ya *contract farming* kule Kilombero, ambapo wakulima wale *out growers* wa miwa wanakatwa kodi katika hatua tatu tofauti, kuanzia uvunaji, usafirishaji na upimaji. Kwa mawazo yetu sisi tunasema hii si haki, lakini pengine Waziri ana ufafanuzi kuhusu hili, naomba nipate ufafanuzi wa jambo hili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamsaidia Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kwa suala linalohusu madeni ya ushirika ni kweli yako madeni ya ushirika na ni kweli vilevile wapo watu ambao wamefanya ubadhirifu. Lakini sisi nchi inayofuata utawala wa sheria, kama mtu amefanya uhalifu na vyombo vya dola bado vinachuguza na havijamchukulia hatua kwa sababu vinatafuta ushahidi, basi hatuwezi kutoka tu ghafla tukaenda tukamhukumu huyu mtu aliyehusika. Lakini Naibu Waziri, alikuwa ameeleza na kutoa mifano ya vyama ikiwemo Nyaza, ambayo watuhumiwa *actually* bado ni wahutumiwa, kwa sababu hawajafika mahakamani wala hawajaonekana na hatia.

Sasa vyombo vya dola vinaendelea na kazi hiyo lakini hiyo haina uhusiano na kulipa madeni haya, madeni haya msingi wake ni kwamba, tunataka vile vyama vikopesheke ili viweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Vyama hivi vilikuwa na madeni ya namna mbili; kulikuwa na madeni mengine makubwa tu ya zamani, ambapo Bunge hili lilihusika katika kupitisha azimio la kufuta madeni yale. Tulifuta madeni hapa na katika madeni tuliyoyafuta, shilingi bilioni 15, yalikuwa madeni ya Vyama vya Ushirka, ambavyo vilikuwa vinahusiana na *NBC Holding, Councils* na *COASCO,* vile vyombo vya kiserikali, haikuhitajika kuwa na fedha za kulipa.

Kwa hiyo, Bunge likatoa Azimio na Hazina ikafuta, lakini kulikuwa na deni la shilingi bilioni 11, ambalo huwezi kulifuta kwa sababu wako wanaodai. Sasa hili tumelikata sehemu mbili yako madeni ya benki, ambayo tunazilipa benki ili vyama vile vikopesheke, hizi ndizo tunazoshughulikia mwaka huu. Halafu yako madeni mengi ya wakulima walipeleka mazao yao hayakulipiwa na vyama hivyo, kwa hiyo, hawa wakulima kama alivyowaulizia Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, wale wa Mkoa Mara tutawalipa na wale wa Chunya. Tuna orodha na madeni haya ni kati ya Decemba, 2004 si zaidi ya hapo. Hayo ndiyo tuna-*commitment* ya kulipa. Kwa hiyo, hili la kulipa madeni halina uhusiano na kushtakiwa kwa watu, watu wale watashitakiwa ushahidi ukishapatikana watakwenda kwenye mahakama kama sheria inavyotaka.

Halafu kuhusu Benki ya Kilimo, haya ni mawazo na nina hakika yatakuwa yanafanyiwa kazi na Hazina kwa sababu sisi sote tunapenda siku moja tuwe na Benki ya Wakulima, kwa sababu nchi hii haina *system* ya kukopesha wakulima. Lakini ni jambo ambalo sitaki kulisema hapa, kwa sababu liko nje ya uwezo wangu. Liko lingine la

Benki ya Ushirika ambalo nalo linashughulikiwa na Wizara yangu, lakini bado ni mawazo, wakati utakapofika, Serikali itasema tumefikia wapi katika ku-*promote* uanzishwaji wa aina hiyo ya benki. Lakini ni mawazo mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na sisi hatuna matatizo na mawazo yake hayo.

Juu ya *contract farming* na mfumo wa kodi, hili kule Kilombero kuna mifumo watu wanalima miwa halafu inanunuliwa na kuna magari yanakodishwa kusomba. Sasa zile ni biashara, ile kulima na kusombaza basi wale wanaobeba au wanaonunua wanatozwa kodi ya *VAT*, mfumo wa kodi ambao nadhani tumeukubali na Bunge lako limepitisha bajeti na hiyo kodi ikiwemo. Sasa kama Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, angependa hiyo kodi iondolewe basi anaweza akatumia nafasi kama Mbunge, kueleza ubaya wa hiyo kodi na bajeti hii itakapo kuja nyingine basi Wizara ya Fedha itakuwa imesikiliza, lakini kwa sasa mimi sina cha kusema juu ya kodi, maana tumeshapitisha bajeti. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kwanza, nimhakikishie tu mzee wangu na Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Stephen M. Wasira kwamba, mimi ninamuunga mkono lakini nataka tu anisaidie kwa sababu programu ya 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 - *Basic Salaries and Pensinable Posts*. Nilipokuwa naangalia katika miradi chini ya *ASDP,* nimeona mgawanyo wa miradi katika karibu kila Mkoa wa Tanzania na huu ni mradi mzuri sana ambao lengo lake kuu ni kupanua na kuendeleza Sekta ya Kilimo nchi nzima. Lakini sasa sifahamu kama Mheshimiwa Waziri, amesahau kuweka Mkoa wa Mara ama kuna sababu maalum? Sasa hilo naomba anisaidie.

Lakini la pili ni kwamba, nikiangalia katika sehemu ya miradi ya Wizara yake, nimeona kwamba pesa nyingi za mradi huu ziko katika Wizara yake, kitu ambacho nilifikiria kwamba labda zingeenda mikoani kule kwenye miradi ili pesa hizi ziweze kuleta mabadiliko ambayo tunataka.

La tatu ni kuhusiana na *PADP*. Nikisoma katika kitabu cha hotuba yake, ukurasa wa 65 wanasema, kazi zilizopangwa naomba ninukuu: "Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo; pamoja na mambo mengine anasema ni kuwezesha jamii kubuni na kutekeleza miradi 3,155 kwa kutumia mbinu shirikishi." Sasa nikienda katika *vote* za mikoa, sioni sehemu yoyote ambapo hizi pesa zimewekwa na mimi nilitegemea kwamba, labda zingeenda huko huko mikoani na vijijini ili ziweze kuleta mabadiliko ambayo Wizara na Serikali ilitaka. Naomba nipate maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kwanza, majedwali yale yameonesha miradi ambayo ilishafanyiwa upembuzi yakinifu, lakini si kwamba Mkoa wa Mara haumo. Ukisoma vizuri pale, utakuta kuna miradi katika Wilaya ya Tarime ambayo ni Mkoa wa Mara, lakini vilevile katika Jimbo la Mheshimiwa Charles Kajege, iko miradi ianyogharamiwa na *DADPS* na *ASDP*, mmoja upo Namhula, ambako yeye anapajua vizuri na mwingine unakusudiwa pale Kasuguti, ambayo ni miradi midogo lakini ndiyo miradi inayotakiwa igharamiwe na *ASDP* kupitia *DADPS*. Kanuni inasema kama mradi utazidi sana Mradi wa *DADPS,* basi mradi huo unaweza ukaletwa ili uweze kupata msaada wa kitaalamu na pengine fedha

kutoka Wizarani. Kwa hiyo, naweza kumwomba Mheshimiwa Charles Kajege, kama atashirikiana na Halmashauri yetu ya Wilaya, pamoja nami nikiwa diwani mwenzake, tukibuni mradi basi mradi ule ukija nao utaingia kwenye kitabu cha mwakani, kama utakuwa umefanyiwa upembuzi yakinifu au kama utakuwa unahitaji fedha. Kwa hiyo, hakuna mkoa ambao umebaguliwa na hasa ikizingatiwa kwamba, fedha za *ASDP* zimepelekwa katika wilaya zote nchini.

Halafu kuhusu kwamba kuna fedha nyingi ziko kwenye Wizara zingepelekwa vijijini, mimi nataka kulihakikishia Bunge kwamba, fedha zilizoko Wizarani zitaenda vijijini kwa sababu ukichukua ile bajeti ya kawaida shilingi 19 bilioni, zinaenda kwenye mbolea na mbolea ile inaenda vijijini halafu shilingi 3.5 bilioni zilizoko kwenye Bodi ya Mikopo zitakopwa kwa pembejeo na matrekta na zana zitaenda vijijini. Kwa hiyo, sisi hapo ni *clearing house,* tunazishikilia kabla hazijaenda. Wale watakaozikopa ndio watakozifikisha huko kwenye vijiji, kwa hiyo kwa kweli hakuna. Halafu 75% ya *ASDP* yote inatekelezwa hata fedha zilizoko kwenye Wizara, shilingi 23 bilioni ambazo ni za *ASDP,* mwisho ya yote zitatumika kufanya kazi ya *irrigation somewhere* katika wilaya au vijiji. Kwa hiyo, kwa kweli hakuna fedha nyingi sana katika Wizara ya Kilimo, ambazo ni za kutumika, zote ni za huduma zinazowaendea wakulima kwa namna moja au nyingine.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika lakini nataka anihakikishie kwamba, mwakani hizo pesa zitakuwa kwenye majedwali na wala hatazieleza kama alivyozieleza tu hapo? Kwa sababu baadaye inakuwa ni vigumu kuzifuatilia katika Miradi ya *DADEPS*; kuna *only four million and five hundred thousand*, ambazo katika mkoa mzima sijui utafanyia kazi gani zikatosheleza mahitaji hayo?

**MWENYEKITI:** Basi wamesikia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jana wakati nikichangia nilieleza juu ya ukulima wa Mkoa wa Singida hususan Jimbo la Iramba Magharibi na nikaeleza wakulima wa jimboni kwangu jinsi wasivyokuwa na shughuli nyingine mbadala zaidi ya kutegemea kulima, kilimo ambacho ni cha jembe la mkono.

**MWENYEKITI:** Kasma?

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani *Vote 43*, programu ya 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sasa uombe ufafanuzi kuhusu suala la sera, usianze hotuba kuhusu malalamiko ya wapiga kura wako, huu sio wakati wake.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nilichokuwa naomba kwa sababu hili fungu linahusiana na utawala, yeye aliyeelezea katika majibu yake, tulikuwa tunazungumzia juu ya kuwahami wakulima ambao wanategemea kilimo na hasa wanapokumbwa na matatizo. Matatizo ambayo niliyaelezea jana nilisema

kwamba, wakulima wa Jimbo la Iramba Magharibi, waliwahi kulima mtama mwaka 2006 na katika kilimo hicho cha mtama ni katika njia ya kujiondoa umaskini lakini ule mtama kwa bahati mbaya ndege waharibifu waliingia wakaushambulia mtama ule, kwa hiyo hawana chakula katika mwaka huu. Lakini pamoja na hayo, Mheshimiwa Waziri wakati akijibu alisema kwamba, yeye yuko tayari kupokea hoja moja kwa moja kwa kupigiwa simu na ili afanye hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe wakati limetokea tatizo hili, niliwasiliana na Mheshimiwa Waziri moja kwa moja na nikamweleza tatizo hili lakini ndege ya kwenda kuangamiza wale wadudu haikufika. Sasa ninachokiomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie; je, wale wananchi ambao wanategemea kilimo ndio waondokane na umaskini; tutawahami vipi katika mwaka huu na chakula wakiwa hawana?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kuwepo ndege aina ya kweleakwelea nilipewa na Mheshimiwa Mbunge tukiwa hapa Dodoma, kipindi hiki hiki. Mimi nilitoa maelekezo kwamba, ile ndege iende Singida kushughulikia kweleakwelea. Anipe muda ni-*check* kama kweli haikwenda, kwa sababu mimi ninajua tumetoa maelekezo na hiyo ndege ilikwenda Singida. Sasa kama imekwenda Singida na mjukuu wangu akawa yuko Dodoma, watakuwa wamepishana na ile ndege. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, ndege ile imefika Singida. Ambacho kinasemwa na ambacho alikisema Mheshimiwa Mohamed Missanga ni kwamba, inaweza kuwa imekwenda imechelewa. Badala ya kwenda Januari, taarifa tulizipata Aprili na ndege ilikwenda Aprili *immediately*. Lakini naweza kusema kwamba, kwa ajili ya *future,* tutajitahidi kwa wakati mwingine, tatizo ndege yenyewe ni moja tu nchi nzima tena ni ya *Redlocust* lakini inatusaidia sana. Kwa sababu tunaelewa maeneo yale yenye matatizo kwa msimu unaokuja, tutajitahidi kuiwekea ratiba mapema zaidi ili tu-*deal* na kweleakwelea ili tusije kuingia katika balaa la kukosa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma H. Killimbah alinieleza na nilichukua hatua na ile ndege imeenda Singida. Ndege ile imeenda Singida, Shinyanga na Magu tena zote hizo zilikwenda katika hizo *stations* kwa kuelezwa na Wabunge wa maeneo hayo. Nadhani tatizo ni kwa sababu ndege ni moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili juu ya hali ya chakula. Mwezi wa nane unaokuja tunafanya tathmini. Nimesema kwenye hotuba hii, tathmini tuliyofanya ni ya awali, lakini tutafanya tathmini tena mwezi wa nane ili kuthibitisha ni wapi na wapi ambapo kuna upungufu wa chakula. Kwa hiyo, ikitokea kwamba katika maeneo hayo watu wameathirika kwa sababu ya kweleakwelea na chakula ni pungufu basi tutachukua hatua za dharura kama tunavyochukua hatua za dharura katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia *Vote 43,* programu 10, *sub-vote* 1100, *item* 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la sera. Nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie kuhusu taratibu za ajira katika vitengo vyake vya masuala ya kilimo. Nilimpa mfano wa shirika lake moja ambalo limewaajiri walinzi kama vibarua zaidi ya miaka ya kumi bila hata ya kuwasimamisha sijui miezi mitatu, mitatu, lakini baada ya pale wakawasimamisha kazi bila hata ya kuwapa chochote. Bahati mbaya kabisa, hawa wafanyakazi wamenipigia simu leo asubuhi, sasa hivi nakuja hapa wamenipigia tena. Kutokana na taarifa yao, Naibu Waziri alipata *documents* hizo. Naomba anisaidie taratibu za ajira katika hizi *Research Institutes* zake zikoje? Je, hawa watu ambao wamefanya kazi kwa miaka kumi katika *Sugar Research*, wakiwa kama vibarua kisha wakaachishwa kazi bila chochote, ni halali? Je, wao wako tofauti na sheria nyingine za kazi? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda angetuma jina la *Research Institute* anayoizungumzia, maana tunazo *Research Institutes* nyingi ili tuweze kumjibu *specifically* kulingana na tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Kama ingekuwa sio tu tutaendelea kupoteza muda, hayo anayoyataka Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama yapo kwenye programu 30, *research development,* lakini nadhani kwa kuwa tumeshalifikia basi umeliwahisha tu. Hebu uwe wazi, nilitaka hata mimi kukuuliza maana unakuwa unafumbafumba na humu sote tunataka tujue na Manaibu Mawaziri wako wawili sijui huyo uliyekaa naye ni yupi na ndio anayo hiyo karatasi. Linakaa katika hali ya sirisiri na hapa Bungeni hatuendi hivyo; hebu uwe muwazi kuna nini hapo?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda nilivyotamka nilitumia sauti ndogo, nimesema *Research Institute* ya Kibaha ambayo zamani ilikuwa inaitwa *Sugar Research,* hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja hili jambo lilijitokeza. Kwa hiyo, nataka anisaidie utaratibu wa shughuli hizi na Naibu Waziri wake anayenong'ona naye sasa hivi hapa, ndiye aliyehusika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa kuweka rekodi sawa, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, tuwe wakweli tu, hukusema Kibaha, hukutaja Kibaha kabisa, sisi tunasikiliza kwa makini sana, ulisema tu *Sugar Research*, wengine tukadhani ni Kilombero.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninazozipata kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye alifuatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba, hili tatizo walilipata kule kwenye *Sugar Institute,* Kibaha na maelekezo yalitolewa na sasa tatizo lile linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, baada ya muda labda tutawasiliana na Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, tumweleze matokeo lakini kwa sasa hivi bado hatuna matokeo, kwa sababu yanashughulikiwa na *management* ya pale *research center*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .......................... Sh.547,317,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ………………….. Sh.1,166,243,600

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza katika *Vote 43, sub-vote 1003, item 250100 - Basic Salaries*, kuhusu suala la *policy*.

**MWENYEKITI:** Haiwezekani hiyo. Mshahara uliopo hapa sio wa Waziri, huu ni mshahara wa Mkurugenzi wa Utafiti na sio kazi ya Bunge kuchukua mshahara wa hawa Wakurugenzi, sisi tuna-*deal* na Waziri tu.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia programu hii hii ya 10*, Vote 43, subvote1003, item 250100 - Basic Salaries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ...

**MWENYEKITI:** Kwa mshahara wa nani sasa? Hapa ni mshahara wa Mkurugenzi wa *Policy and Planning.*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Ya *policy and Planning?*

**MWENYEKITI:** Wabunge hatuwezi kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya watumishi walio chini ya Waziri. Kwa hiyo, kama ungetaka kupenyea kwenye mshahara ulikuwa ni wa Waziri. Sasa sehemu yote iliyobaki ya vitabu hivi inabidi twende kwenye kasma mahususi ambayo inahusu suala lenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Agriculture Training Institute* .................... Sh.2,029,599,000

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Programu hiyo hiyo, *subvote* 1004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kujua ni kwa nini *subvote* hii haijagawanywa katika vifungu vidogo vidogo kama zilivyo *subvote* nyingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri au yote ni mshahara tu? Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri, ile Sh.2,029,599,000 inaonekana kama ni mishahara ya vituo vya mafunzo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *vote* inashughulika na mambo ya mafunzo. Katika bajeti ambayo nimeiwasilisha hapa, tutaajiri Wakufunzi 116 katika mwaka huu wa fedha, kwa ajili ya kuendeleza *training* kwa wanachuo tarajali 3,000. Kwa hiyo, utaona kwamba bajeti ya mishahara katika kifungu hicho itakuwa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, hii ni mishahara tu.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia *Vote 43,* programu ya 10, *sub-vote* 1004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbeya kuna Chuo cha Wakulima wa Inyala, ambao wanatoa mafunzo ya kilimo cha maksai. Mheshimiwa Waziri hapa alikuwa anasema kabla hatujaanza kukimbilia kwenye matrekta ni vizuri kama tungetumia wanyama zaidi kwa sababu hiyo iko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi chuo hiki huwa hakitumiki. Kwa hiyo, kuna watu ambao wanapata mishahara lakini kunakuwa na mafunzo mara moja kwa mwaka au wakati mwingine mwaka mzima kunakuwa hakuna mafunzo. Je, mwaka huu kutakuwa na utaratibu wa kuweza kutumia chuo hicho sawawa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunavyo vyuo vya namna hiyo, ambavyo vinashughulika na mafunzo ya wanyama kazi chini ya mpango wa kupeleka madaraka kwa wananchi. Vyuo hivi vingi tunavihamishia katika *District Council*. Lakini vilevile Wizara yangu itaendelea kushirikiana na *District Council* kuhakikisha kwamba mafunzo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho chuo anachokizungumzia Mheshimiwa Richard Nyaulawa, kitakuwa kimojawapo. Kama kina matatizo tutakifuatilia ili kiweze kutimiza wajibu wake kama kilivyokusudiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Crop Development* ........................... Sh.35,842,155,400

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya 20, *sub-vote* 2001, nafikiri *item* 280500, kama nimekosea nitamwomba Waziri anisahihishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maamuzi mawili yanayohusiana na bodi za mazao. Moja ni kwamba, bodi hizi zitakuwa *financed fully* na Serikali kwa hiyo, hazitagharamiwa tena kutokana na makato ya wakulima. Pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikutana na viongozi wa mazao yote na ikawekwa programu ya kukuza uzalishaji wa mazao haya. Sasa ombi langu lilikuwa ni kujua haya mambo mawili yamezingatiwa vipi katika bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nijulishwe Rubada imezingatiwa vipi katika bajeti hii, inapewa pesa ngapi na katika mwaka unaokuja inafanya shughuli gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sina hakika hapo Mheshimiwa alipochomeka lakini ninayo imani na Mheshimiwa Waziri, masuala haya anayafahamu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi bodi zilikuwa zinajiendesha kwa kutumia *cess*. Lakini Serikali kwa ajili ya kutaka kulinda bei ya mkulima, tuliamua kuondoa *cess* na badala yake zinapewa fedha moja kwa moja kutoka Serikalini. Sasa fedha kiasi gani na zitafanyaje kazi, nimewahi kuonana nao karibu wote na nimewapa ushauri, kwa sababu kuna kazi zile wanazofanya *regulatory* ambazo kwa kweli fedha wanazopewa zinaweza zikasaidia lakini kuna kazi ya *promotion* ambayo pengine wanaweza wasiweze kuifanya vizuri.

Kwa hiyo, nilichowaagiza ni kwamba, wawe wana-*touch* na *District Councils* ili fedha za *ASDP* ziweze kutumika katika mpango ambao utakuwa umefikiwa kati ya Bodi na Halmashauri za Wilaya zinazoshughulika na mazao haya. Hicho ndicho tulichoweza kufanya, kwa sababu uwezo wa bajeti hii kuwapa fedha zote wanazotaka, haupo. Kwa hiyo, upande wa *promotion* kwa mfano, watu wa korosho tumewaambia wakitaka kupanda miche mipya, mpango huo unaweza kugharamiwa na *DADPs* katika *District* na hivyo hivyo kwenye mazao mengine kama kahawa na kadhalika. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tunavyosema lakini fedha zinazokwenda huko haziwezi kutosha *hundred percent,* maana hata bajeti hii nayo haitoshi.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Rubada, Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Kuhusu Rubada, nayo ni bodi ila yenyewe iko *multipurpose* kidogo. Lakini kazi inayofanywa na Rubada pale zaidi ni ya kiutafiti zaidi pamoja na kuandaa miradi ambayo inaweza kutumiwa na wawekezaji. Hiyo ndiyo kazi inayofanywa hasa katika eneo lile la *Rufiji Basin,* ambako kuna maeneo ambayo ni *potential* kwa wawekezaji. Tulikuwa tumeuliza *policy* gani tunafanya lakini Rubada tunaitumia kufanya kazi hiyo ili wawekezaji wakija wa-*identify* maeneo kama lile Shamba la Kotako liko chini ya Rubada.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia *Vote 43,* programu ya 20*, sub-vote 2001, item 310700 - Feasibility Studies, Project Preparation and Design.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilijaribu kuwaomba watueleze kama kuna *study* yoyote iliyofanyika ya kuangalia kama kuna uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha matunda, kwa sababu matunda katika nchi yetu inaonekana ni kama hayajalimwa. Kuna maeneo mengi ambayo yanazalisha matunda, Tabora kuna maembe, Geita kuna mananasi mengi sana na Lushoto kuna matunda mengi sana, lakini unakuta tunapokea matunda kutoka nje. Mimi nimefika Uganda, nilipoangalia uzalishaji wao ni kidogo sana na Kenya hata uzalishaji wao ndio wanazalisha lakini sio kwamba wanatuzidi sana. Sasa nikauliza; je, wanaweza kuanzisha kiwanda sehemu kama Geita?

Bahati mbaya sana katika kifungu hiki mwaka 2006 hakikupewa fedha na mwaka huu hakikupewa fedha. Je, wanafanyaje *crop development programmes* bila *study* hizi? Naomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafunizi, utafiti wa *reservation* ya matunda?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kutafiti kwa ajili ya kuanzisha viwanda inafanywa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kwa kweli wao ndio wanatakiwa kufanya hiyo *feasibility studies,* kwa kutumia vyombo ambavyo viko chini ya Wizara hiyo. Kama ni kiwanda kidogo sana inaweza ikafanywa na *SIDO* lakini sisi hatufanyi *feasibility study* kwa ajili ya viwanda.

**MWENYEKITI:** Nadhani *point* imechukuliwa, kwa sababu ni ujumla wa Serikali kwamba kuna haja ya kuwa na utafiti kuhusu viwanda vya *agro processing*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye *Vote 43,* programu ya 20*, sub-vote 2001, item 310700 - Feasibility Studies, Project Preparation and Design.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda Mheshimiwa Waziri aeleze ni kwa nini ilichukua muda mrefu sana kuleta mazao mapya kwa wakulima na hatimaye wananchi waweze kuishi na kusomesha watoto wao wengine wakaanza kulima kilimo haramu cha bhangi katika Mikoa yote na wakapata matatizo makubwa sana ya kisheria wakati ambapo ilibidi hili suala liwe limeangaliwa kabla? Je, anaweza kuwaomba radhi wananchi kwa niaba ya Serikali kwa sababu hili lilisababishwa na Serikali yenyewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, tabia ya kulima bhangi ni uhalifu tu haiwezi kutokana na kwamba mtu amekosa zao mbadala basi analima bhangi, vinginevyo Mikoa yote tungelima bhangi. Kwa hiyo, mimi silioni hilo kama ni *correct.* Kama unazungumzia kuhimiza utafiti, mwenzio Mheshimiwa Faustine Rwilomba amekwishasema kwamba, utafiti uendelee ili tuweze kusindika mazao yetu. Yanayotokea Tarime sio lazima yawe ni ya nchi nzima. Ninyi ndio mnaolima bhangi sana nyie. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali sisi tunalima lakini pia kuna wanaolima zaidi kama Morogoro, Arusha na Mbeya, kwa kweli ni nchi nzima. Hilo zoezi la kuteketeza linaendelea nchi nzima. Ndio maana nasema wale wakulima walilazimika, haikuwa hiari yao na ni kwa sababu ya Serikali kuchelewa kuwapa mazao mbadala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, huna hata hoja. Mara kwa mara tumeona Polisi wanapofuatilia wanakuta bhangi imezungushiwa mazao yaliyo halali. Huwa inagunduliwa katika sehemu za vificho. Sasa hicho sio kilimo cha kusema mtu haelewi anachofanya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Directorate of Irrigation and Tech. Service*….Sh.2,200,466,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Research Development* ………………Sh.13,377,357,100

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia programu ya 30, *sub-vote* 3001, *item* 250300 - *Employment Allowances* na vilevile *item* 260800 - *Training Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *trend* kwanza katika *Employment Allowances* kuanzia mwaka 2005/2006, utaona kidogo ilikuwa ni *reasonable* lakini baadaye ika-*balloon*. Swali langu kama *Training Expenses* ambayo ni 260800 ime-*balloon* mpaka kwenye 2,434,750,000; inakuaje ifikie hapo wakati huo huo *Employment Allowance* ni kubwa? Kwa sababu nilitegemea kwamba, kama *Training Expenses* zinakuwa kubwa maana yake ni kwamba, wafanyakazi wengi wamekwenda kusoma kwa hiyo, *Employment Allowances* ingekuwa ndogo. Posho kubwa ni *overtime,* hawawezi kuwa wanasoma *at the same time* wanalipwa posho ya ziada. Nilikuwa naomba maelezo hapo.

**MWENYEKITI:** Sina hakika kama unacholinganisha ni sahihi. Anachosema Mheshimiwa ni kwamba, kwa sababu watumishi wengi sana chini ya 260800 wanakwenda kusoma maana yake imetoka kwenye 381. Hapana, Mheshimiwa Charles Kajege kwanza, *ballooning* sio kweli kwa sababu hizo ndio zinaombwa. Hiyo unayoiita *ballooning* ni ya mwaka 2007/2008, haijaanza ndio inaombewa fedha. Kwa hiyo, husemi sasa ime-*balloon*. Kwa miaka miwili iliyopita ilikuwa 210,381, ambayo sio *ballooning* na hiyo *Employment Allowances* ambayo ni 414 kwenda shilingi 1.8 bilioni labda hiyo ndio unaweza kuuliza kwamba zinahusu nini hizi. Kwa sababu unacholinganisha ni miaka miwili ya utekelezaji. Huwezi kuhoji kinachokuja kwa sababu hicho ndicho tunachotaka kukipitisha sasa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka kujua kwa sababu kuna *correlation* hapa kama *Training Expenses* inakuwa juu maana yake ni kwamba, *Employment Allowances* ambayo mojawapo ya *item* ni *overtime*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege, kwa hapa tunachokisoma kwa miaka miwili ya utekelezaji, *there is absolutely no correlation*. *There is a normal rise* ya kutoka 210 kwenda 381. Unachotaka labda kujua ni *Employment Allowances* ambazo ndio zilitoka 414 zikawa 1,861,000,000. Kwa hiyo, sioni hoja yako kwenye 260800. Lakini nadhani una uhalali wa kuhoji ongezeko hili la 250300 ambalo ni 400 milioni kwenda shilingi 1.8 bilioni. Unaendelea?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisiendelee kuhoji. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Cooperative Development* .....................Sh.6,332,474,700
Kif. 5001 - *National Food Security* ................... Sh.867,622,800
Kif. 5002 - *Strategic Grain Reserve* …………. Sh.6,650,807,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1001 - *Administration and General* .......................Sh.100,000,000
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ………………… ....Sh.21,894,007,900
Kif. 2001 - *Crop Development* ……………………....Sh.19,461,860,000
Kif. 2002 - *Directorate of Irrigation and Tech. Serv.* ….Sh.7,472,506,000
Kif. 3001 - *Research Development* ………….............Sh.8,997,488,400
Kif. 4001 - *Cooperative Development* ………….............Sh.537,300,000
Kif. 5001 - *National Food Security* ……………........Sh.60,061,912,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni Na.49(8), kwa ruhusa yako naomba niisome. "Katika mjadala wowote, Mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa zao na Wabunge wengine wote watatajwa kwa kutumia neno Mheshimiwa kabla ya majina yao." Sasa sikutaka kuingilia wakati wa mjadala tukiwa katika Kamati. Kanuni hii imevunjwa mara kadhaa hasa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, alipokuwa anasema Waziri Mungai alifanya hivi, Waziri Wasira kafanya hivi. Kifungu hiki kinajaribu kutusaidia kuonesha *continuity* na kwamba Wizara si ya mtu mmoja, kila Waziri anaendeleza yale yale ambayo mwenzake amekuwa akiyafanya. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Mwenyekiti, utukumbushe tuzingatie kifungu hiki katika mijadala yetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nadhani hilo limesikika na tujitahidi tutii kanuni zetu. Ahsante sana.

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kuipitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika - Fungu 43 kwa mwaka 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuipitisha bila mabadiliko. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo tumefikia mwisho wa shughuli za leo. Naomba nikumbushe tena kwamba, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa tutakuwa na Wizara kwa mpangilio ufuatao ili mjiandae: Tarehe 9 Julai (Jumatatu) na tarehe 10 Julai (Jumanne) itakuwa ni zamu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Tarehe 11 Julai na tarehe 12 Julai (Jumatano na Alhamisi) ni zamu ya Wizara ya Miundombinu na tarehe 13 Julai (Ijumaa) na tarehe 16 Julai (Jumatatu) ni zamu ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, mjiandae kwa hayo.

Lingine, mtaona kwamba hatukupanga semina kesho, kwa sababu tuliheshimu siku ya sabasaba, wengi huwa wanapenda kwenda Dar es Salaam kuona Maonesho ya Sabasaba. Kwa hiyo, kesho hakuna semina.

Sasa naomba kutangaza kwamba naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.35 usiku Bunge lililiahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 9 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*